ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.

24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.

36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.

51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.

72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 25 Juni, 2010

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika,(Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:
Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hati ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa Mwaka Fedha 2010/2011. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamad Masoud Hamad (Waziri Kivuli Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya kwa upande wa upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 8

Hisa za SMZ Benki ya Posta

Mhe. Said Ali Mbarouk (Kny: Mhe. Juma Duni Haji) - Aliuliza:-

Shirika la Posta ni Shirika la Umma ambalo ni taasisi ya Jamhuri ya Muungano. Shirika hilo linamiliki na kuendesha Benki ya Posta ambayo inafanya shughuli zake za biashara Zanzibar na Tanzania Bara.

Mhe. Waziri, Je, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ina hisa kiasi gani katika Banki hiyo?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 8 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Bank ya Posta ina hiza zake na benki hiyo niseme kwamba inamilikiwa na Shirika la Posta, lakini hilo Shirikala Posta sio peke yake wenye hisa hili ni shirika la umma ambalo ni taasisi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Shirika hilo linamilikiwa na kuendesha Benki ya Posta ambayo inafanya shughuli zake za biashara Zanzibar na Tanzania Bara.

Mhe. Spika, serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina hiza 63.8.%

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina hisa	7.4%
Shirika la Posta la TPC	21.9%
Wafanyakazi wa WTP na TC (SACCOS)	6.9%
	100%

Hivyo Mhe. Spika, Shirika la Posta ni miongoni tu wa wamiliki wa benki hiyo na sio mmiliki peke yake.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Muda mrefu hatujaona mgao wa faida unaotokana na shea ya SMZ kutoka benki ya posta.

a) Je, kwa mwaka jana 2009/2010 SMZ ilipata shilingi ngapi kutokana na mchango wake katika benki hiyo ya shirika la Posta?

b) Je, wafanyakazi wanaotoka Zanzibar katika benki hii nao wana asilimia gani?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mgao kwa mwaka jana sikumbuki lakini nitakwenda kuitafuta figa halafu nitamletea Mhe. Muwakilishi, lakini nataka kusema tu kwamba kulikuwa na makubaliano kwa hawa *share holders* wote kwamba kuna haja ya kuongeza mtaji, yaani *investment zaidi kwenye capitol* kwa hivyo ule mtaji hasa wa mwaka jana walikubaliana wauongeze ili benki iwe na mtaji mkubwa zaidi. Sasa hili la figa naomba nilichukue nitakwenda kulifanyia kazi.

Kwa upande wa wafanyakazi wa Zanzibar kama nilivyosema kuna wafanyakazi wa *TP* na *TC* lakini pia kuna Shirika la Posta la *TPC* lina hisa 21.9% na wale wengine wako kwenye saccos, sasa sina uhakika hasa wafanyakazi wa Zanzibar wameingia kiasi gani, hili naomba Mhe. Spika, pia nilichukue nilifanyie kazi.

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hisa zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika taasisi tofauti ni hisa ambazo wananchi wanachangia kwa njia moja au nyengine, na kwa kuwa taasisi hii ya Shirika la Posta sio pekee ambayo serikali yetu ina hisa.

Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba ipo haja ya kuandaa utaratibu maalum kwa taasisi hizi zote ambazo serikali ina hisa ziwe zinawasilishwa kwa wananchi ili waweze kuelewa?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Nakubaliana na ushauri wake kwamba kweli ni jambo jema sana wananchi wetu wakajulishwa hizi hisa na mgao wake kwenye makampuni kama haya.

Lakini ukipeleleza hasa hii benki ya Posta wanajitahidi sana na wanatoa vipeperushi ukenda pale unapewa hivyo vipeperushi na wanaelezea utaratibu ukweli wako *very open* nawashukuru wafanyakazi wao pia tayari kuelezea utaratibu na hasa kukusaidia, ka hivyo nazidi kumshukuru Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi kwamba ushauri wake tumeupokea kwa hivyo tutatanua wigo way ale wanayoyafanya.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Benki ya Posta ni benki ya muda mrefu kwa paha petu na inafanya biashara zake kwa nyumba ya kukodi. Je, benki hii haina mpango wa kujenga jengo lake kama BOT ili kupunguza gharama hizo?

b) Hivi sasa tunasikia pale walipo mabatini Afisi zimekuwa ndogo kutokana na biashara kukua. Je, wana mpango wa kuhamia pengine?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Kweli nakubaliana nae kwamba pale mahala walipo nafasi imekuwa ndogo, jengo limekuwa dogo na

shughuli zimekuwa nyingi zimetanuka na hii yote inaonyesha vipi zile fursa ziliopo kwenye Benki ile wananchi wetu wanazitumia vizuri ukenda pale muda wote pamevamiwa na watu. Kweli jengo ni dogo na kulikuwa na juhudi za kupata jengo jipya nakumbuka walijaribu sana kulitaka lile jengo lililokuwa wamehama *BOT* lakini tukasema tuipe benki yetu ya nyumbani PBZ na wao wanataka kujikita kwenye maeneo haya ya biashara yaani Darajani.

Hivi sasa na wao wanahangaika kutafuta kiwanja waweze kujenga jengo jipya nakubaliana na yeye kwamba ni kweli ipo haja hiyo.

Nam. 72

Magari Yanayokubalika Kuwa Daladala

Mhe. Hija Hassan Hija- Aliuliza:-

Zipo taarifa kupitia madereva na wamiliki wa vyombo vya usafiri wa barabarani (Daladala) kuwa kuanzia sasa Serikali imepiga marufuku kuingiza magari yenye magurudumu manne kwa matumizi ya abiria na kwa zile zilizopo basi zimewekewa muda maalum ili zisionekane hapa Zanzibar.

(a) Je, Mhe. Waziri nini malengo ya amri hiyo na je itakuwa inakwenda sambamba na mpango mkuu wa usafiri hapa Zanzibar *(Zanzibar Transport Master Plan)?*

(b) Baadhi ya wamiliki hao wa Daladala wanadai kuwa hizo ni njama tu za baadhi ya matajiri kwa kuwa wao wanataka kuingiza aina mpya za magari kutokana na uwezo wao kifedha. Je, dai hilo lina ukweli?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:

Mhe. Spika naomba kumjibu Mhe Mwakilishi swali lake nambari 72 lenye vifungu a na b kwa pamoja kama ifuatavyo:-

a) Amri ya kupigwa marufuku kwa magari yenye maringi manne haipingani na mpango Mkuu wa Usafiri wa Zanzibar *(Zanzibar Master Plan) ;* na

b) Sio sahihi kuwa kuna njama kwa baadhi ya watu wenye uwezo wanataka kuingiza magari yenye maringi sita na kuondosha magari yenye maringi manne kwa sababu ya uwezo wao, Idara ya Usafiri na leseni ndio yenye jukumu la kutathmini na kusimamia vyombo vinavyofaa kwa ajili ya kuchukulia abiria hapa Zanzibar, kama

ilivyoelezwa kwenye sheria *No. 7 "Commercial Vehicle"* ya mwaka 2003 kifungu No. 80, Idara ya Usafiri na Leseni ndio iliotoa agizo la kuondosha gari zenye maringi manne baada ya kuona kuwa magari hayo hayakidhi mahitaji. Aidha mtu yeyote anaruhusiwa kuingiza magari yalioruhusiwa na Idara ya Usafiri na Leseni *(Six Wheels).* Napenda kuliarifu tena Baraza lako tukufu kwamba gari hizo zimepigwa marufuku kufanya biashara ya Daladala tu, hivyo zinaweza kufanya kazi za *Tax, private Hire* na kuchukulia watoto wa Skuli

Mhe. Hijja Hassan Hijja: Mhe. Spika, baada ya majibu ambayo sikuyapenda ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c).

Amesema kwamba Idara ya Usafiri na Leseni ndio yenye mamlaka ya kuagiza vyombo vya kuweka kanuni na utaratibu wa vyombo vya usafiri, nataka kujua kwamba maamuzi ya kupiga marufuku dala dala hizi yameanzia mwaka gani na kwa nini zaidi ya miaka ishirini magari haya yanafanyakazi na Idara hii ipo.

a) Maamuzi yameanzia lini?
b) Wizara yako itakuwa sahihi ina magari mangapi yenye magurudumu manne hapa Zanzibar?
c) Je, magari ya magurudumu manne unaweza kuyabadilisha hapa hapa Zanzibar yakawa na magudumu sita na kama uwezekano huu upo Idara yako ina hatua gani kwa Wazanzibar wenye magari haya?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Maamuzi haya yameanza mwaka huu na tunasema mpaka mwakani Oktoba itakuwa ni tarehe ya mwisho.

Kuhusu nani mwenye maamuzi hayo ya kuzuia magari kama nilivyosema Idara ya Usafiri na Leseni ndio mwenye dhamana hiyo. Kuhusu takwimu za magari hili itabidi anipe muda kwa sababu magari ni mengi, lakini suala la kubadilisha kutoka maringi manne kwenda sita, kwa kweli kwa magari kama dungu sio rahisi, zile gari nyengine za *Hiace* ukibadilisha difu ya nyuma unaweza ukabadilisha kutoka maringi manne kwenda sita.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa asilimia mia moja mungu akujaalie urudi tena kwenye kiti hicho, ishaala kwa uwezo wake mwenyezi Mungu na dua hii ninayoiomba leo ijumaa basi utarudi.

Mhe. Spika, katika maisha yangu ya vipindi vitatu kukaa kwenye baraza hili sijawahi kuzuia bajeti hata siku moja na tukizingatia serikali yetu hii ya Chama cha Mapinduzi ndio iliyotoa taarifa rasmi watu wajitafutie ajira kwa njia za halali, tukiangalia Zanzibar kwa asilimia kubwa vijana wetu wamepata ajira kutokana na daladala madereva na makondakta. Na kama tulipitisha sheria hapa mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ndio tulikaa paha juu muda wa siku tano ulitupa kubadilisha mambo ya usafiri, kuondoa gari za mbao ringi moja na kuleta gari za aina mpya vibasi.

a) Hivyo tukiacha haa kwetu Zanzibar lakini tuna wenzetu wametuzunguruka Afrika ya Mashariki ni nchi gani ambayo haitumii dala dala hizi zilizokuwepo?

b) Hizi daladala tulizokuwa nazo kama zinasababisha zogo katika mji wetu huu ni zogo la kiasi gani ambalo limeleta usumbufu gari zisitembee?

c) Nasema kama kutakuwa na utaratibu wowote utakaobadilika kwa mara ya kwanza nakupa taarifa nitaizuia bajeti hii na sitopitisha kwa asilimia mia moja na wenzangu nitaomba waunge mkono?

Mhe. Spika: Hili la (c) sio suali lakini anatoa taarifa au tahadhari.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Kabla ya kujibu suala naomba nitoe maelezo yafuatayo, lazima tukubali kwamba Zanzibar ni sehemu ya dunia kwa hivyo kama ni sehemu ya Dunia nayo vile vile inapaswa kwenda na wakati na mabadiliko yanayotokea Duniani, tukilinganisha wenzetu Tanzania Bara nafikiria vipanya na gari zote ndogo hivi sasa hazitembei pale mjini Dar es Salaam zimepelekwa nje.

Lakini vile vile kwa kujibu suala la Mhe. Muwekilishi nataka kumjibu kwamba jambo ambalo limesababaisha kuzuia magari sio zogo, tunachokizungumzia hapa ni gari za maringi manne zina usalama mdogo kwa ajili ya kuchukua abiria sio suala la zogo, tena tumesema hatukuyazuia kabisa wanaweza kufanya kazi nyengine ziliopo kama vile kwenye *private hire* kwenye sehemu za utalii, kuchukua watoto wa skuli n.k

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi na kunipa nafsi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa sababu nchi yetu ya Zanzibar ina MKUZA na madhumuni yake ni kupunguza umasikini kwa wananchi wetu na wananchi wetu ni masikini na wameshauza umasikini wao mpaka wameshapata daladala za gurudumu nne kwa

ajili ya kujipunguzia umasikini, leo serikali inasema daladala hizi hazifai na watafute daladala za maringi sita.

a) Je. Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba huko ni kuongeza umasikini au kuwapunguzia umasikini?

c) Mhe. Waziri anasema kwamba gari hizi zitumike kwa ajili ya kuchukua wanafunzi na mizigo. Je hao wanafunzi sio watu kama wengine na hiyo mizigo itakayochukuliwa wale watu watakuwa hawamo kwenye gari au ikitokea ajali wao watakuwa hawapati?

d) Je. gari hizi za ringi nne zinasababisha katika nchi yetu ni ajali ngapi za gari za ringi nne zilizotokea na watu wangapi wamekufa kwa gari hizo?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Katika jibu langu mama nimesema kwamba bado serikali haipigi marufuku magari haya kabisa kabisa, kilichopigwa marufuku ni kuchukua abiria kutokana na usalama.

Jengine la kuhusu kuchukua mizigo nafikiri kwa hivi vidungu havikupangiwa kuchukua mizigo tumesema vichukue wanafunzi, Mhe. Mwakilishi aliulizia kwamba je unapochukua hawa wanafunzi wao sio watu, tunachokizungumza ni kwamba gari hizi wanapochukua abiria wa kawaida wanakwenda mwendo wa kasi na kupishana sehemu ambazo sio za kupishana. Lakini unapochukua wanafunzi maana yake unawapeleka moja kwa moja kwa hutokwenda mbio kiasi hicho.

Mhe. Spika, jengine ambalo la ajali siwezi kumwambia ni ajali ngapi zimetokea kwa wakati huo kwa sasa hivi, lakini tutafanya utafiti na tutamueleza ni ajali ngapi zimetokea lakini ongezeko la ajali kama unavyosikia taarifa zinapotolewa na wenzetu wa polisi barabarani ajali zimekuwa nyingi na mara nyingi zinatokana na mwendo wa kasi lakini pia hizi sababu tunazosema gari inatembea kwa maringi manne, kwa hivyo gari ikipasuka mpira kwa haya maringi manne inakuwa na uzito mkubwa na wepesi mkubwa zaidi na uwezekano mkubwa zaidi wa kuweza kuanguka.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji Ujenzi Nishati na Aridhi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa liingie katika Kamati ya Matumizi ili niweze kutoa maelezo kuhusu shabaha na malengo yaliyomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji Ujenzi Nishati na Ardhi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kutujaalia afya njema na uzima na kwa kuniwezesha kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu kuwasilisha hotuba ya Wizara hii mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, nikiulizwa takwimu ya mhula wetu wa uongozi tunaomaliza na hata nisipoulizwa sitosita kupongeza mambo matatu, chama changu kwa ilani yake, serikali katika utekelezaji wake na baraza hili katika usimamizi wa shughuli zake yote matatu yanadhihirisha tumetekeleza ahadi kwa kiwango kikubwa sana, kwa hivyo hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kiasi hiki ametujaalia siha na nguvu zilizotuwezesha utekelezaji huu, akatujaalia ujathiri na kuthubutu kuliko kutuwezesha kujiamini kwa maamuzi mazito tuliyoyapitisha hapa kwa wepesi. Akatujaalia imani na upendo miongoni mwetu vilivyotuwezesha kufanya kazi zetu ngumu kwa bashasha na utulivu tunamuomba azidishe nema na amani nchini mwetu tuzidi kufanikiwa kwenye kila lengo tunaloliadhimia, mradi tu kwa maslahi ya nchi hii na mustakbali wake.

Mhe. Spika, vilevile naomba kuchukuwa fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Makamo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Dokta Amani Abeid Karume, na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Sharif Hamad kwa uamuzi wao wa busara wa kukutana na kukubaliana juu ya mambo ya msingi ya kuiweka nchi hii katika hali ya usalama na amani, hali ambayo matunda yake tumeanza kuyaona katika kipindi chote hichi baada ya kukutana kwao huko.

Inshaallah hali hio itaendelea na kuzidi kuimarika kwa maslahi ya Wazanzibari na ninawasihi na kuwaomba Wazanzibari wenzangu kuitumia fursa hii aliyotujaalia Mwenyenzi Mungu vizuri na ifikapo tarehe 31 July maamuzi yetu Inshaalah yalenge katika kujenga upendo,heshima na mshikamano wa nchi yetu hii na watu wake. Sote tanajuwa kuwa Umoja na Mshikamano ni Sera ya Chama Cha Mapinduzi,Chama ambacho kwa sera na busara zake kinaheshimiwa na Watanzania na jamii ya Kimataifa na ni msimamo wa Chama Cha Mapinduzi kuwa Kura ya Maoni ya Tarehe 31 Julai 2010 ni kura ya "**NDIO".** Huu ni wakati

kwa Wazanzibari wote kuwa na Umoja na kuwa Wastahamilivu hasa pale panapokuwa na tofauti ya fikra na maoni kati yao na hilo lisisababishe kuweko na mwanya kwa umoja wao kwa maslahi ya Zanzibar. Inshaalah Mwenyenzi Mungu kwa uwezo wake atatujaalia Wazanzibari wote kheri,salama na mafanikio katika dhamira yetu ya kuleta Umoja,Amani na Mshikamano ndani ya nchi yetu, Amin.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mhe. Dokta Jakaya Mrisho Kikwete ambaye kwa ujasiri mkubwa kwenye hotuba yake ya mwanzo kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aliwaeleza Watanzania kwamba hali ya siasa iliyokuwepo Zanzibar inamsononesha. Kaahidi kutafuta ufumbuzi wa kudumu. Juhudi zake hizo sasa zimeanza kuzaa matunda.

Naendelea kumpongeza kwa busara kubwa anayoitumia. Katika kuwashajihisha viongozi na wanachama wa Chama cha Mapinduzi kuunga mkono maamuzi ya chama chao ya dhamira hiyo ya kutafuta suluhu ya kudumu ya matatizo ya siasa Zanzibar na kujenga Zanzibar mpya. Zanzibar yenye umoja, mshikamano na siasa za kiungwana.

Mhe. Spika, nakushukuru wewe Mhe. Spika wangu na wetu kwa miaka kumi hivi sasa. Jinsi ulivyoiongoza kwa busara Baraza letu hili tukufu ambalo katika kipindi kinachomalizika limeweza kufikia maamuzi mazito yatakayokumbukwa milele na wananchi wetu. Kadhalika Wajumbe wote wa Baraza hili kwa jinsi tulivyotekeleza majukumu ipasavyo kwa kuweka kando maslahi yetu binafsi na badala yake kuweka Wazanzibari na Uzanzibari wetu mbele. Kwa hilo hatutosahaulika kwa pamoja tumewaumbua wasiyoitakia mema nchi yetu.

Mhe. Spika, ni fahari kubwa kwangu kuwa mjumbe wa Baraza lenye sifa kama hili na unaloliongoza wewe Mhe. Pandu Ameir Kificho. Ni fahari zaidi kuwa miongoni mwa wajumbe wako hawa waliothibitisha kwa kauli na matendo kwamba wapo kuitumikia nchi yao bila ya kujali nchi yao itawatumikiaje. Tumuombe Mwenyezi Mungu muelekeo huu uendelee kuwa ndio dira ya Baraza hili na lijalo na Inshallah utaliongoza tena wewe.

Mhe. Spika, ninawashukuru pia wananchi wote wa Zanzibar kwa uzalendo na ushirikiano wao mkubwa na imani yao kwangu muda wote wa uongozi wangu katika wizara hii. Nasoma na kusikia katika vyanzo tofauti kwamba Wizara yangu imepiga hatua kubwa kuliko vipindi vyengine. Naomba Wazanzibari waelewe na kuamini kwamba kama ni mafanikio basi chachu ni imani ya ushirikiano wao. Mimi na viongozi wenzangu hatuna uchawi wala miujiza ya kuibua maajabu haya ya mafanikio wenyewe bila ya mshikamano thabiti wa wananchi wenzetu.

Nawashukuru sana wananchi kwa pamoja tumeweza kwa pamoja zaidi na tutaweza zaidi. Shukurani mahsusi ziwaendee wananchi wa jimbo langu la uchaguzi Jimbo la Kiembe Samaki, kwa ushirikiano wao mkubwa ulioniwezesha mimi na chama changu kutekeleza ahadi zetu kwa mafanikio makubwa. Wameifanya kazi yangu ya kuwawakilisha kuwa nyepesi mno. Hali inayonishawishi zaidi kuwaendelea kuwatumikia wakinikubalia. Lakini pia wameniwezesha kuifanya kazi yangu ya uwaziri kwa wasaa zaidi. Sina cha kuwalipa isipokuwa kuzidi kuwatumikia. Lakini naomba waamini kwamba kokote nitakokuwepo vyovyote itavyokuwa nitaendelea kuwaenzi milele moyoni na akilini mwangu. Naamini sana na wao hawatanisahau.

Mhe. Spika, kumkumbu za wananchi kisiwani Unguja kukosa umeme kwa miezi takriban mitatu kuanzia tarehe 10/12/2009 bado hazijafutika akilini mwetu. Ni kipindi ambacho tuligubikwa na giza totoro lililotuduwaza na kutufadhahisha. Lakini halikutuduwaza wala kutudumaza dhamira yetu ya kufanya kazi pamoja katika kukabiliana na hali hiyo. Kwa uvumilivu na ushirikiano mkubwa tukafanikiwa kuondokana na janga hili.

Nawashukuru sana wananchi kwa uvumilivu na ustahamilivu wao huo kwa kipindi chote kile kigumu mno kwetu. Juhudi zilizochukuliwa na serikali katika kulifumbua tatizo hili hazitamalizika kwenye kurejesha umeme tu kisiwani Unguja. Wizara yangu inajitahidi na itaendelea kujitahidi kuchukua hatua zote za tahadhari kuhakikisha tokeo kama hili halitarejea tena Inshallah kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu. Tumejidhatiti vya kutosha kuhakikisha ufumbuzi ndani ya muda mfupi na mrefu ujao.

Nina furaha kuliarifu Baraza hili tukufu kwamba sasa majenereta ya akiba yaliyoagiziwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yamewasili nchini tangu tarehe 19/06/2010. Kazi ya kuyafunga inaendelea kwa kasi na inakabiribia kumalizika karibuni. Naamini pia kwamba Wajumbe wa Baraza hili na wananchi wote wanaelewa kwamba mkataba wa utengenezaji wa waya mpya wa umeme kupitia baharini kutoka Dar-es-Salaam hadi Funga umetiwa sahihi Ikulu ya Zanzibar mbele ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dokta Amani Abeid Karume tarehe 30/4/2010.

Matarajia kuwa ifikapo mwaka 2012 umeme wa hakika kupitia waya huo utakuwa umepatikana kwa maelezo zaidi Waheshimiwa Wajumbe nawaomba muangalie vifungu 75 na 76 ukurasa wa 41-42 kwenye kitabu cha hotuba hii.

Mhe. Spika, kama sio tatizo hilo utekelezaji wa malengo ya Wizara yangu kwa mwaka unaomalizika umekuwa wa kuridhisha mno, Pemba na Unguja, mijini na vijijini. Wizara yangu imekamilisha miradi mikubwa katika sekta mbali mbali

ambayo kwa kweli ni mama wa maendeleo ya kudumu nchini mwetu. Kisiwa cha Pemba kimepata umeme wa uhakika kutoka Tanga baada ya kuwashwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 3/06/2010. Pemba imetakata tangu asili lakini inang'ara zaidi hivi sasa kutokana na mradi huu wa karne.

Mhe. Spika, kisiwa cha Tumbatu nacho kinatazamiwa kupata umeme ufikapo mwezi wa Agosti mwaka 2010, ingekuwa kabla ya hapo kama si kuchelewa meli ya kuleta waya huo mahsusi wa kulazwa baharini uliotengenezwa nchini Norway. Fedha za kazi hii zimetokana na bakaa iliyotokana na mradi wa usambazaji umeme vijijini awamu ya nne ya nyongeza. Hii ishara bayana ya usimamizi makini ya wizara yangu kwa fedha tunazoingiziwa.

Kwa upande wa ardhini maandalizi karibu yote yamekamilika kisiwani Tumbatu na Mkokotoni. Tumbatu ni safi tayari na inshalla itakuwa safi zaidi ifikapo mwezi Agosti mwaka 2010.

Mhe. Spika, ujenzi wa nyumba za maendeleao Michenzani umekamilika rasmi tarehe 6/4/2010 baada ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dokta Amani Abeid Karume kukabidhi baadhi ya nyumba hizo kwa waliokuwa wakidai fidia zao. Ni ukamilishaji wa historia ndefu ya ukombozi wa nchi yetu iliyoanzishwa na muasisi wa mapinduzi yetu, baba wa Zanzibar huru Mzee Abeid Amani Karume Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amin. Kwa maelezo zaidi Waheshimiwa Wajumbe angalieni kifungu 42 na 43 ukurasa wa 25 na 26 wa kitabu cha hotuba hii.

Mhe. Spika, mzizi wa fitina kuhusiana na Wazanzibari kumiliki raslimali zao wenyewe umekatwa rasmi kupitia Baraza hili pale ilipoagiza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulitoa suala la mafuta na gesi asilia kutoka kwenye orodha ya mambo ya muungano. Tayari Mhe. Waziri Kiongozi ameshamuandikia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanza mchakato au utaratibu wa kulitoa suala hilo kwenye orodha hiyo.

Nalipongeza sana Baraza hili kwa konesha ujasiri na ukomavu uliojengea heshima kwa wananchi wetu waliokuwepo na wajao. Wizara yangu inaendelea na maandalizi ya kisheria na kitaasisi ya kulibeba jukumu hili au hilo zito.

Sera ya nishati imeshapitishwa na Baraza hili na inaingia katika hatua ya utekelezaji. Viongozi wa ngazi za juu wamepatiwa mafunzo ya msingi juu ya jinsi sekta ya mafuta inavyofanya kazi. Waheshimiwa Wawakilishi wamepata fursa hiyo kwenye semina iliyodhaminiwa na ubalozi wa Norway na watendaji wakuu wa serikali na asasi za kiraia wamepata fursa hiyo kwenye semina nyengine iliyofanyika kwenye ukumbi wa *Zanzibar Beach Resort* .

Serikali ya Norway kupitia ubalozi wake hapa nchini umekubali kuisaidia Zanzibar kuandaa tathmini mkakati ya mazingira, kwa maana S*trategic Environmental Impact Assessment* ambayo ndiyo itakuwa dira ya uchimbaji wa mafuta na gesi asilia hapa nchini.

Sambamba na hayo Kampuni ya Mafuta na Gesi Asilia imekubali kugharamia masomo ya muda mrefu ya vijana wetu katika fani mbali mbali ya taaluma ya uchimbaji na uendeshaji sekta ya petroli. Kundi la mwanzo lenye wanafunzi 10 wa shahada ya kwanza inatazamiwa kuanza masomo kuanzia mwezi Oktoba mwaka huu katika vyuo mbali mbali duniani.

Maelezo zaidi yanapatikana katika kifungu cha 61 na 63 ukurasa wa 33 hadi 35 kwenye kitabu cha hotuba hii.

Mhe. Spika, baada ya matengenezo bustani ya Forodhani ambayo ndio kiunganishi kikuu cha watalii na wenyeji hapa nchini ambayo ndio wajihi wa Mji Mkongwe na ndio kioo kimoja wapo cha utamaduni wetu. Imefunguliwa rasmi wa Rais wa Zanzabar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dokta Amani Abeid Karume pamoja na Mstahiki Agakhan tarehe 30/7/2009.

Matengenezo hayo yameirejeshea bustani hiyo sifa yake ya kuwa ndiyo maarufu zaidi katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, hivyo kuongeza thamani kwenye hadhi ya Mji Mkongwe ya urithi wa kimataifa. Kwa maelezo zaidi nawaomba muangalie kifungu 50 ukurasa wa 29 kwenye kitabu cha hotuba hii.

Matengenezo hayo yamefuatiliwa na kurejesha kwa eneo jengine la wazi pembeni mwa hoteli ya Tembo kwa matumizi ya jamii. Weledi wa masuala ya urithi wa ulimwengu kwa heshima ya Mji Mkongwe walifanya kikao chao hapa Zanzibar. Kikao kilihusu dhana mpya ya mandhari ya kihistoria *(History land escape)*, kama aina moja wapo ya maeneo stahiki kwa urithi wa ulimwengu. Wameisifia sana Zanzibar hadi kwenye maazimio yao kwa jinsi mambo haya mawili yanavyoendana moja kwa moja na dhana yenye mandhari za kihistoria. Ni tanbihi nzito kwamba tusijidharau. Ulimwengu unatuheshimu hivyo ndio faida moja wapo ya kuwa na urithi wa kimataifa katika ardhi yetu.

Sambamba na hayo Baraza hili likapitisha sheria mpya ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe kwa nia ya kuimarisha nafasi ya mji wenyewe kama urithi wa kimataifa lakini pia kukabiliana na changamoto nyingi mpya ambazo zisingekubalika kwa sheria ya awali. Hii sio silaha pekee ya usimamizi wa sekta ya wizara yangu iliyopitishwa na Baraza hili kwa mwaka uliomalizika.

Mbali na sera ya nishati iliyotajwa awali. Baraza hili pia ilipitisha sheria ya Bodi ya Kudhibiti wakandarasi na kudhibiti wataalamu wa ujenzi ambazo tayari zinafanya kazi, kanuni kadhaa za sheria hizi na nyenginezo hasa kwenye nyanja za ardhi na utawala wake nazo zimetungwa au zinafanyiwa mapitio.

Mhe. Spika, mradi mwengine mama uliohusu wizara yangu ndani ya mwaka huu unaomalizika ni wa maji wa Mkoa wa Mjini/Magharibi unaofadhiliwa na Serikali ya Japani. Awamu ya pili iliyo mahsusi kwa Wilaya ya Magharibi imo katika hatua za mwisho za kukamilika. Utakapokabidhiwa rasmi mwezi Agosti mwaka 2010 hali ya upatikanaji maji ndani ya Mkoa huu na maeneo jirani itakuwa inategemewa kwa asilimia zaidi ya 90. Ikizingatiwa kwamba Mkoa wenyewe umebeba zaidi ya asilimia 40 ya Wazanzibari wote. Maana yake zaidi ya asilimia 40 yenye matatizo ya maji kwa Zanzibar itakuwa yametatuliwa na mradi huu pekee.

Maelezo zaidi yanapatikana kifungu cha 27 na 18 kwenye ukurasa wa 17 na 18 za kitabu cha hotuba hii.

Miradi mengine iliyokamilika mijini na vijijini inafaa kuwa zaidi ya nusu ya asilimia kasoro ya 60 iliyosalia miji ya Wete, Chake-Chake na Mkoani tayari imo katika mradi unaoendelea wa maji mijini.

Sambamba na miji hiyo Benki hiyo inagharimia pia mradi wa maji vijiji kadhaa vya Unguja na Pemba hasa vinavyokaliwa na wakaazi wengi. Hivi ni vile ambavyo upatikanaji wake wa maji umezidiwa sana kutokana na wingi wa wakaazi na uchakavu wa mifumo ya maji iliyopo. Vijiji vya Matemwe, Machui hadi Dunga hadi Tunguu kwa Unguja na Wambaa, Mizingani, Ndagoni, Vitongoji na Kambini hadi Mchangamdogo kwa Pemba vitanufaika na mradi huu.

Maelezo zaidi kuhusu mradi wa maji mijini na mazingira yapo kwenye vifungu 29 na 30 kwenye ukurasa wa 19 na 20 za kitabu cha hotuba hii.

Mhe. Spika, miradi hii inachanganywa na ile ya Tumbatu, Miwani, Kangagani, Junguni, Gando, Kigongoni, Kizimkazi, Shumbaviamboni, Micheweni na Mkwajuni, ambayo baadhi imekamilika na mengine ipo katika hatua mbali mbali ya utekelezaji inapatikana taswira nzuri zaidi ya mafanikio ya utekelezaji wa malengo ya Wizara hii kwa sekta ya maji ndani ya mwaka unaomalizika.

Maelezo zaidi Waheshimiwa Wajumbe yanapatikana kwenye jadweli Nam. 1 iliyopo ukusara 13 kwenye kitabu cha hotuba hii.

Wananchi nao kupitia miradi ya TASAF au inayofadhiliwa moja kwa moja na wahisani kama Serikali ya Japan au Umoja wa Ulaya, wamekuwa wakiibua na utekelezaji wa miradi kadhaa ya maji ambayo wizara wizara yangu ilishiriki kama washauri na wataalamu. Mingi yao imeshakamilika na baadhi ipo katika hatua nzuri. Hiyo ni pamoja ya Ubago, Kidimni, Chaani kubwa, Michungwani, Koani, Fumba, Mtambwe, Mpakanjia hadi Nyali na Mfenesini, Bumbwini.

Maelezo zaidi yapo katika jadweli Nam. 2 na kifungu 25 hadi 26 ukurasa wa 16 na 17 wa kitabu cha hotuba hii.

Mhe. Spika, picha hii njema ya hali ya maji safi na salama imekuwa ikitibuliwa mara kwa mara na uharibifu wa pampu unaotokana na kukatika kwa umeme. Kadhalika uchakavu wa mabomba. Katika kukabiliana na hali hii wizara imesimamia uagiziaji wa mabomba mengi sana ya saizi tofauti hadi *nchi 13* ambayo tayari yameshawasili nchini, pamoja na pampu zinafungwa vifaa vyote vya kuzikinga na athari za umeme na radi. Hizi zinategemea kuwasili muda wowote kuanzia sasa. Fedha za ununuzi na shilingi bilioni moja zinazotokana na msaada wa misamaha ya madini *(Multilateral Debt Relief Initiatives – MDRI).*

Kwa maelezo zaidi Waheshimiwa Wajumbe ninawaomba muangalie kifungu cha 21 hadi 23 kwenye ukurasa wa 15 cha kitabu cha hotuba hii.

Mhe. Spika, sekta ambayo imekuwa ikilalamikiwa sana na wizara yangu ni ya ardhi kutokana na kugusa maslahi ya moja kwa moja ya kila mwananchi. Nakubaliana na lawama hizo na ndio maana wizara yangu imekuwa ikichukua hatua madhubuti na endelevu ya kuondoa kasoro za kweli ziliopo ndani ya mwaka uliopita wa fedha. Tumerekebisha sheria ya Mahakama ya Ardhi ili kuchapuza usikilizaji wa kesi zinazohusu ardhi. Makamo Wenyeviti wa Mahakama hiyo kwa Unguja na Pemba wamechaguliwa na wote wanashiriki katika kusikiliza kesi na kuzitolewa hukumu. Tumetafuta majengo ambayo yanatengenezwa ili kuongeza idadi ya sehemu ya kusikiliza kesi. Tumeanza na Mkoa wa Kaskazini Unguja na Pemba ambapo majengo yaliyokuwepo Gamba na Wete yanahusika.

Hivi sasa kumebaki kesi 152 zinazosubiri kutolewa hukumu, tayari kesi 19 zimeshahukumiwa au kuamuliwa nje ya Mahakama. Nakiri kasi bado ni ndogo lakini naamini ni hatua kubwa zaidi kuliko iliyokuwa awali. Imani na mikakati yetu ni kwamba baada ya kukamilika matengenezo ya majengo haya ya Mahakama, kasi ya usikilizaji kesi itakuwa kubwa zaidi.

Maelezo zaidi yanapatikana kwenye jadweli Nam. 5 ukurasa wa 54 wa kitabu cha hotuba hii. Lakini kuna haja ya mikakati zaidi itakayofafanua baadaye.

Mhe. Spika, chango kimoja wapo cha migogoro inayolalamikiwa ni ukosefu wa kumbukumbu za umiliki wa matumizi ya ardhi. Tumeanzisha Afisi ya Msajili wa Ardhi kwa nia ya kuondokana na kasoro hii. Tumeanza na usajili wa ardhi Wilaya ya Mjini. Mji Mkongwe tayari utambuzi wa wenye haki ya matumizi ya ardhi umekamilika. Hatua inayofuata ni uhakiki na hatimaye utoaji wa hati zenyewe za usajili.

Hivi sasa utambuzi unaendelea mitaa ya ng'ambu kati ya fomu 4688 za maombi ya usajili zilizotolewa 2510 ndizo zilizorejeshwa hadi mwezi wa Marchi 2010.

Jadweli Nam. 4 liliopo ukurasa wa 53 wa kitabu cha hotuba kinaainisha zaidi.

Kasi hii ndogo ya urejeshaji fomu hizo ni kiashirio cha uelewa mdogo. Tatizo moja wapo kuu na migogoro ya ardhi ambayo nitaifafanua baadaye. Tumeanzisha pia bodi ya uhaulishaji ardhi ambayo inaendelea vyema na kazi yake zinazoishia kwenye ardhi hizo kusajiliwa moja kwa moja. Hadi Machi 2010 maombi 843 ya uhaulishaji yalikwisha kushughulikiwa kati yao 161 yamekubaliwa na 11 kukataliwa.

Angalieni jadweli Nam. 6 iliyokuwepo ukurasa wa 55.

Mhe. Spika, bila mipango madhubuti ya utawala sahihi wa ardhi iliyopo inakuwa ni vigumu kuitumia ardhi chache iliyopo kwa ufanisi. Mradi wa matumizi endelevu wa ardhi na mazingira unaofadhiliwa na Serikali ya Finland umeingia katika awamu yake ya pili ndani ya mwaka unaomalizika. Wahisani wameridhia awamu hiyo baada ya kuridhishwa na mafanikio ya awamu ya kwanza.

Hadi sasa ramani ya anga yote imeshakamilika. Hali hii itawezesha upangaji na ufuatiliaji wa matumizi ya ardhi kuwa rahisi na sahihi kuliko awali. Kwa ufanisi zaidi hatua inayofuata ni ya picha halisi ya anga. Tayari miji ya mjini Unguja, Wete na Mkoani imekamilisha uchukuaji wa picha hizo ambazo ni sahihi, madhubuti sana katika usimamizi wa matumizi ya ardhi na ufuatiliaji wake.

Kifungu 106 ukurasa wa 56 na kifungu 112 ukurasa wa 60 vinafafanua zaidi.

Miradi mengine ya matumizi na usimamizi wa ardhi inayoondelezwa moja kwa moja na wizara yangu au kushirikiana na taasisi nyengine ni pamoja na mradi wa Huduma Mijini. Huu unahusisha upangaji wa matumizi ya ardhi kwa Mji wa Zanzibar na vitongoji vyake. Mradi unaratibiwa na Wizara ya Fedha na unagharamiwa na Benki ya Dunia. Unakusudia kushughulikia matatizo na kuukabili mji huu, kwa sasa ukizingatia kwamba mara ya mwisho matumizi ya ardhi kwa mji huu yalipitishwa mwaka 1982, bila shaka yamepitwa mno na wakati.

Mradi mwengine wa aina hiyo ni wa urasimishaji wa rasilimali za biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA) unasaidiwa kwenye mapitio ya sera ya ardhi, sambamba na shughuli za usajili wa ardhi hususan kisiwani Pemba ikiwa ni majaribio urasimishaji huo. Kuna pia mradi wa kuimarisha mazingira ya biashara Tanzania (MKUMBITA) ambao pia unaratibiwa na Wizara ya Fedha, unasaidiana na wizara yangu katika kusimamia utawala wa ardhi ikiwa ni namna moja wapo ya kuimarisha mazingira ya biashara kwa kutumia ardhi yetu na kujenga usalama zaidi kwa watumiaji wa ardhi.

Kadhalika mradi wa kuimarisha mazingira mwambao (*MACEMP*) ambao kwa upande wa wizara yangu unasaidia pia katika utayarishaji wa ramani za ardhi za Wilaya. Ripoti za Wilaya nne tayari zimekamilika, vifungu 113 hadi 115 ukurasa wa 61 hadi 63 za kitabu cha hotuba hii waheshimiwa wajumbe kwa heshima na taadhima vinafafanua zaidi.

Mhe. Spika, baada ya hatua zote hizi sambamba na upimaji viwanja 400 unaoendelea hivi sasa upo Tunguu na vyengine 490 vilivyopimwa kwenye maeneo mbali mbali visiwani humu kwa shughuli tofauti, watu wangejiuliza kwa nini migogoro ya ardhi haipungui. Ukweli ni kwamba imepungua kama takwimu za kesi za ardhi na malalamiko yanayofikia wizara yangu zinavyoainisha. Migogoro imepungua lakini haionekani kupungua sababu ni nyingi.

Kwanza ni uelewa wa watu juu ya haki yao unaowafanya wasikae kimya kila wanapohisi haki yao ya matumizi ya ardhi zimepokwa. Hali hii inazidishwa na matumizi ya ardhi kwa uwekezaji unaosababisha kuibuka kwa wajanja wengi, kujifanya wamiliki au mawakala wa wamiliki kwa wawekezaji wengi wa wakala hao wanaongezeka kila kukicha, lengo lao ni kujinufaisha binafsi kuliko maslahi ya muwekezaji wala mwananchi mwenye haki ya matumizi ya ardhi zao. Mwisho wake ni kudhulumiana na hatimae lawama kwa wizara na serikali.

Mara nyingi walalamikaji hudhani kwamba uwakala huo ni rasmi na una baraka za wizara yangu. Lakini pia kuna tatizo la kuzielewa hizo haki za msingi. Kesi na malalamiko mengi zinazokwenda Mahakama ya Ardhi au kufikishwa wizarani kwangu ingawa zinahusiana na ardhi. Kwa kweli huwa zinatokana zaidi na mmong'onyoko huo wa uaminifu miongoni mwa wanajamii kuliko udhaifu wa utendaji wa serikali kupitia wizara yangu. Nyingi zao zina muelekeo wa jinai, zinatokana na dhuluma nilizozitaja za watu kwa watu. Mfano ni watu hata taasisi za umma wenye hati halali za kumiliki ardhi wanapolalamika ardhi hizo kuvamiwa na watu wengine.

Wizara yangu ikishakutoa hati na ikiwa haijafuta hati hiyo wala haijafanya kosa ya kutoa hati nyengine juu hati hiyo huwa imemaliza kazi yake. Ni juu ya

mwenye hati hiyo sasa kutetea maslahi yake ya ardhi hiyo inapovamiwa au kuona tatizo jengine, kwa sababu uvamizi huo unakuwa ni kosa la jinai sio la madai tena kuilalamikia wizara yangu kwa uvamizi wa aina hiyo ilhali yenyewe haihusiki kwa vyovyote na uvamizi huo, ni kuliibua tatizo ambalo la kimsingi halilihusu tena. Tatizo kama hilo halipasi kuhesabika kuwa ni migogoro ya ardhi inayohusu wizara yangu.

Mhe. Spika, inasemekana kwenye baadhi ya kesi kama hizo, wafanyajikazi wa wizara yangu wanashiriki. Lakini walalamikaji daima hushindwa kuwabainisha wafanyajikazi wanatuhumiwa. Labda zana za vitendea kazi vilivyotumika ndio hutajwa kama ni vya wizara. Lakini tusisahau tumepitisha katika sheria zetu na Kanuni fursa, sasa ya kuwa na wapimaji binafsi. Hali hii inaipa uzito wizara yangu kuchukua hatua bila ya kuwabainisha wahusika. Jambo hilo linabaki kuwa ni dhana. Kwa misingi ya utawala bora wananchi wanayohaki ya kuwahoji bila ya kuwabugudhi watu wowote wanaowaona kufanya kazi za aina hiyo kwenye maeneo yao.

Mhe. Spika, wanayo haki ya kudai kuoneshwa vitambulisho na kama bado watakuwa na shaka wawasiliane na vyombo husika ikiwamo wizara yangu. Atakayekataa kujitambulisha maana yake ni kwamba hayupo hapo kwa niaba ya wizara. Kwa hivyo mwananchi au wananchi wanayo haki ya kumchukulia hatua zaidi ya kiutawala na ikibidi hata za kisheria.

Mfano mwengine wa kesi za watu wawili zaidi kuuziwa kienyeji eneo moja. Huu ni wizi wa kuaminiana ambao ungeshughulikiwa zaidi na vyombo vya dola kuliko taasisi za ardhi. Au wenye haki za matumizi ardhi kama vile eka ama mashamba wanaposhtukia maeneo yao yanatwaliwa na nguvu au ujanja. Au wananchi wanapodhulumiana ardhi kama ni sehemu ya mirathi au wawekezaji wanapowadhulumu wenye haki za matumizi ya ardhi iliyowekezwa.

Kiutaratibu fidia inapaswa kumalizwa kwanza kabla ya muekezaji hajapata vibali vya kuekeza, isipokuwa hivyo mgogoro huo ingawa chanzo chake ni ardhi lakini wa kuhojiwa si wizara yangu wala Mahakama ni utaratibu wa kisheria unaofuatwa. Kwa ufupi migogoro ya aina hii ingawa inahusiana na ardhi, lakini chanzo chake ni ukosefu wa uaminifu miongoni mwa wana jamii kuliko udhaifu wa utekelezaji wa wizara yangu au Mahakama ya Ardhi ni migogoro sawa na mengine ndani ya jamii inayohusu kudhulumiana mali, kupoka, kughushi hati ili kujihalalishia umiliki wa mali. Wizi wa kuaminiana na kadhalika ambayo yanapatikana katika kila nyanja na sekta zote za maisha yetu, sio ardhi peke yake.

Ndio maana nyingi ya kesi ziliopo baina ya wananchi wenyewe kwa wenyewe ambazo zinaihusu wizara yangu ni chache mno nyingi zao zikihoji haki ya serikali kwa matumizi ya ardhi husika au uwekezaji kufutiwa hati za kodi za

ardhi. Sipaswi kusemea hizi kwa kuwa zipo Mahakamani. Lakini tukifuatilia hoja zilizopata kuwasilishwa Barazani hapa na kujibiwa na wizara yangu tutabaini msingi wa hatua ya wizara yangu inayolalamikiwa.

Mhe. Spika, kuna tatizo pia la wahusika wa udhibiti ujenzi mijini na kwenye Halmashauri kuwa wasiri kwa ujenzi wanaoidhinisha. Taratibu za kiistaarabu katika kudhibiti ujenzi wowote ulimwenguni ni ujenzi huo huwekewa matangazo ya wazi kabla haujaanza, yanayoanisha aina ya ujezi wenyewe na kibali kinachohusika.

Wananchi wataelewa kwamba ujenzi huo ni halali na kama wana hoja za msingi dhidi yake, hiyo ndio fursa ya kuziwasilisha kwenye mamlaka zinazohusika. Utaratibu huu huepusha malalamiko na hatimaye migogoro mingi halisi, kama sio yote ya ardhi kwa kuwa hili halitendeki ni tabu jamii kuelewa iwapo ujenzi husika ni halali ama la.

Kasoro yoyote inayotokana na usiri huu hasa inayohusu upatikanaji wa ardhi wenyewe huonekana kuwa ni tatizo linalotokana na wizara yangu. Hali hii inahusu pia miradi ya uwekezaji, angalau basi masuala kama hayo yangewasilishwa wizarani kwangu au Mahakama ya Ardhi mapema.

Lakini mara nyingi huripotiwa muda mrefu baada ya kutokea hali inayofanya ufumbuzi wake kuwa mgumu kwa kuwa mathalan mlalamikaji ameshakwisha hata kujenga nyumba kwenye eneo linalolalamikiwa.

Mhe. Spika, kasoro kama hizi ambazo ni ndogo lakini nyingi zikishughulikiwa ipasavyo kinachoonekana kuwa ni migogoro ya ardhi zitapungua kwa asilimia kubwa mno. Mhe. Spika, kupitia Baraza hili ninawaomba wananchi wote kufuata miongozo na maelekezo haya na zisisitiza Halmashauri za Miji na Wilaya nazo kuchukua hatua hizo mwafaka, miji na mitaa si ya mtu wala taasisi yoyote ni yetu sote.

Kwa hivyo, tunapaswa kujua na kushiriki katika maamuzi ya kile tunachoendelezwa ndani yake isibaki kuwa ni siri ya mamlaka husika kuamua zitakaa vipi. Uwazi na ukweli ndio silaha pekee yakinifu katika udhibiti wa ujenzi na utawala wa ardhi zetu, bila ya hivyo migogoro hii isiyo ya lazima haitamalizika wala kupungua hata wizara yangu ikiwa makini kiasi gani.

Navisihi pia vyombo vya sheria na vya dola visipuuze malalamiko ya wananchi wanaokumbwa na maswahiba kama haya. Asilimia kubwa sana ya matatizo haya itapungua iwapo masheha, madiwani, vituo vya polisi sisi wawakilishi na wote wenye jukumu la kusimamia haki za wananchi. Tutajilazimisha kuchukua hatua mara moja malalamiko hayo yanapotufikia kadri tunavyochelewa kuchukua

hatua ndivyo mambo haya mepesi yanapokomaa hadi kuwa migogoro iliyoshupaa.

Mhe. Spika, ukusanyaji wa mapato kwa wizara yangu umekuwa ni wa kuridhisha pia, kufikia Machi, 2010 tulikwishakusanya asilimia 55.65 ya kima kinacholengwa cha shilingi bilioni mbili, milioni mia sita na kumi laki moja. Uzoefu unaonesha kwamba lengo hili linaweza kufikiwa au hata kuvukwa kwa sababu msimu hasa wa makusanyo kwa vyanzo vikuu vya mapato ya wizara yangu ni Machi hadi Juni. Maelezo kamili yako kifungu cha 6 ukurasa wa 3 kwenye kitabu cha hotuba ya bajeti hii. Bajeti ya wizara yangu kwa mwaka uliomalizika ilikuwa ni shilingi milioni mia tisa sitini na saba ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2010 asilimia 68.93 zilikwishaingizwa angalieni ukurasa wa 4 kifungu cha 7 kwenye kitabu cha hotuba hii kwa maelezo zaidi.

Picha hii inaanisha uwiano mzuri wa mapato na matumizi kwa wizara yangu ambao umefikiwa kwa mashirikiano makubwa miongoni mwa watendaji wa wizara yangu wenyewe na pia baina yao na Wizara ya Fedha na Uchumi. Nawapongeza sana watendaji wa wizara yangu kwa utekelezaji wao mzuri na watendaji wote wa serikali kwa jumla kwa kufanya kazi pamoja kama timu moja.

Mhe. Spika, kwa mwaka ujao wa fedha wizara yangu itajihusisha zaidi na uendelezaji wa miradi na programu zilizopo. Kama nilivyokwishaanisha hatua muhimu na za misingi tayari imeshafikiwa kwa miradi na programu hizo zote. Programu na miradi hiyo ni ya usambazaji maji vijijini na mijini, kuijengea uwezo ZAWA unaofadhiliwa na *African Development Bank.*

Ujenzi wa nyumba za maendeleo Mpapa, usambazaji umeme vijijini, kuweka laini ya pili umeme Ubungo hadi Mtoni unaofadhiliwa na MCC, ufungaji mita 1000 za TUKUZA, kuimarisha Shirika la Umeme, utekelezaji wa Sera ya Nishati, Usimamizi Endelevu Ardhi na Mazingira, Kuijengea uwezo Idara ya Mipango na Sera, Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Pwani Mji Mkongwe na Mradi wa Kuimarisha Biashara Kupitia Sekta ya Ardhi MKUMBITA. Maelezo kamili yanapatikana kuanzia kifungu 117 hadi 150 ukurasa wa 64 hadi 83 kwenye kitabu cha hotuba hii.

Mhe. Spika, naomba niwashukuru Washiriki wetu wa Maendeleo kwa misaada yao iliyosukuma sana gurudumu la maendeleo yetu. Tumefarajika sana kwa imani yao kwetu na tunawaahidi tutaendelea na juhudi ili kuhakikisha miradi na programu wanazotusaidia zinakuwa endelevu. Pia tunaahidi kuendelea kuitumia misaada hiyo kwa uadilifu wa hali ya juu na kwa malengo yaliyokusudiwa. Ni imani yetu kwamba wataendelea kushirikiana na sisi zaidi ili kuimarisha uhusiano mwema ulioko baina yetu. Lakini pia kupunguza pengo la kipato baina ya wananchi wetu na baina ya nchi zetu na za kwao, tunawashukuru sana.

Mhe. Spika, niruhusu pia kukushukuru tena wewe binafsi na Waheshimiwa Wajumbe wote Baraza lako hili tukufu kwa usikivu na umakini wao wakati wote wa uwasilishaji wangu. Nawaomba wajumbe wote wa Baraza lako wapokee shukurani zangu kwa kazi yao kubwa iliyowawezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa kiasi hiki katika kipindi chetu cha kuwemo Barazani.

Shukurani mahsusi ziende kwa Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu Mwenyekiti, wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa ukaribu wake na wizara yangu, na mchango wake mkubwa katika kufanikisha malengo ya wizara yangu. Pia shukurani mahsusi zimuendee Mhe. Hamad Masoud akiwa Waziri Kivuli wa Wizara hii, alitoa mchango mkubwa kwangu na ametusaidia sana, tumuombe Mwenyezi Mungu amjaalie kila mmoja wetu anayewania kurejea tena hapa Barazani kwa muhula ujao apate matokeo yaliyo na manufaa kwake binafsi na kwetu sote kama Wazanzibari.

Mhe. Spika, kwa waliotangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awajaalie malazi mema. Tutaendelea kuwakumbuka na kuwaombea, inshaallah kazi walioifanya pamoja na sisi kwa maslahi ya wananchi wenzao itachanganyika na dua zetu kwao kuwa sadaka yao ya milele. Naomba kwa mara nyengine nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Amani Abeid Karume kwa kuifikisha nchi yetu katika upeo mkubwa wa maendeleo ndani ya mihula ya utawala wake. Anamaliza muda wake akiwa ameiweka nchi yetu katika njia sahihi ya umoja na maendeleo.

Maamuzi mengi ya kijasiri yaliyofikiwa katika wizara yangu kama vile mustakbal wa mafuta na gesi asilia Zanzibar, Sera ya Maji, Mabadiliko ya Sheria ya Shirika la Umeme, mchango wa SMZ kwa waya wa umeme wa Pemba – Tanga, mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye waya wa pili wa Unguja hadi ushughulikiaji wa tatizo la kuzimika kwa umeme kisiwani Unguja, kwa kweli yalikuwa mazito. Ni maamuzi ambayo yangetishia umaarufu kwa mwana siasa yoyote duniani hata nje ya wizara yangu hali ilikuwa ndio hiyo hiyo lakini hakuyumba wala hakutetereka.

Mhe. Spika, aliangalia zaidi mustakbal wa vizazi vijavyo kuliko hatma ya chaguzi zijazo. Tunamshukuru sana na tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu yeye na aila yake awajaalie kila la kheri katika maisha yao. Pia tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie uchaguzi wenye kheri, salama na mafanikio, utakaoimarisha mshikamano, uliopo na kuiondolea nchi yetu kila fitna na hasada na utakaotuletea nchi yetu mafanikio na maendeleo zaidi na zaidi.

Mhe. Spika, sasa kwa heshima na taadhima naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni nne, milioni mia nane na ishirini na moja kwa

kazi za kawaida, na shilingi bilioni tatu mia nane na thamanini milioni kwa kazi za maendeleo kwa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa mwaka wa 2010-2011.

Mhe. Spika, pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya shilingi bilioni mbili mia tatu sitini na moja mia sita na kumi na tisa elfu kwa mwaka huu wa fedha viambatanisho (f1) na (f2) kwenye kitabu cha hotuba hii vinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima kubwa sana naomba kutoa hoja.

HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI UJENZI NISHATI NA ARDHI MHESHIMIWA MANSOOR YUSSUF HIMID (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2010/2011 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

UTANGULIZI

Mhe. Spika**,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa liingie katika Kamati ya Matumizi ili niweze kutoa maelezo kuhusu shabaha na malengo yaliyomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji Ujenzi Nishati na Ardhi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika**,** napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kutujaalia afya njema na uzima na kwa kuniwezesha kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu kuwasilisha hotuba ya Wizara hii mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, vilevile naomba kuchukuwa fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Makamo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Dokta Amani Abeid Karume, na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Sharif Hamad kwa uamuzi wao wa busara wa kukutana na kukubaliana juu ya mambo ya msingi ya kuiweka nchi hii katika hali ya usalama na amani, hali ambayo matunda yake tumeanza kuyaona katika kipindi chote hichi baada ya kukutana kwao huko. Inshaallah hali hio itaendelea na kuzidi kuimarika kwa maslahi ya Wazanzibari na ninawasihi na kuwaomba Wazanzibari wenzangu kuitumia fursa hii aliyotujaalia Mwenyenzi Mungu vizuri na ifikapo tarehe 31 July maamuzi yetu Inshaalah yalenge katika kujenga upendo,heshima na mshikamano wa nchi yetu hii na watu wake.

Sote tunajua kuwa **Umoja** na **Mshikamano** ni **Sera ya Chama Cha Mapinduzi**,Chama ambacho kwa sera na busara zake kinaheshimiwa na Watanzania na jamii ya Kimataifa na ni msimamo wa Chama Cha Mapinduzi

kuwa Kura ya Maoni ya Tarehe 31 Julai 2010 ni kura ya "**NDIO".** Huu ni wakati kwa Wazanzibari wote kuwa na Umoja na kuwa Wastahamilivu hasa pale panapokuwa na tofauti ya fikra na maoni kati yao na hilo lisisababishe kuweko na mwanya kwa umoja wao kwa maslahi ya Zanzibar. Inshaalah Mwenyenzi Mungu kwa uwezo wake atatujaalia Wazanzibari wote kheri,salama na mafanikio katika dhamira yetu ya kuleta Umoja,Amani na Mshikamano ndani ya nchi yetu, Amin.

Mhe. Spika, naomba kuchukuwa nafasi hii kutowa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa Zanzibar hasa wale wanaoishi katika Kisiwa cha Unguja kwa ustahamilivu wao waliouonyesha katika kipindi chote ambacho huduma ya umeme ilikosekana kwa kipindi cha siku 87 kuanzia tarehe 10/12/2009 hadi tarehe 8/03/2010. Ni dhahiri kwamba uvumilivu wao huo umetokana na imani kubwa walionayo kwa Serikali yao hii pamoja na uongozi uliopo madarakani. Serikali ilichukua juhudi kubwa sana ya kuhakikisha kuwa huduma muhimu ya maji inapatikana kwa kipindi chote cha kukosekana kwa huduma ya umeme angalau kwa kima cha msingi (basic level of supply). Aidha huduma ya umeme wa dharura ilitolewa kwa sehemu nyeti za huduma muhimu kwa wananchi kama vile Hospitali kuu n.k. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kutupa nguvu za kuweza kuirudisha huduma hiyo ya umeme na tunawapongeza mafundi wote wa ndani na nje walioshirikiana pamoja katika kufanikisha kazi hiyo hadi kurejea kwa huduma.

Mhe. Spika, aidha nachukuwa nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wote ambao walistahili kupewa fidia baada ya nyumba zao za asili kuvunjwa kwa kutoa nafasi ya ujenzi wa nyumba mpya za maendeleo Michenzani kwa kukaa kipindi kirefu wakisubiri kumalizika kwa nyumba hizo ambazo hatimae zilimalizika na kutolewa kwa wananchi hao tarehe 6/04/2010. Katika tukio hilo, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikamilisha ahadi ya ASP na ya Rais wa Awamu ya Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Marehemu Abeid Amani Karume ya kuwajengea wananchi makaazi bora. Shukurani maalum ziende kwa Vikosi vyote vya Ulinzi, Mafundi wa Wizara hii na kwa kila aliyeshiriki kwa njia moja au nyengine katika kukamilisha ujenzi huo.

Matumizi na Mapato

Mhe. Spika**,** suala la ukusanyaji wa mapato ni kiashiria muhimu sana katika kupima mafanikio ya utekelezaji. Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2009/2010 ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 2,610,100,000 kutokana na vyanzo mbali mbali vya taasisi zake. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2010 jumla ya Tsh 1,452,586,242.96 tayari zilikwishakusanywa sawa na asilimia 55.65 ya makadirio. Matarajio ya Wizara yangu kuwa ifikapo Juni 2010 tutakuwa

tumefikia hatua nzuri ya malengo, hasa kwa kuzingatia uzoefu, inaonesha kwamba mapato mengi hukusanywa baada ya mwezi wa Machi kila mwaka.

Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho “A”

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2009/2010, Bajeti ya Wizara yangu ilikuwa ni Tsh. 11,967,000,000 Kazi za Maendeleo zilipangiwa Tsh 7,280,000,000 na kazi za kawaida zilipangiwa Tsh 4,687,000,000. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2010 Wizara yangu ilikwishapatiwa Tsh 5,258,144,623.62 kwa kazi za Maendeleo sawa na asilimia 72.23 na Tsh 2,991,043,711 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 63.82 ya makadirio, hivyo kufanya jumla ya fedha zote tulizozipata kuwa ni Tsh 8,249,188,334.62 sawa na asilimia 68.93 ya makisio yote.

Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho “B1 na B2”

Mhe. Spika, baada ya kukamilisha muhtasari huu wa Matumizi na Mapato ya Wizara yangu, sasa naomba uniruhusu kuelezea kwa kina utekelezaji wa kazi za Kawaida na za Maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 kupitia kila taasisi iliyomo ndani ya Wizara hii.

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2009/2010, Idara hii ilisimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ifuatayo:

1. Mradi wa Kuijengea Uwezo Idara ya Mipango na Sera
2. Usambazaji Maji Vijijini
3. Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini
4. Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji
5. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Michenzani na Mpapa
6. Mradi wa Kuukuza na Kuutambulisha Mji Mkongwe
7. Mradi wa kupeleka Umeme Pemba kutoka Tanga
8. Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Nne Nyongeza.
9. Mradi wa Kuweka Njia ya Pili ya Umeme Ubungo hadi Mtoni
10. Mradi wa Kufunga Mita 20,000 za TUKUZA Unguja na Pemba
11. Mradi wa Kuliimarisha Shirika la Umeme kifedha
12. Mradi wa Kupeleka Umeme Tumbatu
13. Mradi wa Kuandaa Sera ya Nishati Zanzibar
14. Mradi wa Kuhuisha Bustani ya Forodhani
15. Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira(SMOLE)

Mradi wa Kuijengea Uwezo Idara ya Mipango na Sera

Ujenzi wa Jengo Jipya la Makao Makuu ya Wizara
Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2009/2010, lengo kuu la Mradi huu ni kuanzisha hatua za awali za ujenzi wa jengo jipya la Wizara ambalo litakuwa la kisasa na kukidhi haja kwa mujibu wa mahitaji. Hatua iliofikia kwa sasa katika utekelezaji wa mradi huu ni kupatikana kwa eneo la Ujenzi, kukamilisha taratibu za umiliki, kujenga ukuta wa kuzunguka eneo la Kiwanja na kukamilisha taratibu za kupata ushauri wa kazi za usanifu wa kazi za awali *(Prelliminary design works)* ambazo zitajumuisha mahitaji halisi ya jengo lenyewe *(functional requirements)*, michoro, makisio ya gharama na nyaraka nyenginezo zitakazosaidia katika kutumiwa kwa kuwasilishwa kwa Washirika wa Maendeleo na Serikali kwa upande wake kuchangia kiasi fulani kulingana na makubaliano ya pamoja na wafadhili hao.

Kazi hiyo ya kupatiwa ushauri tayari imeelekezwa kwa taasisi zetu za ndani ambazo ni Idara ya Ujenzi, Idara ya Nyumba na Mamlaka ya Mji Mkongwe na tunasubiri miongozo yao kwa hatua za utekelezaji. Jengo hilo linatarajiwa kujengwa katika eneo la Kilimani. Taswira kamili ya jengo hilo itapatikana baada ya kazi ya Ushauri Uwelekezi wa ujenzi huo itakapokamilika.

Uendelezaji Rasilimaliwatu (Human Resource Development)
Mhe. Spika**,** Ili kuendeleza uwezo wa Wizara hii katika kukabiliana na majukumu yake kwa sasa, Idara imeweka mbele ujengaji uwezo wa wafanyakazi wake. Hii ni pamoja na ajira mpya kwa sehemu ya mipango na mafunzo ya nje na ndani ya nchi kwa kuwapeleka masomoni wafanyakazi wake wa divisheni zake kwa mujibu wa mpango wa mafunzo ikiwa ni pamoja na uwanja wa Mafuta na Gesi Asilia. Maelezo kamili yatatolewa katika kifungu kinachofuatia.

Uendeshaji wa kazi za Utumishi
Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara yangu kwa kushirikiana na wakuu wa Taasisi zake imeweza kusimamia vya kutosha suala zima linalohusiana na maslahi ya wafanyakazi hali ambayo inashajihisha utekelezaji wa majukumu ya kazi zetu za kila siku.

Mbali na hayo, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara imeweza kuajiri wafanyakazi 3, wafanyakazi 44 wamestaafu kazi baada ya kufikia umri wa lazima, wafanyakazi 5 wamestafu kazi kwa hiari baada yakufikia umri, wafanyakazi 2 kwa kumaliza muda wa mikataba yao, mfanyakazi 1 amefukuzwa kazi kwa ukosefu wa nidhamu. Aidha wafanyakazi 4 wamefariki dunia. Mungu aziweke roho za marehemu peponi **Amin**.

Usimamiaji na Uimarishaji wa Sera na Sheria za Wizara

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kwamba kuwepo kwa sera ndio chanzo cha kuwa na muelekeo ulio sahihi wa utowaji wa huduma mbalimbali za kijamii na kimaendeleo. Kwa kufanya hivyo Idara ya Mipango na Sera imeendelea na jukumu la kusimamia uimarishaji wa Sera na Sheria mbali mbali zinazohusiana na Wizara yetu ikiwa na lengo la kuimarisha utowaji wa huduma kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu na wananchi wake. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara yangu imefanikiwa kusimamia matayarisho ya Sera ya nishati na marekebisho ya Sera ya ardhi pamoja na Sheria za sekta zilizo chini ya Wizara hii. Shughuli hizo zimetekelezwa kwa hatua tofauti kama zifuatavyo:

1. Sera ya Nishati tayari imekamilika na kuwasilishwa na kuridhiwa rasmi na Baraza la Wawakilishi na kinachosubiriwa hivi sasa ni kukamilisha taratibu kwa hatua za utekelezaji.

2. Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe na mambo mengine yanayohusiana na hayo imesharekebishwa na kupitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi.

3. Sheria ya "*Condomonium*", sheria hii imeshamalizika kutungwa na kamati ya Wanasheria wa Wizara, na vikao vya washirika tayari vimefanyika kwa kuijadili sheria hiyo na hivi sasa kinachoendelea ni kuingizwa kwa baadhi ya marekebisho na maoni kama ilivyoshauriwa katika kikao cha Makatibu Wakuu.

4. Marekebisho ya Sheria ya kudhibiti kodi za nyumba yameshafanywa na kamati ya Wanasheria wa Wizara na kwa wakati huu inasubiri maoni ya Taasisi husika ili kamati hiyo iendelee na hatua nyengine
5. Sera ya ardhi imeendelea kufanyiwa mapitio kwa kutumia wataalamu wa ndani ambapo vikao mbali mbali viliandaliwa kwa ajili ya kufanikisha kazi hiyo.

6. Mapitio ya sheria ya Uhaulishaji wa Ardhi na Sheria ya Umilikaji ardhi yanaendelea kufanyiwa kazi na wataalamu wa Wizara, hata hivyo kanuni za sheria ya uhaulishalishaji iliyopo tayari imeshapitishwa na karibu zitaanza kazi.

7. Sheria ya Usambazaji Mafuta *(Petroleum Supply Act)* imeshatungwa na inasubiri maoni ya Kamati Tendaji ya Wizara.

8. Rasimu ya Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia imeshafanywa. Hatua za kuipitisha katika mchakato wa kawaida ili kuiwasilisha Serikalini

unasubiri kukamilishwa kwa baadhi ya taratibu kama vile kumalizika kwa Mpango Utekelezaji *(Work plan)* ya Sera ya Nishati ikiwa ni pamoja na Kuundwa kwa Taasisi husika za Mafuta na Gesi Asilia kama Baraza hili Tukufu lilivyoagiza.

Mafunzo kwa wafanyakazi

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara imeendeleza jitihada zake katika kuwapatia nafasi za masomo wafanyakazi wake kwa mujibu wa mahitaji ya Wizara na Taasisi zake, ili tuende sambamba na mabadiliko ya dunia na teknolojia inayoendelea kubadilika siku hadi siku duniani. Jumla ya wafanyakazi 57 wanaendelea na masomo yao ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi kwa viwango tofauti vya elimu.

Aidha kuhusu mafunzo ya muda mfupi, Wizara imefanikiwa kuwapeleka masomoni wafanyakazi wake 18 ambao wengi kati yao wamebahatika kupatiwa nafasi hizo kwa ufadhili wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Taasisi zao kwa kuwa ni sehemu ya malengo ya miradi hiyo na kuzijengea uwezo Taasisi hizo kwa njia ya mafunzo kwa wafanyakazi wake. Kwa ufafanuzi zaidi nakuombeni muangalie kiambatanisho C1 na C2.

Masuala ya Jinsia na Ukimwi

Mhe. Spika**,** kwa mwaka 2009/2010 Wizara yangu imeyapa kipaumbele masuala ya jinsia na Ukimwi kwa kufanya mambo yafuatayo:-

1. Kutoa mafunzo ya Ukimwi kwa wafanyakazi na familia zao, yanayokumbusha umuhimu wa kuondosha Ubaguzi na Unyanyapaa kwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi .

2. Kufanya mafunzo ya Utawala kwa kamati ya Jenda/Ukimwi, kwa washirika wa Wizara (kampuni za petrol, Watengenezaji wa maji safi ya chupa, watengezaji wa Ankara za malipo katika Afisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Maji Ujenzi Nishati na Ardhi), ili kusaidia Wizara kutoa matangazo ya kujilinda na Virusi vya Ukimwi/Ukimwi.

3. Kuanzishwa kwa mfuko wa hiari wa afya ya dharura kwa wafanyakazi wa Wizara (MADWA) ili kuweza kusaidia kujali na kuondosha Unyanyapaa kwa mfanya kazi aliepata maradhi. Matumizi ya mfuko huo yatafuata muongozo na taratibu zilizo tayarishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mfuko huo ambao utamsaidia mfanyakazi atakaepata maradhi mazito ya ghafla, atakaepata maambukizi ya virusi vya Ukimwi, na matatizo mazito ya mfanyakazi anaeishi na ulemavu.

Mashirikiano na Nchi/Taasisi za nje

Mhe. Spika, katika kuongeza ufanisi wa majukumu yake, Wizara hii kupitia Idara ya Mipango na Sera, imeweza kufanya mawasiliano na Washirika wa Maendeleo kadhaa kwa nia ya kujieleza na kutoa changamoto zinazoikabili Wizara hii kwa washirika hao. Washirika hao ni pamoja na Norway, Japan, Egypt, Sweden na Taasisi za Umoja wa Mataifa.

Mbali ya kupata msaaada wa kiufundi na vifaa, Wizara hii kwa mara ya mwanzo imepata nafasi ya kuhakikishiwa Zanzibar kupata ushiriki katika majukwaa ya mikutano inayoandaliwa na Jumuia za Kimataifa kwa kuanzia na *UN HABITAT* na kwa mara ya kwanza Viongozi wa Zanzibar walipata nafasi katika Mkutano wa Rio De Janeiro mwezi wa Machi 2010 ambao ulihudhuriwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii katika kuelezea matatizo ya Zanzibar katika sekta zake husika.

Kupitia mazungumzo na *UN HABITAT*, Taasisi za Nyumba na Makaazi, Mji Mkongwe, Ujenzi, Maji,Mipango na Sera, tayari zimewasilisha mahitaji yake muhimu kwa Mkurugenzi wa Shirika hilo kwa hatua muafaka ambae alifika nchini tarehe 7/01/2010. Vilevile, Mashirika hayo yamejiandaa kuendelea na kufungua Ofisi zake Zanzibar ili nchi hii iweze kufaidika moja kwa moja na huduma za Mashirika hayo.

MAMLAKA YA MAJI

Mhe. Spika, moja kati ya majukumu ya Wizara yangu ni kuwapatia wananchi maji safi na salama katika maeneo wanayoishi. Kazi hii hufanyika kwa kutumia uwezo wa Serikali na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na nguvu za wananchi. Ni katika juhudi za Wizara yangu katika kufanikisha kazi za upatikanaji wa maji mijini na vijijini kwa utekelezaji wa malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA), Ilani ya Uchaguzi ya CCM pamoja na kufanikisha malengo ya Milenia ambayo yanayoelekeza kuwa nusu ya idadi ya watu waliokuwa hawana huduma ya maji na usafi wa mazingira *(water and sanitation)* iwe imepunguzwa ifikapo mwaka 2015.

Mhe. Spika, mahitaji ya maji yanazidi kukuwa kutokana na kutanuka kwa maeneo ya miji na hata kuimarika kwa maeneo ya vijijini kwa kuwepo na harakati zinazohitajia maji mengi. Ongezeko hilo linapelekea kuzidiwa kwa baadhi ya miundombinu iliyopo ikiwemo mabomba na visima ambapo matokeo yake ni kujichomoza kwa tatizo la upungufu wa maji.

Kufuatia hali hiyo, Wizara yangu ilijitahidi kuendeleza kazi za uhuishaji wa miradi ya maji kwa kurekebisha miundombinu iliyopo, kuweka mabomba mapya yenye uwezo mkubwa, kuweka pampu mpya, kuchimba visima vipya, kujenga

matangi mapya na pia kuanzisha miradi mipya ya maji katika maeneo ambayo huduma hiyo haipatikani vizuri.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara yangu ilipanga kutekeleza miradi ifuatayo:-

1. Usambazaji wa Maji Vijijini;

2. Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini; na

3. Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji.

Usambazaji wa Maji Vijijini

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, kupitia mradi huu Wizara yangu iliahidi kutekeleza miradi 14 pamoja na miradi mengine itakayoanzishwa kwa juhudi za wananchi na kubahatika kupata ufadhili. Jumla ya miradi 11 imetekelezwa na 3 haikutekelezwa kutokana na kutoingiziwa fedha kama inavyoonekana katika Jaduweli namba 1

Jadweli nambari 1

	JINA LA MRADI	**UTEKELEZAJI HALISI**
1	Tumbatu	• Kazi ya kuyaunganisha mabomba kutoka eneo la Chupa panapotarajiwa kujengwa tangi hadi Gomani na pia kuelekea Jongowe zimekamilika. Aidha Mamlaka imenunua mabomba ya ziada ya inchi 4 na inchi 3 yenye urefu wa mita 1500 kwa kukamilisha ufungaji wa mabomba katika maeneo yaliyohitaji usambazaji zaidi wa mabomba yalioko Jongowe na Gomani. • Kazi ya uchimbaji visima viwili (2) katika eneo la Kipange kwa ajili ya kuongeza wingi wa maji yaendayo Tumbatu bado haijaanza.
2	Miwani (Kiboje)	• Mradi umeendeleza kazi za ujenzi wa kituo. Shughuli nyengine za ufungaji mabombazinaendelea.
3	Kangagani	• Ujenzi wa tangi katika eneo la Kianga bado haujaanza. • Mamlaka imekamilisha kazi ya ujenzi wa kisima na ujenzi wa kibanda kwa kuwahudumia wananchi wa Dodeani.
4	Junguni	• Kazi za ufungaji wa umeme, ujenzi wa

		kituo na uungaji wa mabomba katika kisima kiliopo Junguni zimekamilika na kituo kinatoa huduma kwa wananchi wa Junguni na Gando.
5	Kigongoni	• Mamlaka imefanikisha upelekaji umeme, ufungaji wa pampu pamoja na uwekaji wa bomba la mita 150 na wananchi wanatumia huduma ya maji.
6	Ziwani	• Kazi za ujenzi wa jukwaa na ukusanyaji wa vifaa vya ujenzi wa tangi zimekamilika. Hatua za matayarisho ya kumimina zege kwenye sakafu ya tangi zinaendelea.
7	Fuoni	• Ununuzi wa mabomba makubwa kwa ajili ya kuukuza mtandao uliopo bado haujafanyika.
8	Matuleni	• Kazi ya kuendelea na ujenzi wa tangi bado hazijaanza.
9	Michamvi	• Kazi za kujenga mradi mpya kutoka Bwejuu hadi Michamvi bado hazijaanza.
10	Jumbi	• Kazi za kujenga mradi mpya bado hazijaanza
11	Kizimkazi	• Kazi za ujenzi wa Mnara wa tangi na ufungaji wa tangi zimekamilika. • Ufungaji wa mabomba mapya kutoka kwenye visima hadi kwenye tangi jipya zinaendelea.
12	Shumba vyamboni	• Kazi za kuendeleza mradi mpya zimeanza kwa ujenzi wa kituo na Mamlaka inaendelea na ufungaji wa mabomba.
13	Kisiwani	• Kazi za kuanzisha mradi mpya bado hazijaanza
14	JP5 Micheweni na Mkwajuni	• Mamlaka imekamilisha kazi za ufungaji mabomba kutoka kwenye visima vilivyopo Kironjo hadi Micheweni, Momongawa na Maziwang'ombe na mradi unatoa huduma vizuri kwa wananchi waliokusudiwa. • Kazi za ujenzi wa tangi la Micheweni hazikuweza kuanza katika kipindi cha 2009/2010 kutokana na kuchelewa kupata fedha.

		• Kazi za uchimbaji wa visima 2 vya Mkwajuni na ufungaji wa mabomba ya chuma yenye urefu wa mita 800 kutoka visimani kuelekea tangi la Mkwajuni imekamilika lakini kunahitajika mabomba zaidi ya mita 300 kuweza kufikisha maji kwenye tangi. Kazi za kupeleka umeme kwenye visima vipya na ujenzi wa kituo zinasubiri fedha kutoka Unicef.

Mhe. Spika**,** Wizara yangu kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi Zanzibar, imepata msaada wa vifaa uliotokana na misamaha ya madeni *(Multilateral Debt Relief Initiatives - MDRI).* Kwa upande wa Zanzibar, Wizara yangu ilitengewa jumla ya Tsh 1,000,000,000 ambazo Tsh 683,601,800 zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa mabomba, Tsh 306,225,540 kwa ajili ununuzi wa pampu na Tsh 10,172,660 zilitumika kwa ajili ya usafirishaji.

Mhe. Spika, mabomba yaliyonunuliwa kutoka msaada huo yana urefu wa mita 32,000 na ukubwa wa kuanzia inchi 12 hadi inchi 3. Mabomba hayo yanatarajiwa kutumika katika maeneo ya Mkoa wa Mjini/Magharibi ambapo Serikali ilitakiwa kutoa mchango wa vifaa hivyo ili kuunganisha na mabomba ya mradi uliojengwa kwa msaada wa Serikali ya Japan, pamoja na maeneo yenye miradi ya wananchi iliyokosa fedha za kununulia vifaa katika mwaka wa fedha 2009/2010.
Mhe. Spika, msaada huo wa msamaha wa madeni pia ulitumika kununua pampu za maji 32 pamoja na vifaa vyote vya kudhibiti kupanda na kushuka kwa umeme zenye ukubwa tafauti kuanzia *75KW* hadi *7KW* ambazo zitafungwa katika maeneo yaliyoharibika mashine zake na maeneo mapya yatakayochimbwa visima.

Miradi ya *TASAF*

Mhe. Spika, Wizara yangu pia ilisaidia ujenzi wa miradi iliyopata misaada kupitia Awamu ya Pili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania *(TASAF II).* Utekelezaji halisi wa miradi hiyo ni kama inavyoonyesha katika jaduweli namba 2.

Jadweli nambari 2

S/NO	JINA LA MRADI	UTEKELEZAJI HALISI
1	Ubago	Mradi unaendelea na ujenzi
2	Kidimni	Mradi umekamilika na wananchi wanafaidika na huduma hiyo
3	Chaani kubwa	Mradi unaendelea na ujenzi
4	Michungwani	Mradi umekamilika na wananchi wanafaidika na huduma hiyo

5	Koani	Mradi umekamilika na wananchi wanafaidika na huduma hiyo
6	Kizimkazi	Kazi za ujenzi wa Mradi zinaendelea

Mhe. Spika, mradi wa Mfenesini- Bumbwini umepangwa kuhudumia wananchi 46,000 wa Shehia 17 za Mfenesini, Kama, Chuini, Mwakaje, Mbuzini, Kitope, Mkadini, Kiombamvua, Matetema, Mbaleni, Fujoni, Mangapwani, Kidanzini, Misufini, Makoba, Zingwezingwe na Mahonda. Mradi huu unategemewa kutumia jumla ya Euro 1,049,000 ambazo ni sawa na Tsh 1,888,200,000 ambapo kati ya fedha hizo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechangia Euro 149,000 sawa na Tsh 268,200,000, Jumuiya ya Ulaya imechangia jumla ya Euro 750,000 sawa na Tsh 1,350,000,000 na *ACRA* imechangia Euro 150,000 sawa na Tsh 270,000,000. Mradi umo katika mwaka wa pili wa utekelezaji na hadi kufikia Machi 2010 kazi zilizotekelezwa na ambazo bado zinaendelea ni :

1. Uchimbaji wa visima Mfenesini na Selem umekamilika. Kisima cha Mfenesini kimeshawekwa pampu na viwili vilioko eneo la Selem vinakamilishiwa taratibu za kuvuta umeme na kuwekewa pampu ili viweze kutowa huduma.

2. Ujenzi wa Tangi la lita 250,000 ulioanza Februari mwaka 2010 umeendelea kwa kukamilisha shughuli zote za ujenzi wa msingi, mnara na tangi. Majaribio ya tangi yatafanyika baada ya kukamilika kazi za ufungaji mabomba.

3. Ufungaji wa Mabomba yenye urefu wa mita 53,013 na ukubwa tofauti wa kuanzia inchi 4, 6, 8 na 12 umeanza kwa kuelekea maeneo yale ya Mradi mradi huu na kazi zinaendelea. Kazi hii inatarajiwa kumalizika mwanzoni mwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, miradi mingine iliyotekelezwa ni ile iliyoanzishwa kwa juhudi za wananchi na kupata ufadhili. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na mradi wa Fumba ambao umesaidiwa na Ubalozi wa Japan kwa kupatiwa jumla ya TSh 106,000,000 zilizotumika kwa ununuzi wa mabomba makubwa ili kubadilisha mtandao mdogo wa zamani. *UNICEF* walisaidia mradi wa Mtambwe Kaskazini na jumla ya TSh 18,000,000 zilitumika kwa ununuzi wa mabomba yaliyosambazwa Mtambwe Mpakanjia na sehemu ya Nyali.

Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini

Mhe. Spika, ujenzi wa mradi huu unahusisha Mkoa wa Mjini Magharibi pamoja na miji mitatu ya Pemba. Mradi wa maji wa Mkoa wa Mjini/Magharibi ambao umeanza kwa awamu ya pili unaendelea vizuri na kutegemewa kumaliza kwa wakati uliopangwa wa mwezi Julai 2010.

Mhe. Spika, jumla ya Yen za Kijapani Bilioni 1.4 sawa na Tsh Bilioni 19.2 na Milioni 550 ambazo ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimetumika katika kazi zilizopangwa za uchimbaji visima 5, ujenzi wa matangi 2, (tangi la Dole na tangi la Kinuni). Tangi la Dole litakuwa na uwezo wa kuhifadhi lita 1,300,000 na la Kinuni litakuwa uwezo wa kuhifadhi lita 2,700,000.

Kazi ya ufungaji wa mabomba ya urefu wa kilomita 21.5 zimekwenda vizuri sambamba na kazi za kuyaunganisha mabomba mapya na matandao wa zamani katika sehemu za Mradi.

Visima 3 vilivyochimbwa maeneo ya Kizimbani vinatumika kujaza maji katika tangi la Dole ili kuwasaidia wananchi wa majimbo ya Bububu, Mfenesini, Mtoni na Dole. Tangi la Kinuni litahudumiwa na visima 2 vilivyochimbwa Kinuni pamoja na visima 3 vya zamani vilivyoko Chunga. Maji kutoka tangi la Kinuni yatatumika katika maeneo ya majimbo ya Magogoni, Fuoni, Mwanakwerekwe, Kiembesamaki na Dimani.

Mradi wa awamu ya pili utakapokamilika Julai 2010 utaungana na ujenzi wa awamu ya kwanza uliojenga matangi 2 Welezo na kuchimba visima Machui 3, Kianga 2 na Muembemchomeke 1na kulaza mabomba kilomita 20 ili kuwahudumia wakaazi wa Mjini/Magharibi.

Wizara yangu imefunga mabomba makubwa ya inchi 8 na 6 katika maeneo ya Magomeni, Mpendae, Meya na Kilimahewa kwa ajili ya kuunganishwa na mtandao mpya wa mradi wa awamu ya kwanza pamoja na maeneo ya Bububu, Kidichi, Melinne, Pangawe na Mombasa kwa awamu ya pili. Visima 2 vimechimbwa katika maeneo ya Kwa Sharif Ali ili kusaidia mji wa Chake-Chake ambavyo ni sehemu ya ahadi za Serikali kwa msaada uliotolewa na taasisi isiyokuwa ya Serikali ya *Ivo de Carneri Foundation* ya Italy na hatua hio imeleta faraja kubwa kwa huduma ya maji kwa mji huo.

Mradi wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira

Mhe. Spika, Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) kwa mashirikiano na *UN-HABITAT* wamekubali kuipatia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar msaada wa Dola za Kimarekani Milioni 7 pamoja na mkopo wa Dola za Kimarekani Milioni 40.5 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira kwa kipindi cha kuanzia miaka 4 (2008-2013). Mchango wa Serikali kwa mradi huu ni Dola za Kimarekani Milioni 6. Mradi huu utajumuisha miji ya Chake-Chake, Wete na Mkoani na maeneo ya vijiji 9 vya Nungwi, Matemwe, Machui na Dunga – Tunguu kwa Unguja na Wambaa, Mizingani, Ndagoni, Vitongoji na Kambini – Mchangamdogo kwa Pemba.

Kazi za ujenzi wa Miradi hii zimechelewa kutokana na kutopata ridhaa ya tamko la kuanza kazi rasmi *(declaration of project effect)* kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) pamoja na kuridhiwa kwa mashauri ya kuwateua wataalamu wa kufanyakazi za usanifu. Tamko la Ridhaa ya Mradi lilipatikana mwezi Oktoba 2009 na lile la ridhaa ya wataalamu lilipatikana Aprili 2010. Mambo hayo yamepelekea kuchelewa kuwasili kwa baadhi ya wataalamu ambao walitarajiwa mwishoni mwa mwaka 2009 kwa kushirikiana na wataalamu wazalendo ili kuendelea na kazi za Mradi huo. Hadi kumalizika mwaka 2009/10, Mshauri pekee wa Mradi aliyekubalika kuanza kazi ni Mtaalamu wa Manunuzi *(Procurement Specialist)* ambae ameletwa na *UN-HABITAT* ikiwa ni sehemu ya msaada.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba Mradi umechelewa kwa sababu zilizotajwa, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji tayari inachambua maombi ya Kampuni 18 zilizowasilisha maombi ya kazi za Usanifu ili kupata Kampuni 3 ambazo zitashiriki katika kazi ya Usanifu wa Miradi, utayarishaji Zabuni na Usimamizi wakati wa Ujenzi. Aidha Mamlaka imo katika hatua ya kumchagua Msimamizi Mkuu wa Mradi kutokana na jumla ya maombi 35 ya Makampuni yaliyowasilisha maombi kwa kazi hio. Mapendekezo ya Wizara kuhusiana na maamuzi ya nafasi hizo yatawasilishwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) kwa kupata ridhaa na kuendelea na taratibu za uajiri na kuanza kazi ambayo inatarajiwa kuanzwa katika mwezi wa Septemba 2010.

Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji.
Mhe. Spika, mradi huu ambao pia unafadhiliwa na Serikali ya Japan una lengo la kuijengea Mamlaka Uwezo wa Kiutendaji ili watendaji wa Mamlaka waweze kumudu majukumu yao ipasavyo. Mradi huu umewapatia wafanyakazi mafunzo mbali mbali ya ndani na nje ya nchi ili kuinua vipaji vyao. Katika mwaka 2009/2010 jumla ya wafanyakazi 9 wamepatiwa mafunzo ya kazi katika Mamlaka ya Maji safi na Maji taka Arusha katika nyanja za uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato, utawala, uhasibu na mahusiano na wateja. Wafanyakazi wengine 10 wamepatiwa mafunzo ya kiufundi katika afisi za Mamlaka na mtaalamu aliyeletwa na *JICA* katika taaluma ya matengenezo na ufungaji wa mita za maji.

Aidha wafanyakazi 2 walipatiwa mafunzo nchini Japan juu ya namna ya kudhibiti upotevu wa maji. Mradi umetoa misaada ya vitendea kazi vikiwemo gari na pikipiki 5 kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji wa kazi za kila siku za ukusanyaji wa mapato, pia mradi umetoa mita 300 za maji ili kuanza zoezi la mafunzo ya kutoa ankara kutokana na vipimo vya mita. Jumla ya Yen milioni 261 ambazo ni sawa na Tsh 1,827,000,000 zimetumika katika mradi huu.

Ukusanyaji wa Mapato
Mhe. Spika, katika kuchangia huduma ya maji ili kuifanya iwe endelevu, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji, imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi kwa njia ya mikutano, redio na televisheni ili wajue wajibu wao katika suala la kuchangia. Pamoja na elimu inayotolewa kwa wananchi, bado kumekuwa na muitikio mdogo katika suala la kuchangia kwani idadi ya wanaochangia huduma hiyo hadi sasa bado haijaridhisha hata kidogo na hivyo kuathiri bajeti ya Mamlaka. Aidha katika kipindi cha miezi mitatu cha kukatika kwa umeme, Mamlaka ilishindwa kukusanya mapato kwa vile katika kipindi hicho cha dharura ni vituo vichache visivyozidi 42 vilivyokuwa vikitoa huduma kwa kutumia majenereta kwa muda kati ya masaa 12 hadi 18 kwa siku.

Ukitoa kipindi cha kukatika kwa umeme katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Mamlaka ya Maji hadi kufikia tarehe 31 Machi 2010 iliweza kukusanya jumla ya Tsh 416,790,639.60 sawa na asilimia 36 ya makadirio.

Kazi za Kawaida za Matengenezo ya Mabomba na Pampu za Maji
Mhe. Spika**,** pamoja na kazi za miradi zinazofanywa na Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji, pia kumefanyika kazi mbali mbali za matengenezo ya mabomba machakavu ambayo husababisha uvujaji na upotevu wa maji mara kwa mara kwenye maeneo hasa yenye mtandao mkubwa.

Baadhi ya maeneo yalilazimika kuwekwa mabomba mapya na yenye uwezo mkubwa ili kuongeza wingi wa maji. Matengenezo ya vifaa vya pampu pamoja na kubadilisha pampu zilizoungua, yalifanyika katika maeneo ya Chumbuni, Welezo, Chunga namba 8, Mwembe Mchomeke, Mfenesini, Bumbwini, Mwanakombo, Pangeni, Jambiani, Mgenihaji, Tazari, Paje na Mkwajuni, Kiembesamaki, Nungwi na Donge kwa Unguja na Michenzani, Kangani, Kwa Sharif Ali, Changaweni na Kironjo kwa Pemba.

Vile vile kazi za usafishaji wa visima vya Welezo na Donge zilifanyika ili kuondoa matope yaliyomo katika visima hivyo kwa madhumuni ya kuyafanya maji yawe safi. Visima vipya 7 vimechimbwa katika maeneo ya Selem(2), Mfenesini(1), Dole(1), Wawi(1) na Kwa Sharif Ali(2).

Mhe. Spika, ili tuweze kuwafungia mita watumiaji wa maji majumbani Wizara yangu kupitia Mamlaka tayari imeshanunua mita 1000 za maji ambazo zitaunganishwa na mita 300 zilizonunuliwa na Serikali ya Japan kupitia Mradi wa kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji ili kusaidia katika kufikia lengo na azma hiyo kwa kupunguza malalamiko ya wananchi pamoja na kuinua mapato ya mauzo ya maji kwa Mamlaka.

IDARA YA UJENZI

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Idara ya Ujenzi ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia na kudhibiti ipasavyo shughuli zote zinazohusiana na sekta ya ujenzi nchini kwa kuimarisha Bodi ya Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji majengo pamoja na ile ya Makandarasi sambamba na kuundwa kwa kanuni zitakazodhibiti ujenzi huo.
2. Kumaliza ujenzi na kukabidhi Serikalini Nyumba za Maendeleo Michenzani na Mpapa.

Utekelezaji
Mhe. Spika, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Bodi ya Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo pamoja na Bodi ya Wakandarasi.

Bodi ya Kusajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo
Mhe. Spika**,** Bodi imeshaanza kazi zake za kusajili wataalamu wa fani husika yaani Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo, hivi sasa tupo katika hatua za mwisho za utayarishaji wa kanuni. Ofisi ya Bodi hii imeshapatikana katika jengo la Idara ya Ujenzi, Michenzani

Bodi ya Kusajili Makandarasi
Mhe. Spika, kwa upande wa sheria ya Wakandarasi ambao watasajiliwa, watakuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa wananchi kwa kujenga nyumba zenye ubora na usalama kwa mujibu wa taratibu na viwango vya ujenzi vinavyokubalika.

Hivi sasa Bodi imeshakamilisha kanuni zake na inaendelea na utekelezaji wake. Afisi ya Bodi hii vile vile imo katika jengo la Idara ya Ujenzi, Michenzani. Matarajio yetu kuwa asilimia 95 ya Wakandarasi wote wa Zanzibar watakua wameshasajiliwa mnamo mwanzo wa mwaka wa fedha 2010/2011.

Nyumba za Maendeleo Mpapa
Mhe. Spika, azma yetu ilikua kukabidhi jengo la Mpapa mwaka wa fedha 2009/2010, lakini haikuwezekana kutokana na mtiririko wa hali ya fedha pamoja na tatizo la ukosefu wa umeme.

Idara imeshakamilisha ujenzi wa "*super structure*" na hatua ya umaliziaji wa kazi za ndani unaendelea.

IDARA YA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAAZI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

Ukusanyaji Mapato

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi, 2010 jumla ya TSh 52,656,355 zimeshakusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 52.66 ya makadirio.

Ukusanyaji wa kodi umeathiriwa kwa kiasi kikubwa kutokana na kukosekana kwa huduma ya umeme kwa muda wa miezi mitatu. Wengi wa wapangaji hawakuweza kulipa kodi zao sawa sawa katika kipindi hicho kutokana na gharama kubwa zilizowakabili wapangaji.

Uuzaji wa Nyumba za Vijiji

Uuzaji wa Nyumba za Vijiji tayari umeshaanza na unaendelea vizuri, maombi ya uuzaji huanzia kwenye Kamati ya Sheha eneo nyumba ilipo, hupitia Serikali ya Wilaya na humalizia Serikali ya Mkoa na baadae maombi hufikishwa Wizarani kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki wa mwisho. Hatua hizi zimechukuliwa ili kuhakikisha kuwa zoezi linakwenda vizuri na kwa uwazi na pia kuhakikisha kuwa aliyemo ndani ya nyumba ndie anaepewa nafasi ya mwanzo. Utaratibu wa kuziuza nyumba hizo unaendelea ambapo jumla ya Nyumba 343 za vijiji Unguja na Pemba zinatarajiwa kuuzwa. Nyumba 245 kwa upande wa Unguja na Nyumba 98 kwa upande wa Pemba.

Kuundwa Kwa Kamati ya Kuwatambuwa Wale Wote Waliopewa Nyumba na Marehemu Mzee Karume

Mhe. Spika, hatua tayari zimechukuliwa za kuundwa kwa Kamati ya kuwatambuwa wale wote waliopewa nyumba na marehemu Mzee Karume na Kamati tayari imeshaanza kazi.

Kamati imetayarisha dodoso *(questionaire)* ambalo kila mdai anatakiwa alijaze na baadae Kamati itayapitia Madodoso yote na kuwasaili wahusika na baadae Kamati itatoa mapendekezo yake kwa Serikali nani anastahiki na nani hastahiki kumilikishwa Nyumba hizo.

Matayarisho ya Sheria ya "*Condominium*"

Utaratibu wa uundaji wa Sheria ya *Condominium* umefikia hatua nzuri na hivi sasa tayari imeshafikishwa katika kikao cha Makatibu Wakuu na kujadiliwa. Hata hivyo katika kikao hicho imeonekana ni vyema baadhi ya vipengele

kuangaliwa upya na vyengine kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kupata sheria nzuri na itakayokidhi haja ya mahitaji kulingana na mazingira ya Zanzibar.

Sheria ya *Condominium* itakapokamilika itawezesha wakaazi wanaoishi katika jengo moja lenye fleti zaidi ya moja kujua haki za matumizi ya jengo na uwajibikaji katika kuchangia gharama za matengenezo kwa sehemu za jengo zinazotumiwa na wakaazi wote (Common Areas).

Ulipaji wa Fidia kwa wale wote Waliovunjiwa Nyumba zao Kupisha Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo

Mhe. Spika, kamati iliyoundwa kwa kazi ya fidia imekamilisha kazi yake na jumla ya familia 94 zimethibitika kuwa zina uhalali wa kufidiwa. Kilichoonekana ni kuwa wengi wa wadai tayari wameshafariki, na tayari tumeandaa utaratibu ambao kila anayestahiki apate haki yake na pia utakaopunguza malalamiko ndani ya familia husika. Orodha ya wafidiwa ambao ni marehemu imekabidhiwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kwa wale waislamu, na kwa wale ambao sio waislamu orodha yao imekabidhiwa kwa Mrajis Mkuu wa Serikali. Zoezi la kuwatambua warithi halali linaendelea katika Taasisi hizo na litakapokamilika wahusika watakabidhiwa nyumba zao.

Matengenezo ya Nyumba za Serikali

Mhe. Spika, Idara imeendelea na zoezi la kuyafanyia usafi makaro katika Nyumba za Maendeleo kama vile Kilimani, Michenzani, Kikwajuni, Mombasa kwa Mchina, Mtemani, Mkoani, na Machomanne. Matengenezo hayo yalihusisha chemba ndogo, na makaro makubwa na pia ubadilishaji wa mabomba yaliyochakaa kwa baadhi ya maeneo.

Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba

Bodi iliendelea kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri mbali mbali yaliyowasilishwa. Jumla ya mashauri 72 yamewasilishwa, kati ya hayo mashauri 18 yametolewa maamuzi. Kati ya mashauri yaliyowasilishwa mashauri 13 yaliwasilishwa na Idara na 59 ni ya watu binafsi.

MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Mamlaka iliendelea kutekeleza kazi zake kama ifuatavyo:-

Ukusanyaji wa Mapato

Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ilitakiwa kukusanya Tsh. 21,000,000 hadi kufikia Mwezi wa Machi jumla ya Tsh 12,949,100 zilikusanywa sawa na asilimia 61.66 ya lengo lililowekwa

Mradi wa Kuukuza na Kuutambulisha Mji Mkongwe
Mhe. Spika, Mamlaka imetekeleza mradi huu uliofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Sida ambao umemaliza muda wake mwezi Machi 2010. Vipengele vyote vya mradi vimetekelezwa isipokuwa kipengele cha kupata mshauri muelekezi wa kujenga uwezo wa taasisi, suala la mshauri muelekezi halikutekelezwa kwa sababu ya uchache wa muda hata hivyo Mamlaka kwa kushauriana na wafadhili hao imeweza kununua Jenereta, kuchangia udhamini wa mafunzo ya muda mfupi kwa mfanyakazi mmoja nchini Italy na pia kufanya kazi za usafishaji na uendelezaji wa baadhi ya maeneo ya wazi katika Mji Mkongwe.

Uhifadhi wa Takwimu na Taarifa Muhimu
Mhe. Spika, Mamlaka iliweza kukusanya taarifa muhimu za maeneo yote ya wazi ya Mji Mkongwe, kazi hii ilifanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Minessota Marekani, jumla ya maeneo kumi yalifanyiwa kazi katika zoezi hili na taarifa hizi zinatarajiwa kuingizwa katika tovuti ya Mji mkongwe.

Mpango wa Matumizi ya Barabara na Maegesho *(Traffic Plan)*
Mhe. Spika, Mamlaka kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili ilikwisha tayarisha mpango huo na kubakia utekelezaji, mpango huo ulifanywa kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali zinazohusiana na mpango huo. Mamlaka itautangaza rasmi mpango huo kwa kushirikiana na taasisi husika ili ufahamike kwa wananchi na utekelezaji.

Sheria Mpya ya Mamlaka
Mhe. Spika, Mamlaka ya Mji Mkongwe mwaka jana iliripoti kuhusu mapitio ya Sheria mpya, kazi hiyo imefanyika vizuri sana kwa kupitia ngazi zote zinazohusika na hatimae kumalizika kwa kuwasilishwa kwenye Baraza lako tukufu, na kukubalika, hivyo tayari tunasubiri kwa kuanza kuifanyia kazi rasmi.

Bustani ya Forodhani
Mhe. Spika, kazi ya matengenezo ya bustani imemalizika na kufunguliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la mapinduzi Mhe. Dk. Aman Abeid Karume tarehe 30 Julai 2009, jumla ya Dola za Kimarekani milioni 3.2 zilitumika kwa ajili ya mradi huo.

Mradi wa Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Bahari
Mhe. Spika, Mamlaka ilishiriki kikamilifu katika hatua za matayarisho ya mradi huu ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia, kazi zilizofanyika ni pamoja na kupimwa kwa eneo lote la mradi, kufanyika kwa kikao cha pamoja cha taasisi zinazohusika na mradi huu pamoja na washiriki wa mradi huu wa taasisi ya Agakhan.

Aidha timu ya watafiti wa athari za mazingira na kijamii ilikutana na wawakilishi wa Agakhan Zanzibar na Mamlaka ya Mji Mkongwe na kujadili utekelezaji wa utafiti huo na mnamo mwezi wa machi kikao cha pamoja kati ya watafiti wa mazingira na taasisi zote husika pamoja na wamiliki wa majengo ambayo yapo karibu na mradi huo kilifanyika. Aidha Mradi una adhma ya kuimarisha mazingira ya Mji Mkongwe na kutengeneza njia ya waenda kwa miguu *(pedestrians)* ili kuleta usalama wao na kupunguza msongamano wa vyombo vya usafiri. Mradi huu unatarajiwa kukamilika 2012 kwa gharama ya jumla Dola za Kimarekani Milioni 5.

Mafunzo ya Wafanyakazi
Mhe. Spika, mamlaka imeendeleza juhudi za kujenga uwezo wa wafanyakazi wake na jumla ya wafanyakazi kumi wanahudhuria mafunzo ambapo watano wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu na watano ya muda mfupi nchini Italy (*ICCROM*), Kenya, Sweden (*Lund University*).

IDARA YA NISHATI NA MADINI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Idara ya Nishati na Madini ilisimamia na kutekeleza mambo yafuatayo:-

Kukamilisha kazi Zote za Mradi wa Sera ya Nishati ambayo ni Pamoja na Kuweka Mikakati ya Utekelezaji wa Sera hiyo
Mhe. Spika, mchakato wa uandaaji wa Sera ya Nishati ya Zanzibar umekamilika baada ya rasimu ya Sera hiyo kupelekwa Baraza la Mapinduzi tarehe 8 Disemba 2009 na baadae kuipitisha na kuwa Sera kamili. Sera ya Nishati ya Zanzibar baadae iliwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi katika kikao chake cha kawaida cha mwezi wa Januari 2010. Waheshimiwa wajumbe wa Baraza waliijadili na kutoa michango yao pamoja na kukubali mpango mzima wa uaandaaji wa sera hiyo.

Vile vile katika utekelezaji wa Sera ya Nishati, Wizara yangu imekusudia kutayarisha na kuziwasilisha katika Baraza lako tukufu sheria zote zinazohusiana na mafuta kama vile sera ilivyo elekeza, kwa mfano "*Petroleum Supply Act*" na "*Zanzibar Energy Act*".

Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Idara ya Nishati na Madini imewafanyia Semina Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu juu ya utawala bora katika Utafutaji na Uchimbaji wa mafuta. Aidha Wizara yangu imeshawafanyia Semina ya masuala ya Mafuta na Gesi Asilia Waheshimiwa Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ni imani yangu kwamba semina hizo zimetoa ufafanuzi zaidi juu ya masuala ya utafutaji wa mafuta kwa ngazi ya Waheshimiwa Wawakilishi na Mawaziri.

Kuendeleza Jitihada zaidi ili kuwafikishia Elimu ya Umeme wa Jua Wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba

Mhe. Spika, juhudi za kufikisha huduma za nishati mbadala kama vile nishati ya umeme wa jua kwa visiwa vidogo vidogo vya Unguja na Pemba inaendelea. Mpango huo unaendelezwa kwa ushirikiano wa Jumuiya ya Ushirikiano kati ya Ujerumani na Tanzania (*DTP*) na Jumuiya inayojishughulisha na Umeme wa jua ya hapa Zanzibar (*ZASEA*).

Hivi sasa wananchi wengi pamoja na mahoteli tayari wamehamasika na wanaendelea kutumia nishati ya jua. Aidha hivi sasa kwa kushirikiana na *ZASEA* (*Zanzibar Solar Energy Association*) tumeanzisha mpango wa kutoa elimu ya umeme wa jua mashuleni *(Solar Programe in Schools)* ili ufahamu wa nishati hiyo uongezeke na kuwezesha jamii kuanza kuitumia kwa kiwango kikubwa.

Kushiriki Kikamilifu Katika Masuala yote ya Nishati ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki

Mhe. Spika, ushiriki wetu katika Kamati za Nishati za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki unaendelea. Kwa mujibu wa kalenda ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Mkutano Mkuu wa Mafuta wa Jumuiya hiyo *(East African Petroleum Conference)* hufanyika kila baada ya miaka miwili tangu ulipoanzishwa mwaka 2003. Mkutano wa tano umepangwa kufanyika Uganda mwezi wa Februari 2011.

Lengo kuu la Mikutano hii ni kuweka juhudi za pamoja miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika masuala ya utafutaji wa mafuta kwenye ukanda huu. Pamoja na lengo hilo Zanzibar inafaidika na mikutano hii kwa kuwaongezea maarifa na taaluma za utafutaji na uchimbaji wa mafuta wafanyakazi wa Sekta ya Nishati.

Sekta nyengine kama vile za Mazingira, Utalii na Uwekezaji za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki nazo pia hufaidika na mikutano hii ya Mafuta kwani mikutano hii huwajumuisha pamoja wataalamu na viongozi wa Sekta hizo katika eneo la Afrika Mashariki.

Kuendelea Kusimamia Upatikanaji wa Mafuta Zanzibar (Dizeli, Petroli na Mafuta ya taa)

Mhe. Spika, upatikanaji wa nishati ya mafuta hapa nchini unaendelea, changamoto ilijitokeza katika siku za mwanzo za ukosefu wa huduma ya umeme katika Kisiwa cha Unguja katika Mwezi wa Disemba 2009 hadi Januari 2010 ambapo mafuta yalikuwa hayapatikani kwa kawaida lakini tatizo hili lilidhibitiwa mapema baada ya Makampuni hayo kuagizwa kuleta mafuta ya ziada tofauti na

utaratibu wao wa kawaida wa kuagiza mafuta kwa kuzingatia hali halisi. Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho "D"

Usimamizi wa '*Depot*' za Mafuta
Mhe. Spika, Idara ya Nishati ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia *Depot* hizi za Serikali Unguja na Pemba. Kwa kuwa Sera ya Nishati imeshapitishwa basi Wizara itatunga sheria inayohusiana na umiliki na usambazaji wa mafuta *(Zanzibar Petroleum Supply*) ili bidhaa ya mafuta iweze kusimamiwa na Sekta husika ili mapato yatokanayo na depot hizo yakusanywe katika Sekta husika kwa ajili ya kuimarisha Sekta hiyo pamoja na kuchangia mfuko wa hazina ya Serikali.

Mafuta na Gesi Asilia

Mafunzo
Mhe. Spika, Wizara ya Maji Ujenzi Nishati na Ardhi inaendelea kufanya juhudi ya kuwapatia Mafunzo wafanyakazi wa Idara hii na Wizara kwa jumla ili kuweza kukabiliana na upungufu wa wataalamu wa fani ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta hapa Zanzibar,

Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Norway kupitia shirika lake la *PETRAD* imempatia mfanyakazi 1 mwenye sifa katika nyanja ya *"Petroleum Policy and Management*" nchini Norway katika kipindi hichi cha 2009/10. Takwimu hii inafanya kuwa jumla ya Wafanyakazi 8 tayari wameshapatiwa mafunzo ya *"Petroleum Policy and Management*" na "*Petroleum Development and Operations*" tokea zoezi hili lianze mwaka 2002. Vile vile semina na warsha kadhaa katika fani ya Mafuta na Gesi Asilia zimefanywa hapa Zanzibar kwa washirika mbalimbali kwa lengo la kutoa ufahamu zaidi katika suala hili.

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana niligusia utekelezaji wa agizo la Serikali la kuwapeleka wazanzibari kusoma utaalamu wa fani ya mafuta na gesi asilia ngazi ya Digrii ya mwanzo na ya pili, kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho "E". Tayari Wizara yangu imetafuta aina ya mafunzo na Mfadhili. Wizara hii ilifanya mazungumzo na wataalam wa *RAK GAS Tanzania Ltd* kwa ufadhili wa mafunzo hayo.

Kwa kufuata maelekezo ya Serikali, Wizara hii ilishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kukutana kwa pamoja na Wataalamu hao na kufanya mazungumzo maalum na ikakubalika kuwapeleka wanafunzi 10 kwa hatua ya mwanzo masomoni. Aidha Wizara ya Elimu ilichukuwa hatua ya kuwatangazia wananchi kwa njia ya gazeti na tayari Wizara ya Elimu imepokea maombi na inayafanyia kazi kwa kuwasilishwa kwa wafadhili hao kwa hatua zaidi. Inatarajiwa mkumbo wa mwanzo wa wanafunzi hao kupelekwa masomoni ndani

ya mwaka wa fedha 2010/11. Aidha Idara ya Nishati katika "*Training Program"* yake ya kawaida imefanikiwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wake wawili katika ngazi ya cheti na mmoja ngazi ya Diploma.

Mhe. Spika, kwa upande wa suala lenyewe la Mafuta na Gesi Asilia, hatua iliyofikiwa baada ya maamuzi ya Serikali ya kupendekeza kulitoa suala la Mafuta na Gesi Asilia katika orodha ya mambo ya Muungano, Baraza la Mapinduzi lilimuagiza Mhe. Waziri Kiongozi kuwasilisha barua maalum kwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulitoa suala hilo katika orodha ya mambo ya Muungano ili kuzipa nafasi hatua nyengine za kisiasa na kisheria kuchukuwa mkondo wake. Mheshimiwa Waziri Kiongozi tayari amelichukulia hatua suala hilo na barua hiyo tayari imewasilishwa na Wizara yangu inasubiri maelekezo ya Afisi ya Mheshimiwa Waziri Kiongozi.

Mhe. Spika, katika maelezo yangu ya kuwasilisha waraka wa Sera ya Nishati katika Baraza hili tukufu, nilielezea umuhimu wa Zanzibar kujiandaa vizuri katika suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na Gesi asilia kwa suala la tathmini ya mazingira yake kutokana na udogo na harakati za uchumi za nchi yenyewe. Wizara yangu tayari imekubaliana na Serikali ya Norway kufanywa utafiti wa kimazingira kuhusiana na Utafutaji na Uchimbaji wa mafuta na gesi asilia *(Strategic Environmental Impact Assessement*) na kazi hiyo imefikia katika hatua za utekelezaji. Serikali ya Norway inafanya mazungumzo na Mshauri Mwelekezi kwa kazi hiyo ili kupanga kazi yenyewe na kujua gharama halisi kwa utekelezaji wa tathmini hio. Hii ni hatua kubwa katika kufikia tulikokukusudia.

SHIRIKA LA UMEME (*ZECO*)

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Shirika limepata matatizo makubwa ya kuunguwa kwa waya wa Umeme katika kituo cha umeme cha Fumba. Tatizo hilo lililotokezea tarehe 10 Disemba, 2009 lilisababisha kukosekana kwa umeme katika Kisiwa cha Unguja kwa muda wa miezi mitatu mfululizo hadi tarehe 08 Machi, 2010 baada ya kukamilika kwa matengenezo yake. Katika kipindi hicho, Shirika lilishindwa kutoa huduma ya umeme kwa Wananchi wa kisiwa cha Unguja lakini kazi ya uzalishaji umeme katika kisiwa cha Pemba ziliendelea kwa kutumia majenereta yake ya kuzalishia umeme yaliopo Wesha.

Matumizi na Mapato

Mhe. Spika, katika makadirio ya mwaka wa fedha 2009/2010, Shirika lilikadiria kutumia Tshs 35,954,427,000.00 kwa uendeshaji wa kazi za kawaida na za maendeleo.

Matumizi halisi ya Shirika katika robo tatu ya mwaka wa fedha yalikuwa Tsh 20,577,379,993.00 kwa kazi za kawaida na za maendeleo. Kati ya fedha hizo, Tsh 10,463,775,373.00 ni kwa ajili ya ununuzi wa Umeme *Tanesco*, Tsh 5,548,664,193.00 zilitumika kwa malipo ya mafuta ya uzalishaji umeme Pemba (*IDO*), na Tsh 4,564,940,427.00 kwa uendeshaji wa kazi za kawaida na za maendeleo ya Shirika.

Mhe. Spika, kuhusu ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa 2009/10 Shirika lilikadiria kukusanya Tsh 37,174,686,000.00. Kati ya fedha hizo, Tsh 34,181,260,000 zilitazamiwa kukusanywa kutokana na mauzo ya umeme na Tsh 1,993,426,000 zilitarajiwa kutoka katika mapato mengineyo. Vile vile Tsh 1,000,000,000 zilitarajiwa kukusanywa kwa niaba ya Bodi ya Mapato Zanzibar ikiwa ni kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na Shirika kupata bakaa ya uendeshaji ya Tsh 1,220,259,000.

Mhe. Spika**,** hadi kufikia Machi, 2010 Shirika limekusanya jumla ya Tsh 21,571,773,460.00 sawa na asilimia 85.4 yakilinganishwa na makadirio yaliyokadiriwa kukusanywa ambayo yalikuwa Tsh 25,235,303,999 kwa kipindi cha miezi tisa. Sababu ya kupungua kwa asilimia hiyo imetokana na Shirika kukosa Umeme wa kuwauzia wateja wake kwa miezi mitatu. Lakini dalili zinaonyesha kwamba mafanikio mazuri katika ukusanyaji wa mapato ya Shirika yanaongezeka kutokana na juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na uongozi wa Shirika wa kuhakikisha kwamba mapato yote ya Shirika yanakusanywa ipasavyo.

Matarajio ya Shirika hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2009/2010 litakusanya jumla Tsh 28,364,354,998.

Utekelezaji wa kazi za Maendeleo

Mradi wa kusambaza Umeme kisiwa cha Tumbatu

Mhe. Spika**,** itakumbukwa wakati nikiwasilisha makadirio ya Wizara yangu mbele ya Baraza lako Tukufu, nilitoa ahadi ya kukamilisha kazi ya kupeleka umeme kisiwa cha Tumbatu chenye wastani wa wakaazi elfu kumi napenda kuwaarifu Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba kazi za ujenzi wa njia ndogo na kubwa pamoja na uwekaji wa vituo vinne vya umeme katika vijiji vya Gomani, Jongowe na Kichangani tayari zimekamilika. Kazi iliyobaki ni ya ulazaji wa waya wa baharini kutoka Mkokotoni hadi Tumbatu ambayo itaanza mara tu utakapowasili waya huo unaotegemewa kufika katika mwezi wa Juni, 2010. Gharama zilizotumika ni Krona za Norway Milioni 6.

Mradi wa kupeleka Umeme Pemba kutoka Tanga

Mhe. Spika, mradi wa kupeleka umeme katika kisiwa cha Pemba kutoka Tanga umefadhiliwa na Serikali ya Norway pamoja na michango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla ya gharama ya Krona za Norway (*NOK*) milioni 400. Mradi huu ulianza mara tu baada ya kutiliana saini mkataba wa makubaliano ya msaada wa fedha za ujenzi kati ya Serikali ya Norway na Serikali ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hatimae kulifuatiwa na utiaji wa saini mkataba wa kuanza kazi ya utengenezaji wa waya kati ya *ZECO* na kampuni ya *NEXANS* ya Norway. Kampuni hiyo ilikamilisha kazi ya utengenezaji wa waya na kuupakia katika Meli ya Mv Skegerrak iliyowasili Tanga tarehe 01/12/2009.

Mhe. Spika, kazi ya ulazaji wa waya baharini ilizinduliwa tarehe 04/12/2009 na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Amani A. Karume katika bandari ya Tanga. Na baadae kazi ya ulazaji wa waya ikaanza rasmi na kukamilika tarehe 15 Disemba, 2009 huko Mkumbuu Pemba. Waya huo una urefu wa kilomita karibu 72 na wenye uzito wa tani 2,998.80 ambao utakuwa na uwezo wa kuishi miaka 40. Waya huu una waya wa "*Fibre Optic Cable*" ambao hutumika kwa mawasiliano ya kisasa na huduma za "Internet". Huduma hio itakuwa ni changamoto kubwa kwa wananchi wa Zanzibar kwa vile itaongeza uwezo wa kusambazwa kwa huduma hio kwa bei nafuu na kuingiza mapato nchini kutoka kwa makampuni yatakayojiunga na huduma hio.

Kazi ya ujenzi wa vituo vya umeme (*substation*) imefanywa na Kampuni ya *ABB* ya Norway na ujenzi wa njia ya juu ya umeme (overhead line) kwa upande wa Tanga imefanywa kwa mashirikiano ya wafanyakazi wa *TANESCO* na *ZECO* na kwa upande wa Pemba imefanywa na wafanyakazi wa Shirika la Umeme la Zanzibar (*ZECO*).

Mhe. Spika, mradi huu ulitarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2009 lakini kutokana na tatizo la kuchelewa kuwasili kwa baadhi ya vifaa hapa nchini, imepelekea mradi huu kutokamilika kwa wakati. Hata hivyo Shirika limeweza kujitahidi na kukamilisha kazi zilizosalia kwa haraka na hatimae mradi huo umeweza kufanyiwa majaribio kwa mara ya kwanza tarehe 08/05/2010 na baadae wananchi wa Pemba wakaanza kunufaika na huduma hii ya uhakika ya umeme kuanzia tarehe 09/05/2010. Mhe. Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefungua rasmi mradi huu tarehe 3 juni 2010 kwa sherehe kubwa zilizoungwa mkono na wananchi Kisiwani Pemba.

Mradi wa kuendeleza ufungaji wa Mita za Tukuza
Mhe. Spika, mradi huu unaoendeshwa kwa mfuko binafsi wa Shirika umeendelea vizuri. Hadi kufikia mwezi Machi 2010, kazi ya ufungaji wa mita 20,000 zilizopangwa kufungwa kwenye maeneo ya Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa Unguja na miji ya Chake-Chake, Mkoani na Wete kwa Pemba imekamilika. Katika hatua za kuendeleza ufungaji wa mita hizo za Tukuza, Shirika limenunua mita 1,700 za ziada kwa gharama ya Dola za Marekani 93,000.00 hivi karibuni na kwa sasa kazi ya ufungaji wa mita hizo mitaani unaendelea.

Lengo kuu la ufungaji wa mita hizo ni:-

1. Kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya mauzo ya umeme.
2. Kupunguza malalamiko na malimbikizo ya madeni kwa wateja.
3. Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wateja.

Aidha, kazi hii inaenda sambamba na kuongezeka kwa vituo vya kuuzia Umeme ili kuwapunguzia Wananchi masafa ya kufuata huduma, Shirika linatarajia kufungua rasmi kituo kipya cha Mwanakwerekwe na kuendeleza ujenzi wa kituo kipya katika eneo la Bububu.
Mradi wa Uimarishaji wa Shirika – kifedha (*Financial Turnaround):*

Mhe. Spika, mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Sweden, azma ya Mradi ni kuliandaa Shirika kuwa na uwezo wa kujiimarisha kifedha.

Mambo yaliyotekelezwa katika Mradi huu ni kama yafuatayo:-

1. Kununua mita zote zilizopangwa na mradi ili Shirika libadilishe mita mbovu kwa wateja.
2. Kufunga programu ya uwekaji hesabu za Shirika *(accounting software).*
3. Kulisaidia Shirika katika kupanga mipango yake ya muda mfupi na mrefu (*Business Plan)*
4. Kutoa mafunzo kwa wateja kuhusu ulazima wa kulipia matumizi yao ya umeme pamoja na kuwafunza wafanyakazi na uongozi wa Shirika kuhusu wajibu wao na njia bora za kufanya kazi zao za kila siku.

Mhe. Spika, utekelezaji wa kazi hizo za mradi zimetekelezwa kwa ufanisi mkubwa. Na hivi sasa Shirika linajivunia mafanikio yaliyopatikana na madi wa *FTA*. Wizara yangu inatoa shukurani za dhati kwa Serikali ya Sweden kwa msaada wao.

Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Pili kutoka Ubungo hadi Mtoni, Unguja

Mhe. Spika, mwaka jana wakati nawasilisha makadirio ya matumizi na mapato ya Wizara yangu niliwaarifu Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwamba mradi huu ulikuwa ukiandaa mipango ya kuwapatia maeneo mbadala wananchi watakaoathirika na mradi *(Resettlement Action Plan).*

Kazi hii ya kupanga mpango wa kuwafidia waathirika wa mradi ndio iliyochukuwa nafasi kubwa ya utekelezaji wa mradi huu tangu ulipotiwa saini ya utekelezaji wake mwezi wa Septemba 2008. Kutokana na utaratibu uliowekwa na *MCC*, waathirika wa mradi wanatakiwa wachaguwe moja kati ya njia mbili za kuwafidia nazo ni:

1. Kupatiwa fedha taslim Mhusika atalipwa fedha zake kwa mujibu wa thamani ya mali yake itakayoharibiwa wakati wa utekelezaji wa mradi.

2. Kupatiwa *(in-kind compensation)* Mhusika kupatiwa fidia ya nyumba kwa mujibu wa thamani ya jengo lake litakalobomolewa wakati wa utekelezaji wa mradi.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba kazi hiyo ya tathmini ya mali na mazao ya Wananchi tayari imeshakamilika kufanyiwa tathmini na hatua za malipo kwa wahusika zinategemewa kuchukuliwa katika mwezi wa Julai, 2010, kiasi cha Tsh Billioni 4 zimetengwa kwa ajili ya fidia hiyo. Mradi huu mpaka sasa umeshakamilisha kazi hizi zifuatazo:-

1. Mshauri tayari amekamilisha ripoti ya tathmini ya kazi ya ujenzi wa njia mpya ya kusafirishia Umeme na Vituo vyake.
2. Kuchaguliwa kwa mtengenezaji na mlazaji wa waya wa baharini, ambapo Kampuni ya *VISCAS* ya Japan ndio iliyochaguliwa baada ya kushinda zabuni na tayari utiaji wa saini na kampuni hiyo umeshafanyika katika Ikulu ya Zanzibar tarehe 30/04/2010.
3. Uchambuzi wa kumpata mkandarasi wa ujenzi wa vituo vya umeme vya Ubungo, *Ras Kiromoni*, *Ras Fumba* na Mtoni unaendelea.

Kuendeleza kazi ya kuvipatia huduma ya Umeme Visiwa vidogo vidogo

Mhe. Spika, nia ya Wizara yangu ni kuvipatia umeme visiwa vidogo vidogo vinavyoishi watu. Azma ya kuwapelekea umeme Wananchi wa Kisiwapanza mara tu baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa njia ya Umeme Tanga –

Pemba ipo pale pale, kilichochelewesha ni kuchelewa kukamilika kwa mradi huo. Tunawaomba Wananchi wa Kisiwapanza wawe na subira.

Mpango wa Umeme Mbadala

Mhe. Spika, katika kufanikisha mradi wa uzalishaji umeme kwa kutumia mawimbi ya bahari, hivi sasa kazi inayoendelea ni kufanyiwa upembuzi yakinifu wa kimazingira *(Environmental Impact Assessment)* katika maeneo ya Kiweni, Kusini Pemba na Mzambarauni Makunduchi Unguja. ili hatimae tuweze kusaini mkataba wa uzalishaji huo. Aidha Shirika la Umeme limo katika hatua ya kutiliana saini mkataba wa maridhiano (MOU) na Kampuni za *Nestor AB* ya Sweden na *Mbamba Marketing Consultant* ya Denmark kwa ajili ya kufanya utafiti wa njia mbadala ya nishati *(renewable power plants).* Vile vile zipo kampuni nyengine kama vile Anhui Tiankang (*group*), *Shares Co. Ltd* na *Alexandria Solutions* kutoka Marekani ambazo zimeonesha nia ya kushiriki katika kuekeza katika nyanja ya nishati.

Majenereta ya Akiba Kisiwani Unguja

Mhe. Spika, lengo la Serikali la kununua majenereta ya akiba limekamilika. Serikali hivi sasa imeagiza majenereta 32 yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa Megawati 25 yaliyogharimu Dola za Marekani (US$) Milioni 12.9 sawa na Tsh bilioni 17, fedha hizi zimetolewa na Wahisani wa Maendeleo pamoja na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Majenereta ya akiba yatawekwa katika kituo cha Umeme Mtoni - Unguja na kazi hio inatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi wa Juni, 2010.

Matengenezo ya Dharura Yaliyofanyika wakati wa kurejesha huduma ya umeme katika kisiwa cha Unguja huko Fumba na Ras – Kiromoni

Mhe. Spika, kama mnavyofahamu, kisiwa chetu cha Unguja kinapata huduma ya umeme kupitia waya uliopitishwa chini ya bahari kuanzia *Ras Kiromoni* Tanzania Bara hadi *Ras Fumba* Unguja. Kwa mara nyengine mnamo tarehe 10 Disemba, 2009 kisiwa hiki ghafla kilikosa umeme kulikotokana na kuungua kwa waya huo unaosafirisha umeme katika kituo cha Fumba.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kupitia Wizara yangu na Shirika la Umeme ilichukuwa juhudi kubwa kuhakikisha kuwa matengenezo yanayofanywa yanakuwa ya uhakika na ya haraka.

Mhe. Spika**,** mara baada ya tukio hilo, Wizara yangu kushirikiana na Shirika la Umeme tuliwasiliana na Kampuni ya *NEXANS* ya Norway watengenezaji wa waya huo kwa kuwataka ushauri wao wa kitaalamu ili hatua za matengenezo ziweze kuchukuliwa na kuirejesha huduma ya upatikanaji umeme hapa kisiwani. Wataalamu hao walipendekeza kubadilisha muundo wa sehemu

za mwisho za waya huo ambapo badala ya kutumia waya wa mafuta walipendekeza utumike waya mkavu (*XLPE*) katika sehemu zote mbili za Fumba na Kiromoni.

Mhe. Spika, kazi ya matengenezo ya waya huo ilianza mara baada ya kuwasili kwa vifaa vyote hapa nchini na hatimae kazi hiyo ilikamilika mnamo tarehe 8 Machi, 2010 na huduma ya umeme kurejea tena katika kisiwa cha Unguja.

Kazi ya matengenezo ya waya imeligharimu Shirika la Umeme Tsh 894,857,282.67,fedha ambazo kwa mara ya kwanza imetokana na vyanzo vya ndani bila ya kushirikisha Wafadhili.

IDARA YA UTAWALA WA ARDHI

Mhe. Spika, Idara ya Utawala wa Ardhi ina majukumu ya msingi ya kuimarisha usimamizi wa shughuli za Utawala wa Ardhi nchini kwa kusimamia matayarisho na mapitio ya Sera na Sheria mbali mbali zinazohusiana na masuala ya Ardhi pamoja na utekelezaji wake kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa kiutendaji katika sekta nzima ya ardhi ili hatimae lengo lililowekwa la kumaliza migogoro inayohusiana na matumizi ya Ardhi liweze kufikiwa pamoja na kusimamiwa. Aidha Idara hii ina jukumu muhimu la kusimamia Utawala wa Ardhi za Eka tatu. Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 Idara hii imeweza kutekeleza malengo iliyojipangia kama ifuatavyo:

Kusimamia Sera ya Ardhi
Mhe. Spika, idara imeendelea na kazi ya kufanya mapitio ya sera ya ardhi ambapo jumla ya vikao 5 viliandaliwa kwa ajili ya kazi za awali za mapitio na kuifanyia marekebisho Rasimu ya mwanzo ya Sera hiyo *(draft land policy document).* Vikao hivyo vilitayarishwa kwa kuijumuisha wataalamu wa ndani (watendaji) wa utayarishaji wa Sera hiyo vikiwa na lengo la kuirekebisha rasimu hiyo kulingana na michango mbalimbali ya kitaalamu ili Sera hiyo baadae iwasilishwe kwa washirika mbalimbali kwa kupata maoni yao kabla ya kuwasilishwa katika baraza lako tukufu kwa kujadiliwa.

Mapitio ya sheria mbali mbali za ardhi
Mhe. Spika, kwa upande wa mapitio ya sheria mbali mbali za Ardhi *(Legislation review)* Idara kwa kushirikiana na Idara nyingine za Ardhi imefanikiwa kufanya mapitio ya awali ya Sheria ya Umilikaji Ardhi *(land Tenure Act 1992)* na Sheria ya Uhaulishaji Ardhi *(Land Transfer Act 1994).* Hata hivyo Idara tayari imekamilisha Kanuni za Sheria ya Uhaulishaji Ardhi iliyopo.

Kusimamia Ardhi za Eka
Mhe. Spika, Idara imeendelea na juhudi zake za kulinda na kusimamia eka kwa kuendeleza kazi za uhakiki wa maeneo mbali mbali yaliyopatiwa eka tatu. Maeneo ambayo yamefanyiwa uhakiki kwa kipindi hiki cha mwaka wa fedha 2009/2010 ni Kianga, Dole, Bumbwisudi, Kizimbani na Mwakaje, ambapo maeneo yote hayo yapo wilaya ya Magharibi Unguja. Zoezi hili linatarajiwa kuendelea kwa maeneo ya Mfenesini, Kama, Maungani na Kisauni kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa fedha.

Kusimamia Maeneo ya Uwekezaji
Mhe. Spika, Idara imeendelea kusimamia maeneo ya uwekezaji pamoja na uhifadhi wa ardhi katika maeneo hayo kwa kushirikiana na Idara ya ardhi na usajili kwa kuendelea kutoa msukumo katika kuzingatiwa kwa Sheria za udhibiti na uchafuzi wa ardhi na mazingira katika maeneo ya mahoteli, viwanda na kilimo kwa mujibu wa mikataba ya ukodishwaji Ardhi. Kwa upande mwengine Idara kwa kushirikiana na Idara nyingine za Ardhi zimeandaa mpango maalum wa kufanya tathmini na kukusanya taarifa juu ya vitega uchumi ambavyo vinaendelea kufanya kazi bila ya maeneo yao kupimwa na kupatiwa mikataba ya matumizi ya ardhi *(Land Lease Agreements).* Hali hii itasaidia kuimarisha mfumo wa utawala wa ardhi hususan kwa maeneo ya uwekezaji pamoja na kukuza ukusanyaji wa mapato kwa Serikali.

Matatizo ya Utekelezaji
Mhe. Spika, katika kipindi cha utekelezaji cha mwaka wa fedha 2009/2010 Idara ya Utawala wa ardhi imekabiliwa na changamoto kama zifuatazo.

Ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuendeleza baadhi ya malengo tuliyojipangia kama vile kuendeleza kazi za mapitio ya Sera ya Ardhi. Kazi hii utekelezaji wake haukuwa wa kasi sana kutokana na ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuendeleza mikutano ya washirika na ile ya kamati za wataalamu *(task force).* Kimsingi kazi hii inahitaji fedha nyingi, zaidi tukizingatia kuwa raslimali ya ardhi inamgusa kila mtu katika nchi hii hivyo matayarisho ya sera hii yanahitaji ushirikishwaji wa washirika walio wengi ili mawazo yao na michango yao iweze kuzingatiwa kwa manufaa ya wananchi wote hapo baadae.

Tatizo jengine ambalo linaonekana kama ni kikwazo cha utekelezaji ni ukosefu wa watendaji wenye taaluma zinazohusiana na masuala ya ardhi, jambo ambalo linapelekea kutegemea watendaji wachache ambao vile vile wanategemewa kutekeleza kazi nyengine katika idara zao.

Mikakati ya Utekelezaji
Mhe. Spika, ili kukabiliana na Changamoto mbalimbali zilizojitokeza Idara tayari imeandaa mikakati ya kuweza kujikwamua katika masuala ya rasilimali watu na fedha. Kwa upande wa rasilimali watu idara imepanga kufanya kazi zake kiushirikiano na taasisi nyengine za ardhi, kwa zile kazi ambazo zinahitaji taaluma maalum. Kazi hizi zitakuwa zinatekelezwa kwa kuanzisha vikundi kazi *(task forces)* ya pamoja ya watendaji kutoka Idara tofauti. Kwa mfano kazi ya kusimamia maeneo ya uwekezaji itaishirikisha watendaji wa Idara ya Ardhi na Usajili na Upimaji na Mipango Miji, na kazi ya Kuandaa Sera ya Ardhi itashirikisha watendaji wa Idara zote za Ardhi na washirika wengine kutoka taasisi na asasi mbali mbali.

Kwa upande wa raslimali fedha Idara imeshindwa kupata fedha za kutosha kwa ajili ya utayarishaji wa Sera ya Ardhi hata hivyo Idara imewasilisha maombi maalum kupitia mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (*SMOLE*) pamoja na Mpango wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (*MKUMBITA*) kwa ajili ya kufanikisha malengo ya ukamilishaji wa Sera hiyo.

IDARA YA ARDHI NA USAJILI

Mhe. Spika, Idara ya Ardhi na Usajili ina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za ardhi hapa Zanzibar. Hii ikiwa ni pamoja na kuratibu na kusimamia ugawaji wa ardhi kwa matumizi mbalimbali yakiwemo uwekezaji na ujenzi wa shughuli za maendeleo kama vile makaazi na huduma, kuweka kumbukumbu zinazohusiana na shughuli za ardhi pamoja na kufanya uthamini (*valuation*) wa ardhi na mali inayoambatana nayo. Idara pia hutatua migogoro ya ardhi .

Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Idara iliendelea na kazi za kutekeleza malengo iliyojiwekea kama ifuatavyo:-

Ukusanyaji wa mapato
Mhe. Spika, Idara imeendelea na juhudi zake za ukusanyaji wa mapato. Kwa upande wa kodi ya ardhi kwa makampuni unaofanywa na Bodi ya Mapato kama wakala wa Wizara, idara imekuwa ikipokea taarifa kila mwezi kutoka bodi hiyo inayoonesha kiasi kilichokusanywa na wawekezaji waliolipa. Hadi kufikia mwezi Machi 31, 2010 Tsh 1,298,217,115.96 zimekusanywa kwa mchanganuo ufuatao:-.

Kodi ya Ardhi
Makadirio ni kukusanya Tsh 1,890,900,000 makusanyo yaliyofanywa hadi 31 Machi 2010 ni Tsh 1,295,556,115.96 sawa na asilimia 68.51 ya makadirio.Kati ya fedha hizo Tsh 1,275,081,715.96 ni makusanyo ya kawaida ya kodi ya ardhi

na Tsh 20,474,400 ni adhabu ya asilimia 10 iliyotozwa kwa mujibu wa sheria kwa wawekezaji waliochelewa kulipa kodi ya ardhi.

Fomu za maombi ya viwanja
Makadirio ni kukusanya Tsh 2,000,000 na makusanyo yaliyofanywa hadi Machi 31,2010 ni Tsh 2,661,000 sawa na asilimia 133.05 ya makadirio.

Usimamizi wa Ukodishaji Ardhi
Mhe. Spika, katika kipindi hicho jumla ya mikataba 58 ya ukodishaji ardhi ilitiwa saini na kupewa wawekezaji mbali mbali. Idara imeendelea kuchukua hatua za Kisheria dhidi ya wawekezaji wote wasioendeleza maeneo waliyokodishwa kwa kuifuta mikataba ya ukodishwaji Ardhi waliyopewa. Jumla ya mikataba 3 ya ukodishwaji Ardhi imeshafutwa kuanzia Julai 2009 hadi Machi, 2010.

Utayarishaji na Utoaji wa Hati
Mhe. Spika, zoezi la utayarishaji na utoaji wa hati pamoja na ubadilishaji wa hati za zamani na kupatiwa za kisasa zinazotolewa kwa mujibu wa sheria linaendelea. Jumla ya Hati za zamani 203 zimebadilishwa na waombaji kupatiwa hati mpya kwa mujibu wa sheria. Hati kwa maeneo mapya na maeneo mengineyo zimetolewa. Hati za muda *'Provisional Certificate of Right of Occupancy'* 807 zimetolewa kwa maeneo mbali mbali.

Kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu
Mhe. Spika**,** katika kuendeleza mfumo mpya wa uwekaji kumbukumbu za ardhi na kutumia njia za kisasa ili kurahisisha uwekaji na upatikanaji wa kumkumbu hizo Idara katika kipindi cha 2009\10, tayari imekusanya kumbukumbu katika maeneo ya *Mazizini Unit 34 (LD), Chukwani Unit 39 (HD*) na *Mombasa Unit 33, 32, 32B,* vile vile katika maeneo ya *Mwanakwerekwe Unit, 22, 21* na *Amani Magogoni Unit 20, Tunguu Unit (3,4,5,6,8,9 na 10)* na *Kijichi (Block A,B,C na D).*

Uthamini
Mhe. Spika, Idara ya Ardhi na Usajili katika mwaka wa fedha 2009/10 imeendelea na kazi zake za Uthamini kwa ufanisi mkubwa. Jumla ya kazi 9 zimekamilika na kukabidhiwa wenyewe, kazi hizo ni kutoka katika taasisi mbali mbali, kama inavyoonyesha Jaduweli Nambari 3

Jaduweli Nambari 3

TAASISI	**IDADI YA KAZI**
MAMLAYA YA MAJI	1
KAMISHENI YA WAKFU	1
WIZARA YA MAJI	3
OFISI YA CCM MKOA	1

CHUO KIKUU CHA TAIFA (SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR)	1
MAHAKAMA KUU	1
SHIRIKA LA UMEME	2
SHIRIKA LA MELI	1
BODI YA UHAULISHAJI ARDHI	109
JUMLA	**120**

Kuimarisha Udhibiti wa Ardhi

Mhe. Spika, katika kuimarisha udhibiti wa matumizi endelevu ya Ardhi Idara imewezesha kukipatia vitendea kazi kitengo husika na hivi sasa kinaendelea na kazi zake vizuri. Idara imefanya ukaguzi kwa ajili ya kuwatengenezea warka waombaji katika maeneo tofauti jumla ya maombi 279 yalikubaliwa,15 yalikataliwa kwa sababu mbali mbali. Idara imeweza pia kufungua kesi katika Mahakama ya Ardhi kutokana na uvamizi wa ardhi unaofanywa na wananchi kwa maeneo kadhaa. Vile vile Jumla ya maombi 18 ya Ukaguzi wa Miradi na maombi 12 ya ujenzi wa nyumba mpya yamefanyiwa ukaguzi.

Afisi ya Mrajis wa Ardhi

Mhe. Spika, Afisi ya Mrajis wa Ardhi imeendelea na utekelezaji wa shughuli zake za Usajili wa Ardhi nchini. Aidha zoezi la kumtambua na kumthibitisha mwenye haki ya matumizi ya Ardhi katika eneo la Mji Mkongwe uchukuaji na urejeshwaji wa fomu za maombi umefanikiwa kwa kiwango kikubwa. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Afisi ya Mrajis wa Ardhi imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

1. Kuendelea kuzichambua na kuthibitisha fomu zote za maombi ya kutambuliwa na kuthibitishwa kwa mwenyehaki ya matumizi ya ardhi katika eneo la utambuzi la mji Mkongwe.

2. Kutayarisha ramani inayoonyesha mipaka ya viwanja katika eneo la Mji Mkongwe ambayo itatumika kwa shughuli za usajili wa ardhi.

3. Kutangazwa kwa maeneo mengine ya Shehia za nga'mbo kuwa la utambuzi na uthibitishwaji wa mwenyehaki ya matumizi ya ardhi ambapo jumla ya shehia 13 zimeshatangazwa.

4. Idara imeshampatia Afisa Utambuzi *(Adjudication Officer)* Afisi pamoja na vifaa vya kufanyia kazi kwa ufadhili wa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (*SMOLE*)

5. Kitengo cha Utambuzi wa Mwenye haki ya matumizi ya ardhi inaendelea na kazi za kutoa fomu katika eneo la Ng‘ambo lililojumuisha shehia kumi na tatu 13 kama inavyoonekana katika Jadweli Nambari 4.

Jaduweli Nambari 4

Eneo la Utambuzi	**Fomu za maombi zilizochukuliwa**	**Fomu za maombi zilizorejeshwa**	**Fomu za maombi zisizorejeshwa**
GULIONI	462	225	237
MLANDEGE	281	182	99
MUEMBELADU	539	206	333
RAHALEO	354	200	154
MCHANGANI	216	195	21
VIKOKOTONI	418	195	223
MWEMBETANGA	319	193	126
KISIWANDUI	150	126	24
KISIMAMAJONGOO	380	150	230
KIKWAJUNI JUU	229	179	50
KIKWAJUNI BONDENI	405	294	111
MWEMBESHAURI	253	222	31
MIEMBENI	682	143	539
JUMLA YA FOMU	**4688**	**2,510**	**2,178**

Mhe. Spika, kwa upande wa Kisiwani Pemba shughuli za majaribio ya Usajili wa ardhi zilizokuwa zinafanyika huko Kiungoni kwa sasa zimesita. Shughuli hizo ambazo zilikuwa zinafadhiliwa na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) zimesita baada ya Wizara yangu kugundua kwamba viwango na taratibu za kazi za upimaji havikidhi haja

ya usajili wa ardhi kwa mujibu wa taratibu za usajili hapa Zanzibar pamoja na usimamizi mzima wa mpango huo kwa upande wa Zanzibar. Mazungumzo yanaendelea baina ya wataalam wa Wizara yangu na Uongozi wa MKURABITA kwa nia ya kukubaliana juu ya viwango na utaratibu sahihi wa kutumia ili kazi hio iendelee.

MAHAKAMA YA ARDHI

Mhe. Spika**,** upokeaji na usikilizwaji wa kesi za ardhi kwa Mahkama hadi kufikia Machi, 2010 jumla ya kesi 89 kwa Unguja na Pemba Kesi 82 zimefunguliwa. Maelezo ya kesi zilizofunguliwa na zilizopatiwa ufumbuzi ni kama ifuatavyo:-

Jadweli Nambari 5

Pahala	**zilizofunguliwa**	**Zilizofutwa na kutolewa hukumu**	**Zilizobaki**
Unguja	89	7	82
Pemba	82	12	70
Jumla	**171**	**19**	**152**

Mhe. Spika, katika kipindi cha fedha cha mwaka 2009/2010 mahakama ya ardhi imefanikiwa kupata maeneo na baadhi ya majengo katika Mikoa ya Unguja na Pemba. Madhumuni ya majengo na maeneo hayo ni kupeleka huduma za mahakama hizo karibu zaidi na wananchi, hivyo kila mkoa unatarajiwa kuwa na mahakama yake. Kazi ya ujenzi na matengenezo inatarajiwa kuanza mwaka ujao wa fedha.

Bodi ya Uhaulishaji Ardhi

Mhe. Spika**,** BODI ya Uhaulishaji Ardhi ya Zanzibar ilianzishwa rasmi mwezi wa Machi mwaka 2009 chini ya kifungu Nam. 9 na 11(1) cha Sheria ya Uhaulishaji Ardhi Nam 8 ya mwaka 1994 na kama ilivyofanyiwa marekebisho kwa Sheria No 10. ya mwaka 2007. Bodi ilianza kazi rasmi mara tu baada ya kuteuliwa Mwenyekiti wa Bodi na Katibu wake mnamo tarehe 05.03.2009 ikifuatiwa na kuteuliwa kwa wajumbe wa Bodi.

Shughuli za Bodi na Utekelezaji wake

Mhe. Spika**,** ki-msingi Bodi ya Uhaulishaji Ardhi ina kazi kupokea, kujadili na kupitisha maombi ya uhaulishaji Ardhi Zanzibar. Katika kuhakikisha hayo taratibu za Uhaulishaji zinawahusisha pia Serikali katika ngazi za Shehia na Wilaya ambapo ardhi inayohaulishwa ipo.Vilevile inawahusisha Mhaulishaji na Mhaulishiwaji kwa pamoja na inapobidi hata wahusika wenye manufaa ya karibu zaidi ya kinachohaulishwa kwa upande wa Mhaulishaji.

Kazi za Uhaulishaji Julai– Machi 2009-2010

Mhe. Spika**,** katika kutekeleza majukumu yake Bodi ya Uhaulishaji Ardhi imeweza kupokea maombi mbalimbali kwa upande wa Unguja na Pemba ambapo inaonekana wananchi wameanza kuhamasika na kuelewa umuhimu wa Bodi hii. Mtiririko wa maombi yaliyowasilishwa katika Bodi ya Uhaulishaji unaonekana katika Jaduweli nambari 6.

Jadweli Nambari 6

Mwezi	**Fomu zilizotolewa**	**Maombi ya yaliyokubaliwa**	**Maombi yaliyokataliwa**	**Hati zisizorejeshwa**
Julai	102	**18**	2	82
Agosti	80	11	1	68
Septemba	107	30	2	75
Oktoba	147	21	1	125
Novemba	117	17	2	98
Disemba	129	23	-	106
Januari	71	16	2	53
Februari	90	25	1	64
JUMLA	**843**	**161**	**11**	**671**

IDARA YA UPIMAJI NA MIPANGO MIJI

Mhe. Spika, jukumu kubwa la Idara hii ni kupanga, kusimamia na kuratibu kazi zote zinazohusiana na upangaji na upimaji wa maeneo mbalimbali nchini kwa madhumuni ya kuendeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi pamoja na utengenezaji wa ramani za ardhi.

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2009 hadi Machi 2010, Idara ilitekeleza majukumu yake hayo kama ifuatavyo :-

Ukusanyaji wa Mapato

Katika mwaka wa fedha 2009/2010, hadi kufikia mwezi Machi, 2010 Idara ya Upimaji na Mipango Miji imekusanya jumla ya Tsh 41,955,000 kati ya lengo la Tsh. 400, 000,000/=. Makusanyo hayo ni sawa na asilimia 10.49

Kuendelea na Kazi za Ukamilishaji wa Ramani za Visiwa vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kazi hii iliendelea, na karibu kazi nyingi za ukusanyaji wa taarifa zinazotumika katika utengenezaji wa ramani zinazopatikana kutoka katika picha za anga ulifanyika. Ukusanyaji wa taarifa hizo katika miji ya Chake-Chake, Wete, Mkoani, Mji wa Zanzibar na Mji Mkongwe umekamilika kwa asilimia mia moja.Kazi ya kukusanya taarifa zinazoonyesha mabonde na miinuko ya ardhi ya visiwa vya Unguja na Pemba nazo zimekamilika.

Kazi za uhakiki wa taarifa hizo zilizokusanywa iliendelea kwa kuyapitia tena maeneo mbalimbali ya miji hiyo kwa madhumuni ya kuingiza mabadiliko yaliyotokea baada ya kupigwa picha hizo za anga(field completion) katika miji na katika maeneo yote ya visiwa vyetu.

Kwa ujumla kazi hii imekamilika. Kazi iliyobakia kwa sasa ni kuzichapisha ramani hizo ili ziweze kuanza kutumika rasmi kwa matumizi mbalimbali yaliokusudiwa. Kwa wale wanaohitaji ramani mpya za visiwa vyetu wanaweza kuzipata baada ya kuwasilisha maombi Idarani.

Upimaji wa Viwanja 2000 vya Makaazi na Maeneo Mengineo

Mhe. Spika**,** kazi za upimaji wa maeneo ya makaazi, huduma za kijamii na vitega uchumi ziliendelea Unguja na Pemba. Hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2010 jumla ya viwanja 490 vimeshapimwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kama inavyoonekana katika jadweli zilizopo hapo chini.

Viwanja Vilivyopimwa Unguja:

Jadweli Nambari 7

MKOA	**MAKAAZI**	**BIASHARA**	**HUDUMA**	**TAASISI**	**MASHAMBA**	**JUMLA**
MJINI MAGHARIBI	64	24	12	11	39	**150**
KASKAZINI	78	6	3	10	16	**113**
KUSINI	46	12	4	8	19	**89**
JUMLA	**188**	**42**	**19**	**29**	**74**	**352**

Viwanja Vilivyopimwa Pemba
Jadweli Nambari 8

WILAYA	MAKAAZI	BIASHARA	HUDUMA	TAASISI	MASHAMBA	JUMLA
CHAKE	57	2	4	14	-	**77**
WETE	3	-	5	9	-	**17**
MICHEWENI	13	1	4	4	-	**22**
MKOANI	10	2	5	5	-	**22**
JUMLA	**83**	**5**	**18**	**32**	-	**138**

Aidha Idara inaendelea na upimaji viwanja 400 katika eneo la Tunguu Unguja. Viwanja hivyo vinatarajiwa kupatikana kabla ya kumalizika mwaka huu wa fedha.

Kuufanyia Mapitio Mpango wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi na Utayarishaji wa Ramani za Matumizi ya Ardhi za Wilaya za Unguja na Pemba

Mhe. Spika**,** katika utekelezaji wa kazi hii Idara inashirikiana kwa karibu na mradi wa MACEMP. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 lengo lilikuwa ni utayarishaji wa ramani za matumizi ya ardhi za Wilaya 9 za Unguja na Pemba. Kazi iliyokwishafanyika hadi sasa ni ukusanyaji wa taarifa za matumizi ya ardhi katika kila Wilaya kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali zinazotumia ardhi nchini. Taarifa hizo hivi sasa zinaendelea kufanyiwa uchambuzi na kuziweka pamoja ili ziweze kutumika katika mpango uliokusudiwa.

Hadi hivi sasa ripoti za mpango wa matumizi ya ardhi za Wilaya 4 tayari zimekamilika na zinasubiri kupata maoni ya washirika mbalimbali.

Upimaji wa Mipaka ya Mikoa na Wilaya

Mhe. Spika**,** kazi hii bado imo katika hatua za mwanzo za utekelezaji wake. Kazi kubwa iliyokwishafanyika hadi sasa ni utengenezaji wa mawe ya alama za mipaka (*beacons*). Hatua inayotarajiwa kuendelea sasa ni pamoja na uzikaji wa mawe hayo katika sehemu zinazohusika na hatimae upimaji wa mipaka hiyo. Kazi hii ikikamilika inategemewa kuleta faida kubwa ya kuondosha baadhi ya migogoro na matatizo ya mipaka iliopo Zanzibar.

Udhibiti wa Ujenzi Mijini na Vijijini

Mhe. Spika, Idara kwa kushirikiana na Baraza la Manispaa, Halmshauri za Wilaya pamoja na Mamlaka ya Vitega Uchumi (*ZIPA*) iliendelea na kazi za kutoa ushauri na miongozo kwa maombi mbali mbali ya ujenzi wa nyumba za makaazi na mahoteli. Madhumuni makubwa ya kazi hii ni kuhakikisha kwamba miji na vijiji vyetu vinaendelezwa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zote za ardhi na mipango ya miji ili kwenda sambamba na malengo ya Milenia ya kuimarisha makaazi na kupunguza umasikini .

Katika kipindi hiki Idara ilipokea jumla ya maombi 84 ya ujenzi wa nyumba mpya na matengenezo kutoka Baraza la Manispaa kwa ajili ya kupatiwa ushauri na miongozo ya kitaalamu.

Aidha Idara ilishirikiana na *ZIPA* na Kamisheni ya Utalii katika kupitisha ramani za ujenzi wa vitega uchumi katika maeneo ya uwekezaji hasa katika kanda za kitalii. Idara pia ilitoa maelekezo na kutayarisha ramani za mapendekezo ya matumizi mbalimbali ya ardhi katika sehemu tofauti nchini kufuatia maombi yaliyopokelewa moja kwa moja kutoka kwa wananchi, taasisi na wawekezaji.

Mhe. Spika**,** Idara ya Upimaji na Mipango ya Miji, mbali ya kuendelea na utekelezaji wa kazi zake za kawaida pia inashiriki katika utekelezaji wa Miradi ya *SMOLE, BEST* na *ZUSP*. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, utekelezaji wa miradi hiyo ulikuwa kama ifuatavyo :-

Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (*SMOLE*)

Mhe. Spika**,** mradi huu ulianza kutekelezwa kuanzia Mei, 2005 na utekelezaji wa awamu ya kwanza ulikamilika Aprili 2009, chini ya msaada wa Serikali ya Finland na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, awamu hii ya mwanzo iliongezewa muda na kumalizika Disemba 2009. Awamu ya pili ya mradi huu ilianza Januari, 2010 na inatarajiwa kumalizika Disemba 2013.

Lengo kubwa la mradi huu ni kupunguza umasikini kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa 2020 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar kwa kupitia sekta ya ardhi. Katika Dira na mkakati huo Usimamizi bora wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira ni vigezo vikubwa katika mikakati ya kupunguza umasikini.

Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha kazi zifuatazo zilitekelezwa:

1. Kuendelea na zoezi la kumtambua na kumthibisha mwenye haki ya matumizi ya ardhi katika shehia 13 za ng'ambo ili hatimae wapatiwe hati za matumizi ya ardhi ya maeneo wanayoyatumia na hatimae kusajiliwa.

2. Ununuzi wa vifaa na usafiri katika utendaji wa kazi za Idara zinazohusika na utekelezaji wa mradi huu.

3. Kuajiri Washauri Waelekezi wa kufanya kazi za ushauri katika nyanja mbali mbali za sekta zinazotaka kutekelezwa na mradi huu.

4. Kuendelea na kazi za kuhakiki matumizi ya eka tatu zilizogaiwa kwa wananchi ili kudhibiti matumizi mabaya ya ardhi hizo.

5. Kujenga paa jipya la jengo linalotumiwa na Idara za Ardhi hapo Forodhani.

Mradi wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (**MKUMBITA)**
Mhe. Spika, mradi huu unaratibiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi Zanzibar na unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Mradi umeshatayarishiwa mpango kazi *(work plan)* kwa kipindi cha mwaka mmoja cha awamu ya mwanzo *(phase I)* kwa kufuata mapendekezo ya Mshauri Mwelekezi. Awamu ya mwanzo ya mradi huu inajumuisha utayarishaji wa taarifa *(studies)* na Washauri Waelekezi watakaowezesha kuandaa mambo yafuatayo:-

1. Kuimarisha mfumo wa Sera ya Ardhi *(National Land Policy Framework)* hadi kufikia kupatikana kwa Sera. Hii itachangia juhudi zinazochukuliwa na Idara za Ardhi katika kutayarisha Sera ya Ardhi ya Zanzibar.

2. Kutayarisha mpango kazi wa kusajili ardhi *(Design of Land Registration Activities).*

3. Sera na taratibu za usajili wa ardhi kimazingira na kijamii. *(Policy framework for Land Registration)*

4. Taarifa za awali za kijamii na kiuchumi zinazohusu maeneo ya ardhi *(Socio-Economic Baseline Data).*

5. Kuanzisha kitengo cha kushughulikia mradi huu na kukipa uwezo wa kusimamia *(Establish Coordination Office/Capacity Building)*

Mhe. Spika, mradi huu umekwisha tayarisha hududi rejea *(Terms of Reference)* na kupata ruhusa "*No Objection*" kutoka Benki ya Dunia, kuwalika Washauri Waelekezi (*Consultants*) wataokuwa tayari kufanya kazi hizo.

Aidha ziliundwa kamati ndogo mbili kwa ajili ya kufanya tathmini (*evaluation*) kwa wale Washauri Waelekezi ambao waliwasilisha maombi yao. Kazi hiyo

ilifanywa kwa kushirikiana na wataalamu wa *'Crown Agents'* kutoka Dar-es-Salaam.

Mradi wa Zanzibar *Urban Service Programme* (*ZUSP*)
Mhe. Spika, mradi huu unaratibiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi na unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Mradi umeshatayarishiwa mpango kazi *(work plan)* ambapo mfadhili amekwisha tenga fedha kwa awamu ya mwanzo *(phase I).* Mradi unajumuisha kuangaliwa kwa matatizo makuu ya mji wa Zanzibar katika masuala mbali mbali kuanzia taasisi, migongano ya kisheria katika usimamizi mzima wa masuala ya mji nakadhalika. Kazi hii imekwisha kamilika na Mshauri Mwelekezi tayari amekabidhi ripoti ya mwisho *(Final Report*) Wizara ya Fedha na Uchumi, ripoti hiyo imeshawasilishwa Benki ya Dunia kwa kupata baraka zao.

Madhumuni ya Kitengo cha Ardhi katika Mradi huu ni kuimarisha huduma,miundo mbinu na Mazingira katika mji wa Zanzibar kwa kutayarisha mpango wa matumizi ya ardhi katika mji wa Zanzibar*(Structural Physsical Plan)* pamoja na Sera ya Kuendeleza Mji na kufanyia mapitio Sheria ya Mipango Miji ya Zanzibar 1955 na jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 2 zimetengwa kwa ajili ya gharama za Mradi.

Matatizo
Mhe. Spika, Idara inakabiliwa na changamoto nyingi katika utendaji wa kazi zake za kila siku. Baadhi ya changamoto hizi ni pamoja na ukosefu wa vyombo vya usafiri, upungufu wa wataalamu, ukosefu wa maeneo ya upimaji wa viwanja.

MALENGO YA UTEKELEZAJI KWA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2010/2011

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Idara ya Mipango na Sera inakusudia kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ifuatayo:

1. Usambazaji Maji Vijijini
2. Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini
3. Mradi wa Kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji
4. Mradi wa maji na usafi wa Mazingira. (*AfDB*)
5. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Michenzani na Mpapa
6. Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini.
7. Mradi wa Kuweka Line ya Pili ya Umeme Ubungo hadi Mtoni (*MCC*)
8. Mradi wa Kufunga Mita 10,000 za TUKUZA Unguja na Pemba
9. Mradi wa Kuimarisha Shirika la Umeme (*FTA*)

10. Mradi wa Utekelezaji wa Sera ya Nishati.
11. Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (*SMOLE*)
12. Mradi wa Kuijengea Uwezo Idara ya Mipango na Sera
13. Miradi wa Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Bahari.
14. Mradi wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Kupitia Sekta ya Ardhi (MKUMBITA)

Mhe. Spika**,** Idara pia itajiimarisha zaidi katika kusimamia ipasavyo ukusanyaji wa mapato ya taasisi za Wizara hii sambamba na kupambana na changamoto zinazoikabili Wizara yangu katika ukushanyaji wa mapato hayo . Aidha Wizara pia itahakikisha kwamba matumizi yote ya fedha za Wizara hii zikiwemo za Serikali na za washirika wa maendeleo yanafanywa kwa kufuata taratibu na Kanuni za fedha nchini kwa mujibu wa sheria zinavyoelekeza.

Mhe. Spika, kuhusu suala la ukusanyaji wa takwimu, Wizara inakusudia kuhakikisha upatikanaji wa takwimu sahihi kwa kuyafanyia mapitio madodoso yanayotumika katika kutowa taarifa za takwimu hizo kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Shehia pamoja na kuanzisha mfumo ya "*Data base*" ya takwimu za mafuta yanayoingizwa hapa nchini.

Kwa upande mwengine Wizara yangu kupitia Idara hii itaendeleza, itaimarisha pamoja na kukuza mashirikiano kati yake na nchi marafiki, Waheshimiwa Mabalozi wa nchi mbali mbali wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini, mashirika ya maendeleo ya ndani na nje pamoja na washiriki wengine mbali mbali wa maendeleo wa Kitaifa na Kimataifa kwa shabaha ya kuleta mafanikio ya kimaendeleo katika sekta za Maji Ujenzi Nishati na Ardhi hapa Zanzibar.

Mradi wa Kuijengea Uwezo Idara ya Mipango na Sera

Mhe. Spika, lengo moja kuu la mradi huu kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ni kuendeleza hatua za ujenzi wa jengo jipya la Wizara ambalo litakuwa ni la kisasa na litakidhi haja kwa mujibu wa mahitaji kutokana na ukweli kwamba jengo tunalotumia hivi sasa sio tu ni la zamani bali pia halilingani na mahitaji ya sasa kwa mujibu wa mazingira ya utekelezaji wa kazi zetu. Kwa kutumia michoro/ramani na thamani ya jengo ambayo itatolewa na Mshauri Mwelekezi(kazi inayoendelea kwa sasa), kazi inayotarajiwa kutekelezwa katika mradi huu ni kuuwasilisha kwa washirika wa maendeleo kwa madhumuni ya kupata mshirika ambaye atashirikiana na Serikali katika kufikia lengo la ujenzi huo.

Kwa upande mwengine,lengo kuu la pili ni hatua ya kuijengea Wizara hii uwezo wa kukabiliana na majukumu yake makubwa hasa katika uwanja wa Mafuta na Gesi Asilia kwa kuendeleza jitihada za kutafuta nafasi za masomo kwa wataalamu wake na kuwaelimisha washirika wote wa ndani katika suala hilo.Vile

vile Idara kwa upande mwengine itaendeleza mazungumzo kati yake na washirika mbalimbali wa maendeleo ambao wameshaanza kuonesha nia kuhusu msimamo wao juu ya uwezekano wa kuifadhili sehemu ya mradi huu wa kujenga uwezo inayohusu ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kutendea kazi na ufuatiliaji ambapo "*Project Proposal*" ya mradi huu ipo tayari kwa kuwasilishwa kwa wafadhili. Jumla ya Tsh. Milioni 120 zinaombwa kutoka Serikalini kwa kukamilisha malengo hayo makuu.

Kusimamia Ufanisi na Ukamilishaji wa Sera, Sheria na Kanuni za Taasisi za Wizara

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Idara ya Mipango na Sera katika mwaka wa fedha 2010/11, imejipanga na kuanzishwa kwa Kitengo kipya cha kusimamia Ufuatiliaji na Tathmini ya ufanisi *(Monitoring and Evaluation Unit)* wa majukumu yake. Kitengo hichi kitaimarishwa kufikia ngazi ya Idara ili kutoa uwanja wa kupatikana kwa taarifa sahihi na za uwazi wa utekelezaji wake.Vile vile, Wizara hii imejipanga katika ukamilishwaji wa Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali kama ifuatavyo:-

1. Sera ya Ardhi
2. kukamilisha Sheria ya "*Condominium*"
3. Mapitio ya Sheria ya Uhaulishaji Ardhi na Sheria ya Umilikaji Ardhi
4. Utayarishaji wa kanuni za Sheria ya Mamlaka ya Mji Mkongwe

MAMLAKA YA MAJI

Mhe. Spika, Mamlaka ya Maji Zanzibar imepanga kutekeleza miradi ifuatayo kwa mwaka wa fedha 2010/2011

1. Usambazaji wa Maji Vijijini;
2. Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini;
3. Maji na Usafi wa Mazingira; na
4. Kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji.

Usambazaji wa Maji Vijijini.

Mhe. Spika, **w**izara yangu itaendelea na kazi za kusambaza maji katika maeneo ya vijiji mbali mbali ambavyo havikuweza kukamilishiwa ujenzi wake kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na pia kutanua huduma hiyo kwa maeneo mapya. Maeneo yatakayohusika na kazi hizo ni pamoja na Tumbatu, Miwani, Kangagani, Ziwani, Fuoni, Matuleni, Michamvi, Jumbi, Shumbavyamboni, Kisiwani, Kojani, Kisiwapanza, Makoongwe, Mtambwe Kaskazini, Fumba, Kizimkazi, Ubago na Chaani kubwa.

Mhe. Spika**, w**izara yangu inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh milioni 318 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu utakaowahudumia wananchi walioko vijijini kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mradi Wa Mfenesini - Bumbwini

Mhe. Spika, mradi huu ambao unatekelezwa katika vijiji vya Shehia 17 za Mfenesini, Kama, Chuini Mwakaje, Mbuzini, Kitope, Mkadini, Kiombamvua, Matetema, Mbaleni, Fujoni, Mangapwani, Kidanzini, Misufini, Makoba, Zingwezingwe na Mahonda unatarjiwa kumalizika katika mwaka 2010/2011. Ili kukamilisha majukumu ya Serikali katika mradi huu, Wizara yangu inaliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Tsh milioni 66. Ujenzi wa visima 2 vilivyobaki kati ya visima 3 vilivyochimbwa, kununua pampu 2 kwa ajili ya visima hivyo, kukamilisha ujenzi wa tangi kwa kufunga mabati ya juu na kumalizia ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 20 hadi 53.

Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira

Mhe. Spika, mradi huu utatekelezwa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa vijijini walioko katika maeneo ya Nungwi, Matemwe, Machui na Dunga Tunguu kwa upande wa Unguja pia maeneo ya Ndagoni, Mizingani, Wambaa, Kambini-Mchangamdogo na Vitongoji kwa upande wa Pemba. Aidha katika maeneo ya miji, mradi utatekelezwa kuhudumia wakaazi wa maeneo ya Chake-Chake, Mkoani na Wete. Matatizo yaliyosababisha kuchelewa kwa kuanza kwa mradi huu katika mwaka wa 2009/2010 tayari yamepatiwa ufumbuzi baada ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) kutoa ridhaa ya kuendelea na kazi za kuwapata washauri waelekezi wa kazi za usanifu na usimamizi wa mradi. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Wizara yangu inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tsh 1,532,000,000 kama ni mchango wa Serikali katika ujenzi wa mradi huo.

Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini

Mhe. Spika, mradi huu unatarajiwa kuendeleza hatua za kutanua huduma ya maji katika maeneo mapya na kuimarisha mitandao katika maeneo ambayo huduma ya maji haipatikani vizuri. Wizara yangu inaomba jumla ya Tsh milioni 256 kwa ajili ya kuendeleza hatua za usambazaji maji katika maeneo mbali mbali ya mkoa wa Mjini Magharibi pamoja na miji ya Chake-Chake, Wete na mkoani.

Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji

Mhe. Spika, mradi huu wa kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji pamoja na shughuli za kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake na pia vitendea kazi unalo jukumu la kuimarisha ukusanyaji wa mapato ili Mamlaka iweze kujitegemea. Katika kukuza kiwango cha mapato, Serikali imetakiwa kufunga mita za maji kwa watumiaji ili walipie kutokana na kiwango halisi cha maji wanayotumia.

Mapato na Matumizi

Mhe. Spika**,** wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji, imejipangia kukusanya jumla ya Tsh Bilioni 1.5, fedha ambazo zitatokana na vyanzo mbali mbali vya ndani vya mapato vya Mamlaka kama vile mauzo ya maji, mauganisho ya maji, huduma za uchongaji vipuri n.k. Fedha hizo zitatumika kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Mamlaka ya Maji inatarajia kutumia jumla ya Tsh bilioni 4.05 kwa kazi za maendeleo na Tsh. bilioni 6. 5 kwa kazi za kawaida ikiwemo ruzuku kutoka Seriklaini.

IDARA YA UJENZI

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Idara imejipanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

1. Kuendeleza shughuli za usajili wa wataalamu pamoja na wakandarasi visiwani kwa kupitia Bodi zetu mbili, (Bodi ya Kusajili Wasanifu Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na Bodi ya Wakandarasi) Kuhakikisha shughuli zote za ujenzi zinafanywa na Wataalamu husika na katika viwango vilivyokubaliwa ili kuepusha ujenzi holela na wa viwango visivyokubalika nchini.
2. Kumaliza kazi za mwisho za jengo la Mpapa ikiwa ni nyumba ya mwisho kwa hivi sasa katika mradi wa nyumba za Maendeleo, pamoja na kuendeleza ujenzi wa maegesho ya magari (*parking*) katika nyumba nne za Michenzani. Bloki nambari 1, 5, 6 na 9.

3. Kuendeleza ujenzi wa Mahkama za Ardhi (Mkoa wa Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba nk)

4. Kuendelea na mikakati yake ya kuimarisha huduma ya ujenzi bora,salama na bei nafuu kwa kuzingatia utaalamu wa kisasa kwa kuelimisha jamii na wataalamu wa ujenzi nchini kwa njia ya mikutano,warsha, vipeperushi, magazeti,vyombo vya habari n.k

5. Kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo,taasisi za fedha na Serikali kuu, kutafuta njia mbadala ya kuandaa mpango wa kugharamia ujenzi wa nyumba za kuishi *(Soft loan Program for Building Construction Industry)* ili wananchi waweze kutumia fursa hizo katika kujipangia na kutekeleza ujenzi wa nyumba bora, salama na bei nafuu hapa nchini.

Mhe. Spika, wizara yangu inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh milioni 374 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

IDARA YA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAAZI

Mhe. Spika, Idara hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011 inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuendelea na zoezi la kuwalipa fidia wale wote waliovunjiwa nyumba zao kwa ajili ujenzi wa nyumba za maendeleo.

2. Kuzifanyia matengenezo Nyumba za Serikali Unguja na Pemba.

3. Kukamilisha Sheria ya '*Condominium*'.

4. Bodi ya Kudhibiti kodi za Nyumba kuendelea kupokea na kutoa maamuzi ya mashauri yanayowasilishwa.

5. Kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi za Nyumba za Serikali.

6. Kuendelea na zoezi la Uuzaji wa Nyumba za Vijiji na Mijini Unguja na Pemba.

MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE

Mhe. Spika**,** Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011 inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuandaa kikao cha kwanza cha washirika baada ya Sheria ya Mamlaka kupitishwa katika Baraza la Wawakilishi na kuandaa utaratibu wa mfuko wa dharura wa matengenezo ya majengo

2. Kutengeneza vitabu vya Sheria baada ya kupitishwa na Baraza la Wawakilishi na kufanya mapitio ya kanuni (*regulations*) za uhifadhi

3. Kuwa na mfumo mmoja wa mabango ya afisi za Serikali zilizopo katika eneo la Mji Mkongwe, na kuondosha sehemu za matengenezo ya magari.

4. Kuendeleza kazi za kutathmini matumizi ya maeneo ya wazi iliyokuwa ikifanywa kwa mashirikiano na Chuo Kikuu cha Minnesota.

5. Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu na kusimamia miradi ya uhifadhi wa majengo.

6. Utayarishaji wa utaratibu wa kutanganza matamasha katika eneo la Mji Mkongwe na udhibiti wa matangazo hayo kwenye kuta za majengo *(posters).*

7. Kutayarisha mkutano wa mwaka kwa miji ya urithi wa ulimwengu (*OWHC*) kwa kanda ya Afrika ya Mashariki

8. Kuandaa maadhimisho ya siku mashuhuri za Kimataifa kama vile siku urithi duniani na siku ya mshikamano wa Miji ya urithi wa Kimataifa.

9. Kuendelea kujenga uwezo wa wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi 8, Aidha kutoa elimu ya umma kuhusu uhifadhi wa Mji Mkongwe kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali.

IDARA YA NISHATI NA MADINI

Mhe. Spika, Idara ya Nishati na Madini katika mwaka wa fedha 2009/2010 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

1. Kuandaa Mpango wa utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Zanzibar kuanza na utekelezaji wa mikakati hiyo.
2. Kuendelea na juhudi za kuwapatia elimu juu ya matumizi ya umeme wa jua ili wananchi wa Unguja na Pemba wapate kutumia huduma hiyo.
3. Kushiriki kikamilifu katika masuala yote ya nishati ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.
4. Kuendelea kusimamia upatikanaji wa mafuta Zanzibar (Dizeli, Petroli na Mafuta ya taa).
5. Kutunga Sheria juu ya kusimamia 'Depot' za mafuta za Serikali na kuhakikisha kuwa Depot hizo zinachangia Idara ya Nishati na Mfuko Mkuu wa Serikali.
6. Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kuandaa programu ya mafunzo ambayo itasaidia Idara ya Nishati na Madini pamoja na Wizara kwa ujumla.
7. Kushirikiana na washirika wa Maendeleo katika kutekeleza programu ya mafunzo ya Mafuta na Gesi asilia.
8. Kushirikiana na Serikali ya Norway katika utekelezaji wa kazi ya tathmini ya mazingira ya Zanzibar *(Strategic Environmental Impact Assessment)* tathmini itakayotoa muelekeo wetu kwenye sekta ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

SHIRIKA LA UMEME

Mhe. Spika, **s**hirika kwa mwaka wa fedha 2010/2011 limelenga kuwapatia huduma bora Wananchi wa Visiwa hivi kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

Matumizi na Mapato
Mhe. Spika, shirika linatarajia kutumia Tshs. 41,681,015,241.00 kwa kazi za uendeshaji na maendeleo. Vile vile linakadiria kukusanya jumla ya Tshs. 47,898,381,000.00 Kati ya fedha hizo, Tshs. 44,789,742,000.00 zinatokana na mauzo ya umeme na Tsh. 3,108,639,000.00 zinatarajiwa kukusanywa kutokana na mapato mengineyo. Shirika limepanga kupata faida ya uendeshaji ya Tshs. 6,217,365,759.00.

KAZI ZA MAENDELEO

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/11 Shirika limepanga kuendeleza miradi ya maendeleo ifuatayo:-

Mradi wa Ujenzi wa njia ya pili ya Umeme Unguja
Mhe. Spika, lengo kuu la Wizara yangu kuendelea kusimamia kwa karibu sana hatua zinazoendelea za maandalizi ya ujenzi wa njia ya pili ya kusafirishia umeme na kuhakikisha unatekelezwa bila ya kukwama. Shirika la Umeme "*ZECO*" na Shirika la Ugavi Umeme Tanzania Bara "*TANESCO*" zitahakikisha zinafikia makubaliano ya ununuzi wa umeme na kuzidisha mashirikiano ya pamoja katika kufanikisha ujenzi wa njia ya pili ya umeme kwa wakati na ufanisi mzuri. Aidha, Wizara itahakikisha kwamba wananchi watakaoathirika na ujenzi huo wanalipwa haki zao kabla ya kazi ya ujenzi kuanza rasmi. Mtiririko wa fidia ni kama unavyoonekana katika jaduweli iliopo chini.

Jadweli Nambari 9

Tathmini	**Gharama (TShs)**
Mali zote zilioko upande wa magharibi mwa njia ya kusafirishia umeme mkubwa *(132kV)*	2,624,405,175.00
Mali zote zizioko upande wa mashariki mwa njia ya kusafirishia umeme mkubwa *(132kV)*	2,156,464,958.00
Uhamishaji wa njia za kusambazia umeme wa 33kV na *11kV* kutoka upande wa magharibi kwenda mashariki mwa njia inayosafirishia umeme mkubwa wa *132kV*	310,000,000.00
JUMLA	**5,090,870,133.00**

Kutokana na utaratibu wa *MCC*, gharama za fidia upande wa magharibi mwa njia inayotumika hivi sasa zitalipwa na *MCC*, fedha hizo ni TShs. 2,624,405,175.00.

Hivyo, fedha zilizobaki Tshs. 2,466,464,958.00 zitalipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo maombi ya fedha hizi yameshawasilishwa Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, jumla ya wananchi 843 wataathirika katika utekelezaji wa Mradi huu, kati ya waathirika hao Wananchi 322 ni wamiliki wa majengo na Wananchi 521 ni wamiliki wa miti ya muda mrefu na mazao ya mwaka katika shehia zifuatazo:-

Fumba, Dimani, Kombeni, Maungani, Kijito Upele, Meli Nne, Mwanakwerekwe, Pangawe, Magogoni, Welezo, Mto Pepo na Karakana.

Orodha ya Misikiti na Madrasa zitakazolipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kama inavyoonekana katika jaduweli nam.10

Jaduweli nam. 10

Jina La Msikiti/Madrasa	**Mtaa/Shehia**	**Tathmini**
Twarikatul Kadiria Mosque	Mwanakwerekwe	46,513,000.00
Madrasa and Nursury School	Mwanakwerekwe	30,683,000.00
Madrasatul Qadiria	Welezo	10,912,000.00
Almadrasatul- Muttaqina	Welezo	21,555,000.00
Almadrasatul Islamiya	Welezo	4,230,000.00
Almadrasatul Hizbullah	Welezo	20,416,000.00
Madrastul Swaaghiriina	Welezo	3,450,000.00
Almadrasatul Huda	Welezo	15,622,000.00
Almadrasatul Maswaabihil Huda	Welezo	13,200,000.00
Idd-taidia Mosque	Mto Pepo	54,300,000.00
Almadrasatul Nuurul Huda	Karakana	10,650,000.00
Almadrasatul Tawba	Karakana	24,080,000.00
JUMLA		**255,611,000.00**

Mhe. Spika, baada ya kukamilika kwa utiaji saini na mjenzi na mlazaji wa waya wa baharini "*submarine cable"* ambae ni Kampuni ya *VISCAS CORPORATION* kutoka JAPAN, hatua za utekelezaji wa makubaliano ya mkataba huu zinatarajiwa kuanza rasmi tarehe 10 Juni, 2010.

Ifuatayo ni ratiba ya utekelezaji wa makubaliano ya ujenzi na ulazaji waya wa baharini:-

1. Matayarisho na kuanza utekelezaji tarehe 14/06/2010 – 28/01/2011
2. Utengenezaji wa waya tarehe 03/01/2011 – 10/01/2012
3. Usafirishaji wa waya kutoka Japan hadi Zanzibar tarehe 10/01/2012 – 08/05/2012
4. Kazi za ujenzi *(civil works)* tarehe 02/02/2012 – 31/05/2012
5. Ulazaji wa waya baharini tarehe 02/01/2012 – 17/05/2012

Mhe. Spika, kazi ya uchambuzi wa zabuni ya kumtafuta mjenzi wa vituo vya kupokelea umeme *Ras-Kiromoni* na *Ras-Fumba* kwa upande wa kiufundi imeanza rasmi tarehe 10/05/2010 na inatarajiwa kukamilika tarehe 17/06/2010.

Baada ya kukamilika uchambuzi wa kiufundi, kazi ya kufanya uchambuzi wa kifedha itaanza rasmi tarehe 21/06/2010 na inatarajiwa kukamilika tarehe 30/06/2010.

Kazi ya utiaji sahihi wa makubaliano ya ujenzi wa vituo vya kupokelea umeme (*Substations*) kati ya Mshindi wa Zabuni na Msimamizi Mkuu wa Mradi, *Millennium Challenge Account*- Tanzania inatarajiwa kutekelezwa mwishoni mwa mwezi wa July, 2010.

Mhe. Spika, zabuni za utafutaji Kampuni ya ujenzi wa njia za nchi kavu za Kusafirishia umeme mkubwa *(132kV)* kutoka Ubungo hadi *Ras-Kiromoni* na *Ras-Fumba* hadi Mtoni zinatarajiwa kutangazwa mwanzoni mwa mwezi Julai, 2010.
Kutokana na utaratibu uliowekwa, ujenzi wa njia za Nchi kavu ndio ujenzi wa mwisho utakaofanywa katika utekelezaji wa mradi ili kuepuka hasara ya kujenga njia hizo na kuendelea kusubiri ulazaji waya wa baharini na vituo vya kupokelea umeme (*Substations*)

Mradi wa Usambazaji Umeme
Mhe. Spika. shirika limejipanga kuhakikisha kwamba kazi ya kuvipatia umeme vijiji vilivyobaki zinaendelea kutekelezwa kwa upande wa Unguja na Pemba. Vijiji vinavyotegemewa kusambaziwa umeme katika mwaka ujao wa fedha ni pamoja na Kidimni, Koani, Mkanyageni, Kiongwe Kidogo, Mgambo, Cheju, Ghana, Kiboje, Dongongwe, Shakani, Nyamanzi, Kombeni, Bweleo, Dimani, Uzi Ng'ambwa, Mbuzini, Pongwe Mwera na Manyame kwa upande wa Unguja na kwa Pemba ni vijiji vya Msengele, Mgeni nje, Uwondwe, Makumbi, Maungweni, Simaungwe, Wambaa, Pujini, Kilindi, Miburani, Kiongoni, Madiwani, Chanjaani, Matangatuwani, Finya, Kwalegongo, Shumindu, Kivugo, Shengejuu, Kunguni, Ngezi, Mgagadu, Kuyuni, Maweni na Jemele. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya umeme vijijini ni Tsh 1.5 bilioni.

Mradi wa Ufungaji wa Mita za Tukuza
Mhe. Spika, kama nilivyoeleza wakati wa kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa kazi za mradi huu kwa mwaka wa fedha 2009/2010, nilieleza lengo kuu la ufungaji wa mita hizo. Shirika kwa mwaka ujao wa fedha limejipanga kuendelea na ununuzi na ufungaji wa mita hizo Unguja na Pemba. Jumla ya mita 10,000 zimepangwa kufungwa katika mwaka ujao wa fedha. Fedha zilizotengwa kwa utekelezaji ni Tsh 1.138 bilioni.

Aidha katika kuwarahisishia wananchi huduma ya ununuzi wa umeme wa TUKUZA, shirika limeongeza kituo cha manunuzi hayo hapo Mwanakwerekwe na pia Shirika lina mpango wa kuongeza vituo katika maeneo ya Kilimani, Mkokotoni na Gamba kwa upande wa Unguja na maeneo ya Konde na Mtambile kwa upande wa Pemba. Fedha zilizotengwa kwa utekelezaji ni Tsh milioni 170.

Kuendeleza Mpango wa Upatikanaji wa Umeme Mbadala
Mhe. Spika, wizara yangu itashirikiana na Shirika la Umeme (*ZECO*) kuendeleza mpango wa upatikanaji wa fedha kwa Wahisani wa Maendeleo kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Nishati ya upepo. Aidha, Shirika litaendelea kufuatilia kwa karibu Kampuni ya *SDE* Zanzibar Ltd, kuitaka ianze kazi ya ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme kwa njia ya mawimbi ya bahari huko Kiweni - Pemba na Mzambarauni huko Makunduchi - Unguja.

IDARA YA UTAWALA WA ARDHI

Mhe. Spika, Idara hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011 inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuendelea kusimamia mapitio ya Sera ya Ardhi, pamoja na kusimamia mapitio ya Sheria za Ardhi.
2. Kuendelea kulinda mustakbal wa eka kwa kuhakikisha kwamba eka zinatumika kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa.Ili kuona lengo hili linafanikiwa Idara itaendelea na uhakiki wa matumizi ya eka tatu'.
3. Kuendelea kusimamia maeneo ya uwekezaji ili kuhakikisha matumizi ya ardhi katika maeneo hayo yanaendelezwa kulingana na miongozo ya mipango ya matumizi ya ardhi.
4. Kuendelea kushirikiana na taasisi nyengine ili kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ukodishaji ardhi na ya utayarishaji mikataba ili kuimarisha mapato ya Serikali.

IDARA YA ARDHI NA USAJILI

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Idara ya Ardhi na Usajili ina malengo yafuatayo:-

1. Kuendelea na kubadilisha hati za zamani kwa kuwapatia wananchi hati mpya,aidha kutoa hati mpya kwa watakaopewa viwanja.

2. Kuendeleza uwekaji wa kumbukumbu za viwanja kwa njia za kisasa.

3. Kuendelea na kuimarisha shughuli za Mahkama ya Ardhi kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi nchini kwa haraka na kushirikiana na Idara ya Mahakama Kuu Zanzibar katika kuwapata mahakimu watano wa Mahkama hiyo ambao bado hawajapatikana. Kuanza ujenzi wa Mahkama za Ardhi kwenye Mikoa.

4. Kuendelea na Utambuzi na uthibitishaji wa mwenye haki ya matumizi ya ardhi ndani ya shehia za N'gambo ya mji wa Zanzibar na huko Pemba na kuanza shughuli za Usajili wa ardhi kwa maeneo ambayo zoezi la utambuzi zimekamilika.

5. Kuendelea kusimamia shughuli za Ukodishwaji wa ardhi *(Land leases)* nchini.

6. Kuimarisha Udhibiti wa Umilikaji wa matumizi endelevu ya Ardhi na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaovamia ardhi.

7. Kusimamia shughuli za Uendelezaji wa Bodi ya Uhaulishaji Ardhi.

8. Kuendeleza kitengo pamoja na shughuli za Uthamini wa ardhi nchini

9. Kushirikiana na Bodi ya Mapato Zanzibar katika kuendeleza juhudi za ukusanyaji wa mapato ya kodi za ardhi.

10. Kushughulikia mpango wa mafunzo katika ngazi ya shahada ya kwanza katika taaluma za usimamizi wa Ardhi.

IDARA YA UPIMAJI NA MIPANGO MIJI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Idara ya Upimaji na Mipango ya Miji inakusudia kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuanza kuzifanyia mapitio (*revision*) ramani mpya za Zanzibar;

- Kupima viwanja vya makaazi, huduma na mashamba Unguja na Pemba;

- Kuendelea na kazi ya upimaji wa mipaka ya Wilaya na Mikoa;

- Kuendelea na kazi za udhibiti ujenzi kwa kushirikiana na taasisi nyengine za Serikali;

- Kuendelea kutayarisha ramani za mapendekezo ya matumizi ya ardhi yatakayotokana na maombi mbali mbali kutoka kwa wananchi na taasisi mbali mbali; na

- Kuendelea kutayarisha ramani za kina (*detail plans*) za matumizi ya ardhi katika vijiji vya ukanda wa pwani kwa kushirikiana na mradi wa *MACEMP*.

Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (*SMOLE*)

Utayarishaji wa mfumo wa taarifa za ardhi *(Land Information System).*

1. Utayarishaji wa miongozo ya ujenzi na uendelezaji wa miji
2. Kufanyia mapitio Mpango wa Kitaifa wa Matumizi ya Ardhi kwa kuwashirikisha washirika mbali mbali na wataalumu wa nje.
3. Kuendelea kuzisaidia Idara zinazotekeleza kazi za mradi huu kwa kuzipatia vitendea kazi mbali mbali.

Mhe. Spika, wizara yangu inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh milioni 200 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mradi wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (*BEST*)

1. Kutayarisha Sera ya maendeleo ya miji.
2. Kutayarisha mpango wa usimamizi na usajili wa Ardhi kwa maeneo yote ya miji na vijiji.
3. Kuifanyia mapitio Sheria ya Mipango Miji na Vijiji.

HITIMISHO

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwa mara nyingine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuitumikia nchi yangu kwa kipindi cha miaka kumi kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara yangu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mashirika ya Kimataifa na yasiyo ya Kimataifa, Sekta binafsi, *NGO's, CBO's* na wananchi

kwa jumla kwa mashirikiano mazuri na Wizara yangu kwa misaada yao ya hali na mali waliyoitoa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yangu. Washiriki hao ni pamoja SWEDEN, NORWAY, JAPAN, MAREKANI, UINGEREZA, CHINA, EGYPT, FINLAND, *UNICEF*, *UNESCO*, *UNDP*, *DFID*, *JICA*, *Sida*, *DED*, *UN HABITAT*, *AfDB*, *AGAKHAN FOUNDATION*, *TASAF*, *AL-YOUSEIF CHARITABLE SOCIETY*, *ZATI*, *IFA*, *RENCO*, ANGOZA, TUME YA UKIMWI ZANZIBAR, *NORAD*, *RED CROSS*, *ACRA*, BENKI YA DUNIA, *RAK GAS TANZANIA*, *EU*, *ICDF*, *PETRAD*, *MCC* ya Marekani. Tumefarijika kwa michango yao kwa maendeleo ya nchi yetu, na tunaahidi kuienzi na kuiendeleza.

Mhe. Spika, naomba kukushukuru wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa wote kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini wa hali ya juu.

Mhe. Spika, nikiwa namaliza muda wangu katika Wizara hii naomba uniruhusu kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Amani Abeid Karume kwa imani yake kwangu na kwa kunipa nafasi ya kuitumikia nchi yangu. Aidha namshukuru Mheshimiwa Waziri Kiongozi na Naibu Waziri Kiongozi kwa msaada wao kwangu wote ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu afya njema na maisha marefu pamoja na familia zao. Shukurani maalum kwa chama changu (CCM) kwa heshima kubwa iliyonipa.
Tunaomba pia kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zilizotembelea na kufanya vikao na Wizara yangu. Maoni, ushauri na maelekezo yao kwetu yamesaidia sana sio tu katika utekelezaji wa kazi bali pia katika uandikaji wa hotuba hii. Shukurani maalum kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inayoongozwa na Mh. Ramadhani Nyonje Pandu kwa msaada wao mkubwa kwetu.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru wananchi wote kwa ujumla kwa ustahamilivu wao hasa pale tulipotokezewa na tatizo la kukatika kwa umeme na kukosekana kwa huduma ya maji.

Mhe. Spika, naomba pia kumshukuru sana Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Wafanyakazi wenzake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuwezesha vitabu vya Bajeti za Wizara zote kupatikana kwa wakati.

Mhe. Spika, shukurani maalum nazitoa kwanza kwa mwenzangu na Ndugu yangu Naibu Waziri wa Wizara ya Maji Ujenzi Nishati na Ardhi Mheshimiwa Tafana Kassim Mzee kwa mashirikiano yake makubwa alionipa katika kuongoza Wizara hii,heshima na udugu tuloishi pamoja katika kipindi chote hicho.

Inshaalah Wananchi wa Jimbo la Uzini watamchagua tena kuwa Mwakilishi wao na Mwenyenzi Mungu atamjaalia Kheri na fanaka na familia yake.

Vile vile shurani za dhati nazitoa kwa Katibu Mkuu Nd. Mwalim.A.Mwalim, Naibu Katibu Mkuu Nd.Tahir.M.K. Abdullah, Mkurugenzi wa Mipango na Sera Nd. Mohamed Abdulla Mohamed ambao kwa pamoja walinipa mashirikiano yao ya hali ya juu kwa wakati wote katika kuendesha, kutekeleza na kuongoza kazi ambazo Wizara hii ilikabiliwa nazo. Msaada mkubwa walionipa Wakurugenzi,Afisa Mdhamini –Pemba, Mameneja,Wenyeviti, Mahakimu na viongozi wote wa ngazi mabalimbali ni ushahidi wa ukakamavu wao katika kuitumikia nchi hii na Mwenyezi Mungu awajaalie wote na familia zao afya njema na maisha marefu, Amin. Napenda kukiri mbele ya hadhara hii kuwa Timu hii ya Uongozi sitoweza kuisahau katika maisha yangu yote.

Mhe Spika, nakuomba uniruhusu nimshukuru kwa dhati kabisa Ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Masoud Hamad ambaye kwa nafasi yake ya kuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi katika kipindi hichi cha miaka mitano, amenisaidia sana katika majukumu yangu kupitia michango yake mbali mbali katika Kamati na Baraza hili Tukufu.

Mhe. Spika, nitakuwa sijatimiza wajibu wangu bila ya kutoa shukurani zangu kwa Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu ambao kwa wakati wote walikuwa karibu sana katika kunishauri na kunipa nasaha ambazo hatimae zimezaa matunda ya ufanisi katika wajibu wangu mbele ya Baraza hili na wananchi wa Zanzibar.Mwenyenzi Mungu atujaalie tufanikiwe tena kurudi hapa pamoja kwa adhma ya kuitumikia nchi hii kwa moyo wa umoja na upendo,Amin.

Mhe. Spika, nakuomba pia uniruhusu kuwashukuru wananchi wa jimbo la Kiembesamaki kwa heshima kubwa waliyonipa kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wao ninawashukuru sana na Inshaallah kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu watanichagua tena kuwa Mwakilishi wao kwa kipindi kijacho ili kuendeleza kazi ya pamoja ya kuijenga nchi hii kwa maslah ya wananchi wake.

Mhe. Spika**,** nakuomba pia uniruhusu kuishukuru familia yangu yote kwa ustahamilivu wao na mapenzi yao kwangu, shukrani maalum ziende kwa mke wangu na watoto wangu.

Mhe. Spika**,** aliyekamilika ni Mwenyezi Mungu pekee, ninawaomba wenzangu nyote munisamehe pale nilipowakosea,ninawashukuru kwa msaada na mashirikiano yenu Mwenyezi Mungu atawajaalia inshallah kheri, mafanikio na afya njema nyinyi na familia zenu.

Mhe. Spika**,** nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wayapokee, wayajadili kwa kina, watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe Makadirio haya.Tuna imani kubwa kuwa michango yao Waheshimiwa Wajumbe itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika**,** ili Wizara yangu iweze kutekeleza kazi, majukumu na malengo niliyoyaeleza, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 4,821,000,000 kwa kazi za kawaida na Tsh. 3,880,000,000 kwa kazi za Maendeleo kwa Wizara ya Maji Ujenzi Nishati na Ardhi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika**,** sasa naliomba Baraza lako Tukufu likubali matumizi ya Wizara yangu jumla ya Tsh 8,701,000,000 na pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya Tsh 2, 361, 619, 000 kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Kwa ufafanuzi zaidi ninaomba muangalie kiambatanisho F1 na F2.

Mhe Spika**,** naomba kutoa hoja

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, niruhusu nitoe hotuba ya maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2010-2011.

Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyeumba mbingu na ardhi kunijaalia uzima na afya njema na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa niaba ya Wajumbe wenzangu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 kwa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardi.

Mhe. Spika, nakushukuru na wewe mwenyewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii adhimu na maalum ya kuwa mchangiaji wa mwanzo katika Hotuba hii ya Bajeti ya Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa mashirikiano makubwa waliyonipa na kuonesha imani na mapenzi makubwa kwangu. Hakika, mashirikiano yao, mapenzi yao, na

imani yao yamepelekea mafanikio makubwa katika kutekekeleza majukumu yetu ya kazi zetu kwa kipindi chote wakati Kamati ikiwa katika kazi zake za kawaida na hata pale tulipo kuwa nje ya majukumu yetu ya kazi.

Mhe. Spika, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kwa dhati kabisa kutoka ndani ya sakafu ya moyo wangu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi Mhe. Mansour Yussuf Himid bin Maftah na Naibu Waziri wake Mhe. Tafana Kassim Mzee pamoja na watendaji wao wote, Katibu Mkuu Ndugu Mwalimu Ali Mwalimu, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Tahir M.K. Abdalla, Mkurugenzi wa Mipango na Sera Ndugu Moh'd Abdalla Mohamed na Afisa Mdhamini – Pemba Ndugu Januari Fussi na viongozi mbali mbali wa wizara kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupa mimi na Kamati yangu, na kwa maelekezo wanayo ipa kamati yangu kila mara na kuwa nayo pamoja wakati wote wa utekelezaji wa kazi za Kamati. Aidha, tunawashukuru kwa kutekekeza vyema yale yanayo elekezwa na Kamati na ushauri mbali mbali unaotolea na Wajumbe wa Kamati.

Mhe. Spika, chini ya Uongozi na Usimamizi wa Waziri Mansour Wizara hii imepata mafanikio makubwa sana na ya kujivunia na kila Mzanzibari anapaswa, na yafaa na anashtahiki kufurahia mafanikio na maendeleo yaliyopatikana.

Mhe. Spika, kupatikana kwa umeme kutoka Tanga hadi Pemba yatosha kuwa ni kielelezo sahihi na halisi cha mafanikio na maendeleo ya wananchi wa Pemba kwani umemem huu wengi waliona ni hatidhi na ni ndoto za Alinacha, Leo HAYAWI HAYAWI – YAMEKUWA na wananchi wa Pemba sasa wana nufaika na huduma hii ya uhakika ya umeme kutoka Tanga.

Mhe. Spika, kukamilika kwa nyumba za Michenzani, ununuzi na kuwasili kwa majenereta 32 ya akiba yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa *mega walt* 25 na ujenzi wa jengo jipya la Makao Makuu ya Wizara ni miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika wizara hii. Haya ni ushahidi na uthibitisho mkubwa wa juhudi, bidii na uwajibikaji katika majukumu ya kiutendaji wa Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi Mansour Yussuf Himid bin Maftah.

Muundo wa Kamati

Mhe. Spika, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kutokana na marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2009 sasa imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 104(c) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi na majukumu ya Kamati yametajwa katika kifungu cha 109.

Kamati yangu imeundwa kutokana na Wajumbe wafuatao:-

1.	Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hamad Masoud Hamad	-	M/ Mwenyekiti

3.	Mhe. Kamal Basha Pandu	-	Mjumbe
4.	Mhe. Ame Ussi Juma	-	Mjumbe
5.	Mhe. Subeit Khamis Faki	-	Mjumbe
6.	Mhe. Zakiya Omar Juma	-	Mjumbe
7.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Mjumbe
8.	Mhe. Omar Ali Jadi	-	Mjumbe
9.	Mhe. Ali Denge Makame	-	Mjumbe
10.	Mhe. Asha Moh'd Hilal	-	Mjumbe
11.	Ndg. Othman Ali Othman	-	Katibu Kamati
12.	Ndg. Rabia Juma Shaaban	-	Katibu Kamati

SHIRIKA LA UMEME

Mhe. Spika, nchi yetu mara nyengine tena ilipata mtihani mwengine mkubwa baada ya kukumbwa na tatizo jengine la kukosekana kwa umeme katika kisiwa cha Unguja kwa muda wa miezi mitatu mfululizo kuanzia tarehe 10 Disemba 2009 hadi tarehe 8 Machi, 2010.

Mhe. Spika, kamati yangu inaipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa kurejesha huduma za upatikanaji wa umeme Unguja. Aidha, tunawapongeza wananchi wote wa Unguja kwa kuonesha hisia zao za kusikitishwa na tukio hilo ambalo kila mmoja wetu lilimgusa. Tunawashuruku sana kwa ustahamilivu wao mkubwa waliouonesha kwa Serikali yao katika kipindi hicho kigumu cha miezi mitatu ya kukaa giza totoro. Ustahamilivu wao ni dalili ya upendo na utii kwa Serikali yao na mustakabali mzuri wa maridhiano yaliyokuwepo ya kutaka kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwani kwa tukio hili wote wana CCM na wana CUF tulilia pamoja.

Mhe. Spika, Shirika la Umeme kwa muda mkubwa sasa linakabiliwa na tatizo la uwakilishi wa mtu hasa au mjumbe husika wa kuwakilisha Uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) katika vikao vya Bodi ya Wakurugenzi wa *TANESCO*. Kuna taarifa kwamba Meneja Mkuu wa sasa wa Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) amepewa likizo ya lazima ili kutathmini utendaji wake.

Kwa kuwa yeye ndiye aliyekuwa Mjumbe halali anae hudhuria na kushiriki katika vikao vya Bodi hiyo kwa nafasi yake ya Mkurugenzi Mkuu, na kwa kuwa kwa sasa amepewa likizo isiyokwisha na isiyo na muda maalumu. Kwa mintarafu hiyo anapaswa pia kuzumzika kushiriki vikao vya Bodi, na kwa bahati mbaya mpaka sasa jitihada za kumwezesha Kaimu Meneja Mkuu *ZECO* kushiriki vikao hivyo nazo hazijafanikiwa.

Mhe. Spika, kamati yangu inajiuliza KULIKONI! Pengine kwa sababu Meneja Mkuu hajaiarifu Bodi ya *TANESCO* na/au mwenyewe anaendelea kushiriki. Kamati inauliza wizara ni nani anaehusika, au angepaswa:-

- Na kutoa taarifa za kusitishwa kushiriki kwenye vikao hivyo vya Bodi ni Wizara, Shirika au yeye mwenyewe.
- Na je, Kaimu Meneja Mkuu wa sasa kutoshiriki au kushirikishwa kwenye vikao hivyo ni kumtendea haki.
- Na je, kwa kuwa Meneja Mkuu huyo hata kama akienda kwenye vikao hivyo hawasilishi taarifa, ripoti na maelezo muhimu kwenye Bodi au Menejiment ya Shirika la Umeme Zanzibar haioni kama haliitendei haki wizara au Shirika la Umeme.
- Na je, Kuendelea kupokea posho kwa kazi isiyotekeleza wajibu wake ni halali.

Me. Spika, kamati inataka majibu ya masuali hayo au ya mchango huo.

Mhe. Spika, kamati yangu haikuridhika na majibu yaliyotolewa na Serikali yake yaliyotolewa na Waziri Kiongozi, na Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi katika kupandishiwa bei za umeme na *EWURA* kwa wateja wa Zanzibar kwa ongezeko la asilimia 168% kutoka shilingi 28 kwa *unit* moja ya kWh hadi kufikia shilingi 75 kwa unit tofauti na asilimia 21.7% kwa upande wa wateja wa Tanzania Bara.

Mhe. Spika, juhudi zilizofanywa na Afisi ya Waziri Kiongozi ya kuwasiliana na Afisi ya Waziri Mkuu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania tunaona hazina thamani, “hazifuidafu” wala “hazizai matunda” kwa kuwa hazikuthaminiwa. Hasa kwa kuwa barua ya Waziri Mkuu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania iliyopelekwa Wizara ya Nishati Tanzania Bara ambayo iliiagiza ongezeko la bei ya umeme kwa Zanzibar liwe asilimia 21.7 kama ilivyo pandishwa kwa wateja wa Tanzania Bara.

Barua hiyo haikufanyiwa kazi imepuuzwa na taasisi zinazohusika amapo hadi leo *TANESCO* wanaendelea kuifanyia bili *ZECO* kwa ongezeko la asilimia 168 ambapo tofauti sasa imefikia Bilioni Ishirini na Tisa (29,000,000,000/=).

Mhe. Spika, hizi ni kasoro, dosari, na hitilafu za Muungano zinazopaswa kushughulikiwa.

MATATIZO YANAYOZIKABILI KAMATI

Mhe. Spika, Kamati za Kudumu za Baraza zipo Kikatiba zimeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 85(1) cha Katiba ya Zanzibar ambapo pamoja na mambo

mengine zina majukumu kama yalivyotajwa katika kifungu cha 104 cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Kamati za Kudumu za Baraza zimepewa nguvu na uwezo wa Kisheria chini ya Sheria No. 4 ya 2007 kuweza kumwita au kumtaka mtu yeyote kufika kwenye kamati husika.

Meh. Spika, bado kamati zako ambazo wewe ndiye mwenye mamlaka kwa mujibu wa Kanuni ya 105(2) kuunda Kamati hizo zinadharauliwa, haziheshimiki, wala hazi heshimiwi na pengine hazitambuliwi wala hazitambuliki.

Mhe. Spika, kamati yangu imesikitishwa na tabia mbaya ya dharau, kutokujali na kuheshimu iliyo oneshwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) kwa kutokujibu barua ya kamati wakati kamati ilipotaka kwenda Tanga kufuatilia matatizo ya umeme pamoja na kwamba yeye mwenyewe alisema atatujibu kwa barua, lakini Mwenyekiti huyo alishindwa kufanya hivyo na badala yake alisema kwenda Tanga ni kupoteza pesa bure na hapakuwa na haja ya kamati kwenda.

Hata hivyo, kamati ilifanya ziara ya Tanga na ilipofika Tanga ilikuta matatizo mengi, makubwa na magumu ambayo yalikwamisha utekelezaji wa Mradi wa Umeme Tanga – Pemba na tatizo hilo lilikuwa ni miongoni mwa sababu za kuchelewa mradi huo. Kamati yangu ilifanikiwa kutatua tatizo hilo baada ya kufanya kikao cha pamoja kati ya Uongozi mzima wa Mkoa wa Tanga na kamati yangu.

Mhe. Spika, dharau nyengine iliyofanyiwa kamati ni ile iliyofanywa na Waziri wa Nishati na Madini wa Tanzania Bara Mhe. William Ngeleja ya kukataa na kushindwa kukutana na kamati yetu tarehe 27/4/2010 wakati yeye mwenyewe ndiye aliyetupangia tarehe ya kukutana nae.

Mhe. Spika, tarehe 26/4/2010 kamati yangu ilitumwa kikazi na Mhe. Waziri wa Maji kwenda Dar-as-Salaam kufatilia suala la ongezeko la bei ya umeme (*Tariff*) ambalo kwa upande wa Zanzibar ongezeko kubwa kama hilo lingeweza kuathiri maisha na ustawi wa Wazanzibar.

Mhe. Spika, mazungumzo ya kwenye simu ya kati ya Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Ujenzi na Nishati na Mhe. Waziri Ngeleja Waziri wa Nishati na Madini wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yalitosha kutukubalia kukutana nae na kwamba tukutane nae saa tano asubuhi.

Mhe. Spika, kamati yangu haikupata kuonana na Mhe. Waziri na badala yake ofisi yake ilitutaka tuonane na Mhe. Naibu Waziri wake Mhe. Malima Kigoma, lakini Kamati yangu ilikataa kuonana nae kwa kujua kwamba kukutana na Naibu

Waziri isingetusaidia kupata mfumbuzi badala yake tungeambulia majuto kwani kuonana na Malima ni sawa na kutwanga maji kwenye kinu.

Mhe. Spika, kamati yangu inaiomba Serikali pamoja na juhudi ilizochukua bado kuna haja ya kuanza upya kufuatilia tatizo hilo linalo ashiria kuwa ni kikwazo kwa Wazanzibar.

Mhe. Spika, wajumbe wako takriban wote walinilaumu, walinishutumu na kunituhumu vibaya wakati tulipo mchagua Mhe. Hamad kuwa Makamo Mwenyekiti kwa dhana ya nafasi yake ya kuwa ni mwanachama wa chama cha upinzani CUF. Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa CCM walisahau kwamba kanuni hailazimishi kuwa Mwenyekiti akiwa mwana CCM na Makamo awe Mwana CCM.

Mhe. Spika, nakushukuru sana Mhe. Makamo Mwenyekiti wangu Hamad Masoud kwa mashirikiano yako na imani yako juu yangu.

Mhe. Spika, nakuombea kheri, baraka na maisha mazuri, aidha nawatakia mafanikio mema Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu nawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu waweze kukabiliana vyema na mchakato wa KURA ZA MAONI na kuweza kushinda tena nafasi zao na kurudi katika Baraza lako lijalo AMIN.
Mhe. Spika, naomba niende moja kwa moja katika kuichangia Bajeti ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kama ifuatayo:-
Katika kipindi cha 2009/2010 Wizara ya Maji Ujenzi, Nishati na Ardhi ilitarajiwa kutumia Tsh. 4,687,000,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 7, 280,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Jumla ya fedha ni Tshs 11,967,000,000/=

Mhe. Spika, katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 wizara ilipewa jukumu la kukusanya mapato ya jumla ya Tsh. 2,610,100,000 hadi kufikia machi 2010 Wizara ilikwishakusanya Tsh. 1,447,288,138.96 sawa na asilimia 55.45,

UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2009/2010
IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika, kamati ilipata nafasi ya kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo iliyomo katika Wizara, kupitia Idara hii kama ifuatayo:-

1. Mradi wa kujengea uwezo Idara ya Mipango na Sera
2. Usambazaji maji vijijini

3. Uhuishaji na upanuzi wa shughuli za maji mijini
4. Mradi wa kuijengea uwezo mamlaka ya maji
5. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za maendeleo Michenzani na Mpapa
6. Mradi wa kuukuza na kuutambulisha Mji Mkongwe
7. Mradi wa kupeleka Umeme Pemba kutoka Tanga
8. Mradi wa usambazaji Umeme vijijini awamu ya nne nyongeza.

Mhe. Spika, miradi mengine ni :-

9. Mradi wa kuweka njia ya pili ya umeme Ubungo hadi Mtoni
10. Mradi wa kufunga mita 20,000 za TUKUZA Unguja na Pemba
11. Mradi wa kuimarisha Shirika la Umeme
12. Mradi wa kupeleka Umeme Tumbatu
13. Mradi wa kuandaa Sera ya Nishati Zanzibar
14. Mradi wa kuihuisha Bustani ya Forodhani
15. Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (*SMOLE*)

Mhe. Spika, kamati ilipata nafasi ya kuitembelea miradi karibu yote iliyotajwa ambayo inaratibiwa na Idara ya Mipango na Sera, na kuridhika na jitihada zinazochukuliwa na zilizokwishachukuliwa za kuwapatia wananchi maendeleo hususan Mradi wa kupeleka Umeme Pemba kutoka Tanga, na Mradi wa uhuishaji na upanuzi wa shughuli za Maji mijini unaohusisha wa Mjini Magharibi pamoja na miji mitatu ya Pemba.

MAMLAKA YA MAJI

Mhe. Spika, Mamlaka ya Maji katika kipindi cha mwaka 2009/2010 ilitekeleza miradi ya usambazaji wa maji vijijini, uhuishaji na upanuzi wa maji mijini na kijengea uwezo Mamlaka ya Maji.

Mhe. Spika, kamati ilipata nafasi ya kutembelea Mamlaka ya Maji na kutembelea Miradi mingi iliyotajwa katika utekelezaji halisi katika Mamlaka hii nakuridhika na utekelezaji wa Miradi hii ikiwemo ya Mfenisini, Kitope na Bumbwini na Miradi ya Tangi la Maji ziwani na Mradi wa maji Kigongoni.

Mhe. Spika, kamati imeridhika na kazi zinazofanywa na Mamlaka ya Maji na kuitaka kuendelea na jitihada za kuwaelimisha wananchi kuhusu kutotumia ovyo maji na kuhifadhi Mazingira katika vyanzo vya maji, ili kuwezesha kupatikana maji kwa wingi katika sehemu zao, na kuyalipia maji kwa wale wanaopata ili kuweza kuipa mamlaka uwezo wa kujiendeleza kifedha.

MAMLAKA YA HIFADHI YA UENDELEZAJI MJI MKONGWE

Mhe. Spika, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kwa mwaka 2009/2010 ilifanya kazi za ukusanyaji wa mapato, uhifadhi wa takwimu na taarifa muhimu, mpango wa matumizi ya barabara na maegesho, sheria mpya ya mamlaka, mradi ujenzi wa ukuta wa ukingo wa Bahari

Mhe. Spika, kamati imeridhishwa na kazi za mamlaka hii hususan ukamilishaji na upitishwaji wa sheria mpya ya Mji Mkongwe ambayo itasaidia sana kuweka mazingira ya mji huo katika hali ya kuridhika katika masuala ya ujenzi unaotakiwa kwa lengo la kuubakisha katika urithi wa kimataifa.

Mhe. Spika, kamati katika kazi zake ilifuatilia ujenzi unaofanywa na Wananchi na Taasisi zinazotumia Mji Mkongwe na kusisitiza kwamba ujenzi wowote unaofanywa katika Mji huu lazima Mamlaka ishirikishwe kwa lengo lile lile la kuujenga inavyotakiwa. Kamati inaziunga mkono jitihada zote zinazochukuliwa na Mji Mkongwe katika kuhakikisha Mji unakuwa safi, biashara zinafanywa inavyotakiwa na mazingira yamekuwa katika hali ya utulivu wakati wote.

Idara ya Nishati na Madini

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Idara ya Nishati na Madini ilijipangia kukamilisha kazi za mradi wa Sera ya Nishati pamoja na kuweka mikakati ya utekelezaji wa sera hiyo, kusimamia '*Depot'* za mafuta za serikali na kuhakikisha kuwa *Depot* hizo zinachangia Mfuko Mkuu wa Serikali kutekeleza agizo la serikali la kuwapeleka vijana katika mafunzo yanayohusiana na mafuta na gesi asilia.

Mhe. Spika, suala la mafunzo kwa vijana ambao wana sifa katika mafunzo hayo ni la umuhimu na linahitaji kuchukuliwa hatua za haraka ili kuweza kupata wataalamu wa kutosha katika fani ya mafuta na gesi asilia, kwa lengo la kuepuka matatizo yanajitokeza katika mataifa mengine wakati wa uchimbaji wa mafuta. Hii itatusaidia kuyaepuka matatizo hayo baada ya kuchimbwa na kupatikana mafuta hayo na utaratibu mzima wa uendeshaji wa kazi hiyo.

Mhe. Spika, kamati inasisitiza kuchukuliwa hatua za matayarisho na kuletwa kwa sheria zote zinzohusiana na mafuta kama *"Petrolleum Supply Act"* na *"Zanzibar Energy Act",* kuletwa katika Baraza la Wawakilishi zitakazowezesha kutekelezwa katika utaratibu uliokamilika.

Idara ya Ujenzi
Mhe. Spika, Idara ya Ujenzi katika kipindi cha 2009/2010 ilipanga kufanya kazi za ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Mpapa, kusajili wataalam wa Bodi ya Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na kusajili Bodi ya Makandarasi.

Kamati katika kazi zake ilionana na bodi zinazohusika na idara hii na kuridhishwa na watendaji wa bodi hizi, na kuitaka idara kuwatengenezea mazingira mazuri ya kuweza kufanya kazi ikiwemo vitendea kazi pamoja na ofisi ili waweze kufanya kazi zao katika hali ya kuridhisha.

Mhe. Spika, kamati ilipotembelea Nyumba za Maeneleo Mpapa, Unguja, ilielezwa kwamba tatizo lililochelewesha kumalizika kwa ujenzi ni uchache wa uingizwaji wa fedha. Na kwa upande wa Pemba, tatizo la upungufu wa wafanyakazi linaathiri utendaji wa kazi na suala la kazi za taasisi za serikali kupewa makampuni au watu binafsi liangaliwe kwa uzito wake, kwani idara itakua na uwezo wa kuchukuwa kazi za Taasisi za Serikali ikiwa itawezeshwa.

Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi
Mhe. Spika, katika kipindi cha 2009/2010 idara ilipanga kutekeleza malengo ya kukusanya mapato, kuuza nyumba za vijiji, kuundwa kwa kamati ya kuwatambua wale wote waliopewa nyumba na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, matayarisho ya sheria ya *"Condominium"* na ulipaji wa fidia kwa wale wote waliovunjiwa nyumba zao kupisha Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo.

Mhe. Spika, kamati imeridhishwa na maendeleo ya uundwaji wa sheria ya "*Condominium*" ambayo itakapoletwa Baraza la Wawakilishi na kupitishwa itaweka wazi na kuwawezesha kujua haki zao wakaazi wanaoishi jengo moja lenye *flat* zaidi ya moja na kuwajibika katika maendeleo ya jengo lao na majengo ya wakaazi wengine.

Kamati imeipongeza hatua ya serikali kupitia Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kuandaa utaratibu wa kuwapatia nyumba wale wote waliovunjiwa nyumba zao kupisha Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo na kuhakikisha wale wanao stahiki tu, ndio wanaopata na baadae kupewa kwa kupangishwa wale wenye matatizo ya sehemu za kuishi.

Idara ya Utawala wa Ardhi
Mhe. Spika, Idara ya Utawala wa Ardhi katika kipindi cha 2009/2010 ilipanga kutekeleza malengo ya kusimamia Sera ya Ardhi, Mapitio ya Sheria mbali mbali za Ardhi na kusimamia maeneo ya utekelezaji.

Mhe. Spika, suala la ardhi ni la kupewa kipaumbele kutokana na umuhimu wake katika nchi yeyote ile, kamati inashauri kuwekwa mkakati wa kuzihakiki na

kuzilinda eka tatu tatu walizopewa wananchi baada ya Mapinduzi kwa lengo la kulima na kupata maendeleo yatakayomsaidia mwananchi kwa kuweza kujiendeleza kimaisha.

Mhe. Spika, ardhi ni mali ya serikali. Kwa hivyo, kamati inaziunga mkono jitihada zinazochukuliwa za kufanya mapitio ya Sera ya Ardhi, kuzifanyia mapitio sheria mbai mbali za ardhi, na kufanyia kanuni za sheria ya uhaulishaji wa ardhi.

Idara ya Ardi na Usajili

Katika mwaka 2009/2010 Idara ya Ardhi na Usajili iliendelea na kazi za ukusanyaji wa mapato, kodi ya ardhi, fomu za maombi ya viwanja, usimamizi wa ukodishaji wa ardhi, kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu, kuimarisha udhibiti wa ardhi na shughuli za Afisi ya Mrajis wa Ardhi.

Mhe. Spika, kamati inapongeza jitihada za idara hii katika ukusanyaji wa mapato kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika malengo iliyojiwekea. Kwani katika nchi husika ukusanyaji wa kodi ni muhimu kwa lengo la kupatikana fedha za kuwasaidia wananchi katika kero zao mbali mbali.

Mhe. Spika, uanzishaji wa Mahkama ya Ardhi ni jambo zuri ambalo wananchi wengi wamelifurahia jambo hilo kwa lengo la kuondoa migogoro ya ardhi inayoendelea kila kukicha, matumaini ya kamati ni kwamaba, matatizo haya yatapungua kutokana na kuongezwa Mahakimu na kasi ya kuhukumiwa kesi hizo.

Idara ya Upimaji na Mipango Miji

Mhe. Spika, Idara ya Ardhi na Mipango Miji katika kipindi cha mwaka 2009/2010 ilitekeleza majukumu yake kwa kukusanya mapato, kuendelea na kazi za ukamilishaji wa ramani za Visiwa vya Unguja na Pemba, upimaji wa viwanja 2000 vya maakazi na maeneo mengineyo. Kuufanyia mapitio mpango wa kitaifa wa matumizi bora ya ardhi na utayarishaji wa ramani za matumizi ya ardhi ya Wilaya za Unguja.

Kamati imeridhishwa na hatua zinazochukuliwa na idara hii, kuwapatia wananchi viwanja wale ambao wana matatizo ya ujenzi na kusisitiza suala la kufikiria kutenga eneo kwa ajili ya kujenga nyumba za ghorofa kwa kumpa mwekezaji ili eneo hilo lijengwe nyumba na baadae wapewe wananchi kwa njia ya kukodishwa. Ila kamati yangu inasikitishwa na kitendo cha baadhi ya viongozi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, kwa kuwachochea wananchi kuzuwia kwa makusudi shughuli za upimaji wa viwanja vilivyokusudiwa kugaiwa kwa wananchi kwa ajili ya makaazi, biashara na huduma za kijamii katika eneo la

Pwanimchangani. Eneo ambalo limetengwa na kutangazwa rasmi kwenye Gazeti Rasmi la Serikali tangu 1997 kwa madhumuni ya mipango miji.

Mhe. Spika, licha ya kutengewa eneo maalum kwa wananchi wa Pwanimchangani kwa ajili ya kujenga nyumba bora za kuishi na kwa madhumuni ya kuendeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi, bado suala hilo limekua ni tete.

Kamati yangu inawashauri viongozi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, kuwa na mashirikiano ya pamoja na kuwa na uongozi wa pamoja kati ya taasisi mbali mbali za chama na serikali, Jumuiya za Kimaendeleo na Kamati za Maendeleo za Wilaya na Mkoa. Katika utatuzi wa matatizo ya wananchi na jamii ni vyema mukaweka mbele maslahi ya wananchi kuliko maslahi ya mtu au watu binafsi. Busara na hekima inabidi vitumike zaidi kuliko jazba katika kutatua tatizo hili.

Kamati inasisitiza suala la kutokujengwa nyumba sehemu za vianzio vya maji. Kwa sababu linaharibu vianzio vya maji na kusababisha uharibifu wa mazingira. Kutokana na sehemu hiyo, huchafuliwa na kusababisha matatizo mbali mbali yakiwemo maradhi ya matumbo na kipindupindu.

Shirika la Umeme

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010 Shirika la Umeme limetekeleza kazi za Mradi wa Kusambaza Umeme Kisiwa cha Tumbatu, Mradi wa Kupeleka Umeme Pemba kutoka Tanga, Mradi wa Kuendeleza Ufungaji wa Mita za Tukuza, Mradi wa Ujenzi wa njia ya pili kutoka Ubungo hadi Mtoni Unguja, kuendeleza kazi ya kuvipatia huduma ya umeme visiwa vidogo vidogo, mpango wa umeme mbadala na majenereta ya akiba.

Mhe. Spika, kamati inapongeza jitihada zilizochukuliwa na serikali kupitia shirika hili na kufanikiwa kuufanikisha suala la kupatikana umeme unaotoka Tanga kwenda Pemba ambalo ni la kihistoria. Kamati imefarijika sana na kazi hii kuanza na kumalizika kwa mafanikio makubwa. Kamati inashauri kuendelea kuchukuliwa juhudi za kutunza miundombinu ya umeme huo ili lengo lililowekwa na nchi liweze kufanikiwa.

Vile vile kamati inapongeza jitihada za serikali kupitia Shirika la Umeme zilizofanikisha kuletwa jenereta za akiba na kuwa yatatumika pale ambapo yatakapotokea matatizo ya kukosekana kwa umeme na kupunguza makali ya tatizo. Kamati inashauri kuendelea na kuchukuliwa hatua za kutafuta umeme mbadala ili kuondokana na tatizo lililokwisha kutokezea kwa kukosa umeme takriban miezi mitatu.

Utekelezaji wa Malengo kwa Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2010/2011

Idara ya Mipango na Sera

Mhe. Spika, kamati imeyajadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2010/2011 kwa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na kuridhika na miradi iliyotajwa katika bajeti hiyo.

Mhe. Spika, miradi yenyewe ni :-

1. Usambazaji wa Maji Vijijini
2. Uhuishaji na Upanuzi wa Maji Mijini
3. Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji
4. Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*AFDB*)
5. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Michenzani na Mpapa
6. Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini
7. Mradi wa Kuweka *line* ya pili ya Umeme Ubungo hadi Mtoni (*MCC*)

Mhe. Spika, miradi mingine ni:-

8. Mradi wa Kufunga Mita 10,000 za TUKUZA Unguja na Pemba
9. Mradi wa Kuimarisha Shirika la Umeme (*FTA*)
10. Mradi wa Utekelezaji wa Sera ya Nishati
11. Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (*SMOLE*)
12. Mradi wa Kuijengea Uwezo Idara ya Mipango na Sera
13. Mradi wa Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Bahari
14. Mradi wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara kupitia Sekta ya Ardhi (MKUMBITA)

Mhe. Spika, miradi ya maji inaendelea vizuri katika Mamlaka ya Maji na kamati imeridhika na kazi zinazoendelea Unguja na Pemba. Jambo linalohitajika ni kuongeza juhudi ili lengo liweze kufikiwa kwani, bado wapo wananchi wanateseka na tatizo la maji hususan katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mhe. Spika, suala la kuwapatia motisha wafanyakazi ni la umuhimu hasa, kwa wafanyakazi wa mamlaka kutokana na kazi wanazozifanya na mazingira ya kazi wanayokabiliana nayo wakati linapotokea tatizo la kukosekana maji na walinzi wanaolinda sehemu za vianzio vya maji wafikiriwe kuongezwa motisha.

Kamati imeridhishwa na hatua inayoendelea na Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Michenzani na Mpapa. Isipokua suala la nyumba za Mpapa, kamati

inashauri idara kupewa fedha za kutosha katika bajeti hii ili kuweza kumalizia kazi za ujenzi katika nyumba hizo.

Matatizo yanayojitokeza katika nyumba za maendeleo ni kutokuwa na mazingira mazuri ya usafi na utunzaji wa nyumba hizo, kufanya wakaazi wa nyumba hizo watakavyo ikiwa pamoja na kubadilisha miundo mbinu ya nyumba hizo. Lazima suala hilo lidhibitiwe kwa kuwekwa kamati za nyumba na kuchukuliwa hatua kwa yeyote atakaekiuka utaratibu wa kuishi katika nyumba hizo.

Mhe. Spika, kamati imeridhishwa na miradi ya Shirika la Umeme iliyotajwa katika bajeti hii, lengo ni kuwapunguzia makali ya maisha wananchi. Matumaini ya kamati ni kwamba, hatua ya Shirika la Umeme itasonga mbele zaidi kwa kuwapatia wananchi huduma ya utiaji wa umeme ndani ya nyumba zao na baadae wawakate kidogo kidogo kwa wale ambao bado hawajaunga umeme, badala ya kutumia mita za zamani ambazo zina malalamiko mengi, wateja wote watiliwe Mita za TUKUZA.

Mhe. Spika, kamati inazipongeza juhudi za serikali katika maendeleo ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia, kwa kuwaandaa na baadae kuwapeleka vijana ambao wana sifa ya kwenda kusoma fani hii, ili watakaporejea kufanya kazi hii kwa niaba ya nchi yao na kuweza kuendesha biashara hii katika mazingira yeyote na kuepusha uharibifu wa mazingira na kuipatia nchi faida itokanayo na mafuta na gesi asilia.

Mhe. Spika, suala la ardhi lina umuhimu katika nchi yetu. Serikali kupitia wizara imepanga miradi ya ardhi kupitia mazingira mbali mbali yakiwemo ya biashara. Kamati inashauri mipango yote inyohusiana na suala hilo lengo iwe ni kupata uwezo, serikali kukusanya mapato yanayotokana na miradi hiyo na jengine ni kuendeleza mwananchi wa kipato cha chini.

Kamati inaziunga mkono jitihada zinazofanywa na Mamlaka ya Mji Mkongwe katika kuhakikisha mji unabaki katika hadhi yake ya urithi wa Kimataifa. Jambo hili ni la kujivunia. Kamati inashauri kwa serikali kupitia taasisi zake mbali mbali kuisaidia Mamlaka hiyo kufikia lengo lake pale inapoomba msaada ili kufanikisha malengo yake.

HITIMISHO

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nimshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Hamad Masoud Hamad (Makamo Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na Waziri kivuli wa Wizara hii ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi) kwa kunisaidia katika nafasi ya uenyekiti wakati wote ninapokuwa sipo na kamati. Mashirikiano yake, michango yake na ufuatiliaji wake katika kazi za kamati

yamenipa imani kubwa juu yake na kwa kweli amenisaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu.

Hakukuwa na hisia na chembembe zozote za kisiasa katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kazi. Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Hamad Masoud na tunasema ahsante sana Mhe. Hamad.

Kwa kukamilisha malengo ya Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, naiomba serikali kuidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi 8,701,000,000 na kuidhinishiwa makusanyo ya mapato jumla ya shilingi 2,361,619,000 kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili bajeti ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa kina kipana, kwa upeo mkubwa na baadae waipitishe.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Muyuni, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.
Mhe. Spika, naomba kuwasilisha, lakini pia naomba uniruhusu dakika tatu nichangie mchango wangu mimi binafsi. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu kama Mjumbe wa Baraza hili la Wawakilishi natoka katika nafasi ya Uenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Mchango wangu utakuwa mdogo tu.

Mhe. Spika, unajua siku hizi matatizo ya sukari yanaongezeka kwa wingi, wagonjwa wa sukari wamekuwa wengi na pahala pa kufanyia kazi ni padogo sana. kiji-*clinic* kilichowekwa cha matatizo ya sukari ni pahala padogo sana wala hapawezi kustahamilika. Mimi kwa niaba ya wagonjwa wote wa sukari wa Zanzibar Unguja na Pemba, kwa sababu mimi ni *trustee member* wa bodi hiyo. Kwa hivyo, nakuomba kwa heshima kubwa na taadhima Mhe. Waziri ambaye unashughulika na unahusiana na masuala ya viwanja, tafadhali, tafadhali, tafadhali, tunakuomba utupatie eneo la kujenga *clinic* kubwa na ya kisasa ya matatizo ya wagonjwa wa sukari. Maombi yetu yapo wizarani kwako kama hayajafika wizarani basi yako idarani, lakini nakuombeni myashughulikie.

Maeneo tumeshatafuta kilichobakia ni utekelezaji wenu. Kwa hivyo, nakuombeni kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii mlifuatilie hilo jambo kwa upeo mkubwa. Tungependa kabla ya kuagana, tungependa kabla ya kuja tena mwakani basi hilo suala lishughulikiwe.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu, nimekuridhia dakika tano ziada kwa kusoma hotuba ile ya kamati na pia dakika tatu kutoa mchango wewe kama *trustee* wa wagonjwa wa sukari. Nashukuru Baraza hili kumbe linashirikiana sana na wananchi. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui alikuwa mshika fedha wa Walemavu wa Akili, Mhe. Ramadhan Nyonje yeye ni *trustee* wa wagonjwa wa kisukari. Baraza linafanya kazi kubwa sana na ninawapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe. Sasa tumsikilize Mhe. Hamad Masoud Hamad (Waziri Kivuli wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na Mheshimiwa huyu anapiga ngoma huku na huku. Karibu. *(Kicheko)*

Mhe Hamad Masoud Hamad (Waziri Kivuli, Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi): Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kwa mara ya tano kuwasilisha maoni ya upinzani katika Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Leo ni kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa leo kwa shughuli za mkutano wa 20 wa Baraza la Saba la Wawakilishi tukiwa wazima, wenye afya na kwa madhumini ya kujadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2010/2011, na leo hii mahsusi kwa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

Mhe. Spika, niruhusu kwa niaba ka kambi ya upinzani nitoe shukrani maalum na pongezi za dhati na za pakee kwa Serikali ya Watu wa Norway kwa msaada wao mkubwa mno na wa kihistoria wa kuipatia Pemba umeme wa uhakika. Tangu tarehe 9/5/2010 Pemba inang'aa, baada ya kiza cha miaka zaidi ya arobaini. Wananchi wa Pemba hawajapata kauli wanayoina inatosha au inakidhi kueleza furaha na shukurani zao kwa neema hii adhimu. Maneno "AHSANTENI SANA WANORWAY" basi yakidhi haja hii.

Mhe. Spika, sasa nikushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kuwasilisha maoni ya kambi ya upinzani ndani ya Baraza hili kuhusu Bajeti ya Wizaea ya Maji kwa mwaka 2010/2011. Na nimalize shukurani zangu kwa kuwashukuru Kampuni ya *ZANTEL*, Benki ya *NMB* (Tawi la Chake Chake) na Taasisi ya *Action Aid* kwa misaada yao adhimu katika kuchangia maendeleo ya elimu katika Jimbo langu la Ole.

Mhe. Spika, ni hivi karibini tu, Chama changu cha Wananchi *CUF*, kimekuwa katika mchakato wa kura za maoni katika matawi yake yote, ambapo wanachama hai wa chama changu walipiga kura za maoni kama hatua za awali za kupata

wagombea wa chama kwa ngazi za udiwani, ubunge na uwakilishi kwa uchaguzi unaotarajiwa kufanyika nchi nzima ifikapo Oktoba mwaka huu.

Nawashukuru sana na kwa dhati ya moyo wangu, wananchi wote wa Jimbo langu la Ole na zaidi wanachama wa chama changu kwa ridhaa yao ya kunipa ushindi mkubwa wa kura 1,742. huu ni ushindi ambao unafanana na Kiongozi wangu wa Upinzani, Mhe. Abubakar Khamis ushindi wa tsunami. Wagombea walionifuatia walimbukia kura 420 na 241.

Mhe. Spika, matokeo haya bila shaka ni kielelezo tosha kinachotokana na kuridhika kwao na jinsi nilivyotekeleza majukumu waliyonipa katika kuliendeleza Jimbo langu, namna nilivyowajali, nilivyowatii, nilivyowaheshimu na namna nilivyokuwa karibu nao kwa dhiki na faraji na kwa hali na mali. Nawashukuru sana waajiri wangu hawa kwa heshima hii kubwa wanayoendelea kunipa. Ni matumaini yangu kwamba, ishara hii ni ya wazi kwamba penye majaaliwa ya Mwenyezi Mungu, wananchi wa Jimbo la Ole watanipa tena fursa ya kuwa Mjumbe wa Baraza la Nane la Wawakilishi, endapo Baraza Kuu la Uongozi la Taifa la Chama changu litaniteua tena kuwa mgombea wa chama; Amin.
Mhe Spika, sasa niruhusu tena kwa mara ya tano katika uhai wa Baraza lako nitoe maoni ya kambi ya upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa mwaka 2010/2011.

Pamoja na kwamba mimi ni Mjumbe na Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza lako hili, na kwamba kamati yangu imeshiriki katika kuipitia, kuifanyia marekebisho, kuikubali na kuipitisha hotuba hii ya bajeti ya wizara hii kwa mwaka 2010/2011, lakini hii haiondoi wajibu wangu kama msemaji rasmi wa kambi ya upinzani wa wizara hii, kuendelea kuonesha mapungufu kama yapo na zaidi kushauri, kuelekeza na inapobidi hata kusifu na kupongeza utendaji wa shughuli za wizara hii kwa madhumuni ya kujenga na kuimarisha.

Mhe. Spika, katika kitabu cha hotuba ya Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi *page* mbili, kimeeleza kwamba, msimamo wa CCM ni kuweka kura ya 'NDIO' katika kura ya maoni itakayofanyika tarehe 31 Julai, 2010. kwa ruhusa yako naomba nithibitishe kwamba mimi mwenyewe binafsi, kambi ya upinzani na *CUF* kama chama huu ndio msimamo wetu vile vile. Kwa hivyo, kama CCM msimamo wao ni huu na *CUF* ni huu, sidhani kwamba yuko mwananchi ambaye ana akili timamu anayependa Zanzibar kwa maendeleo yake na kigezo hiki cha miezi minane tangu maridhiano ya viongozi wawili yafanyike anaweza akatia kura ya 'HAPANa'.

Mhe. Spika, baada ya kujadili kwa kina na kupendekeza marekebisho husika katika vifungu mbali mbali vya hotuba ya wizara hii, natamka kwamba, kambi ya upinzani imeridhika na inakubali kuidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi 4,821,000,000/- kwa kazi za kawaida na shilingi 3,880,000,000/- kwa kazi za maendeleo na kuafiki makusanyo ya shilingi 2,361,619,000/-

Baraza lako hili tukufu litakumbuka kwamba hata kabla ya maridhiano ya kisiasa ya viongozi wetu wakuu wa kisiasa hapa Zanzibar, maridhiano yaliyoleta utulivu wa kisiasa, amani endelevu na mapenzi baina yetu Wazanbari, wizara pekee iliyopata heshima na hadhi ya kambi ya upinzani kwa kuungwa mkono kwa bajeti zote mbili, ile ya 2008/2009 na 2009/2010 ni Wizara hii ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

Bila shaka siri ya mafanikio haya kwa wizara hi yalitokana na mambo yafuatayo:

1. Mashirikiano makubwa baina ya uongozi wa wizara, watendaji wake na kambi yetu ya upinzani.
2. Usikivu, uzingatiaji na utekelezaji wa ushauri na maelekezo yaliyotokana na kambi ya upinzani kwa wizara hii.
3. Ujasiri uliyooneshwa na uongozi wa wizara hii katika kuyakabili mambo mazito ya kitaifa.
4. Nanma wataalamu wa wizara hii wanavyotumiwa vyema kwa maendeleo ya wizara.
5. Utekelezaji wa miradi migumu ambayo huko nyuma ilishindikana.
6. Kauli thabiti na za kujiamini za ahadi na utekelezaji wa kweli wa kauli hizo zinazotolewa na waziri wa wizara hii Mhe. Mansour Yussuf Himid.

Mhe. Spika, maamuzi ya kihistoria yaliyofanywa na Baraza lako hili tukufu na ambalo chanzo chake ni msingi wa maamuzi hayo, yalitokana na ujasiri wa kujiamini kwa waziri wa wizara hii Mhe Mansour Yussuf Himid, Bin Maftah ee? Yamelipamba sana Baraza lako kwa wananchi wa Zanzibar wa ndani na wa nje.

Katika miaka hii mitano Baraza lako la saba, kwa miswada iliyowasilishwa na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi limefanya mambo yafuatayo:

1. Limeanzisha rasmi Mamlaka ya Maji Zanzibar (*ZAWA*)
2. Limeanzisha rasmi Shirika la Umeme, Zanzibar (*ZECO*)
3. Limeanzisha sheria mpya ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe
4. Limeanzisha Bodi ya Usajili wa Wahandisi Wasanifu na Wakadiriaji Majengo.
5. Limeanzisha Bodi ya usajili wa Makandarasi.
6. Limefanya marekebisho ya sheria ya uhaulishaji ardhi.

7. Limejadili na kupitisha Sera ya Nishati na Sera ya nyumba.

Mhe. Spika ukamilishwaji wa mradi wa umeme wa Pemba kutoa Tanga, ukamilishwaji wa ujenzi wa *Block No. 10* nyumba za Michenzani, mradi mkubwa wa maji kwa Mkoa wa Mjini-Mgharibi, kukamilika kwa awamu zote nne na nyongeza zake kwa mradi wa umeme vijijini. Juhudi za kumaliza usambazaji wa umeme katika kisiwa cha Tumbatu ni miongoni mwa shughuli ambazo kambi ya upinzani ilitoa msukomo mkubwa katika mijadala ndani ya Baraza lako hili tukufu na ambalo sasa ni historia.

Idara ya Ujenzi

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana kuona kwamba, Bodi ya Usajili Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo (*Engineers, Architects and Quantity surveyors registration Board*) iliyoanzishwa na Baraza lako hili tukufu miaka miwili iliyopita, haijafanya kazi zake kwa *standard* (kiwango) ya wizara hii.

Sababu za ukosefu wa fedha za kuiwezesha bodi hii muhimu kufanyakazi zake inavyotakiwa zisiifanye bodi kama mauti. Inakuaje Kanuni za Bodi hii ziwe hadi leo hazijawa tayari? Pamoja na hayo, lakini imebainika kwamba, baadhi ya wajumbe wa bodi hii wana shughuli zao nyingi na inakuwa vigumu hata vikao vingine kufanyika.

Mhe. Spika, shughuli za msajili (*Registar*) aliyepo ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Ujenzi, hazimpi muda wa kutosha wa kufanya shughuli za bodi. Hata yule Mhandisi anayemsaidia msajili huyu haonekani kupewa mamlaka kamili ya kumsaidia. Kambi ya upinzani inaitaka Wizra hii iondoe haraka kasoro hii na kuanzia Julai 2010, Baraza hili lisikie kupatikana kwa msajili asiyekuwa mkurugenzi wa idara nyengine yoyote ya wizra hii na bodi hii iwezeshwe kutenda kazi zake kifedha.

Mhe. Spika, bodi ya usajili wa makandarasi ambayo ilianzishwa miaka miwili iliyopita nayo hadi sasa haijaweza kufanya kazi zake.

Mhe. Spika, kambi ya upinzani inaishauri wizara hii kuweka umuhimu wa pekee katika kuziwezesha bodi hizi mbili kuweza kutekeleza majukumu yake vizuri kwa kuzipatia fedha na ofisi hasa ukizingatia wimbi kubwa la ujenzi wa majengo makubwa ya kiofisi za serikali na taasisi nyengine za watu binafsi.

Idara ya nyumba na Maendeleo ya Makaazi

Mhe. Spika, pamoja na kwamba sheria ya *Condominium* inaendelea kukamilishwa, tunahimiza uharaka wa sheria hii kuletwa Barazani hapa ili

kuwapa fursa wale wanaotarajiwa kuuziwa nyumba za serikali zilizopo mjini, kuweza kununua nyumba hizo.

Kwa kuwa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi tayari imeshatoa waraka unaoelekeza utaratibu wa kuuzwa kwa nyumba za Serikali zilizoko vijijini, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba endapo mnunuzi wa nyumba hiyo hana uwezo na kulipa kwa pamoja, basi fursa ya kulipa kwa awamu itolewe ili lile lengo la Serikali la wananchi wanyonge waweze kuishi katika nyumba hizi za maendeleo litimie, vyenginevyo nyingi ya nyumba hizi zitaangukia katika mikono ya matajiri, huku wanyonge walioishi katika nyumba hizi kwa miaka wakibaki kuwa wapangaji na hata kuondolewa katika nyumba hizi.

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani inakumbusha ahadi ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ya tangu mwaka 2007/2008 juu ya mambo yafuatayo:-

- Sheria ya Uanzishwaji wa Shirika la Nyumba; na
- Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Kodi za Nyumba.

Ardhi

Mhe. Spika, Zanzibar inaingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki chini ya mwamvuli wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *Protocol* ya jumuiya hii iko wazi juu ya uwekezaji inatamka kwamba “Mwana Afrika Mashariki atakuwa na haki ya kuwekeza popote katika eneo la Afrika Mashariki na atawekeza kama mwenyeji (raia) wa pale atakapowekeza na kwa masharti yale yale ya mwekezaji mwenyeji.

Ni dhahiri kuwa mfumo huu ujao, wawekezaji kutoka Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi na Tanzania Bara watakuwa na haki ya kuwekeza hapa kwetu Zanzibar. Uwekezaji huo utahitaji ARDHI. Wako Wazanzibari wengi wenye ardhi zao na bila shaka kwa maendeleo yao na ya Zanzibar watapenda kuwa wabia katika uwekezaji huo, huku mchango wao ukiwa ardhi zao, na mtaji/mchango wa wawekezaji matajiri na wasiokuwa Wazanzibari utakuwa ni **FEDHA**.

Kwa mantiki hii, Kambi ya Upinzani inaishauri Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kuanzisha kitengo maalum kwa ajili upimaji wa ardhi, kufanya tathmini ya ardhi hizo *(land evaluation)* na kutayarisha Hati miliki au nyaraka *(Title Deed)* kwa Wazanzibari wenye ardhi zao, ili Wazanzibari nao wajiweke tayari kukabili wimbi la wawekezaji wanaokuja.

Mhe. Spika, mwananchi anayemiliki ardhi iliyopimwa, iliyotathminiwa na yenye nyaraka rasmi ana wepesi wa kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha kwa ajili ya mipango yake ya kibiashara na za kuwekeza na hii itasaidia sana juhudi za Serikali za MKUZA.

Mhe. Spika, imegundulika kwamba taasisi nyingi za Serikali hazina Hati miliki za maeneo wanayoyatumia. Hii ni hatari kwa vile wananchi wengi wanajitokeza kuhoji na kudai asili ya umiliki wa mashamba yao. Kambi ya Upinzani inashauri kwamba Serikali itoe muda maalum kwa taasisi zote za Serikali kuwa na Hati miliki ya maeneo yao.

Mhe. Spika, kompyuta imeruka kwa hivyo haya ambayo nitayasoma wewe hunayo, wala waziri hanayo, nafikiri mtayakuta kwenye *hansard*.

Mhe. Spika, imebainika kwamba katika shehia mbali mbali za hapa Zanzibar baadhi ya masheha na madiwani wamekuwa na tabia ya kuvamia na kuchukua madaraka ambayo si yao na kuchukua ardhi za serikali na mashamba ya watu binafsi na kuyapima viwanja na kisha kuviuza viwanja hivyo. Kama inavyofanyika hivi sasa katika Shehia ya Mtoni Kidatu, Fuoni Kibondeni, Mbuyuni Mkoani na maeneo mengine.

Tunaishauri Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwamba kila wanapopata taarifa za malalamiko haya wachukue hatua za haraka na masheha na madiwani na hata watu wengine binafsi wanaohusika na haya wachukuliwe hatua.

Mhe. Spika, tangu mwaka 1997, hii Mwenyekiti wangu ameisema kwa mkazo mkubwa, mimi naisema si kwa kuripiti lakini kwa kutilia mkazo zaidi ili ionekane kwamba kamati pamoja na huku upinzani letu moja katika hili.

Mhe. Spika, tangu mwaka 1997 serikali ilitenga eneo la Pwani Mchangani, Kiwengwa, Matemwe kuwa eneo maalum kwa viwanja kwa matumizi mbali mbali ya serikali, taasisi za serikali, uwekezaji, makaazi na huduma. Ni hivi karibuni serikali imetaka kutekeleza mipango yake hiyo.

Mhe. Spika, eneo la Matemwe mipango ya serikali ilipewa viwanja 220, eneo baina ya Matemwe na Pwani Mchangani viwanja 310, eneo la Pwani Mchangani ni viwanja 597, eneo la Kiwengwa viwanja 268. Huduma zilizopangwa ni skuli za maandalizi, skuli za msingi, skuli za sekondari, misikiti, madrasa, masoko, *supermarket* na maeneo kwa ajili ya mawizara na taasisi za serikali, pamoja na viwanja kwa ajili ya makaazi ya watu wengine binafsi.

Vile vile kuna asilimia kubwa ya viwanja hivi ni kwa ajili ya wanakijiji wa Matemwe, Pwani Mchangani na Kiwengwa. Viwanja hivi ni kwa ajili ya makaazi ya wanakijiji hao.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa upimaji wa viwanja hivyo kama utekelezaji wa mpango wa serikali kwa mujibu wa ilani ya CCM umeshindikana

kabisa, umegongwa mwamba. Kamati yangu ya Mawasiliano na Ujenzi juzi tarehe 23 Juni, 2010 ilikutana na viongozi wa Chama na Serikali wa Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na wa Wilaya ya Kaskazini 'A' na 'B' kutaka kujua kulikoni. Maana yake haiwezekani mipango ya Serikali ya CCM halafu ikashindikana kutekelezwa kwa sababu wanaohusika kuvuruga au kuzuia ni wana CCM tena pengine ni viongozi wa Serikali. Hii tunajiuliza kulikoni? Kuna nini?

Ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa suala hili na hivyo Serikali kuendelea na mipango yake Mhe. Spika, baada ya majibizano ya muda mrefu ilibainika wazi tatizo ni kwamba wananchi wanachochewa na baadhi ya viongozi wa Chama na Serikali kwa kutumia nyadhifa zao kufanya vitendo viovu vya kuwafukuza watendaji wa Serikali, wapimaji kutoka wizarani kwa mapanga, kung'oa alama zilizowekwa *(beckons)* na matusi ya nguoni kwa watendaji hawa ambao wametumwa na Serikali.

Hii ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, suala hili halina budi kupatiwa ufumbuzi haraka na wa kudumu ili Serikali iendelee na mipango yake. Mhe. Spika, endapo suala hili litaachiwa libakie hivi hivi, nakuhakikishia hakuna pahala pengine popote Serikali itakapoweza kutekeleza mipango yake kwa mujibu wa mipango waliyoipanga. Kwa sababu kila wanakijiji na kila pahala watasema kama Matemwe haikuwezekana na hapa kwetu haiwezekani.

Hii ni *precedence* na naomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuchukue muda wa kulijadili hili, ili tutakapoondoka hapa waziri na watendaji wake na viongozi wanaochochea wananchi, sisemi Chama wala sisemi Serikali, nasema viongozi hawa wanaochochea wananchi katika maovu haya, basi wajitambue nafasi zao, uchaguzi kesho kutwa.

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani kwa kweli inasikitishwa sana lakini inalaani vitendo vya viongozi wa vyama na serikali wanaotumia nyadhifa na uwenyeji wao kuchochea wananchi kupinga kutekelezwa kwa mipango ya maendeleo ya Serikali.

Nishati

Mhe. Spika, tatizo la *TENESCO* na *ZECO* ni tatizo la Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar. Tatizo hili ninalolizungumzia hapa ni juu ya ongezeko la bei ya umeme ambalo ni zito, ni kubwa, ni gumu na linahitaji ufumbuzi wa haraka.

Mwaka 2007 – *TANESCO* iliongeza bei ya umeme kwa asilimia 168 kwa Zanzibar, pia hapa juzi wameongeza tena bei kwa asilimia 34, kabla ya kuongezwa kwa asilimia 34 ya juzi, Shirika la Umeme Zanzibar *(ZECO)* lilikuwa na bili ya deni la shilingi bilioni 29. Kwa sasa bili hii ni zaidi ya kiwango hiki.

Mhe. Spika, uwekezaji mkubwa umefanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuanzia ule waya wa baharini unaotumika, waya wa baharini kutoka Tanga hadi Pemba uliogharimu 400 milioni *Norwegian Kronner* na huu unaotarajiwa kuwekwa kwa msaada wa *MCC* – kutoka Ras – Kiromoni hadi Ras – Fumba. Endapo tatizo hili halitapata ufumbuzi wa haraka, yawezekana kabisa uwekezaji huu mkubwa wa kihistoria na uliowashirikisha washirika wa maendeleo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na ambao ni muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi wetu na ustawi wa jamii ya Wazanzibari, ukawa ni joka la mdimu.

Aidha, kutopatikana kwa ufumbuzi wa tatizo hili kunaweza kuathiri sana maisha na ustawi wa Wazanzibari. Kwa kuwa miundo mbinu ya miradi hii (waya za baharini, waya za juu, maguzo, vituo vya umeme) ni mali ya *ZECO*, hivyo ni kwanini *TANESCO* wasiiuzie *ZECO* umeme kwa bei ya chini ya ile ya wateja wengine wadogo (*ZECO* ni mteja mkuu wa *TANESCO*) au angalau kwa bei ile ile ya Tanzania Bara. Hapa tunajiuliza kulikoni?

Mhe. Spika, hakuna lisilowezekana. Kama iliwezekana Baraza hili kuzungumzia suala la mafuta na gesi lisiwe jambo la Muungano na ambalo hilo kesho kutwa *inshaallah* litakuwa limefunguka na majawabu yatakuwa ni hayo hayo ya maamuzi yetu ya hapa. Ni kwa nini tusifanye mapinduzi katika hili na hili kulichukua kama funzo na kama changamoto, baada ya muda mfupi chini ya Serikali ya Umoja ya wa Kitaifa itakayoundwa mara baada ya uchaguzi wa mwaka 2010 ***(Insha Allah),*** kugeuza miundombinu hii niliyoitaja (waya za umeme chini ya bahari, waya za juu, maguzo, vituo vya umeme) badala ya kutoa umeme kutoka Bara kuja Visiwani, itoe umeme kutoka Visiwani kwenda Bara.

Mhe. Spika, haya yanawezekana, mambo mengi tulifikiria hayawezekani lakini Baraza hili hili limewezesha, ni *determination.* Nasema tunaingia katika awamu inayokuja *inshaallah* kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu na hili iwe ni *priority* katika wizara hii, inawezekana kabisa.

Mhe. Spika, *TANESCO* imesau kwamba sisi (Zanzibar) ni wateja wake wakubwa, imesahau kwamba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini ni nchi. Hili la kutuongezea bei na kututaka tulipe mabilioni ya shilingi (hata baada ya kutakiwa na Rais wa Muungano wasifanye hivyo) ni vitimbi vinavyoashiria hali mbaya ya huko twendako.

Kambi ya Upinzani inapongeza juhudi za Serikali za kupata majenereta mapya 32 (25MW) kwa ajili ya matumizi ya Unguja, kama hatua za awali za chanzo mbadala kwa umeme huu tunaoutumia sasa hivi.

Kambi ya Upinzani tunashauri kwamba kutokana na uchakavu wa vinu vya umeme huko Pemba, basi juhudi za mapema zichukuliwe ili kuipatia Pemba majenereta matano **5 (4MW)** kwa ajili ya matumizi ya huko, pia vile vinu vichakavu viuzwe mara baaada ya kupatikana kwa majenereta matano haya.

Mhe. Spika, kingine ambacho kompyuta imeruka ni hichi nitakachokisoma. Mhe. Spika, katika suala hili la nishati Kambi ya Upinzani inaendelea kumhimiza Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kuleta mbele ya Baraza lako hili tukufu mswada wa kuanzishwa kwa mamlaka itakayoshughulikia mambo ya nishati ya mafuta na gesi Zanzibar.

Tumefanya kazi kubwa, kazi ya msingi, kazi ya mfano, Wazanzibari wote wanacheka, lakini hatujaimaliza. Hichi kilichobakia Mhe. Waziri hebu tukimalize. Katika *briefing* ya mara hii tuliambiwa kwamba inawezekana kabisa kukawa na mkutano au kikao chengine baada ya hiki. Nashauri kabisa kabisa kama Mhe. Waziri utajipinda kweli hili tunaweza tukalimaliza katika Baraza hili la Saba. Nafikiri Baraza hili kwa kuongezwa siku moja au mbili kujadili mswada huu wa kuanzisha mamlaka itakayoshughulikia maendeleo ya petroli na gesi Zanzibar, hasa kwa vile baada ya kikao hicho itakuwa kila mtu anakwenda kufunga ng'ombe ambaye hana kamba, Mhe. Waziri tumalize kazi hii ambayo imeanza vizuri japo ilihatarisha maisha yako.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri asisahau kwamba kazi hii ilikaribia kugharimu maisha yake, ilijenga uadui mkubwa na watu wasiopenda maendeleo yetu. Sasa tusiishie hapa, umeianza – uimalize.

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani inaisihi sana Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme waache na waruhusu menejimenti ya *ZECO* kuwaajiri mafundi ambao wamewatumia karibu miaka kumi sasa. Wakati wa umeme vijijini Shirika la Umeme Zanzibar waliwachukua vijana wengi. Vijana hao katika kazi hizo za miaka kumi na hata hapa juzi mradi huu wa umeme kutoka Tanga kuja Pemba ni wao walioshiriki kikamilifu. Lakini taarifa tulizonazo ni kwamba bodi imezuia na pengine sababu zilizotajwa ni kwamba kuna *over employment*.

Mhe. Spika, mimi nasema kuwe na *over employment* lakini Shirika la Umeme Zanzibar lina upungufu wa mafundi. Sasa kama ni *over employment* pengine ni kwa watu wengine wasafishaji, wapiga taipu, watu wa bustani. Mimi nazungumzia *ZECO* ni shirika la kifundi na ufundi ni kusoma na uzoefu. Hawa kama hawana madigrii lakini wana uzoefu wa miaka kumi na ndio waliookoa katika miradi yote.

Tunawasihi Bodi ya *ZECO* iipe nafasi menejimenti ya *ZECO* watafute miongoni mwa vijana waliowatumia miaka kumi hadi leo ambao wanaajirika. Maana

wengine mtu ana miaka sitini huwezi ukamuajiri, lakini wako vijana, shababi, wana nguvu na wana uzoefu wa miaka hiyo kumi ni mafundi hata kama hawana madigrii wachukue nafasi hii. Mhe. Spika, *over employment* sawa, lakini nasema Shirika la Umeme wana mapungufu makubwa ya mafundi.

Mhe. Spika, nihitimishe kwa kuwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza. Nawaombea Wajumbe wa CCM hatma njema katika mchakato wao wa kupata ridhaa ya Wanachama wa Chama Chao na nawaombea wote waliomo Barazani humu awajaalie wawe wagombea katika uchaguzi wa Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi utakaofanyika Oktoba mwaka huu.

Aidha, nikushukuru wewe tena kwa kunipa fursa hii na nitamke bila kigugumizi kwamba **Naunga Mkono** hutoba ya Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2010/2011, nikiamini kwamba yale yote ambayo yatajadiliwa na Wajumbe wako yatazingatiwa kwa kadri inavyostahiki.

Mhe. Spika, hotuba yangu ilikuwa iwe ndefu lakini status uliyonipa kuwa Waziri Kivuli, Mjumbe wa Kamati ni kwamba yale yote ambayo yamezungumzwa hapa nilishiriki vizuri sana katika hotuba ya Waziri, nilishiriki vizuri sana katika kuandaa hotuba ambayo ameisoma Mwenyekiti, na hii nasema ni yale mambo ambayo niliona kwamba huku hatukuyazungumza. Kwa hivyo, hii ni ziada na nyongeza ya mchango wangu katika Baraza hili. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea katika mchango wa jumla, nimepata taarifa hapa kwamba kuna ndugu yetu, mwenzetu kutoka *Trustees Tanzania Limited* huyu anaitwa Chris Cooperman. *Can I request Mr. Cooperman to stand up to be seen at members. You are most welcome*. Yeye ni mwenzetu katika kampuni hiyo niliyoitaja na ndio ambao wametoa uhisani wa kuwafundisha vijana wetu pale Ras El Kheima. Tunamshukuru sana kuwa nae katika bajeti hii ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe sasa tuendelee na mchango wa jumla. Tuanze kumsikiliza Mhe. Ali Suleiman Ali, baadae tumsikilize Mhe. Ali Moh'd Bakari.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako hili tukufu kuchangia hotuba ya Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini Pemba, Wakurugenzi, Mameneja na wafanyakazi wote wa wizara hii

kwa kazi nzuri ambazo tunaamini zinatupa mwangaza tuliokuwanao hapa na mengineyo tunayotumia katika sehemu mbali mbali za nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi ya kusema, lakini kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii nzuri tu ambayo ina kila mwelekeo wa maendeleo katika nchi yetu. Kwa sehemu nisizozigusia kuzisema nimeshazipongeza na kwa nitakazozisemea kidogo ndio naongeza.

Mhe. Spika, mimi nawapongeza Mamlaka ya Maji toka kipindi cha mwaka 1995 nimo katika Baraza hili na pahala pangu ndio hapa hapa tulikuwa tuna matatizo makubwa sana Zanzibar nzima kutokana na huduma ya maji. Lakini mpaka kufika mwaka 2010 Mhe. Spika, pana kila sababu na si vibaya kuwaambia kwamba serikali kupitia wizara husika na mamlaka yenyewe kwamba imefanya mengi mazuri na bado bidii yao inaendelea nawapongeza kwa dhati kabisa.
Lakini Mhe. Spika, pamoja na pongezi hizo kuna kasoro moja ndogo tu hii inataka ushauri mzuri utekelezwe ili wananchi wangu wawe radhi na miundo mbinu hii ya maji inayoendelea.

Mhe. Spika, kwa bahati nilipoingia katika Baraza hili nilikuwa na wito wa mradi wangu mkubwa wa SEMUSO. Mradi huu uliunganisha kwanza majimbo mawili, Jimbo la Mikunguni wakati huo na Jimbo la Amani. Lakini baada ya marekebisho ya kukatwa majimbo upya mradi huu umeingia katika sehemu tatu, Jimbo langu la Kwahani sasa hivi, Jimbo la Magomeni, pamoja na Jimbo la Amani yenyewe wamebakia kama tulivyo. Sasa tatizo la maji hayaendi kama kawaida yalivyokuwa yanakwenda huko nyuma kwa sababu wanasema mradi sasa hivi umejiendeleza zaidi, mamlaka hii imetoa huduma ya maji mengi zaidi kuliko huko nyuma, lakini wananchi wangu bado katika baadhi ya sehemu hasa maeneo ya juu huku Muungano hawayapati maji.

Mhe. Spika, naiomba wizara kupitia Mamlaka ya Maji, namuomba sana Mkurugenzi kabla hatujamaliza Baraza hili tatizo la maji kwa wananchi wangu wanaoishi sehemu za Muungano juu wahakikishiwe wanayapata. Sizuii kitu hapa Mhe. Spika, wizara niliyoitangaza nitakuja kuizuia baadae, lakini leo nazungumzia maji sina matatizo nayo.

Mhe. Spika, hakuna jambo zuri katika maisha kuliko unayemwambia akufahamu. Lakini naamini Mamlaka ya Maji kuanzia Mkurugenzi na watendaji wake ni watu wanaofahamu na mradi huu kwao wao pia ni kama jina ambalo halitoki katika vifua vyao na nyoyo zao. Kwa hivyo, namuomba sana Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji suala hili ahakikishe linafanyiwa kazi ili wananchi waondokane na shida. Hakuna shida kubwa kama tunakotoka angalau afadhali,

lakini ile afadhali yenyewe iwe inapatikana mpaka hapo muhula wa mwisho utakapokamilika kuwe hakuna tatizo kabisa katika eneo hili.

Mhe. Spika, jengine ni Shirika la Umeme Zanzibar. Nilikwambia mapema tu Mhe. Spika, kwamba sina mazungumzo mengi kwa bahati kipindi cha miaka miwili na nusu iliyopita nyuma nilikuwa Mwenyekiti wa Wizara hii na miaka mingine kama mitatu minne nyuma vile vile, kwa hivyo nimekuwa mwenyeji sana.

Lakini kubwa tunaloliomba Mhe. Spika, Shirika la Umeme wanajitahidi na wameendelea kujitahidi, hata tukiangalia mazingira ya nchi yetu yaliyotokea si madogo. Nchi ilikuwa kama tuko vitani, Mwenyezi Mungu atunusuru tusiingie huko. Kwa sababu nchi ikifika katika vita maadui na mimi nilikuwa mwanajeshi najua mbinu zile za kufanya kwanza kata umeme. Tulikuwa katika giza ambalo halitabiriki. Kwa hivyo, nasema ile ni kama hali ambayo imejitokeza lakini bahati nzuri baada ya kutokea hitilafu hiyo ambayo hatuna uwezo nayo kuizuia, wizara kwa juhudi yake kupitia na serikali yetu kuu imehakikisha kwamba umeme ule unarudi kwa kipindi kinachofaa.

Mhe. Spika, wengine walithubutu kusema umeme utarudi baada ya miaka miwili na mengineyo, lakini Shirika la Umeme walisema tu kwamba kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu umeme utarudi na wananchi watafaidika na tumeona. Mhe. Spika, nawapongeza sana kwa hili.

Lakini pia kubwa ambalo wamelifanya wenzetu hawa baada ya serikali kuona kwamba pana haja ya kuweka kitu cha akiba imenunua majenereta 32 pamoja na matenki ya mafuta, wakati wowote inapotokea dharura basi wao watakuwa tayari kuwasha umeme wananchi wataondokana na adha hiyo. Kwa hivyo, nawapongeza kwa maandalizi hayo ambayo yanaendelea Mtoni kuweka *standby* katika mambo yote yatakayotokea huko mbele.

Lakini jengine Mhe. Spika, ambalo limetupatia faida kubwa sana wakati huo ndio nipo mimi, nasema lazima nijisifu kwa yale niliyoyafanya. Mradi wa umeme kutoka Tanga kwetu mpaka kufika Pemba, tuna wajibu kama alivyosema Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu, lakini hata Mhe. Hamad Masoud Hamad kwamba si jambo la masihara, ni jambo la kupigiwa mfano. Mhe. Spika, basi angalau wale Waheshimiwa Wawakilishi wa Pemba wangeandaa mikutano katika maeneo yao kumpongeza Rais wa Zanzibar, Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na kuwapongeza wafanyakazi wote wa Shirika la Umeme Zanzibar.

Mhe. Spika, si jambo dogo, serikali hapa imefanya jambo la historia katika nchi yetu hii. Mhe. Spika, Mhe. Hamad Masoud Hamad alisema karibu miaka 40,

mimi nasema sio 40 inafika hata miaka 70 hakuna umeme Pemba, lakini leo kuna umeme mzuri kuliko hapa Unguja.

Maana umeme wa Unguja bado hauna uhakika, lakini Pemba unawashwa umeme ule tarehe 9 nipo kule tulishtukia kwamba kama uliwasha feni lilikuwa linakwenda mwendo wa *slow match*, basi siku ile ilikuwa *goose match*. Kwa hivyo, hii inamaanisha wazi kwamba tumepata umeme wa uhakika ambao unakwenda kwa mwendo wa haraka unaotakiwa. Mhe. Spika, kama mwanajeshi *slow match* unakuwa hupati faida, lakini ukenda ule *goose match* ndio unapata faida. Mhe. Spika, tuishukuru serikali.

Mhe. Spika, katika Baraza hili tulipitisha sheria hapa na Mhe. Waziri alisimama hapo katika kiriri hicho hapo kama sisahau kuhusu tatizo la vifaa vya umeme hapa nchini. Mhe. Spika, dunia ya leo ni biashara huru, zamani wakati sisi wadogo tunasoma kulikuwa na Shirika la Mabasi Zanzibar, gari za abiria moja moja, lakini baadae likaondoshwa. Hata biashara ya maduka ilikuwa biashara zote unazotaka ukanunue mchele duka la ukoo. Lakini serikali ikasema biashara iwe huru. Hapa Mhe. Waziri alitoa kauli kwamba kuanzia leo wafanyabiashara wanaoweza kuleta vifaa vyao Zanzibar, basi walete, lakini vipitie katika kiwango kinachokubalika.

Mhe. Spika, bahati nzuri au bahati mbaya naweza kusema bahati nzuri maana wananchi wengi wamejitokeza wafanyabiashara. Lakini bado kuna adha ambayo inatokea, wananchi wanachelewa kuunganishwa umeme wao kwa kukosekana huduma hii ya vifaa mbali mbali. Ikiwemo nyaya za umeme hakuna. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kwa kuwa bodi ni chombo ambacho kimewekwa kisheria, lakini bodi sio watu wa *management* kama wao ni watendaji katika shughuli yoyote, wao ni wapangaji au kuelekeza.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri awape fursa wafanyakazi wetu wa Shirika la Umeme wawe na uwezo wa kusema kwamba tuleteeni vifaa hivi bodi isiingilie, hii inaleta adha sana. Mhe. Spika, kila mjumbe anayesimama hapa unasikia lawama zinakuja kwenye bodi. Siku nyengine bodi inakuwa sio bodi, maana kiongozi tu anaweza kuwa mmoja akaleta matatizo yake, ikaonekana bodi yote ni mbovu, kumbe sio kweli. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili aliangali, bado wananchi wana utata kwamba umeme haupatikani kuungwa kwa wakati kutokana na vifaa vya ukosefu kama nyaya na mambo mengineyo. Namuomba sana Mhe. Waziri ili kuendelea vizuri na watu kutafuta miradi yao ya maendeleo na kupata huduma hii, basi iwe kuna haja ya kufanya kazi.

Mhe. Spika, jengine ambalo nitaligusia hapa kidogo tu ni hili suala la ujenzi wa nyumba zetu za Michenzani. Mhe. Spika, katika ilani ya chama cha Mapinduzi pia nasema kwamba Rais kwa uwezo wake na anayekuja yeyote Mwenyezi

Mungu atakayemchagua, yaani anamjua yeye keshamchagua, sisi hapa tunapiga kelele tu. Lakini Rais ameshachaguliwa zamani na Mwenyezi Mungu, iliyobakia ni mchakato wetu mbio hapa na pale. Siku nyengine atatokea hapa hapa tulipo au kwengine, lakini anajua yeye Mwenyezi Mungu, tukiri kwamba anayechaguliwa ndio kamleta yeye mwenyewe Mwenyezi Mungu, hatuna ugomvi.

Lakini ninaloomba tu kusema kwamba Rais atakayekuja nyumba zetu zile zilizobakia za Bambi ambazo zimeendelea vizuri sana, bado mambo madogo madogo tu, kazi kubwa imeshafanywa, iliyobakia sio kubwa sana, kwa hivyo aziendeleze zile nyumba ili radhi za mzee wetu Marehemu Mzee Abeid Aman Karume ziwafikie viongozi wetu na wananchi wetu kule aliko alale vizuri awe hana mashaka. Kwa hivyo, nasema hilo ni suala zuri ambalo litaweze kuifanisha wizara hii ambayo imefanya kazi nyingi na nzuri.

Mhe. Spika, kuhusu Idara ya Ardhi na Usajili. Ukisoma kitabu hiki kuna malengo uliyojiwekea katika kukusanya kodi na mambo mbali mbali, lakini imepiga hatua kubwa sana. Mimi nampongeza Mkurugenzi na watendaji wake kwa kazi nzuri ambazo wamezifanya. Naamini kwamba hii ni ishara tosha kwamba hivi sasa hivi mwananchi wetu anajua kuwa ukitaka kiwanja uende panapohusika na kodi ulipe pale panapotakiwa ndipo mapato yao yanapopatikana.

Mwisho Mhe. Spika, ili kuokoa muda, na nilisema mapema leo sina mengi. Mhe. Spika, suala kubwa la nchi yetu hvi sasa ni uchumi na uchumi unatokanana mambo mengi. Tukiangalia hali halisi inavyokwenda katika ulimwengu wa leo, basi kila mwenye chake hujitahidi kukikamata na kukiendeleza ili apate maslahi.

Mhe. Spika, mimi naipongeza wizara pamoja na serikali yetu kwa mchakato mzima unaoendelea juu ya uchimbaji wa mafuta na gesi. Mhe. Spika, najua hili suala lina sheria zake na ninajua hiyo sheria imo katika mchakato wa dhati kabisa, lakini sio vibaya kwa sababu kama leo nimesikia katika *BBC* Mhe. Spika, wenzetu Democratic Republic of Congo, hivi sasa wamepata visima ambavyo wametiliwa hitilafu na hawa wachimbaji kutoka Uingereza, wameleta hitilafu kidogo. Wengine wanalaumu na wengine wanasema wanapongeza.

Mhe. Spika, lakini najua suala la mafuta lina hatari yake na suala la mafuta lina utaratibu wake. Kwa hivyo, mimi naiomba serikali kwamba wenzetu wa Norway ni watu wazuri, ni watu waliojitolea na ni watu wako karibu sana na Zanzibar. Kwa hivyo, tuwatumie wenzetu hawa ili kuhakikisha kwamba wanavifanyia kazi visima vyetu ili tupate mafuta. Congo wamesema wamepata visima viwili lakini vikubwa sana, vimekwenda karibu na mpaka wa Uganda. Kwa hivyo, anayewahi kuchimba ndio amewahi. Siku nyengine ukichelewa akichimba Uganda ndio umepoteza wewe. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri pamoja na juhudi hii

inayoendelea na Mhe. Waziri Kiongozi inasemekana rasmi kwamba barua ya mchakato huu kaipeleka kwa Mhe. Waziri Mkuu ili ifanyiwe kazi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na wenziwe wasichoke waendelee, kwa sababu madhali wewe unacho na mwenzako anataka kikuponyoke ili akucheke, sitegemei kama atakuwa na furaha kama ukipata moja kwa moja, sijui kwa mambo yetu ya Kiswahili tunajuana. Lakini mimi napenda kama mwenzangu anacho, basi aongezeke zaidi ili maisha yao watu yaende vizuri.

Mhe. Spika, baada ya hayo nampongeza sana Afisa Mdhamini Pemba kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa miaka 10. Mhe. Spika, kama angekuwa anapewa usheha, basi Afisa Mdhamini Pemba angekuwa keshaku Sheha bwana, tena keshakuwa mwenyeji kuliko hao wenyeji. Lakini nasema tu kwamba kasimamia kazi zake vizuri na kenda vizuri na anafaa Mhe. Waziri kwa hali na mali umwangalile Afisa Mdhamini Pemba kasimamia vizuri utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi bila ya kujali hofu wala kitu chochote.

Baada ya hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima narudia tena kauli yangu kwamba naikubali hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa bajeti yake ya mwaka 2010/11. Nawaomba na wajumbe wenzangu wote waikubali. Mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani naikubali bajeti hii kwa asilimia mia moja, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataallah, kwa kutuwezesha kuifikia siku hii ya leo tukiwa hai na wazima wa afya zetu, kwa sababu hiyo tukaweza kutoka huko tunakotoka na mpaka kufikia hapa ambapo sasa hivi tupo na kuweza kuendelea na mipango ambayo imetuleta hapa ndani.

Lakini pia nikushukuru na wewe kwa kuweza asubuhi hii kunipatia nafasi kuwa mchangiaji wa pili ili na mimi kutoa mawazo yangu kwa uchache.

Mhe. Spika, naomba sasa uniruhusu nimshukuru Mhe. Mansour Yussuf Himid ambaye ni Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa kuwa mfano na kielelezo bora katika nchi yetu hii kwa kupitia wizara yake na kazi aliyopewa kwa kushirikiana na watendaji wenzake.

Mhe. Spika, Mhe. Mansour Yussuf Himid, kama Mansour asingeweza kuifanya kazi hii peke yake kama sio mashirikiano ya karibu mno aliyopewa na watendaji wake. Alipata mashirikiano ya kitaalamu na yale mawazo tu ya kawaida ndio leo kila mjumbe mmoja anayesimama hapa, basi sifa yake ni kubwa zaidi kwake na wizara yake kuliko kile anachokichangia.

Kwa hali hii Mhe. Spika, naomba nichukuwe nafasi hii maalum, na niwaombe na mawaziri wengine wote waige mfano wa Mhe. Mansour Yussuf Himid pamoja na watendaji wake. Pia nisiwe mwizi wa fadhila kwa wizara hii ina Naibu Waziri Mhe. Tafana Kassim Mzee.

Mhe. Spika, Mhe. Tafana Kassim amefanya kazi ngumu katika mazingira magumu sana, kabla ya maridhiano haya ambayo yamefikiwa na viongozi wetu hawa wawili wakuu. Mhe. Tafana Kassim alikuwa akija kwenye vijiji vyetu kule Pemba, yeye mwenyewe haamini hata maisha yake yatakuaje. Kwa sababu kuingia katika vijiji halafu ukajulikana kuwa ni waziri wa CCM, kwa kweli inakuwa inatia mashaka, lakini aliweza kufanyakazi kwa kushirikiana na jamii. Kwa kweli kila alikokuwa akienda watu walikuwa wakimpenda sana, kwa sababu hakuweka itikadi ya aina yoyote mbele, alikwenda kushughulikia lile ambalo waziri na wizara imemtuma. Kwa sababu hiyo ndio akaweza kukaa katika hali nzuri sana pamoja na jamii katika mazingira magumu na leo hii baada ya maridhiano haya ameweza kujipatia sifa zaidi kule kwetu kuliko waziri yeyote mwengine.
Mhe. Spika, kabla sijasahau nataka nianzie huku juu kwenye huu mradi wa usambazaji wa umeme vijijini. Mhe. Spika, kwanza nashukuru sana kwa wizara pamoja na vitengo vyake kuona kwamba sasa ipo haja ya kumalizia umeme katika maeneo ambayo hayajafikiwa. Mhe. Spika, hili ni jambo jema na ni jambo zuri. Kwa sababu kila mtu aliye hai au kila mmoja anahitaji umeme na maji na kwa hivyo, ni jukumu la serikali kwa kupitia wizara hii kuhakikisha kwamba maeneo yote ya Zanzibar yamepata umeme na maji, libaki tu suala la kwamba nani ana uwezo avute na mwengine hana uwezo basi, lakini iwe ule umeme umefika katika maeneo ili kufanya kwamba watu wote waishi katika hali moja.

Mhe. Spika, umeme unasaidia uchumi na mambo mbali mbali. Kwa hivyo, nadhani ukishafika umeme huko, basi yale manung'uniko ya wapi wamepata na wapi hawajapata yataondoka na zile shutma za wawakilishi kwamba labda wamependelewa au wabunge wamependelea tu maeneo yao wanayokaa, lakini mengine hawayasemei basi itakuwa imeondoka.

Lakini kwa hali hii Mhe. Spika, mimi niseme kwamba nampongeza Mhe. Mansour Yussuf Himid, kwa sababu ya vijiji vyangu viwili ambavyo vimebaki kupatiwa umeme. Kijiji cha Mgeni nje ambapo Mhe. Naibu Waziri alitaka mke kule lakini hatapewa na kijiji cha Uondwe. Vijiji hivi vimeingizwa katika bajeti hii, hata wao wakisikia kwamba vijiji hivi navyo vimeingizwa katika bajeti hii watapata matumaini ya kuamini kwamba jambo hili wakati wowote litawafikia na wao.

Mhe. Spika, kama suala hili lisingezungumzwa humu, basi ingekuwa sasa ni kupapatua, lakini madamu limezungumzwa humu, maana yake ni kwamba sasa

hivi ni ufuatiliaji tu uliobakia, ni mimi na wizara kwa wakati ule ambao utakuwa ni muafaka kutenda hili. Lakini kazi iliyobakia ni ndogo mno. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba mno kwa imani yako, nia yako na watendaji wako hivi vijiji navyo viweze kupata umeme haraka.

Lakini Mhe. Spika, sambamba na hili. Kule kwetu kuna kijiji kimoja kinaitwa Kikunguni ambacho Sheikh Said Ali Mbarouk alizaliwa huko. Pia nashukuru kwamba kimetajwa na nashukuru kwamba utaratibu wake unaendelea. Lakini kwa sababu kutaja tu sio kitu, unaweza ukataja halafu ukawa hufanyi. Lakini kwa nia ya wizara hii na Mhe. Mansour anavyofanyakazi na mimi Ali Moh'd, anavyofanya kazi zake kwa uadilifu, kwa karibu zaidi na kwa kutaka kwamba kila mtu apate kile kizuri, basi naamini na ufumbuzi wa kupatiwa maji watu wa Kikunguni Begelei na wenyewe utafikia pahala ambapo ni matarajio yao wao. Kwa sababu zimepita siku nyingi toka Sheikh Said Ali Mbarouk anapapatua mpaka nimekuja na mimi mwakilishi napapatua na leo *Alhamdullilah* tumefikia pahala ambapo wao wenyewe wakisikia basi watakuwa wamepata matumaini zaidi.
Licha ya kwamba hivi karibuni tulikwenda na Mkurugenzi wetu wa maji kule Sheikh Moh'd na tukazungumza na wenyeji wa kule, badala yake Sheikh Said akaleta halua kidogo kwa ukarimu wake basi na mambo yakazidi kuwa mazuri kutokea hapo. Sheikh Said mnamjua tena Mhe. Spika, ni mtu mmoja mzuri sana, tokea arudi Maka basi amekuwa ni kielelezo kizuri.

Mhe. Spika, mimi nataka niipongeze wizara tena kwa kusimamia vijana wetu wa Zanzibar, kwenda kupata mafunzo ya kitaaluma yatakayokuja kuwawezesha kusimamia suala hili la uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

Mhe. Spika, hata kama tungechimba mafuta kesho na keshokutwa, basi tungelazimika kupata wataalamu na wakati mwengine kumpata mtaalamu mmoja tu, anaweza kuwa yupo, lakini kwa kuwa anajua mimi ninahitajika na hawa hawana, basi akakuambia mimi ni lazima unilipe kiasi fulani. Kwa sababu sisi katika nchi yetu tumezowea kufanyakazi kwa kujitolea zaidi kuliko kile kipato, basi tungeathirika na kwa sababu wanajua kwamba haya mafuta yana thamani kubwa zaidi, kwa hivyo na mimi nilipwe kwa thamani ile ile ya kitu nitakachokifanya.

Mhe. Spika, mimi nimefurahi sana na ninaipongeza sana serikali kwa kuamua kwa makusudi kufanya lile la kwanza, kuliko lile la tatu ambalo litafikiwa nalo. Mhe. Spika, kuwasomesha vijana ni jambo moja muhimu mno. Wakija hapa watakuwa na ushauri, watatumia taaluma yao vizuri, wataishauri serikali na watashauri nini kifanyike kwanza ili tuweze kufikia haya malengo ambayo tumekusudia.

Mhe. Spika, katika hili licha ya kwamba bajeti hii imetaja na hata bajeti ya Waziri Kiongozi imetaja na bajeti ya Waziri wa Fedha na Uchumi haikutaja, lakini baadae yeye mwenyewe alikuja kutaja. Ni kwamba suala hili la mafuta na gesi asilia limeandikiwa na Mhe. Waziri Kiongozi kuwa litolewe katika orodha ya mambo ya Muungano kama Baraza lilivyopitisha. Mimi hiyo ndio imani yangu kuwa hili litatolewa.

Mhe. Spika, lakini binadamu ana kasoro zake, unaweza kumtarajia kwamba afanye lile ambalo wewe umeshaliamua. Mhe. Spika, kule kwetu kuna mtu mmoja alikuja kutaka mke mahala, halafu akatoa pesa, baadae ikapangwa harusi. Ile siku aliyokuja kuoa ndio siku aliyorejeshewa pesa na kuambiwa hatukutaki. Sasa yeye keshafanya mambo mengi tu huko, keshapata matumaini na mpaka siku ile keshaalika karamu na watu wameshakula, wameshakuja kule Tumbe kuoa, halafu akiwa amekaa kwenye jamvi, lilitokea jambo dogo tu, akaambiwa bwana chukua pesa zako hizi ondoka. Kisha akatafutwa mtu ndugu na yule mke akaozeshwa na mpaka leo anaye yule mke.

Mhe. Spika, sasa wasi wasi wangu ni upi, kwamba tumepitisha maamuzi hapa kila mmoja kachangia, kila mmoja katowa mawazo yake kuhusiana na suala hili la uchimbaji wa mafuta kwamba iwe ni rasilimali ya Zanzibar kwa maslahi ya Wazanzibari wenyewe. Maamuzi hapa yameshafikiwa na mambo mengi yameshaletwa hapa. Halafu hii barua aliyoandika Waziri Kiongozi kama agizo la serikali. Halafu mtu mwengine huko analeta barua na akileta hiyo barua kama tulivyokubaliana hapa itakuwa *Alhamdulillah* uungwana umepita. Lakini akifanya vyenginevyo Mhe. Spika, bado hili ni suala la Wazanzibari.

Mimi binafsi Mhe. Spika, ikiwa nitakuwepo katika Baraza hili na Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake atanijaalia niwemo, lakini ikiwa sikuwemo hao watakaokuwemo basi bado suala hili wataling'ang'ania kwamba ni la Zanzibar popote pale. Suala hili tunahitaji ushauri kwa njia zile za kistaarabu, kwa sababu chama ni kimoja kinachounda serikali mbili. Kwa hivyo, wakati mwengine lazima ustaarabu ule wa kutawala ufuatwe, lakini ikipelekea kwamba suala hili linashauriwa sana, aah! Subiri kwanza nimtafute nani tushauriane.

Mhe. Spika, itakuwa hizo ni dalili kwamba watu hawataki na hii ni mali. Ingekuwa ni maembe huko angekuambia kaokote tu, lakini hii ni mali, sasa kama ni mali iko ndani ya mishipa ya damu ya kila mtu. Kwa hivyo, mtu anaweza kukubali kirahisi na mwengine akaona hapana, mimi hapa sikubali mpaka na mimi nipate shea yangu na kwa sababu wenzetu hawa wanapata shea zaidi katika kisiwa chetu hiki kuliko sisi tunayoipata kwao, basi wanakuwa na ugumu wa vitu kama hivyo.

Mhe. Spika, tulipofikia ni pazuri ni karibuni asilimia 90, lakini asilimia 90 hiyo unaweza ukapigwa buti, ukarudi tena kule kule kwenye asilimia 0. Mhe. Spika, mimi nasema kwamba katika jambo hili ikiwa barua imeletwa kwa njia zile zile za dhamira na makusudio yetu, basi yatabaki kuwa hayo ni maamuzi ya Baraza. Lakini ikiwa hilo halikupita Mhe. Waziri Mansouri Yussuf bin Himid bin Maftah utalazimika kuendelea kujitoa muhanga kwa sababu ya Wazanzibari, uhakikishe kwamba rasilimali yao imebaki kuwa ni mali ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, tunahitaji ustaarabu uchukuwe nafasi yake, lakini kama pakipita mambo mengine, ukiwa bado ni waziri na ukiwa utakuwa bado uko hai basi usijali nafsi yako, wajali Wazanzibari walio wengi. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atakupa lililo na kheri na atakupa heshima kubwa sana kwa Wazanzibari, utakapokuwa hupo duniani basi itakuwa ni kielelezo kizuri sana kwa Wazanzibari kuwa alikuwepo Mansour Yussuf Himid hapa. Ndio atakapokuwa hayupo duniani basi watu watamsema kwa mema yake.

Mhe. Spika, pia niwashukuru Wazanzibari wote na niwashukuru Wazanzibari kwa sababu gani. Lilipotokea tatizo la umeme hapa basi Wazanzibari walikuwa wastaarabu sana, hata kama sisi tulikuwa wapinzani tunayo ya kusema tungeilani serikali, huwa yakitokea matatizo kama yale na kwa muda mrefu kama ule, hata kama tatizo lile halikusababishwa na serikali, lakini unalo la kusema. Lakini sisi hatukusema tulikaa kimya.

Mhe. Spika, siku moja nilikuwa Tumbe kule. Wewe unakujua Mhe. Spika, unakuja kila mara. *(Vicheko/Makofi).*

Mhe. Spika: Anataka kuanza kutoa siri zetu.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Nilimuandikia ujumbe Mhe. Mansour Yussuf Himid, nikamwambia Mhe. Mansour mtu yeyote atakayekusema kuhusiana na tatizo hili la suala la umeme, basi iambie ile Kamati ya Wajinga Barazani tutafanya kazi sisi, wewe kaa kimya.

Sisi hapa Mhe. Spika, tuna kamati yetu tunaita Kamati ya Wajinga, ikiongozwa na Sheikh Omar Ali Shehe. Lakini Mwenyezi Mungu alijaalia kwamba kila Mzanzibari mwenye akili timamu aliliona suala hili kuwa sio la serikali, aelewe suala lile ni bahati mbaya imetokea. Kwa hivyo, watu wakashirikiana katika subira na watu wakashirikiana katika kutafuta ufumbuzi. Leo *Alhamdulillah* umeme umekuja.

Lakini si hilo tu ambalo limeanyika serikali pia imechukua hatua za tahadhari ambazo kama litatokea tatizo kama lile, basi lisijirejee tena kwa kiwango kile. Ndio maana kumeletwa majenereta mengi. Kwa hivyo, mimi napongeza hatua hii

sana tena sana. Naipongeza kuwa ni hatua ya kiungwana kabisa na kwa sababu muungwana Mhe. Spika, haumwi na nyoka mara mbili kwenye shimo moja.

Mhe. Spika, baada ya kutokea tatizo lile serikali ikaona hapana, wacha tufuatilie hili, lakini baadae tufuatilie suala la ziada. Hapa ulitajwa umeme wa jua na kadhalika, ni kuonesha kwamba tunatafuta hatua nyengine madhubuti zaidi, kama litatokea tena lile basi lisiathiri jambo lolote katika nchi hii.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba wewe mwenyewe binafsi, kwa niaba yangu mimi na watu wangu wa Tumbe nipelekee salamu zangu za dhati, na kwa sababu leo ni siku ya Ijumaa, Mhe. Sheikh, Al Haji, Dk. Amani Abeid Karume kwa uongozi wake na kwa ujasiri wake aliotupelekea mpaka tukafikia hapa leo. Hapa vingozi wengi walitaka wafikie lakini hawakufikia.

Hapa panahitaji ujasiri na roho ngumu na sidhani kama kila wakati alikuwa akisifiwa tu na watu wa chama chake. Hufika wakati akasifiwa, lakini mambo mengine yanahitaji ujasiri wa uongozi wa utawala. Kwa sababu mtawala yeyote ni lazima afike mahali atowe ile *administrative language*, kwamba hapa natoa lugha hii kwa sababu ya maslahi ya watu fulani, hata kama kuna watu wengine wao hawayataki. Lakini atakapokuwa katika lugha hiyo, basi siku za mbele ataeleweka na leo Dk. Aman Karume kaeleweka nini dhamira yake katika nchi hii.

Mhe. Spika, ndio maana kila mtu mwenye akili timamu akiwa ndani ya nchi hii au akiwa nje ya nchi, basi anapaswa kuiga mfano huo. Kuna wengine waliodiriki kuamua kusema kwamba aongezwe muda, watu walitaka aongezwe muda kwa sababu ya mema yake. Lakini kwa sababu sisi hapa tunaongozwa na katiba, hatuendeshwi na mizengwe basi katiba ikachukua mkondo wake kwamba hapana, tumpe heshima yake, tumsifu, tumpe matarajio na baadae tumwambie apumzike atakuwa mshauri basi. Lakini kama ni suala la kwamba anastahili apatiwe muda, basi ni Dk. Aman Karume ndiye alistahili kupatiwa muda kutokana na mema yake aliyowafanyia Wazanzibari leo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nakupa ujumbe huu ambao ni utumwa na utumwa usipotekelezwa basi bado itakuwa hujatenda haki. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya watu wa Tumbe kampelekee salamu hizo Dk. Aman Karume kwamba watu wa Tumbe wanampongeza sana na tunamtakia afya njema, tunamtakia maisha mema atakapokuwa nje ya madaraka bado aendelee kutushauri. *Inshaallah* yeye ni Mzanzibari na tunahitaji ushauri wake wakati wowote na popote pale kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, niende sasa kwenye Mamlaka ya Maji. Mhe. Spika, Mamlaka ya Maji zamani kabla hakujakuwa na mamlaka hii, ilikuwa tuna usumbufu mkubwa

sana wa kupata maji. Lakini wizara na serikali ilipoona kwamba sasa imilikishe maji kwenye mamlaka kwa kweli tumefikia pahala pazuri, licha ya kwamba kuna changamoto ndogo ndogo, kwa sababu katika kila jambo jema lolote gumu ni lazima hapa katikati kabla ya kufikia malengo halisi basi unapata mashakili mbali mbali.

Kwa hivyo, wale ambao wamewahi kupatiwa huduma hii, wao wanaona wamependelewa na wengine ambao wanaona kama wamechelewa wanaona kwamba wao hawapendwi. Ndio kawaida kwa sababu hatufanyi vitu kama *Kunfayakun*, maana yake Mwenyezi Mungu ndio anasema jambo kuwa likawa pale pale, ama nchi au pahala au vyovyote vile, amri ile anayo yeye tu. Lakini sisi binadamu lazima tufanye taratibu leo tuanze hapa na kesho pale kwa awamu.

Kwa hivyo, wale waliopata maji mapema basi wasijione kwamba wao wamependelewa zaidi na wengine ambao hawajafikiwa wakaona kwamba wao hawapendi, hapana. Ni masuala ya utaratibu, kwa hivyo mimi nayasifu Mamlaka ya Maji kwamba imetimiza na imetekeleza wajibu wake. Naamini kabisa utafika wakati huu usumbufu wote utaondoka, kwa sababu kazi zinafanyika kila siku tunaona miundombinu mbali mbali, ile mibovu inaondoshwa na mingine mipya inawekwa ili kuhakikisha kwamba wanapunguziwa Wazanzibari usumbufu wa kupata maji.

Mhe. Spika, katika hili niseme kwamba kuna hii mifereji ya nje inayowekwa, ile inasababisha mazalio ya mbu tu, maana yake wanakwenda watu wazima wenye akili timamu wanamwaga maji ovyo tu au watoto wanamwanga maji ovyo ovyo na ukisema wazee wao wanakuwa wakali, wanataka wakupige au wanakutukana. Kwa hivyo, mimi nadhani mamlaka ya maji isimamie suala hili ili kuhakikisha kwamba mirefeji iliyoko kule inaundiwa kamati, licha ya kuwa hizo kamati zipo lakini zinafanyakazi kwamba yale maji ni hidaya hayatumiki ovyo ovyo au watu wanakwenda wakiyamwaga tu.

Mhe. Spika, nizungumzie suala la Mamlaka ya Mji Mkongwe. Mji Mkongwe Mhe. Spika, ndio Mji Mkongwe. Hapa kwetu unahitaji kufanyiwa kazi sana. Mhe. Spika, watu wengine wanautaja Mji Mkongwe kwamba ni kielelezo kizuri sana hapa Zanzibar. Lakini mji wetu Mhe. Spika, unanuka na haufai, ukiwacha hiyo bustani aliyosema Mhe. Mansour ya Forodhani kule, pale tu ndio pazuri. Lakini ukiingia humo kwenye majumba yenyewe na muna mwahali mwengine ni muchafu, kunamwagwa vinyesi ovyo ovyo na kunafanyiwa kila aina ya balaa.

Kwa hivyo, mimi nadhani mamlaka hii ione kwamba lile ni eneo pekee ambalo linatembelewa na wageni zaidi kuliko huko mahoteli, wale wageni wanakwenda mahoteli kwa kulala tu. Kule kwenye Mji wetu Mkongwe huwa ndio wanakuja pale kwa muda mwingi sana na kupiga picha zao, halafu baadae wanakwenda

kwao na kutudharau na vitu kama hivyo. Kwa sababu ya kushindwa kusimamia ile mamlaka hasa na tukaiweka katika mazingira halisi na mazuri. Mji umekua ni mchafu.

Kwa hivyo, hilo jina la Mji Mkongwe Mhe. Spika, na huo uchafu uliomo mule ni sawa sawa tu. Ni lazima Mhe. Spika, madamu kuna mamlaka basi isimamie wajibu wake kama inavyosimamia Idara ya Mamlaka ya Maji, isimamie majukumu yake na ihakikishe kwamba inaweka mazingira ya mji wetu katika hali ya usafi.

Mhe. Spika, ukija pale Darajani hapafai pananuka, wakati wowote tu, pakiwa pana uchafu pananuka na ikiwa hapana uchafu pia pananuka, hii imekuwa ni balaa. Sasa mimi naomba Mhe. Spika, mambo ya kuyafanya yapo tu. Mhe. Spika, unapompa mtu kazi huwa zile kazi za kuzifanya zipo, kwa hivyo lazima kazi wazifanye.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, kwa sababu namuona Mhe. Omar Ali hapa, kamanda wangu ananiashiria kitu fulani hivi na wewe unaniangalia, basi niseme kwamba naunga mkono bajeti hii kwa asilimia zote zile mia tulizokubaliana hapa. Pia nimalizie kwa kusema kwamba nawapongeza watendaji wote pamoja na waziri mwenyewe na endeleeni kuwa hivyo kwa maslahi ya nchi na wananchi wenyewe pamoja na vizazi ambavyo kesho na keshokutwa vitakuja. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa mashirikiano makubwa katika kutekeleza shughuli zetu. Waheshimiwa Wajumbe kuna tatizo, kwamba inapofika wakati wa kikao cha jioni kwa kweli hali inakuwa ni ngumu sana humu ndani ya ukumbi. Chombo chetu hiki tunategemewa tuwe wajumbe kama 78 nafikiri kama hivi, lakini wanaokuwepo pale tunapoanza kazi jioni hawafikii 15. Sasa hali inakuwa ni ngumu sana, huwa inanipa tabu sana hasa pale tunapokaribia kutaka kupitisha shughuli zetu, ambapo kiutaratibu ni lazima *quorum* ipatikane ya zaidi ya nusu.

Sasa niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe, inaeleweka kwamba msimu huu tuna mazingira magumu sana katika maeneo yetu huko. Lakini pia inaeleweka kwamba jukumu la Baraza hili ni kupitisha bajeti ya serikali itakayotumika kwa mwakani wa fedha. Kama itashindikana kupitishwa kwa kweli haitokuwa vizuri kwa serikali ijayo kuweza kutimiza majukumu yake, kwa mujibu wa taratibu za katiba na taratibu za matumizi.

Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe tukumbukie wajibu wetu huo, ili tufike katika ukumbi huu mapema tuendelee na shughuli zetu tusije tukamaliza ule muda ambao ratiba tumeipanga na tukashindwa sasa kujadili

baadhi ya hotuba za bajeti za wizara nyengine. Kwa sababu muda ukiendelea zaidi ya tarehe 16, kwa kweli hali itakuwa ngumu sana huko mbele, yale majukumu yanayotufanya tusiweze kuja hapa yatakuwa ndio sasa yameingia katika wakati wake hasa.

Kwa hivyo, niwaombe sana kwamba jioni tuwe tunafika mapema saa 11:00 ili tuweze kuendelea na shughuli zetu hizi bila ya matatizo yoyote. Kwa maana hiyo basi niwakumbushe waheshimiwa, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Haji Faki Shaali, Mhe. Said Ali Mbarouk na Mhe. Hija Hassan Hija. Hawa pamoja na wengine wote basi tujitahidini kufika saa 11:00, lakini hawa watakuwa wa mwanzo katika kuwaita kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru na baada ya hayo basi naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika. *Bismillah Rahman Rahim*.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kutuweka jioni hii ya leo tukiwa hai. Vile vile nikushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi (*Alhajj*), Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu, Wakurugenzi pamoja na watendaji wake wote kwa jumla *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, nilijua kwamba nikimwita *Alhajj* watu watacheka. Lakini kuhiji hapa unaweza kuhiji. Kwa kweli kuna mambo ndani ya kitabu ambayo nitayaeleze, ambapo ni ishara kuwa ya kuhiji na kupewa jina la *Alhajj (Kicheko/Makofi)*.

Kwa kuwa kuna mambo ambayo Mwenyezi Mungu ametuambia tuyafanye hapa duniani, ambayo yenye kuleta heri na hiyo ni benki kubwa kwa akhera tunakokwenda. Mhe. Spika, naomba kuyataja hayo mambo yenye ni kama hivi yafuatayo. Kusaidia jamii, kusambaza maji, umeme, kuwatengezea nyumba masikini waliokuwa hawajiwezi. Sasa haya yote kwenye kitabu hiki yamo. Je,

bado hajahiji hapo? Mhe. Spika, tayari ameshahiji Mhe. Waziri *(Kicheko/Makofi)*.

Baada ya hayo nianze na mchango wangu kuhusiana na Mamlaka ya Maji naanzia hapo kuonesha kwamba kijana wetu tayari ameshahiji. Mhe. Spika, sote ni mashahidi katika miaka ya nyuma wakati sisi tulipokuwa wadogo, kwa kweli tulikuwa tukipata tabu sana ya maji.

Lakini leo *Alhamdulillah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kumpa kijana wetu nguvu kujiamini na kuhangaika na wataalamu pamoja na wakurugenzi wahusika wa Mamlaka hii, kwa ajili ya kutafuta miradi na leo tunaiona, yaani tumekuwa mashahidi sote. Kwa mfano, tunaona mabomba yanalazwa, barabara nzuri mpya lakini zinakatwa kwa ajili ya kupitisha mabomba ya maji, yote ni heri na wala tusilalamike *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, hii ni moja miongoni mwa neema iliyotuingilia katika nchi yetu. Kwa kuwa wananchi wanapiga kelele maji. Sasa katika maeneo mengine Mhe. Spika kweli kuna matatizo nakubali maji hakuna, lakini sehemu nyengine yapo yanakuja taratibu.

Kwa mfano, hivi sasa *Alhamdulillah* katika Jimbo la Kitope baadhi ya sehemu pamoja na majimbo ya jirani ya Mfenesini na Bumbwini tunao mradi wa *ACRAA*. Kwa kweli wananchi wenyewe wamejidhatiti kuyalaza mabomba na wala hawakungojea Mamlaka, wamesema wakati neema imetufikia basi tuiwahi pamoja na kukidhi haya kutokana na ule mradi ulivyotakiwa umalizike. Hivi sasa kwa kiasi kikuwa tumeshatandika mabomba mengi.

Hii ni heri kubwa au benki na kuliko kuchukua fedha na kupeleka kule *PBZ* au *Barclays*. Mhe. Spika, hii ni benki ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu unawatafutia wale waja wake na hususan kwa wale watu wanaoswali. Kwa mfano, wakati mwengine msikitini maji inakuwa ni matatizo, lakini leo *Alhamdulillah* maji kwenye misikiti yamo mengi tu. Kwa hivyo, hii ni moja miongoni mwa neema ambayo tunasema tayari ameshahiji Mhe. Waziri, yaani *Alhajj (Makofi)*.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba yapo maeneo maji hakuna na ninaamini Mhe. Waziri atayatimiza. Kwa mfano, Kiwengwa hivi sasa maji hakuna na Mhe. Waziri nataka anisikilize vizuri na sababu kubwa inayofanya ukosefu wa maji ni ile *Hotel* ya *Going* umeme umekatwa, Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme ananisikiliza na *Inshaallah* na wewe Mwenyezi Mungu atakupeleka kuhiji, lakini anzia hapa.

Kwa kweli umeme umekatwa na wale wenzetu hatujui kama hawalipi au kumetokea matatizo. Lakini kisima chao wale wanatumia mashine, ambapo wananchi wanafaidika kutokana na kisima hicho pamoja na mashine hiyo. Mhe. Spika, wananchi wangu wanapata tabu sana.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri (*Alhajj*) kwa mashirikiano na Naibu Waziri pamoja na watendaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar. Kwa hivyo, tusaidie hali ni ngumu wananchi hawapati maji kabisa. Ikiwa ni tatizo la ufundi basi Meneja wa Shirika la Umeme tusaidie, ikiwa ni deni ni vyema wakalipa kwa *installment*, lakini almuradi wananchi wapate maji kama si hivyo tutafute mbadala, ili tuweke *line* nyengine kwa ajili ya kupata maji wananchi wale bila ya kutumia kupitia sehemu za hoteli.

Hili nalo tulione Mkurugenzi wa Mamlaka na tujitahidi kuondoa njia ile kwa sababu itakuwa kila siku hawalipi umeme kwa makusudi na wala sio lengo lao. Hivi sasa tayari *season* imeshafika hawawezi kuwa wasilipe umeme, kwani wageni wakija itabidi wakae kwenye kiza na hivyo haiwezekani.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar nakuelewa umekwenda kuhiji na itimize hija yako hii. Kwa kweli ninayo imani kubwa sana kwa uongozi wa Mamlaka hii, yaani hawa watu wanatusaidia sana *Alhamdulillah*, kwa sababu wanafanyakazi kama vile Wachina.

Mhe. Spika, nikisema niwatafute saa 1:00 za asubuhi, basi wanasema niko afisini na ninawakuta kweli, niwape pongezi, yaani sijui wakati gani wanakula, kusali pamoja na mambo mengine, lakini wanajua wenyewe. Kwa kweli wanafanyakazi masaa 24 naweza kusema Mhe. Spika, vile vile saa 12:00 asubuhi tayari wameshafika, utawauliza wamelala hapo. Hivyo, yote haya kwa ajili ya kuwatafutia wananchi maji safi na salama, ili tuondokane na tatizo la maji kutokana na kuokota maji ovyo, ambayo si safi na salama.

Sasa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba suala hili lipatiwe ufumbuzi wa haraka, ili wananchi wangu wa Kiwengwa wapate maji safi na salama. Kwa hivyo, atakapokuja kufanya majumuisho Mhe. Waziri anieleze kwamba kesho wananchi wako watapata maji, basi nitainua mikono na hasa mimi nilivyokuwa sharifu wa Mchangani *Allahhuma Amina (Makofi)*.

Pamoja na hayo, bado ninalo deni kwa Mkurugenzi wa Mamlaka kisima cha Kinduni. Mhe. Spika, niliambiwa baada ya kumaliza Chaani basi gari itakuja kwa *free*, lakini baada ya kufuatilia naambiwa gari mbovu. Sasa ubovu wake na mimi nitafute, ili tuweze kuchangia labda limesimama tulisukume na hatimaye sijui limekwenda wapi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, ili aweze kutusidia na wananchi wa Kinduni waweze kufaidika. Kwa maana hiyo, ule Mradi wa *ACRAA* sijui kama maeneo yake utafika, isipokuwa maeneo ya Kitope A na B, pia sehemu ya Mkaduni, Fujoni, Kiombamvua naamini huko wataneemeka mara moja kutokana hatua iliyofika, lakini Kinduni tutakawia. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, aturejeshe kwa kutuletea kisima hicho.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa wa 25 kuhusu uuzaji wa nyumba, hapa naomba kuuliza swali dogo. Kwa kuwa tulipitisha hapa vizuri kwamba hizi nyumba kongwe ziuzwe, watu walijitokeza ambao wako tayari kwa ajili ya kununua.

Lakini baadaye tukasikia zimezimamishwa zisiuzwe tena. Je, suala hili ni kweli Mhe. Waziri? Kama ni kweli kuna sababu gani, ambazo zimepelekea hali hiyo ya kusitishwa, kwa sababu maboma yapo mengi tena yanaota mwitu, ambayo yanakuwa ni maficho ya wadudu hatari kama vile nyoka na hata chuwi na watu wanapiga kelele. Hivyo, watu wanasema itakuwaje Baraza la Wawakilishi tayari limeshatoa maamuzi na halafu baadaye kuna mtu anatengua, basi mimi nikawa na wasi wasi kuhusiana na suala hili.

Kwa hivyo, nilijua wazi Mhe. Waziri atakuja kutusaidia hapa kwa ajili ya kututoa wasi wasi pamoja na wananchi kwa jumla, ili kuweza kujua jinsi gani suala hili lilivyo aidha ni kweli au si kweli.

Vile vile kwenye ukurasa wa 26 kuhusiana na ulipaji wa fidia kwa wale waliovunjia. Mhe. Spika, hapa naomba kutoa tahadhari, kwa sababu hivi sasa watu wengine zile fedha zinawauma, sasa wale wanaofanya zinawauma ndio wanaowafanyia tathmini ya kile kitu kichovunjwa pale na kupewa kidogo.

Kwa mfano, nimeona sehemu ya utengenezaji wa barabara, wananchi wengi hususan wa Pangeni na Kilombero wanalalamika, yaani ile fidia haiendani na hali halisi ilivyo kama vile nyumba au shamba na kadhalika. Wakati mwengine unaweza kumkuta mtu ameathirika sehemu kubwa sana na ukimsikia ujenzi wake pamoja na ulipwaji wake uko tofauti.

Mhe. Spika, kuhusiana na hili la umeme nadhani Mhe. Waziri akae nao watu wake vizuri kwa lengo la kufahamiana kwenye ulipaji huu, kwa sababu fedha za wahisani zinakuja, lakini watu wetu katika ulipaji wao ah! mimi nashangaa sana, yaani wanaona tabu kuzilipa.

Mhe. Waziri kwa kweli hizi zichunge na uendeleze na *Alhajj* wako Mhe. Waziri lazima iendane na hali halisi hata hiyo njia ya umeme inayopita mpya iangaliwe vizuri, kwa sababu kuna nyumba nyengine ni nzuri sana.

Hivyo, nadhani usimamizi uwe mzuri na wala tusione tabu tuwalipe, kwani tunatengeza kitu na wala tusione hasara. Kwa maana hiyo, usimamizi uwe mzuri wa hizi fedha kwa wananchi, ambao watakaoathirika kwa nyumba au mashamba yao.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye suala la mafuta na gesi asilia. Kwa kweli suala hili tumelizungumza sana na wala sitaki nirejee tena, lakini tunapaswa tuyatilie mkazo, yaani tushitue na hii ni kuonesha kwamba Baraza hili linazo nguvu. Suala hili tayari tumeshalipitisha, kwa hiyo jambo la msingi ni kuendeleza na haraka sana tuwe na idara yetu hapa wakati ndio huu, yaani hapa tupatize na sisi sote neema ya hii ya thawabu, kwa sababu suala hili la heri sana.

Jana nilimsikia Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora amesema kabisa kwa mujibu wa sheria ya wizara yake imempa alitaja mpaka kifungu kilichompaka mamlaka kwa bahati mbaya nimekisahau. Kwa kweli amejidhatiti na kwa sababu gani amejidhatiti, anaelewa wazi suala hili litakuwa na manufaa kwa nchi ya Zanzibar. Lakini watu wengine wanatutisha na kusema mazingira, hivi kweli mazingira kwenye utajiri, mazingira utayaharibu wewe, rushwa ukiitaka basi itakuwepo. Sasa tunaambiwa rushwa na kupewa tahadhari, na wala lisitutishe suala la rushwa, kwa sababu hakuna mafuta na rushwa ipo nani asiyejua.

Kwa hivyo, hili lisiwe ni kigezo na tusimame imara, tuyatetee kabisa mafuta yetu Mhe. Spika, hasa nilivyoambiwa tayari wanafunzi wetu tumeshawapeleka wenyewe, yaani watoto wetu wanachukua vitu. Sasa watakaporudi hapa iwe vipi? Mhe. Spika, kuna mtu alikwenda kusomea ufundi wa magari, basi matokeo yake akapelekwa kwenye ufundi wa kuchonga.

Kwa maana hiyo, kama mtu ameshakwenda kusoma masuala ya uchimbaji wa mafuta ndio fani yake, baadaye tukamuweka kwenye *desk* hapa na kumwambia asubiri na hatimaye tunampa kazi nyengi tofauti na fani yake. Hivyo, katika kulishughulia suala hili tufanye haraka.

Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa wa 35 kuhusu Shirika la Umeme. Kwa kweli hapa natoa shukurani zangu za dhati kabisa, kwa sababu juzi mwenyewe nilishuhudia kule Pemba wenzetu wanapata raha ya umeme. Mimi nilikuwa ni mmoja na nilibeba bendera ya Norway na hata picha yangu iko kule, yaani walifurahi sana, kumbe hawajui furaha yangu mimi kwamba wao

wametuwezesha kupata umeme Pemba. Basi niliitembeza sana ile bendera kutokana ile heri waliotuletea.

Kwa mfano, zamani tulikuwa tukikaa pamoja na Mhe. Ali Suleiman Ali, Mhe. Ali Haji Ali na kujiuliza kama vile watoto yatima, kweli ni yatima. Lakini wakati mwengine hali ilikuwa inazidi, yaani tukiwa pamoja tunajiuliza haya mpaka lini. Lakini Mwenyezi Mungu ameleta neema yake hivi sasa Alhamdulillah Pemba umeme hauna wasi wasi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, katika mradi wa kusambaza umeme nashukuru nao umekwenda vizuri, yaani katika hali ya uadilifu kabisa na wahusika wametumia vile ipasavyo inavyotakiwa na wenyewe, kwa sababu hakuna ubadhirifu wa aina yoyote. Kwa hivyo, tunaweza kusema tumeneemeka majimbo yote viongozi ama Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa kweli hili tuliseme na tutoe pongezi na kila atakayekuja hapa basi atoe pongezi kuhusiana na suala hilo *(Makofi)*.

Lakini kuna maeneo mengine bado umeme haujafika. Sasa nadhani kama Mwenyezi Mungu akitujaalia Mhe. Waziri utakuwa na uwezo wa kwenda kuomba tena kama ile ilikuwa *Phase IV* basi sisi tuko tayari kwa *Phase V*, kwa sababu sehemu nyengine bado haujafika na hasa umeme wenyewe unakuwa ule wa *main line*. Kwa hivyo, ule wa *main line* kama Makame Mshimba Mbarouk hawezi kufikisha kwa wananchi na wala hili tusidanganyane. Mhe. Spika, tunaomba suala hili tulirejshe tena na atakapokuja Mhe. Waziri atupe maelezo mazuri kuhusiana na suala hili kwamba tutapa *Phase V*.

Vile vile Mhe. Waziri alitoa ahadi wakati alipofanya ziara katika Jimbo langu la Kitope katika kijiji cha Matetema, alisema kwamba atawasaidia umeme. Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa ukaribu wake (*Alhaj*) atusaidie nguzo kumi na nyengine kumi tutatoa mimi pamoja na Mhe. Mbunge wangu.

Kutokana na hali kuwa ngumu na wapo watu wanapita na kusema watapeleka umeme. Wanatupiga hivyo na sisi tunayo nia ya kutaka kurudi. Kwa kweli tumwambie Mhe. Waziri kwani hapa ndipo pa kuomba na wala sio sehemu nyengine. Mhe. Spika kwa sababu Waheshimiwa Mawaziri wakitaka kuturejesha sisi ndio watarejesha, kwani sisi ni wenzetu na wanaona kwamba bajeti zao tunazisifu kutokan na hali ilivyo na kwenye kasoro basi tunakosoana au kuelekezana na kwenye utendaji tunawambia watende *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, hali hii lazima tuiseme kwa sababu zinahitajika nguzo ishirini, lakini nguzo kumi tu atusaidie na tayari wafanyakazi wa shirika wameshapita. Hata

hivyo, watu tayari wameshaanza kuleta *generators* pembeni pembeni, tunaumia na watatupiga.

Siku moja nilikaa na Meneja na kuzungumza *plan* au mradi mzuri tu kama amesahau basi nakumbusha. Mradi huo tulisema hivi Waheshimiwa Wawakilishi kama mtasaidia nguzo, shirika tutasaidia waya, kwa ajili ya kutafuta wateja.

Kama *plan* hiyo imefutika au ipo, basi tuendelee nayo, kwa sababu sisi tunasadia kufikisha kule kwa wananchi na nguvu zetu ndogo na nyinyi tumalizieni waya, kwani inakuwa tayari tumeshakutafutiani wateja wengi. Kwa hivyo, kama Meneja amesahau basi namkumbusha kwamba ni mimi ndiye niliyezungumza naye, kwa sababu tayari katika sehemu za Pangeni tumeshaweka nguzo na tunasubiri waya, basi tunaomba tusaidiwe hilo.

Lakini la kusikitisha kama ni kweli basi lishughulikiwe na hilo nasema kwa unyonge kabisa. Mhe. Spika, nakumbuka hapa tulipitisha hapa kuhusu suala la maduka ya kuuza vifaa vya umeme. Sasa jambo hili sijui vipi kwa sababu tunasikia tusinunue waya mpaka twende kwenye shirika ah! Inawezekana pengine hawa wenye maduka wanatuletea vitu ambavyo havina viwango, lakini naamini shirika haliwezi kutuletea vifaa visivyo na kiwango, labda kwa hili ndio wamezuiliwa.
Kwa hivyo, ni vyema kuwaelimisha wenye maduka walete vifaa ambavyo vina kiwango na wala wasituletee vifaa vya Kichina. Kwa kweli vifaa vya Kichina baada ya siku mbili au tatu basi vinaleta vinaharibika na ile ni hatari kubwa.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, suala hili alione na kuweza kutusaidia kwa maana ya kutuwezesha, yaani kama tunao uwezo wa kuchukua wenyewe basi tununue kwenye maduka ambayo yanakubalika na ikiwa hatuna uwezo, shirika lililetee vifaa kwa wakati.

Mhe. Spika, naomba kumalizia kwa Idara ya Upimaji na Idara ya Usajili wa Ardhi. Kwanza nataka nizipongeze idara hizi kutokana na utekelezaji wa majukumu yake. Lakini idara hizi watu hawazifahamu, yaani wao wanaona Mkurugenzi wa Usajili ndiye Mpimaji na hivi sivyo, yaani ni idara mbili tofauti.

Kwa hivyo, ni vyema wananchi wakafahamishwa sio kila siku ataje mtu fulani tu. Kwa maana hiyo, tunamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wananchi wafahamishwe kuhusiana na suala hili la hizi idara zilivyo, kwa sababu kila idara inaye Mkurugenzi pamoja na utendaji wake.

Kwa kweli wanafanyakazi vizuri na wanaendelea na kazi zao katika hali nzuri bila ya matatizo yoyote, *Alhamdulillah* na hivyo viwanja vya Matemwe

tutavipata kwa utaratibu mzuri kabisa bila ya matatizo na wala kuathiri sehemu yoyote *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa hayo machache lakini nilikuwa na mengi ya kusema na wala sitaki kuendelea tena kwa sababu mwisho naweza kumkosoa Mhe. Waziri (*Alhajj*).

Kwa hivyo, naunga mkono kwa asilimia 99 pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope. Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atakapokuja kufanya majumuisho anipe raha na mimi *(Makofi)*.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi kulia huku nikikamata kichwa changu, maana Waswahili wanasema "kila mwenye kulia hukamata kichwa chake".

Mhe. Spika, kwanza nianzie kwenye utangulizi wa Mhe. Waziri. Kwa kweli utangulizi wake umenivutia na kwa sababu tunayo nia safi ya kuleta mshikamano kwa Wazanzibari. Basi nimeona hili nilichangie kidogo. Mhe. Waziri katika ukurasa wa pili kwenye kitabu hiki Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Ukurasa wa pili unasema hivi:-

> "Sote tunajua kwamba Umoja na Mshikamano ni Sera ya Chama cha Mapinduzi, chama ambacho kwa sera na busara zake kinaheshimiwa na Watanzania na Jamii ya Kimataifa, huo ni msimamo wa Chama cha Mapinduzi kuwa Kura ya Maoni ya tarehe 31, Julai 2010 ni Kura ya Ndio".

Mhe. Spika, maelezo haya kwa kweli yamenivutia na nilisema nimpongeze waziri kwa kuendelea kuwa na msimamo huu wa umoja *(Makofi)*.

Nafikiri ni msimamo cha Chama cha Mapinduzi. kwa hivyo, na sisi kama alivyosema Mhe. Hamad Masoud Hamad (Waziri Kivuli) wakati wa asubuhi na huo ndio msimamo wa Chama chetu cha CUF. Kwa hivyo, nadhani tutakwenda pazuri na *Inshallah* hili likitokea, basi tutaweza kutatua matatizo yetu mengi ambayo huko nyuma tulishindwa kuyapatia ufumbuzi, kwa hiyo nashukuru sana.

Nikiendelea na mchango wangu kuzungumzie kuhusu jambo kubwa sana ambalo la kihistoria umeme wa kutoka Tanga mpaka Pemba. Mhe. Spika, sipingi kwa miaka mingi sana wananchi wa Pemba tulikuwa tukipata tabu sana kwa umeme.

Hata hivyo, nathubutu kusema hali ya maisha kuwa ngumu zaidi kule Pemba, basi ilisababishwa na tatizo la umeme, kwa sababu umeme unachangia sana maendeleo pamoja na masuala ya kiuchumi. Kwani *investments* nyingi zinatokana na umeme. Tulikosa fursa hii kwa muda mrefu. Lakini kutokana na ustahamilivu wetu Mwenyezi Mungu ametujaalia kheri tumepata umeme kutoka Tanga *(Makofi).*

Sasa katika hili kwanza nataka niipongeze Serikali ya Awamu ya Sita. Mhe. Spika, zimepita awamu tano, kwa kweli suala hili tuliambiwa hakuna uwezekano, mara nyingi tulikuwa tukihoji tukiambiwa hivyo. Lakini Serikali ya Awamu ya Sita iliona kama uwezekano upo na tumeona kwa vitendo hasa umeme umevuka kina kikubwa cha maji ya bahari kutoka Tanga na sasa tunao Pemba tunautumia *(Makofi).*

Vile vile naipongeza sana Serikali ya Norway, kwa sababu sisi pamoja na nia yetu nzuri. Lakini kutokana na gharama za umeme huo tungeshindwa kwa miaka mingi tusingeupata, wenzetu wamekuwa waungwana sana na hasa pale gharama za umeme zilipoongezeka hawakurudi nyuma, walisema wataendelea hivyo hivyo.

Tuliambiwa kwa mara ya kwanza Serikali ya Norway kutoa msaada mkubwa sana wa pamoja kwa Tanzania kuhusu umeme huu. Kwa hivyo, naipongeza sana Serikali ya Norway *(Makofi).*

Mhe. Spika, hivi juzi na hata kwenye kitabu hiki limo Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi wakati alipokuwa akijibu swali la nyongeza asubuhi alitupa moyo sana kuhusu umeme mbadala. Vile vile kwenye kitabu hiki cha Mhe. Waziri suala hili limezungumzwa kwa kina.

Suala la umeme mbadala kwa Wazanzibari ni jambo la lazima na nimewahi kulizungumza sana katika bajeti zilizopita, lakini na leo natilia mkazo sana. Mhe. Spika, tunakwenda na wenzetu na tunayo mahusiano mazuri, lakini hufika pahala sisi wengine tukaona mashaka kidogo na kuona giza huko usoni. Kwa mfano, kama hivi sasa tunaambiwa kuna mgogoro kati ya Shirika la Umeme la Zanzibar (*ZECO*) na *TANESCO* kuhusu bei ya umeme na wala hatujui hatma ya mgogoro huu itakuwaje.

Lakini siku moja na Mwenyezi Mungu asitujaalie, ikija kutokea makubaliano hayakufikiwa vizuri na *TANESCO* wakaamua kutukatia umeme wao. Kwa kweli hapo tutakuja kuona umuhimu mkubwa sana wa kuwa na umeme mbadala.

Kwa hivyo, nadhani suala hili kama ambavyo wizara hii pamoja na serikali kwa jumla, ililivalia njuga suala la umeme kutoka Tanga hadi Pemba na kufika, basi

nafikiri uwezekano mkubwa upo wa kuhakikisha kwamba Zanzibar inakuwa na umeme mbadala.

Mhe. Spika, tumetajiwa ambao hauna tatizo sana hivi sasa ni *Solar Power*. Nafikiri tukijipanga kidogo tunaweza kuupata na kuutumia. Vile vile ni vizuri Mhe. Spika, kwa sababu tunavyo vyanzo vyengine na pengine vikifanywa utafiti wa kina vinaweza kuonekana vya uhakika zaidi.

Kwa hivyo, serikali kupitia wizara hii ifanye juhudi kubwa sana kuhakikisha tunakuwa na vyanzo vyetu vya umeme hapa.

Mhe. Spika, wakati mwengine hupata maelezo ya kitia moyo kidogo, kwamba tayari utafiti umeshafanywa kupitia visiwa vyetu hivi na kuna maeneo ambayo yamegundulikana kuna mkondo mkali kidogo, ambao huo kama ukifanyiwa kazi vizuri, basi tunaweza kupata umeme mwingi na hata siku moja tukawauzia hawa wenzetu. Kwa hivyo, nadhani ni jambo muhimu la kulitia maanani sana na wala tusilipuuze hata kidogo.

Kwa mfano, tumeona hapa kutokana na hitilafu za umeme kwa muda wa miezi mitatu, yaani tuliona hasara ambapo mpaka leo serikali imeshindwa kuitathmini, lakini kama watafanya tathimini ya hasara tuliyoipata miezi mitatu ile tunaweza kukamata vichwa hapa. Sasa ikija kutokea kwamba tumekatiwa umeme mwaka mzima na *TANESCO* itakuwaje. Nadhani ni muhimu sana tulifuatilie suala hili.

Mhe. Spika, kuhusu mafuta kwanza nataka tujipongeze sana wenyewe tumo Barazani. Kwa kweli tumekuwa na misimamo imara, umoja na tukaamua kijasiri sana na bila ya kujali maslahi ya mtu binafsi mpaka suala hili la mafuta tumelifikisha pale tulipolifikisha.

Vile vile tumpongeze Mhe. Waziri, kwa sababu wamepita mawaziri wengi kwenye wizara hii, lakini hakuna waziri aliyethubutu kulichokoza hili. Kwa hivyo, natoa pongezi maalum kwa Mhe. Waziri kwa kujitolea muhanga katika suala hili na yalimkuta yaliyomkuta tunasikia, lakini msimamo wake umezaa matunda. Pamoja na hayo, tuipongeze tena Serikali ya Awamu ya Sita kwa suala hili kuweza kulitia katika mchakato.

Mhe. Spika, nataka niseme jambo moja, tumefika hapa tulipofika lakini nataka tujue kwamba safari yetu ya mafuta ni kubwa. Kwa kweli mimi binafsi nimepata mshituko kidogo baada ya kusikia maelezo kwamba serikali kupitia Mhe. Waziri Kiongozi imeandika barua kwa Mhe. Waziri Mkuu kuomba suala hili litolewe kwenye masuala ya Muungano.

Kwa hivyo, nimepata wasi wasi mkubwa kwa sababu moja. Suala hili kama ni kutolewa, basi itabidi liende Bungeni, kule Bungeni hawataki nina hakika na bunge la Tanzania siku hizi linaanza kuota meno, sio kila alichokiamua Rais na wao wanakikubali moja kwa moja Rais anaweza kuwa anataka hivi bunge likasema hapana sisi tunakwenda huku na haya mambo yameshatokea. Sasa mimi ninapata wasi wasi kwa sababu moja katika kulifanya jambo liwe la Muungano katiba iko wazi inasema tuwaulize Wazanzibari tupate *two third majority ya* Wazanzibari, tuwaulize Wabunge kutoka Tanzania Bara tupate *too third majority* ya wabunge wa kule wakikubali jambo linakuwa la Muungano.

Lakini sasa wasi wasi wangu *formula* ya kwamba jambo fulani tumeona halina maslahi kwa upande mmoja tunataka kulitoa *formula* hiyo ya *two third majority* ya kila upande haifai Mhe. Spika na mfano mzuri ni huu sasa hivi wabunge kutoka Tanzania Bara wao hawalitaki hili sasa wabunge kutoka Zanzibar watapiga kura itapatikana *too third majority* lakini ukifika wakati wa kuulizwa wabunge kutoka Tanzania Bara wao wakisema hatutaki *two third majority* ikikosekana. Sasa tukifika hapo sisi tutakuwa tumekwama ndio nikasema *formula* hii haifai na hili mimi nadhani ni tatizo la kikatiba, maana tukifika hapo wakikataa wale inakuwa jambo halikutoka na kama halikutoka je safari yetu tumefika wapi, si itakuwa tumemaliza pale.

Sasa nafikiri sijui ni Waziri wa Katiba na Sheria au nani lakini kuna haja ya Wazanzibari sasa hivi kukaa tukaanza kutafakari *formula* ambayo itatusaidia tena pande zote mbili, pale ambapo tutahisi jambo fulani halina maslahi kwa upande fulani kuwe na *formula* maalum itakayorahisisha lile jambo kuwa litoke, lakini tuking'ang'ania hii *formula* hii ya *two third majority* kulitoa nakuhakikishieni tutakwama njiani.

Mhe. Spika, niondoke hapo kwa sababu naona muda unakimbia mno na kuna mambo nilisema mtu akilia hukamata kichwa chake.

Mhe. Spika: Kwa mujibu wa waombaji kuzungumza naona tukuongezee dakika kumi na tano tulikubaliana sasa wewe umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, wacha nitumie dakika mbili kusema maneno mawili, neno la kwanza katika bajeti ya mwaka jana nililia sana kuhusu wananchi wangu wa jimbo la Chonga kanda ile ya Magharibi Tundaua na vijiji vyake, wale watu hawana maji ni miaka mingi walikuwa hawana umeme *alhamdulillahi* tumepata lakini hawana maji wala barabara wanahangaika muda mrefu na mimi ni muwakilishi wao na nina wajibu wa kuwatetea.

Mhe. Spika, lilitoka tamko hapa kwa Mhe. Waziri kwamba atapeleka watu wake wenda kuangalia uwezekano wa kuchimba kisima kwa ajili ya maji nilisikia

walikwenda lakini walikagua kagua wakaondoka na hawakuendelea, sitaki nimlaumu sana Mhe. Waziri ana mambo mengi lakini namkumbusha kwamba kwa mwaka huu sasa alifuatilie angalau hawa watu wapate maji, kuna matatizo mara kwa mara kunatokea maradhi ya mirupuko kwa sababu ya maji ya kuokota.

Halafu la pili Mhe. Spika, ni kuhusu usambazaji wa umeme vijijini alhamdullihi tumepata umeme wa Tanga ni MW.20 lakini tulikuwa tunaatumia MW. 8 sasa hivi ni ishirini sasa kuna watu wengi umeme uko Pemba lakini vijijini hakuna zile laini hazijafika, kwa mantiki hiyo kuna MW. 10 karibu zitakuwa hazitumiwi watu wa Kuungeni wameniomba umeme siku nyingi sana na sasa hivi pale mimi nikitoa ata salamaaleykum siitikiwi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alisema hapa nyinyi Mawaziri mukitaka ndio mtakaoturudisha majimboni na kama hamkutana nyinyi haturudi mimi pale asalama allaykum yangu haitikiwi tena. Ulinambiwa kwamba mmezungumza na sijui kama Meneja kule Pemba lakini walilianza hili suala wakapewa ahadi halijatekelezwa, umeme umepita chini ya migomba yao lakini hawawezi kuutumia kwa sababu umekwenda kutumika Tundaua pale nyuma hautumiki nafikiri hiyo picha Meneja wa Umeme Pemba ataikumbuka vizuri kwa sababu anavijua hivyo vijiji, naomba sana wale watu wasaidiwe angalau pale nikipita niulize hali niitikiwe.
Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache nakushukuru. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kwanza sina budi kukushukuru wewe kwa kunipa hii fursa, lakini pia kumshukuru ndugu yetu waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi Mhe. Mansour Yussuf Himid kwa jinsi anavyosimamia wizara yake barabara, lazima tumpongeze kama tunavyowapongeza mawaziri wengine naye kama hatukumpongeza itakuwa hatukumfanyia haki maana matu akifanya vizuri lazima umpongeze, wala hatumuigi Mhe. Ali Suleiman Ali kwa sababu yeye akikupongeza hujui kama anakupongeza kikweli kweli yeye amekuwa na tabia ya kupongeza tu. Sisis tunapongeza kikweli kweli hasa.

Baada ya pongezi na mimi nataka nieleze wasi wasi wangu binafsi nilionao katika huu mchakato wa suala la mafuta, kwa sababu hotuba ya Waziri imeeleza wazi wazi kwamba hata ile rasimu ya sheria ya mafuta na gesi asilia tayari imeshatayarishwa lakini wakati huo huo tunaambiwa Waziri Kiongozi amepeleka barua kwa Waziri Mkuu, sasa sisi tunaendelea na maandalizi yetu lakini kule hatujapata *go are head* sasa kuna Mhe. Ali Moh'd Bakari katoa mfano mzuri wa harusi iliyotokezea kwao Tumbe. Sasa na mimi nina wasi wasi yasije yakatukuta kama yale yaliyotokezea katika harudi ya Tumbe, kwamba shughuli zote zimeshakamilika dakika ya mwisho anaambiwa huyu hatukupi akaozeshwa mtoto wa ami yake mambo yote yakaharibika.

Lakini pamoja na hayo lazima tututoe pongezi kwa kuendeleza matayarisho ya rasimu ya sheria mbili hizi tunazozitaja sitaki kuzirudia na ishaalla Mwenyezi Mungu atajaalia wenzetu hawatotukwamisha, kwa sababu suala la bandari ni suala la muungano lakini kuna Tanzania *Port Audhority* na hapa tuna *Zanzibar Deport Corporation* lakini kimuungano ni kitu kimoja, sasa nadhani ilivyokuwa hili tumeweza kuvumiliana basi vile vile na hili tutaweza kuvumiliana hasa ilivyokuwa sisi ni ndugu wema.

Mhe. Spika jengine kwa sababu muda ni mfupi nataka niende moja kwa moja katika jimbo langu na nipeleke salamu za wananchi wa Kisiwapanza walizonituma. Mhe. Spika, kama muda ungeruhusu siku moja ningekwita ugeni ukaja kuona dhiki wanayoipata wananchi wa Kisiwapanza juu ya maji, suala hili imekuwa ndio hadithi yangu kila siku katika Baraza hili na nashukuru wenzangu ahadi wananipa nyingi kulitatua tatizo hili maana huwa nalifuatilia sana katika utendaji wa ngazi zote, Mhe. Waziri tunazungumza Mkurugenzi wa maji nakwenda mimi na hata mbunge wangu lakini mafanikio bado hayapo. Lakini kwa ufupi muda haupo sasa hivi zaidi ya mwaka wananchi wa Kisiwapanza kuna sehemu moja inaitwa Panza kule mwisho kabisa kusini zaidi ya mwaka hawajapata maji ya bomba wanakunywa maji yenye uchumvi uchumvi tu ambayo ndio maji yao sasa wamekuwa wanapata dhiki.
Sasa hii sehemu ya mwanzo chini huku ambayo inaitwa Mtondooni wao kiasi cha miezi sita walipata maji siku moja kiasi mwezi mmoja uliopita, sasa mwananchi anapokosa maji na Mwenyezi Mungu akajaalia kule hata wakichimba hivi visima vya kawaida wanayopata ni chumvi ni watu wa kuonewa huruma. Kwa hivyo mimi sichoki hii ndio kazi tuliyoiomba na kukata tama na rehema za Mwenyezi Mungu si vizuri kwa muislam kwa hivyo nitaendelea kuwakera Mhe. Waziri na wenziwe na nafikri na wao ni binaadam ubinaadam utawajia ile shida wanayopata wenzetu wataiyona na watawasaidia. Hiyo ilikuwa ni salamu ya wananchi wa Kisiwapanza ambayo wako katika idhilali kubwa lakini ishaalla Mwenyezi Mungu wenzetu hawa atawatia huruma kufikiriwa na kutatuliwa tatizo lao.

Halafu jengine mimi nije kwenye Shirika la Umeme *(ZESCO)* nayo lazima tuipongeze imefanya mengi na inafanya mengi, lakini kuna kitu kimoja Mhe. Spika, nawaomba kidogo wajitutumue kinasua sua hili suala la ufungaji wa mita za *TUKUZA* mimi bahati nzuri nyumba yangu hapa Unguja iko ng'ambo kabisa natumia mita hizi hizi za kizamani, kwa hivyo wakati mwengine hukaa nikajisahau mpaka jana nimekwenda kulipa umeme shilingi hamsini na moja elfu. Sasa inakuwa tabu sana na inatia usiri kwenda kule nasema jana nimekwenda kulipa umeme lakini kama ingekuwa ni wakununua isingenifika tabu hii kama hivi.

Vile vile nyumba yangu nyengine iko katika Mji wa Mkoani Pemba ipo pwani kabisa mpaka leo vile vile natumia mita hizi za zamani kwa hivyo inakuwa napata tabu sana halafu nina nyumba yangu ambayo iko kwetu kijijini nayo vile vile mita ya zamani sasa inakuwa ni tabu, kwa hivyo mimi naona huu mradi unasua sua sana ningemshauri Mhe. Waziri huu mradi wakausimamia vizuri wakatusaidia kwa sababu simu kama ingekuwa tunalipia hizi za mkononi hizi kama ingekuwa ni kwenda kulipia basi wengi wetu ingekuwa imeshatushinda hizi, lakini leo hipigi simu mpaka ununue *voucher* uweke ndio utumie ndio sababu ukaona inalia miziki humu ndani na watu wakitoka nje milangoni humo. Lakini nyingi sasa hivi zingekuwa hazifanyi kazi hizi huu ni ulimwengu wa *pree paid* sio ulimwengu wa *post paid* tena.

Halafu Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa mara ya pili kurejea kunipa ahadi ya kupeleka umeme Kisiwapanza, bajeti ya mwaka jana hili kalizungumza na mimi na Mhe. Mbunge tukenda tukawaambia wananchi na tukawaonyesha mpaka kile kitabu wakaona wakafurahi, kila siku wanatuuliza tunawaambia haya mambo yako mbioni lakini wanatwambia hizo mbio zenyewe ni mbio gani hizo tunawaambia hizi mbio za kweli kweli hasa. Sasa namshukuru Mhe. Waziri kwamba kalirudia tena inatia moyo.

Lakini sasa nilipoangalia mradi wa umeme vijijini kwa mwaka wa fedha huu tunaokwenda nao hamna Kijiji cha Kisiwapanza, kuna vijiji vilivyokusudiwa vimetajwa kwa maana hiyo shilingi bilioni 1.5 zilizoombwa kwa ajili ya umeme vijijini Kisiwapanza haimo, sasa sijui Mhe. Waziri ikiwa pesa hazijaombwa na unatuahidi kutusaidia suala hili fedha itakuja patikana wapi katika utekelezaji hilo ilikuwa ndio suala langu.

Mhe. Spika, sasa nataka nije Idara ya Utawala wa Ardhi hapa nataka niungane na Mhe. Hamad Masoud Hamad msemaji wa kambi yetu katika matatizo ya ardhi ambayo mimi bahati nzuri mengine nina ushahidi nayo, kwanza mimi nataka nizungumzie kuhusu hizi eka tatu tatu. Rais wa Kwanza wa Zanzibar Mzee Karume aliposema wananchi wapewe eka tatu tatu alikuwa na nia njema, lakini baadhi ya watu waliozipokea eka hizi hawakuwa na nia njema wengi wameshaziuza, nyengine zimetelekezwa sasa hivi yamekuwa mapori baada ya kumalizika ile mali iliyokuwemo, baada ya kumalizika mikarafuu na minazi iliyokuwemo hakuna hata moja anayeshughulika na kupanda kwa hivyo imekuwa mapori na mengine yametupiliwa mbali.

Nyengine bahati nzuri wenyewe wamefariki Masheha wanadhidhibiti na familia zao na kuna wajanja wengine wachache wanajichukulia chukulia. Sasa suala hili bado linataka udhibiti wa hali ya juu kama utafuatilia eka nyingi zimeshauzwa hasa maeneo ya mijini mijini watu wanauza wanapima viwanja ndio maana ukaona miji inajengwa jengwa ovyo ovyo.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye Idara ya Ardhi na Usajili ushauri wangu mimi kwamba Idara hii ifanye utafiti kwana kabla haijatoa ardhi kwa wawekezaji au kwa shughuli nyengine zozote zile za maendeleo zaidi hizi za uwekezaji, ninaleta matatizo nafikiri Mhe. Waziri ni shahidi mwaka jana nilimletea kijana mmoja wa Chokocho walikuwa na matatizo kama haya, watu wana mashamba yao tena wana hati hasa *register* kwamba yale mashamba yao walinunua wazee wao. Lakini anakwenda kupewa muwekezaji bila ya wenyewe kuambiwa baada ya kupiga kelele mnaambiwa mtalipwa minazi yenu na kila mnazi utapigwa thamani na mihogo yenu mliyopanda. Sasa wananchi wanahisi kwamba serikali inatumia nguvu kuwanyang'anya ardhi zao sasa nadhani mashauriano yangefanyika kwanza kabla ya ardhi yao kuchukuliwa. Kwa sababu wananchi wasijenge mawaz`o kwamba serikali yao inatumia mabavu kuchukua ardhi.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Waziri alitaja mfano wa Mbuyuni ambako yapo matatizo kama haya sehemu za Mkoani kuna sheha mmoja matata kule yeye anaweza kwenda kuchukua watu kule wakaja kupima na ardhi wakapewa watu kumbe mashamba ya watu, sasa nasema wawe na utaratibu mzuri. Lakini namkumbuka kijana mmoja ambae sasa hivi ni marehemu akiitwa Shaibu Amour alikuwa na shamba la babu yao Wambaa tokea wakati wa Mzee wangu Mhe. Burhan Saadat Haji kesi hii niliwahi kumpa akahangaika sana namshukuru lakini mafanikio hayakupatikana, walikuwa na warka na sehemu kubwa ya shamba lao kapewa muwekezaji wao wenyewe hawakupata chochote mpaka leo.

Sasa wananchi wanabakia kunung'unika na juzi juzi nilikutana na bwana mmoja wa Chake Chake anaitwa Said Kassim ananambia na wao wana shamba yao kule Kiuyu kwa Manda kule karibu na ile sehemu iliyotangazwa eneo la historia kule wana shamba yao ambayo wamenunua na waraka wanao wamepanda miembe yao sasa hivi wamenyang'anywa! Imekuwa eneo la historia, lakini wenyewe hawakuambiwa chochote. Sasa mimi nafikiri ni heshima angalau wale wenyewe wangeitwa wakaambiwa kwamba hili eneo tutalichukua pengine wangekubali, lakini likichukuliwa tu hivi hivi bila ya kuambiwa lolote mna mali zao kidogo wanaona serikali haikuwafanyia haki.

Halafu jengine nataka nije Mahakama ya Ardhi katika hotuba yangu mimi ya Utawala Bora nililizungumza suala hili nikijua kwamba Mhe. Waziri wa Utawala Bora hahusiki moja kwa moja na suala la Mahakama ya Ardhi, lakini niliona nilizungumze sasa na hapa nitalizungumza tena. Mhe. Spika, Unguja nzima Mahakama ya Ardhi ni moja tena ipo mjini hapa sasa fikiria mwananchi anatoka Makunduchi anatoka Nungwi, anatoka Michanvi inakuwa ni tatizo. Narudia ushauri wangu angalau kila Mkoa ingewekwa Mahakama hii au hii Mahakama ikawa inakwenda sehemu mbali mbali kufanya kazi kama inavyofanya Mahakama ya Rufaa hapa haina ofisi lakini inakuja kusikiliza kesi za rufaa hapa

Zanzibar kwa kutumia jengo la Mahakama Kuu hapa. Sasa nadhani hii Mahakama wakati mwengine ingekuwa inafuatilia wananchi ili kuwapunguzia shida kuliko mwananchi kutoka kijijini kufuatilia huduma mjini.

Mhe. Spika: bado dakika mbili.

Mhe. Haji Faki Shaali: Jengine Mhe. Spika, la haraka haraka nije katika kutoa kilio cha wananchi kuhusu umeme, wananchi wanashukuru kwamba umeme umepita karibu katika vijiji vyote sasa hivi hasa katika jimbo langu lakini gharama za ufungaji umeme ni kubwa kwa wananchi masikini, sasa wananchi wana mawazo mawili kwanza gharama zipunguzwe lakini pili ikiwezekana kuwe na mikataba ya watu kukopeshwa na walipe kwa awamu kama tatu au nne kama watakavyokubaliana katika mkaraba. Na hili likifanyika Mhe. Spika, huu umeme utatiwa katika majumba lakini utakuta umeme unakwenda katika kijiji wanaotumia ni watu wanne, watano mpaka sita lakini utaratibu kama huu niliopendekeza ukikubaliwa nadhani wananchi wengi wataweza kutia umeme.

Mwisho Mhe. Spika, naomba ufufanuzi wa jaduweli namba nane inayohusu viwanja vilivyopimwa Pemba, inaonekana katika Mji wa Wete ni viwanja vitatu tu vilivyopimwa, sasa nikiangalia ukuaji wa Mji wa Wete kasi inayokuwa ikiwa kwa mwaka kuna maombi matatu ya viwanja vya nyumba za makazi napata tabu, je wananchi wa Wete wanajenga bila ya utaratibu wanajijengea tu au takwimu hapa kidogo kompyuta imeruka.

Mhe. Spika, nakushukuru sana. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Said Ali Mbarouk: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi jioni ya leo kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi naomba na mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri na Naibu wake na watendaji wake kwa namna ambavyo wanatekeleza majukumu yao katika nchi yetu, hakika taasisi takriban zote za Wizara hii zimejitahidi sana kuona kwamba malengo yake yamefikiwa na Wizara ambayo inagusa maisha ya kila mtu kwa kila siku.

Sasa namna ambavyo wanafanya kazi naomba niwapongeza sana, ningesema kwamba sijui nifanye *loabing* kwa Mhe. Waziri kwamba anapaswa kupewa dhamana hii katika awamu inayokuja, sasa wakati mzuri hivi sasa aliyekuwepo humu ndani ni mgombea mmoja tu wengine hawapo sasa akifanikiwa basi namuombea kabisa la amekuwa Makamo basi pia ana ushauri mzuri kwa hivyo hili nafanya *loabing* kabisa kwamba amefanya kazi nzuri anapaswa kupewa tena.

Mhe. Spika, naomba nianze na shughuli za maji kwa kweli na mimi naomba sana niwapongeze watu mamlaka ya maji wamefanya kazi nzuri hasa katika jimbo

langu nawashukuru sana, Gando vijijini sasa upatikanaji wa hali ya maji ni mzuri sana ilikuwa ni tatizo lakini nashukuru mpaka kwenye vile visiwa vidogo vidogo vya Njau, Vinje na Fundo hali sasa ni ya kuridhisha sana kinyume na iliyopo Kisiwapanza kwangu mimi hali ni ya kuridhisha sana.

Isipokuwa kuna tatizo la Gando Mjini, Popwe na Kizimbani sasa hapa ningeomba ule mradi wa maji mijini wa ADB usukumwe zaidi naona kazi yake ni ndogo kidogo kwa hivyo ningeshauri ifanywe kazi hiyo, lakini zaidi ningeomba kiimarishwe kitengo cha matengenezo cha mamlaka ya maji na zaidi kina tatizo la vifaa na uasafiri mara nyingi tatizo lake ni hilo. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri aangalie namna gani kitengo hicho cha matengenezo kitakuwa na vifaa vya kutosha na usafiri na amesema hapa kwamba amepata uwezo wa kununua mabomba mengi, sasa ningeshauri mabomba haya yanayonunuliwa pia basi yawe na spea vile viungio na vifaa vya kuzibia mabomba yanapopasuka, haitokuwa vizuri kuwa na mabomba mengi lakini hatuna viungio vyake.

Katika suala la maji ningemalizia katika suala la Shumba Viamboni Mhe. Ali Moh'd Bakari mchana alipokuwa anazungumza, alizungumzia suala la Shumba Viamboni ni kweli wale wananchi walikuwa wanapata shida sana na Mamlaka ya Maji iliahidi kufanya chochote, bahati nzuri Mhe. Spika, Mhe. Ali Moh'd Bakari kawa koa! Anatembea na nyumba yake, yaani kila akiondoka Jimboni Tumbe huja na nyumba yake huku mjini huwa harudi sana yeye. Miongoni mwa koa wa Baraza hili hata tulipokwenda ziara ya Malaysia alikwenda na nyumba yake mpaka Dubai, sasa inakuwa mtihani kidogo.

Mimi nyumba yangu nzito kidogo haibebeki inabidi nirudi rudi kidogo lakini niliporudi nikaona kuna maendeleo makubwa ya huu mradi unafanyakazi vizuri kwa hivyo nawapongeza katika hili.

Mhe. Spika, waheshimiwa koa ni kono kono ee.!

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, suala la umeme na mimi ningeomba nishukuru sana wale wote ambao walimsaidia Mhe. Waziri kukamilisha suala la umeme la Tanga – Pemba, na mimi naomba niwapongeze sana serikali ya *Norway*, serikali ya Jamhuri ya Muungano na hapa ya Zanzibar kuoa kwamba umeme sasa Pemba unapatikana, naomba niwapongeze sana. Lakini naomba niungane na Mhe. Haji Faki Shaali kwamba gharama za kuungia umeme ziangaliwe ni kubwa! Wananchi wetu ni wanyonge ingawa nilipozungumza na Meneja wanasema kwamba ule mpango wa kukopesha umeshaanza, naomba wananchi wengi wafahamu kuna mpango huo.

Pia naomba nizungumzie umeme Fundo, nimeona humu kwamba kuna mpango wa umeme wa jua kisiwa cha Fundo kina watu wafikao elfu mbili, kuna skuli ya *primary na secondary*, kuna hospitali ambayo Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ameijenga kwa kasi sana pamoja na nyumba ya madaktari, pia kunashughuli za uvuvi ambazo zinahitaji Mafriji. Kwa hivyo jambo la upatikanaji wa umeme pale litatusaidia sana wananchi kwa hivyo nimeona kuna *program* ya umeme wa jua ningeshauri na Fundo nao waangaliwe.

Mhe. Spika, jambo jengine katika suala la umeme *ma – transformer* ya akiba yaangaliwe sana ni muhimu kuwa nayo kwa sababu wakati mwengine yanaungua katika sehemu nyengine na huchukua muda mrefu.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulizungumza ambalo silipendi ni kwamba meneja huyu aliyekuwepo amefanya kazi nzuri, amevusha shirika na nchi katika kipindi kigumu sana, sipendi mpaka leo mtu kama huyu anaitwa kaimu Meneja! Sijui mambo haya huwaje? Ningeomba Waziri au Idara ya Utumishi haipendezi kuwa mtu kafanya kazi nzuri lakini bado anaitwa kaimu meneja kazi ambayo amefanya kipindi hiki ilitosha kupewa sifa ya kwamba apewe umeneja kamili wa shirika hili na awe na uwezo wa kulinda.

Mhe. Spika, ningeomba nimkumbushe Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi wale watu wa Madaniwa wanauliza vipi hukurudi tena kwa hivyo wewe mwenyewe umeshafahamu kwamba una kijiahadi kidogo wanataka waende wakakimalize, kwa hivyo naomba urudi kwa hilo.

Mhe. Spika, katika suala la nishati ya mafuta ningeomba masuala ya *regulatory autority* wa Idara ya Nishari upewe umuhimu wakati mwengine huwa tunapata mafuta ambayo ni mabaya lakini baya zaidi ni kwamba bei huwa sio nzuri. Wenzetu wafanyabiashara wanachukua hii fursa mafuta kuyapandisha, juzi EURA kule bara walipunguza bei ambayo wafanya biashara walishapandisha. Kwa hivyo naomba Idara ya Nishati ipewe mamlaka haya kuona kwamba ina uwezo wa kupanga bei na sampuli ya mafuta ambayo yanaingia nchini mwetu.

Halafu nishati ya umeme kutoka Bara ni ghali suala ambalo Mhe. Waziri amelizungumza la umeme mbadala hili naungana na wenzangu kwamba hili suala linahitaji kupewa kipaumbele sana.

Suala jengine matumizi ya nishati ya gesi ya kupikia hili jambo nchi yetu inaangamia sana kwa matumizi makubwa ya kuni, sasa idara ya nishati lazima iangalie uwezekano wa kupata nishati ya kupikia ya gesi kutoka nje wenzetu wa nchi za Magharibi wanachukua nishati ya umeme ya gesi kutoka Urusi pahala ambapo ni mbali sana. Sasa na sisi tuangalie vipi na wapi tunaweza kupata

nishati ya gesi ya kupigia tuondokane utaratibu wa kutumia kuni kwa ajili ya kupikia ardhi ya nchi inapotea sana kwa habari suala hili la kupikia kuni.

Katika suala hili la nishati ya gesi na mafuta asilia hapa naomba jitihada kubwa sifanywe kuona kwamba yale yote tuliyoyazungumza humu hatua tulizochukua zinapata ufanisi. Mimi nimetishika sana na hili suala la barua ya Mhe. Waziri Kiongozi kwa Mhe. Waziri Mkuu. Nimetishika kwa sababu najua *sentiment* ambayo wanayo wenzetu. Mwaka jana kipindi kama hichi ulinipeleka Zambia kuhudhuria Kikao cha Mabunge ya *Common Wealth* bahati nzuri kule nilikutana na jamaa mmoja wa Bunge kutoka Bara ni Mbunge ambaye ana *waster* sana katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, sipendi kumtaja. Katika mazungumzo yetu walisema hivi naomba kumnukuu.

> "Siku yoyote ambayo Zanzibar itapata uwezo wa kuchimba mafuta yake basi hali ya Muungano utakuwa matatani sana"

Sasa hiyo ndiyo *sentiment* ambayo wenzetu wanayo katika vichwa vyao. Hasa ikiwa wao ndio watu ambao wana *sentiment* hizo na sisi ndio kwanza tunakwenda kuwaomba idhini ya kutumia rasilimali yetu. Kwahivyo ni lazima kama alivyosema Mhe. Abdalla Juma lazima tutafute *full back position* itakuwaje *in case* wao wamekataa lazima kuwa na utaratibu ambao rasilimali hii sasa haitabaki katika ardhi lazima wananchi wa Zanzibar, sasa waitumie kwa maslahi ya uchumi.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa suala la ardhi. Matumizi ya Ardhi ya Zanzibar lazima yawekewe sera muhimu zaidi ambayo tutaiona kwamba ardhi iliyopo inatumika vizuri zaidi kuliko hivi sasa. Hivi sasa makaazi ya watu yanachukua eneo kubwa la ardhi ya Zanzibar. Tusipokuwa makini sana kuna siku tutakosa hata pa kulima mboga. Mzee Karume alikuwa na *vision* kubwa alipoanza ujenzi huu kwa majumba ya juu, bahati mbaya yamekwama mpaka yamekuja kumalizwa juzi. Mimi naamini kama angelikuwa yupo haya maeneo ya Kikwajuni na maeneo mengine yote haya tayari yangelikuwa yameshapata *mushroom* ya majengo yale, lakini bahati mbaya tumeacha na kwa kweli tunaathirika sana. Mji sasa unakuwa na ukuwaji wenyewe unakuwa kwa makaazi ya watu. Hili ni jambao ambalo ni lazima tuliangalie.

Mhe. Spika, juzi tena ulitupa nafasi ya kwenda Malesia kwa kweli wale jamaa wako mbali sana katika kuona kwamba ardhi waliyonayo wanaitumia vizuri sana. Nyumba zao zote za kuishi watu zinaanza na gorofa 15 kwenda mbele, hakuna mjini hakuna vijijini. Tulikuwa tuna Mwenyekiti, Mhe. Thuwaibah kwenye basi tunatoka Malesia tunakwenda Singapoor tulikuwa tunaitafuta nyumba ya chini vijijini hakuna. Sasa matokeo yake ni kwamba vijiji baina ya kijiji na kijiji katikati mote kuna mashamba, utaona ardhi yao wanaitumia vizuri. Kwa hivyo

tunaomba kwa ardhi ndogo ya Zanzibar suala hili ni muhimu sana na kwa kweli tusipotanabahi hivi sasa baada ya miaka 10 au 20 ijayo pahali pa kulima mboga au ndizi ya gando itakuwa si rahisi.

Pia ningeshauri kwamba katika Wizara hii kuungwe kitengo au. Idara ya ku – *reclaim* ardhi. Kwa sababu ardhi nyingi inapotea kwa sababu ama ya mawingi ya bahari au mkondo wa maji ya mvua. Tukiwa tunakaa tu hivi tunaiachia ardhi inapotea na katika nchi yetu hakuna hata kitengo kimoja cha serikali ambacho kinahusiana na *land reclamation* basi kwa kweli hali hii itatufanya baada ya muda mfupi hali ya ardhi yetu itakuwa kila siku inapungua kwa kasi na sisi tunakaa tunaangalia. Hili haliwezekani na ningemshauri Mhe. Waziri aunde kitengo au itadara ya ku –*reclaim* ardhi ili kuona kwamba tunapiga hatua nzuri katika hili.

Mwisho Mhe. Spika, naomba nimpe salamu Mhe. Tafana na salamu ni deni wanasema watu, usipoitoa huenda ikakuletea matatizo kidogo wanavyosema watu. Pale Jimbo la Gando katika mtaa wa Kizimbani kuna mama mmoja mzuri mzuri anaitwa Asha Baby kanambia nimpe salamu Mhe. Tafana. Sasa naona bora nimpe mbele ya jahara ya watu wengine wajue kwamba salamu ya bi Asha Baby imemfika. Kwa hivyo namna gani, sababu gani wanayodaiana watajuana wao kwa wao. (*Vicheko*).
Nakuheshimu sana Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii muhimu ya Mhe. Mansour Yussuf Himid (Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi).

Mhe. Spika, mimi nianze na mchango wangu moja kwa moja kwenye Shirika la Umeme. Nianze kusema kwamba kwa ujumla Shirika la Umeme limefanya kazi nzuri kwa Unguja na Pemba. Nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mhe. Waziri baada ya kuona kwamba Msengele mara hii wameiingiza kwenye kitabu cha Bajeti, Msengele ni sehemu ya malengo ya wizara hii kwa mwaka 2010.2011.

Mhe. Spika, sambamba na pongezi hizo kwa Shirika la Umeme nimwambie tu kwamba Pemba hivi sasa kuna upungufu wa transfoma nyingi zimeungua ikiwemo transfoma ya Muwambe. Hivi sasa ni mwezi mmoja na nusu watu wa Muwambe hawapati huduma hii kwa sababu ya transfoma zimeungua ni pamoja na transfoma ya Tondooni jimbo la Mhe. Muhidini ambayo nayo hii ni ya muda mrefu.

Mhe. Spika nimuombe Mhe. Waziri waharakishe sana upatikana wa transfoma hizi ili wananchi wa Pemba wa Jimbo la Kiwani na wao wafaidike na huduma hii ya umeme wa Tanga Pemba. Nina hakika kwamba Mhe. Waziri anajua kwamba

mimi namuheshimu sana. Nina hakika kwamba na Mhe. Tafana kwamba namuheshimu sana, lakini nina hakika kwamba wao wanajua kwamba mimi mtaji watu ni wananchi wa jimbo la Kiwani, nisiposema hapa pamoja na heshima zangu nitakuwa sina mtaji wa kujivunia 2011. Namuomba Mhe. Spika, Mhe. Waziri anistahamilie ili nilinde maslahi yangu ndani ya jimbo.

Mhe. Spika, Wizara ya Maji, Ujenzi na Nishati ni wizara .moja katika *cluster* tatu muhimu na imo katika *cluster* ya huduma. Lakini kwa masikitiko makuba sana inaonekana kwamba *ZEC* kwa upande wa Pemba badala ya kutoa huduma wamejipanga kwa kutoa wajasiri amali. Wakati wenzetu wa Pemba wakifurahi na umeme kutoka Tanga wananchi wa Mwambe mbali ya ukosefu wa transfoma wamekuwa na masikitiko makubwa ya huduma mbovu wanazozipata kutokana na danedane ambayo *ZEC* wanasababisha.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu haiwezekani miaka miwili tangu 2009 hadi leo baadhi ya wananchi wa Mwambe ambao wamejaza fomu na kutoa hela nyingi hadi leo hawajaungiwa na huduma hiyo ya umeme. Jambo kubwa zaidi la kusikitisha ukiangalia huduma ya mtu mwengine pengine wa Kengeja au Kangali na huduma ambayo mtu wa mwambe ametozwa fedha ni tofauti sana. Lazina nikiri kwamba miaka 40 ya ukosefu wa umeme Mwambe tulikuwa wajinga hatujui huduma ya umeme ilivyo na harama zake. Harama ambazo watu wa Mwambe wanatolewa haziendani gharama sawa na watu wengine wa Kangani, Mtambile, Kengaja na sehemu nyengine.

Mhe. Spika, nimeshuhudia watu wanatozwa huduma ya umeme shilingi lakini 8. kwa nguzo muja na waya wake. Hilo si baya tumenunua hii huduma, lakini miaka miwili kuwa huduma hii haijapatikana na baada ya kufatilia kwamba hakuna fomu Shirika la Umeme maana yake hii si huduma ni wajasiri amali. Kwa hivyo nimeamua kuzuia fungu hili na ninayo orodha ya watu ambao wametoa laki nane nane hivi sasa ni miaka miwili mpaka Mhe. Waziri akubali kwenda Mwambe tukawaite na kuona nini tatizo.

Mhe. Spika, mwambe iko misikiti ambayo imeungwa umeme bila ya mita, Mtu wa mwambe vijijiini ukimuungia umeme yeye haulizi mita anajua haja yake yeye umeme uwake tu. Wanapopita watu wasoma mita wakiona hakuna mita maana yake huo ni wizi, Msikiti umeme umakatwa. Nasema kwamba ZECO Pemba kuna wajasiri amali na lazima nizuie fungu hili ili Mhe Waziri twende Mwambe tuwakusanishe watu uwaone uso kwa uso ili ujue tatizo ni nini. Ninachoamini mimi ni kwamba *management* ya ZECO Pemba wamekaa afisini sana na kwa hivyo wanahitaji kuja Unguja na wao kufanya kazi Unguja.

Mhe. Spika, haiwezekani wakati serikali inawanasua wananchi kwenye umasikini lakini Wazanzibari wanyonge wale wa Mwambe ikiwa miaka miwili

hawajaungiwa huduma hii ya umeme, huku wakiwa wametoa gharama kubwa ya fedha kuliko wnegine. Mhe. Waziri nakuomba sana ili nisizuie fungu hili unilikubalie twende Mwambe ukawaone watu wasiopungua 15 ambao wamefanyiwa kadhia hii, uwasikilize, uwaone na baadaye Wizara yako iamue kwa maslahi ya Wazanzibari na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningelisema hapa nitoe pongezi kwa Idara ya Mipango na Sera kwa kuwa miradi mingi ambayo mwaka jana walitueleza wameifikia malengo. Natoa pongezi za dhati kabisa na nawaomba kwamba waendelee na mwendo huo wa kuwatumikia Wazanzibar na huo ndio uungwana na huo ndio uwajibikaji.

Mhe. Spika, jengine nililotaka niseme kwa wazi, nitoe pongezi kwa Mhe. Mansour kwa kujiamini, kujituma na kutekeleza malengo ya Chama chake cha Mapinduzi. Kwa hakika hawa ndio mawaziri ambao tunaowataka na tukijaaliwa Raisi atakayekuja mwakani yeyote hatafanya haki ikiwa Mansour atamuacha na kuwa sio waziri wake. Ningemuomba kuanzia Kiongozi wangu Seif Sharifu akishinda na wale CCM kumi na moja wakishinda mmoja wapo Mansour wasimuache huyu ndiye kiongozi na huyu ndiye anayewajibika.

Nisisahau kumsifu Mhe. Tafana. Yeye ameitikia agizo la serikali la kuwataka Manaibu Waziri kwenda Pemba kwa vitendo. Ni Naibu Waziri peke yake aliyekubali kwenda Pemba wengine wakafikiria kuwa Tafana anakwenda kuoa. Tafana anakwenda kufanya kazi ya Serikali hii.

Mhe. Spika, miradi mingi ya Pemba Mhe. Tafana ameifatilia kwa vitendo. Ningetoa na Manaibu Mawaziri wengine wakaiga mfano wa tafana. Juzi tulivyokuwa tupo kwenye sheria ya umeme wa Tanga Pemba bahati mbaya sikupata taarifa. Lakini wananchi wa Jimbo la Kiwani walikuja Chakechake na gari yao watu 20 kufika pale wakanambia tuna haja ya Mhe. Mansour. Niliwapowauliza wakanambia mwaka huu wa tatu tangu ilipofunguliwa na Rais Kikwete maji hayatoki kwa hivyo leo atatwambia hapa. Nikawambia Mhe. Mansour hatumpati lakini nitawatafutia Mhe.Tafana, tukamtafuta wale watu akawaona wakamwambia mwaka huu wa tatu tangu 2007 maji hatupati Kichale na Chwaka. Tukienda Mamlaka ya maji Pemba tunapigwa danedane.

Namshukuru sana Mhe. Tafana pale pale waliwaandikia barua akawapeleka Mamlaka ya maji na baada ya siku tatu mbele hadi leo maji hayapumziki yanatoka asubuhi, usiku na mchana. Huo ndio uwajibikaji Mhe. Spika, na huo ndio uwaziri, uwaziri haufanywi kwa koti wala kwa elimu kubwa ni vitendo na uwajibikaji. Mhe. Tafana Mwenyezi Mungu amjaalie Uzini watu wamuone wasimuache na wakimuacha watu wa Uzini watajuta kwa sababu wanaweza wakapata mtu asiyekuwa na nia nzuri kama Tafana.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningependa niseme nimpongeze Katibu Mkuu wa hii kwa kweli anauwezo wa hali ya juu. Ana uwezo wa kitaalamu lakini wenzangu wananambia pengine huyu ni msanii, maana utaalamu mbali na usanii mbali. Nampongeza kwa jinsi alivyomahiri katika kufanya majukumu yake na Mwenyezi Mungu amjaaliye naye vile vile mwakani tuweze kumbakisha hapa au kupandisha juu.

Mhe. Spika, jengine masuala ya mafuta na gesi suala hili Mhe. Mansour usiliwache, ingawa ningetaka unifahamishe kwa sababu kauli yako mwaka jana ulisema kwamba upatikanaji wa wanafunzi wa fani hii mafuta utakuwa ni wa wazi na wa kidemokrasia. Leo watu 10 wameteuliwa kupelekwa nje, ningetaka kujua ule uwazi ulikuwaje je, umezingatia ile Mikoa ya Unguja na Pemba au vipi. Hili kama umelifanya kwa mujibu wa kauli yako basi bila shaka utakuwa umefanya kazi kubwa ambayo ndio wajibu wa serikali.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningeligusa ni suala zima la majenereta 32, Niipongeze serikali na Shirika la Umeme kwa uwamuzi huo na niwaombe kwamba waendelee kuyashughulikia kwa ajili ya kuleta athari pale ambapo huduma ya umeme Zanzibar itakuwa hatarini.
Mwisho kabisa Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza Mapinduzi kwa kumchagua Waziri Mansour kwa sababu ndio Waziri pekee hadi hivi sasa ndiye aliyetamka wazi ndani ya kitabu hiki kwamba Wazanzibari wapige kura ya "**NDIO''** kwenye kura ya maoni Sasa huo ni ujasiri nadhani Mhe. Mansour waliomwita kuwa ni Mzanzibari halisi ni hakika kwamba ni halisi kweli.

Mhe. Spika, tafadhali Mhe. Waziri suala la Mwambe la Umeme nipate majibu kabla ya kuzuia fungu ili tuende muambe tukaone wajasiri amali wanavyotuathiri kule mwambe ili wananchi wa mwambe wapate huduma ya umeme. Mhe. Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa jioni hii ya leo na mimi kuchangia Wizara hii ya Maji, Ujenzi na Nishati. Kwa kweli mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza hili. Wizara ya Maji ndiyo Wizara ambayo kuwa naifanyia kazi, kwa kweli nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitowapongeza kwa sababu jitihada zao naziona kwa dhati na naziona kwa vitendo.

Mhe. Spika, kwa kweli Wizara hii nawapongeza wafanyakazi wake wote, Waziri Katibu Mkuu na timu yake yote, kwa sababu jitihada zao zimeonekana. Kwa kweli Mhe. Spika, mimi Micheweni kuna Kijiji kimoja cha Shumba Mjini hicho kijiji kilikuwa kina shida ya maji ajabuu ya Rahmani anayejua ni yeye Mwenyezi

Mungu. Kwa sababu kwanza maji yao ni ya chumvi na hayo maji ya chumvi basi hayapo karibu na pale kijijini hata ukichimba hupati. Watu hao kwa kweli walikuwa wanateseka maji walikuwa wanachukua Kwale ya mjini.

Serikali hii ya awamu hii kwa ujasiri wake, tunashukuru kwamba wamefanikisha matatizo yale ya maji yameondoka Shumba Mjini na sasa hivi maji ni bururu mchana na usiku. Nawapongeza sana kwa suala hili na mimi naungana na wenzangu kusema kama wagombea wa uraisi yeyote atakayepata nafasi ishallah Mhe. Mansour msimuache tuwe nae.

Mhe. Spika, suala jengine nawapongeza kwa suala la kufanikisha Pemba kupata umeme kutoka Tanga, Alhamdulillah tumepata. Lakini na mimi nina wasi wasi mkubwa kama wenzangu waliotangulia walivyosema. Kwa sababu wenzetu, ndugu zetu, wahisani wetu, wametupandishia bei ya umeme kubwa ambayo wao wanatumia umeme asilimia ndogo siye wametupandishia asilimia 168. kwa kweli tumebebeshwa mzigo mzito Serikali ya Zanzibar ambapo wakati wowote wanaweza wakatukatia umeme kwa sababu sasa hivi ikiwa tuna deni ya bilioni 29 kwa kweli ni mzigo mzito. Wakati huo huo kuna bei nyengine imeongezwa na deni linaongezeka. Sasa je, wenzetu wakijawakaona kwamba hawa hawalipi wakitukatia umeme. Kwa hivyo huu ni wasi mkubwa. Wakati wowote tunaweza tukajakupata lile janga la kukaa kiza, sasa na kiza chenyewe kitakuwa ni kibaya zaidi kwa sababu kitakuwa ni Unguja na Pemba. Na wakati juzi tu tumefanya sherehe kubwa leo umeme unakatwa tena itakuwa ni balaa kubwa.

Naiyomba serikali Mhe. Waziri nakuomba na naiyomba serikali yote sio Waziri peke yake ifanye jitihada ya suala hili kulipatia ufumbuzi mara moja kabla ya kuja kukaa kiza Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, suala jengine kutokana na suala hili naungana na wenzangu kusema kwamba Zanzibar ili tujinasue na matatizo haya basi inastahiki kupata umeme mbadala. Naipongeza serikali kwa kupata majenereta 32 lakini tusibweteke kwa hayo majenereta. Pamoja na majenereta hayo tuliyonayo kwa sababu ni robot u ya mahitaji ya Zanzibar au kisiwa cha Unguja kwa maana hiyo ili tusibweteke lazima serikali ijipinde ifanye jitihada zake zote tupate umeme mbadala Zanzibar, hiyo ndiyo itakuwa tumenasuka na matatizo haya.

Mhe. Spika, pamoja na sifa nzuri zote lakini kila panapouzuri basi na kasoro haikosekani. Mimi nina masikitiko makubwa kwa wizara, kwa sababu transfoma iliyopo Chuo cha Kiislamu Kiuyu imeungua huu ni mwezi wa sita, pale watu wapo giza hawapati umeme na wakati pale kuna watu wanafanya mitihani ya Diploma, kuna watu wanafanya mitihani kidatu cha nne, kidatu cha sita, umeme hamna.

Kwa hiyo nakuomba Mhe. Waziri pamoja na timu yak oleo hii tunavyozungumza huku mfanye jitihada yetu yote pale ni pahali muhimu muwarudishie transfoma Chuo cha Kiislamu Kiuyu ili na wao wajione kama wapo katika shuhuli zao za kusaoma wafaidike, wale jamani ndio wasomi wetu tunaowategemea. Leo hii tunategemea kwamba keshokutwa tunachima mafuta, wasomi wanatoka pale, pale ni sehemu moja inayotoa wasomi. Nawaomba mfanye jitihada yenu yote na nguvu zetu zote basi pale Chuo cha Kiislamu Kiuyu *transfoma* iyekwe.

Mhe. Spika, jambo jengine ninachowaomba ni kwamba mimi katika jimbo langu la Micheweni kuna vijiji viwili tu ambavyo kuwa havijafika maji umeme na maji safi ni kijiji kimoja. Kwahiyo nawaomba mfanye jitihada Ishalla vile vijiji viwili munimalizie. Kwa sababu mkinimalizia mimi nitakuwa sina cha kudai tena kuhusu suala la umeme na maji na umeme hauko mbali, uko karibu sana.

Mhe. Spika, suala jengine ninalolizungumza ni suala la watu wa upimaji wa ardhi. Nawaomba hawa watu wa upimaji wana kazi ngumu lakini nyenzo zao wambazokua wamepewa ni ndogo, hasa usafiri. Naomba wizara iwaangalie kwa sababu wanakazi ngumu, wanakwenda wakipima sehemu ambazo ni ngumu. Kwa maana hiyo wanahitaji wawe na usafiri wa kutosha wa kwenda zile sehemu ili watufanyie kazi yetu. Hii kazi wanayotufanyia wanatufanyia siye ili kazi yao iwe vizuri basi wawe na usafiri wa kutosha. Kule Pemba wana gari ukiliona kama Kifaru ndio wanalofanyia kazi. Naomba Wizara iwaangalie, iwasaidie wapatiwe usafiri ili wapate wafanye kazi zao.

Mhe. Spika, Idara ya Majenzi kule Pemba kuna majumba ambayo kuwa yameshachoka sana kwa hivyo naomba Serikali iyaangalie yale majumba kwa sababu ni kumbukumbu zile za Rais wetu wa mwanzo Mhe. Mzee Abeid Amani Karume, majumba yaenziwe, kuna majumba yameshachoka, yameshachakaa, yanatisha kwa hiyo hetu yaangaliwe kidogo kwa ajli ya matengenezo.

Mhe. Spika, suala jengine ni suala ambalokuwa wamelizungumzia wenzangu kuhusu mashamba ya maheka. Hebu naomba Wizara pamoja na kuwa walituambia kuna kitengo kinatembelea kuyaona mashamba ya maheka na kufanya hesabu ili kuyajua, lakini hiki kitengo labda kinakwenda kwa slow sana. hebu nikiharakishe, masheha wayalazimishe kuna watu wanalazimishwa mashamba yao na masheha na hasa karafuu zinapozaliwa, masheha wanachuma karafuu wanauza karafuu na mashamba si yao.

Kwa hiyo haya mashamba yakiwa serikali inayajua watayajua kwamba nani mwenyewe kafa, shamba hili mwenyewe hayupo na halina warithi serikali itakabidhi ijue kama watapewa nani au kama italichukua hiyo serikali.

Mhe. Spika, kwa hayo machache kwa sababu mimi nimo katika Wizara hii naifanyia kazi Wizara hii naona kwa hayo niliyofikia naunga mkono mia juu ya mia.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuongea machache kuhusiana na hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi naomba nianze kwa kuwapongeza uongozi mzima wa Wizara nikianza na Waziri mwenyewe, Naibu Waziri, Wakurugenzi wote, Katibu Mkuu bila ya kumsahau Afisa Mdhamini bwana Fusi, aliyeko kule Pemba lakini pia na watendaji wote wa Wizara hii.

Mhe. Spika, ni wizara ambayo ni nyeti inabeba majukumu mengi na ina kazi nyingi ambazo zinawagusa wananchi katika maisha yao ya kila siku. Kwa hivyo wanajitahidi sana. kawaida mimi huwa nakwenda kwenye vitabu vilivyopita kama cha mwaka jana kuangalia malengo na utekelezaji wake, kila ninaposoma bajeti kabla ya kuchangia. Mara nyingi katika Wizara hii nakuta kwamba utekelezaji wa malengo unakwenda vizuri kama ambavyo tunaahidiwa. Vile vile na matumizi ya fedha nayo yanachungwa vizuri. Kwa hiyo kwanza nianze kwa kuwapongeza.

Nitakayoongeza hapa leo ni vilio vya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe na nitaanza na hili ambalo ni *very basic* la ukosefu wa maji safi kwa baadhi ya maeneo ya Mjimkongwe.

Mhe. Spika, tatizo la maji katika Mji Mkongwe limekuwepo kwa kipindi kirefu kwa baadhi ya maeneo ya hususan kipande hichi ambacho kiliongezwa katika jimbo la Mji Mkongwe la Vikokotoni, Mwembetanga, Michenzani yake na baadhi ya mapande ya Mkamasini. Ni ajabu kwamba katika sehemu moja baadhi ya nyumba zinapatikana maji lakini nyengine hazipatikani, ni tatizo kubwa. Hata hivyo niwashukuru sana Mamlaka ya Maji kwa kila ambapo ninapokuwa nakwenda kwa kiasi fulani napata utatuzi, ingawa kuna maeneo yamekuwa sugu. Niliongea hapa siku ya bajeti ya Waziri Kiongozi lakini napenda na leo niongee.

Nimeangalia hiki kitabu kwa miradi ambayo ingehusu katika jimbo langu iwe kwamba matatizo ya maji yakwisha mmoja umekuwa ndio huu ambao unaitwa "Uhishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Katika Mjini Magharib" awamu ya kwanza ilikamilika lakini matatizo bado yapo. Awamu ya pili kwa mujibu wa taarifa tuliyoipata humu inakamilika Julai mwaka 2010 ni keshokutwa Mhe. Spika, lakini bado matatizo ya maji yapo.

Inaelekea kwa majumba yale ya Michenzani hususan kama ni maisha kwamba mtu lazima aweke maji kwenye ndoo siku tatu atumie ndio apate tena maji. Mimi nilikuwa naomba maelezo katika hili ni lini serikali itajipanga ili majumba yale

kama yalivyokusudiwa wananchi waishi na wapate maji kikawaida kama ambavyo sisi wengine katika maeneo mengine tunapata maji. Zaidi eneo sugu kabisa ambalo halina maji kipindi kirefu ni la Mwembetanga kati kati.

Nilikuwa naomba maelezo katika hili, tumeshakwenda na mafundi nawashukuru sana, unapokwenda Mamlaka ya Maji kwa kweli unapokelewa vizuri na unapewa mafundi wakati huo huo unaondoka nao Mhe. Spika, lakini kwa kadri wanavyokwenda jibu la mafundi wanasema eneo hili ni sugu haiwezekani kupatikana maji. Mimi huwa najiuliza fedha hizi zinazotengwa wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe wanafaidika vipi. Mhe. Spika, wengine wanafaidika lakini bado kwa nini kuna maeneo sugu ambayo maji hayapatikani.

Mhe. Spika, nikaendelea kusoma nikakuta tena kuna mradi mwengine mzima ambao ni Mradi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira wa *ADB* pamoja na *UN HABITAT*, fedha nyingi zimetengwa. Lakini ukisoma huoni eneo la Mji Mkongwe ambalo limetajwa ukasema labda suluhisho litapatikana. Kwa hivyo, hicho ni kilio cha wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe kwamba baadhi ya maeneo mpaka leo maji hayapatikani. Kwa kweli ni tatizo sugu na ningeomba maelezo katika hili na jitihada za serikali kuona kwamba hili linaondoka.

Mhe. Spika, la pili ambalo pia ni kilio cha karibuni katika jimbo langu ni katika Shehia ya Mchangani mimi mwenyewe naishi katika eneo hilo, linalohusiana na Idara ya Ardhi. Mhe. Spika, ni kwamba kuna mgogoro wa ardhi, katika kipindi cha nyuma hapa wakati mimi bado niko mwalimu na niko katika shughuli nyengine kabla sijaingia kwenye siasa, tulikuwa tunaona vitu vya ajabu vinatendeka katika Idara nzima hii ya Ardhi na jinsi ardhi inavyogaiwa na mambo kama hayo.

Mhe. Spika, tumeshuhudia maeneo ya wazi ambazo watoto wetu walikuwa wanatumia na Mhe. Mansour anajua tulikuwa na eneo letu Malindi mbele ya barabara ya Bwawani lilikuwa ni eneo la wazi. Mhe. Spika, hilo ndilo eneo ambalo watoto wa Malindi walikuwa wanacheza, eneo hilo hivi sasa limejengwa sijui kwa sera gani ambayo imefuatwa na hivi sasa lile eneo la uwazi halipo.

Mhe. Spika, sasa hivi tumebakiwa na eneo moja ambalo wananchi sio wa Mji Mkongwe tu lakini wa maeneo mengi ya karibu ndio wanalitumia kwa shughuli za mipira, shughuli za michezo mbali mbali ni huu uwanja wa Darajani. Mhe. Spika, hivi karibuni kumetokea mambo ambayo wananchi hawakuamini macho yao, lakini yana historia yake huko nyuma.

Mhe. Spika, kuna mtu amejitokeza pale ameweka *fence* kutaka kujenga na wananchi wakasema hili haiwezekani huyu ni mvamizi na sisi tuliokuwepo hapa karibu kwa ajili ya kulinda *interest* ya wengine wana jamii ambao tunatumia

eneo hili kwa kweli hili hatuwezi kuliruhusu. Mhe. Spika, wakati huo mimi nilikuwa katika ziara ile tuliokwenda Malaysia kujifunza kwenye Kamati ya *PAC*, Lakini yalitokea na yaliripotiwa katika vyombo vya habari na ni kitu ambacho mpaka vyombo vya usalama vilibidi visogee pale. Mhe. Spika, baadaye walijaribu kuondosha yale majengo, kukatokea purukushani za hapa na pale.

Mhe. Spika, kidogo ukirudi nyuma ni kwamba lile eneo kumbe amepewa mtu ameshamilikishwa. Baadaye likaenda likahamisha mkono kwa mkono na huyu ambaye alikuwa anajenga pale anasemekana ana vielelezo vyake halali kwamba lile eneo amepewa na serikali. Mhe. Spika, inawezekana huku nyuma tumefanya makosa mengi sana, lakini mimi naomba Mhe. Waziri katika hili busara itumike.

Mhe. Spika, juzi Mhe. Waziri alikuwa akijibu suala hapa. Nilifahamu sana kwamba ardhi ni mali ya serikali. Wakati wowote serikali inapolihitajia eneo au kwa kulinda *interest* ya jamii, basi inaweza kubatilisha matumizi ya ardhi hiyo kwa ajili ya manufaa ya serikali yenyewe au pia kwa ajili ya matumizi ya jamii.

Mhe. Spika, katika mgogoro huu ambapo wananchi wa Shehia ya Mchangani wao wakiwa ni wanao-*represent* jamii nzima kwa sababu pale kiwanja kile hakitumiki tu na watu wa Mchangani lakini ni maeneo yote wanaotoka Mwembeladu na maeneo mengine yote wanakuja kucheza pale.

Mhe. Spika, hili eneo ambalo linataka kujengwa na kwa bahati mwengine alipoona huyu anayemiliki sasa hivi kuna wengine wanatafuta sehemu ya pili nayo waichukue. Mhe. Spika, ni sehemu ambayo watoto wadogo wanapofukuzwa kwenye viwanja vya vijana wakubwa wanaocheza mpira wao ndio wanapocheza. Kwa hivyo, wananchi wanajiuliza baada ya hapa watoto wetu watacheza wapi. Kwa kweli maeneo ya wazi yote yamemalizwa kwa kujengwa. Mhe. Spika, kwa kweli Mji Mkongwe hakuna nafasi ya kujenga hususan nyumba ya kuishi. Mhe. Said Ali Mbarouk aliyemaliza kuchangia, alikuwa anaeleza kwamba tuwe na sera ambayo sasa itatupeleka kuweka misingi ya kujenga nyumba ambazo zitakuwa zinakwenda juu kwa sababu ya uchache wa viwanja.

Mhe. Spika, hili ni moja, inawezekana tuna shida ya viwanja wakati huyo mtu alipewa hapo na mimi siamini kwamba yalikuwa ni maamuzi ambayo ni sahihi. Mhe. Spika, kwa sababu wananchi wamejitokeza wakidai kwamba jamani hapa chonde chonde watoto wetu, jamii itaathirika na mambo kama hayo hili eneo liachiwe. Mhe. Spika, ni mgogoro kwamba anapoweka fito wengine wanakuja wanaziondoa na mambo kama hayo. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri wizara yako itumie busara katika kutatua mgogoro huu ili usalama upatikane. Mhe. Spika, ndani ya chombo hiki cha Baraza tumekuwa tukisisitiza amani na utulivu ndani ya nchi.

Mhe. Spika, amani na utulivu wa nchi haitaondoka tu kwa matatizo ya siasa. Lakini pengine migogoro kama hii ambayo ina mmiliki na wengine wananchi walio wengi, ambao wao nao wanaona wana haki ya kutumia kile kiwanja. Kwa kipindi chote ambacho walikuwepo pale na leo wanaona mtu anakuja kujenga inakuwa ni ngumu sana. Hali iliyokuwepo nyuma ilikuwa ni ya kuhatarisha amani. Mhe. Spika, mimi nisingependa siku moja nione, katika eneo hili tayari vyombo vya dola na wananchi wanapambana wakizuia mtu asijenge. Naomba sana Mhe. Waziri usikie kilio cha wananchi wa Mji Mkongwe. Suala hili mlitumie kwa busara za wizara yako ili kulimaliza na mwenzetu ambaye anahitaji kiwanja atafutiwe katika maeneo ambayo bado tunakata viwanja ili aweze kujenga nyumba kwa ajili ya makaazi.

Mhe. Spika, jengine ambalo napenda kulizungumza na mimi ulinipa fursa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti na wizara ikatualika kuhudhuria sherehe za uzinduzi wa umeme Pemba. Kwa bahati nilipata nafasi ya kuhudhuria. Mhe. Spika, kwanza nataka niipongeze Serikali ya Zanzibar, Serikali ya Muungano na pia ndugu zetu wa Norway kwa kuweza kufanya ndoto ya wananchi wa Pemba ambayo ilikuwa ya muda mrefu ionekane kwamba ni kweli.

Mhe. Spika, sasa hivi kweli umeme uko Pemba na sio siri kwamba wengi tulikuwa tukienda kwenye kamati unachagua ukae wapi. Utapata jenereta, maana yake sehemu nyengine hazina majenereta. Kwa hivyo, sasa hivi kilichobaki katika hili ni kuona kwamba sawa umeme umeshafika, lakini basi unawafikia wananchi katika majumba yao, yaani waweze kufanyiwa utaratibu ambao gharama za kuunga zisiwe kubwa mno, pia na urasimu upunguzwe.

Mhe. Spika, ile ndoto ya muda mrefu waliokaa nayo wakisubiri umeme huu sasa hivi umekuja basi ifanywe haraka ili wale ambao wako tayari waongezewe mara moja lakini gharama zipunguzwe ili wengine nao waweze kuunga umeme. Mhe. Spika, sina haja ya kurejea lakini bajeti iliyopita tulitoa data ambazo zinaonekana katika *house budget survey* kuonesha kwamba bado idadi ya Wazanzibari ambao wameunga umeme wanaotumia ndani ya nyumba zao bado ni ndogo sana. Kwa hivyo, naomba tuwezeshwe lakini matatizo haya ya kupanda kwa umeme ambayo yanasababishwa na wenzetu wa *TANESCO* Bara tuyatafutie ufumbuzi ili wananchi wapate unafuu.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo napenda kulizungumza katika suala hili la umeme ni kwamba mimi nimesikitishwa sana na hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati. Mhe. Spika, Kamati ya Baraza la Wawakilishi inafanyakazi kwa niaba ya Baraza na ripoti inayotolewa wanapokwenda, wale wanaifanyia kazi Baraza ikidharauliwa kamati maana yake limedharauliwa Baraza lako tukufu pamoja na wewe Mhe. Spika, ambaye ndiye mwenyekiti wa hiki chombo.

Mhe. Spika, kwa kweli sikupendezewa awali huko nyuma tulimsikia Mhe. Abasi Juma Muhunzi wakati huo akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* kwamba kamati yake ilidharauliwa katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na Waziri alikuwa akaomba radhi hapa. Mimi ilinijia tu kwa sababu huyu bwana ni mpinzani na ile kamati inajulikana kwamba ni ya pinzani, labda ilikuwa ni kwa sababu hiyo. Lakini kumbe inaonekana watendaji wetu hawafahamu wawakilishi ni watu gani, na nini wajibu wao.

Mhe. Spika, mimi naomba sana kipindi hiki tunamalizia Baraza lakini kwa kipindi chengine kuna umuhimu mkubwa kwa serikali kuwaelimisha watendaji wake wajue hiki chombo, mamlaka waliyonayo na vipi wao wanawajibika kwa chombo hiki. Mhe. Spika, hili ni jambo la muhimu sana ili kuondosha hizi dhana kwamba Mwenyekiti wa Bodi, Mkurugenzi au Katibu Mkuu, au Naibu Waziri ameidharau kamati. Mhe. Spika, kwa sababu haikudharauliwa kamati tumedharauliwa sote hapa pamoja na kiti chako hicho, hayo sio mambo ya kupendeza. Mimi ningependa serikali ilichukue hilo kwamba wakati wowote baada ya uchaguzi ni vyema watendaji wawe makini kwa jambo hilo. Kwa hivyo, mimi naomba sana Mkuu wa Shughuli za Serikali hilo mlichukue kwamba hawa wenzetu inapaswa waelimishwe wajue wajibu wao kwa chombo hiki. Mhe. Spika, baada ya hayo naomba nikushukuru.

Mhe. Mkongwe Nassor Juma: Ahsante Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika hapa leo tukawa tuko katika hali ya uzima na afya njema. Pia nakushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kutoa mchango wangu mdogo. Mhe. Spika, naipongeza hotuba ya Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi yeye mwenyewe binafsi pamoja na watendaji wake wote jinsi walivyotusomea hotuba hii.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu uko katika Mamlaka ya Maji. Mimi naipongeza Mamlaka hii ya Maji jinsi wanavyosambaza maji kuanzia mijini hadi vijijini. Pia napenda nimueleze Mkurugenzi katika sehemu ya Michungwa miwili kuna sehemu inavuja maji. Kwa hivyo, namuomba Mkurugenzi alifuatilie suala hili.

Mhe. Spika, katika kijiji cha Kijichi na Bububu suala hili siku nyingi mimi nalisemea kuhusu maji, kijiji hicho hakina maji. Lakini katika wiki hii nimeona kuna mabomba yamelazwa nafikiri ile nyota njema Mwenyezi Mungu anataka kutujaalia ile kheri ya maji ya Bububu labda itafanikiwa. Mhe. Spika, namuomba Mkurugenzi kabla Ramadhani haijafika watu wa Bububu waweze kupata maji kwa sababu kipindi cha Ramadhani maji mengi yanatumika.

Mhe. Spika, nikija katika Mradi wa Akra mimi naupongeza kwa sababu umetuchimbia visima vitatu, visima viwili wamevichimba sehemu ya Selemu na kisima kimoja wamekichimba Mfenesini. Mhe. Spika, hatua ya kulaza mabomba katika sehemu nyengine pia yameshalazwa na watu wameshachimba.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya sehemu za shehia kazi hii haifanyiki sijui kuna tatizo gani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri labda suala hili alifuatilie ili tujue kuna kitu gani au sijui wale wachimbaji hawajapewa pesa au hajawapata. Mhe. Spika, kwa sababu wachimbaji wa mitaro huwa wanachimba tunavyosikia bomba moja shilingi 3000/- na sehemu nyingi wameshachimba, lakini sehemu nyengine bado hawajachimba. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri sehemu hii aifuatilie.

Mhe. Spika, vile vile mimi nampongeza Mhe. Waziri pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar jinsi ulivyosambazwa waya wa umeme katika Kisiwa cha Tumbatu. Mhe. Spika, katika kitabu cha Mhe. Waziri amesema kwamba ameshachukua hatua ya kuweza kusambaza waya wa umeme kwa kuupeleka katika Kisiwa cha Tumbatu na vijiji vinne amefanikiwa imebakia kidogo tu pengine waya umemalizika. Mhe. Spika, mimi namuombea dua ya kheri Mwenyezi Mungu ampe salama, uhai na uzima ili aweze kuimaliza ile sehemu iliyobakia kwa sababu watu wa Tumbatu na wao wana haki kama tunavyopata haki upande mwengine.

Mhe. Spika, sasa nije katika Shirika la Umeme ni kwamba mimi nalipongeza shirika hili kwa hali na mali jinsi wanavyozifanya kazi zao. Lakini hivi sasa kidogo kumetokezea matatizo, matatizo yenyewe kwa wale wanaosoma mita. Mhe. Spika, katika sehemu zile za vijijini kuna msoma mita mmoja tu, msoma mita huyo kwa mfano ataanzia Nungwi halafu anataka afike Bumbwini huwa inafika mwezi nzima sehemu ya Bumbwini hajafika. Kwa hivyo, utaona kila mwezi unaandikiwa bili, kwa bahati hata akija kipindi cha mwezi mwengine ile bili imeshaongezeka mtu badala ya kulipa shilingi ishirini elfu inabidi alipe shilingi sitini au sabiini. Kwa hivyo, tunaliomba Shirika la Umeme ikiwa kama wafanyakazi ni kidogo basi waongeze wafanyakazi ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, mimi kusema kweli najali muda wako, mimi nilikuwa sina mengi isipokuwa nataka niunge mkono hotuba hii. Mhe. Spika, mimi naunga mkono hotuba hii mia juu ya mia, ahsante sana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii tukaweza kukutana hapa, vile vile nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi nafasi hii ndogo yakuweza angalau kusema chochote katika wizara hii muhimu. Mhe. Spika, wenzangu wamesema mengi na

jinsi walivyosema ilikuwa kwa kweli leo ni siku ya kupitisha tu, lakini nikaona na mimi si haki kukaa kimya bila ya kusema chochote katika wizara hii muhimu.

Mhe. Spika, wizara tunayoizungumza ni Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, wajumbe wako wengi wamekuwa wakisifu utendaji wa wizara, bila shaka wana sababu za kusifu. Mimi kama miongoni mwao nataka nianze kwanza kabisa kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri jinsi alivyopewa jukumu na akaweza kusimamia kazi zake. Vile vile Mhe. Waziri sio peke yake ana na msaidizi wake Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wake wote ukijumuisha na Afisa Mdhamini aliyeko Pemba. Mhe. Spika, naomba niitumie fursa hii kwa kuwapongeza kwa sababu kazi hii iliyofanywa ni mjumuko wa watendaji wakiongozwa na Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, na mimi kama walivyoomba wenzangu namuombea Mhe. Waziri kila la kheri na kwa kuwa leo ametangaza nia katika kauli yake hapa hakusema moja kwa moja, lakini ametangaza nia. Naomba nia yake iwe ni thabit na wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki tunawaomba waturejeshee tena na Rais atakayekuja ampe kazi kwa sababu tunamuhitaji mtu anayeweza kusimamia majukumu. Mhe. Spika, hatutaki mtu ambaye anakuja hapa akitupiga hadithi za alifu ulela ulela.

Mhe. Spika, jukumu la kwanza ni nishati. Katika kipindi hiki cha awamu ya sita kwa wizara hii chini ya usimamizi wa Mhe .Mansour tumeshuhudia maendeleo, tumeanza pazuri. Mhe. Spika, suala la nishati tumelizungumza, limezungumzwa katika Baraza hili. Kwa kweli katika kila hali inaonekana kwamba sasa zile ndoto zetu za siku nyingi zinaelekea kupata jawabu, pongezi Mhe. Mansour kwa hatua hii. Lakini kama walivyosema wenzangu naomba basi kwa kuwa tayari tumeshaanza kuwa na wasi wasi, wenzetu wa upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kweli wanakwenda kwa kasi mno katika suala hili. Juzi nimesoma katika gazeti fulani kuna mtaalamu ameletwa kule na yeye amethibitisha kabisa kama yapo katika ukanda wa Tanzania Bara na wao sasa hivi wanaelekea kuchimba.

Mhe. Spika, tahadhari yangu ni kwamba hili suala tusiliburute sana, hatua ya kwanza tayari, hatua ya pili lakini sasa kabla hatujenda katika hatua hiyo ambayo tunaikusudia kama walivyopendekeza na mimi napendekeza hivyo kwamba ikiwezekana basi tutangulie sisi kushona nguo kabla hatujaa mtoto. Mhe. Spika, sio vibaya Mwenyezi Mungu atatujaalia mtoto huyu tutazaa salama.

Mhe. Spika, kwa hivyo ile haja na hoja ya kuwepo kwa sheria, kuwepo kwa chombo kinachosimamia suala hili naomba kabisa ikiwezekana wizara ifanye juhudi tuweze kuunda vyombo hivi ili wataalamu wetu wende watakaporudi watakuja kuta tayari tumeshajitayarisha kila kitu. Kwa hivyo, napendekeza suala

hili tuunde taasisi zinazohusika, tulete sheria hapa inayohusika ili ionekane kwamba na sisi tunapiga hatua katika suala hili.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limempatia sifa sana ni suala la umeme. Ni kweli kwamba katika vijiji vingi asilimia kubwa ya vijiji vya Unguja na Pemba sasa hivi vimefikiwa na umeme. Hilo ni suala zuri sana, hilo limefanywa na serikali hii ya awamu ya sita chini ya usimamizi wa wizara ya Mhe. Mansour.

Mhe. Spika, kitendo cha kuleta umeme Pemba ni kitendo cha kihistoria hilo lazima tujisifie na lazima tujivunie. Mhe. Spika, katika hili suala la kuwa na umeme wa uhakika ndio tayari sasa hivi tunao, lakini tahadhari ni lazima zichukuliwe. Ni lazima tuwe na mipango ya muda wa kati na muda mrefu ili tuhakikishe kwa sababu sasa hivi huwezi ukatimiza wiki mbili au tatu kama hujasikia tangazo Bara likitoa indhar kama aidha Dar es Salaam au Mikoa mengine ina *shortage* ya umeme. Kwa hivyo, kwa vile sisi tunategemea Tanzania Bara hili litaendelea kutuandama.

Mhe. Spika, ninachopendekeza kwa serikali pamoja na hatua hii na pamoja na hatua ya kuwa na umeme wa dharura kwa magenereta haya yaliyoletwa, lakini pia tuweze kufikiria mpango wa kuwa na umeme wa hakika ambao utakuwa ni mali yetu wenyewe Zanzibar. Mhe. Spika, hilo lina umuhimu sana na kama walivyopendekeza wenzangu majenereta yaliyopo Wesha yale ikiwezekana yafanyiwe ukarabati mkubwa ama kama walivyopendekeza wengine hapa majenereta mapya yaliyoletwa basi angalau matatu yapelekwe Pemba ili kama kutatokezea tatizo lolote na Pemba isirudie kule ambako ilitokea.

Mhe. Spika, kilio cha watu binafsi katika kuuziwa vifaa serikali ilikuja ikatwambia kwamba inafikiria kuwapa mamlaka watu binafsi uwezo wa kuuza vifaa vya umeme. Lakini sijui utekelezaji wa suala lile umefikia wapi kwa sababu hadi sasa tunavyozungumza leo kama Pemba ukitaka baadhi ya vifaa, juzi kuna msikiti wangu fulani kule Kichangani walitaka vifaa basi ilibidi waje Unguja wanunue. Kwa hivyo, suala hili la upatikanaji wa vifaa vya kuungia umeme Mhe. Spika, kama ilikuwa ni sera au vyengine vyovyote naomba itekelezwe ili tuone kwamba wananchi hawapati usumbufu katika suala la kupata vifaa vya kuunganishia umeme.

Mhe. Spika, wawakilishi tunafanya kazi kubwa sana na yote tunafanya kwa kuisaidia serikali, mathalan wakati mwengine utawaona wawakilishi wanatumwa na wananchi wao kununua nguzo za umeme, kazi hiyo tunafanya. Mhe. Spika, katika kusambaza umeme vijijini mara nyingi huwa tunakwama, na tunapokwama huwa tunahitaji kuomba msaada wa wizara, Mhe. Waziri nakuomba uwe na utaratibu maalum wa kuwasaidia wawakilishi katika kuwatumikia wananchi hususan suala la kupeleka umeme vijijini.

Mhe. Spika, huwa tunanunua nguzo lakini nguzo huwa zinaoza chini ya ardhi kwa mfano nilimuomba Meneja hapa kwamba tuna tatizo la waya wa kuunganishia umeme. Mhe. Spika, wananchi pamoja na wawakilishi wao wamechukua juhudi kubwa ya kununua nguzo tatizo kubwa ni waya. Mhe. Spika, laitani wizara ingelikuwa ina mipango mizuri angalau basi kwa kushirikiana na wawakilishi tungelifika hatua kubwa sana ya kutatua umeme katika vijiji vyetu.

Kwa hivyo, naiomba serikali na naiomba wizara ikiwezekana iandae mpango maalum kwa kushirikiana na wananchi hususan tatiza zima la waya. Mhe. Spika, kijiji changu pale Meli nne Shungi wananchi tayari wameshaweka maguzo yao lakini tatizo lao kubwa ni waya Mhe. Waziri tunaomba msaada wako katika hili.

Mhe. Spika, tatizo la upimaji wa taasisi nyingi ni kwamba tasisi nyingi hazina hati, hiki ni kilio kwani kuna taasisi nyengine hazijui umuhimu na nyengine zinajua umuhimu. Lakini tatizo kubwa linalojitokeza ni kwamba ule urasimu wa kupata hati kwa taasisi nyingi kwa sababu serikali inapoteza fedha nyingi katika kuweka rasilimali hususan za majengo, lakini rasilimali hizo hazina hati.

Kwa hivyo, serikali haiwezi ikafika pahala ikajinasibu kwamba ina rasilimali kama ikiwa haina hati. Kwa hivyo, tunaomba taasisi zinazohusika ambazo hazina hati lakini zaidi tunaiomba wizara kupitia Idara hii ya Ardhi na Upimaji itoe muongozo kwa taasisi za serikali ili taasisi hizo ziweze kumilikishwa ardhi zinazotumika.

Mhe. Spika, mwisho kabisa kama walivyosema wenzangu tatizo la Meneja wa Shirika la Umeme lazima tumpongeze sana Kaimu Meneja kwani amefanya kazi kubwa sana katika kipindi kifupi. Kwa hivyo, haipendezi kwamba amekaa katika kipindi hicho amefanya kazi kubwa na nzuri lakini akazidi zaidi ya mwaka ama miaka miwili kukaa anakaimu tu. Waswahili husema kwamba “mcheza kwao hutuzwa”. Kwa hivyo, kutunzwa kwa Meneja basi Mhe. Waziri nakuomba ufuate taratibu zako zinazokuruhusu ili mumthibitishe Meneja katika nafasi yake hiyo. Mhe. Spika, nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Ame Ussi Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni hii kupata nafasi kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Mhe. Spika, na mimi ni miongoni mwa wana kamati nafikiri maelezo yangu yatakuwa sio mengi sana na hata muda wako nitauokoa kidogo. Kwa hivyo, unaweza ukawapatia wengine.

Mhe. Spika, kwanza niipongeze Wizara ya Maji, Nishati na Ardhi ikifuatiwa na waziri mwenyewe, Afisa Mdhamini Pemba, Wakurugenzi na Katibu pamoja na watendaji wake wote kwa juhudi zao nzuri kwa kuwa karibu sana na kamati yetu.

Mhe. Spika, nawapongeza kwa dhati kabisa kwa kazi ambayo wanasimamia na inatekelezwa na inatekelezeka.

Mhe. Spika, watu hawa si kwamba labda tunawasifu wametoa hongo, si suala la hongo ni utendaji wao mzuri hasa. Kwa sababu wanaambilika, wanasikiliza mahitaji ya watu kwa umakini na wanajua anayekwenda ni nani. Hivyo wanajali. Kuanzia wizara yenyewe, Mamlaka ya Maji, Shirika la Umeme, Mipango Miji (ardhi na upimaji) wote wanatekeleza lile jukumu walilopewa na kukubali hasa kwamba sisi tumepangiwa kutekeleza moja, mbili, tatu, kama wanavyofanya.

Nafikiri ingekuwa vizuri Mhe. Spika na wizara nyengine wakaiga mfano huu. Siku zote waheshimiwa wako wanasema hivyo, waige mfano huu, lakini wizara nyengine wakienda waheshimiwa wanafikiri labda sisi tunakwenda kuwatafuta siri zao, sio hivyo. Sisi tunakwenda kufanya kazi kwa sababu tumetumwa na wananchi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, wanastahili kupongezwa wizara nzima na watendaji wote kwa ujumla kwa kazi nzuri. Kwa sababu sera ambayo wanasimamia kwenye Idara ya Mipango na Sera, wao wanasimamia vizuri na wanajua dhamana yao ni nini.

Labda kwa kuwa Mhe. Waziri wao kalelewa na jeshi. Kwa sababu jeshi utekelezaji wake wa amri ndio hivyo. Hata Afisa Mdhamini Pemba (Januari Fusi) naye ni mtoto wa jeshi. Sasa kwa sababu wamelelewa na wale jeshi ndio maana wanafanya hizo kazi kwa uadilifu, basi na wengine wangefuata na wao maadili haya, sio kwamba tunawasifu tu, ni ukweli usiofichika hawa wanafanya kazi.

Kuna baadhi ya waheshimiwa wengine ukiwaendea wizarani wanakwambia hilo suala haliko kwetu, sasa liko kwa nani? Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi shahidi au mimi ni shahidi wake, kila tunapokwenda na kamati inataka kuona hiki na kile yeye yupo, na yeye ni naibu waziri. Takriban Waheshimiwa wengi wa Pemba naweza kusema Mhe. Naibu Waziri wa Maji amewafanyia kampeni na ndio maana wamerudi kwenye majimbo. Hiyo ni kweli kabisa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa sababu tumepita mtaa baada ya mtaa ambamo labda umeme au maji hakuna na mambo mengine, lakini hadi leo tunazungumza kwamba Pemba kuna umeme, maji yanapatikana, isipokuwa kasoro ndogo ndogo tu ambazo hutokezea. Kwa hivyo, tuwapongeze sana Mhe. Spika hawa kwa kazi zao.

Chengine ninachotaka kusema kwenye Mipango na Sera 2009/2010 tumeona utekelezaji wake sasa tunakwenda kwenye mwaka 2010/2011, nayo pia inazungumzwa mipango. Tayari wizara imekusudia kufanya jambo moja sasa

tuone basi utekelezaji wake unakwenda vipi na hizo zera zenyewe ambazo tayari zinaonesha zimo kwa ukamilifu wake.

Jambo jengine ninalotaka kusema Mhe. Spika, ni Mamlaka ya Maji. Mamlaka nayo imefanya kazi kubwa sana, mimi napongeza kwa dhati. Nafikiri pale Mamlaka siku hizi hakuna asiyenijua, kwa sababu natafuta na hajawahi kunifukuza hata mtu mmoja. Sasa nimekuwa mwenyeji ninafahamika na muhimu kwamba nafuatilia suala la maji kutoka kwa wananchi ambao wamenituma.

Mhe. Spika, lakini kuna tatizo dogo tu. Maji tunaweza kuwa tunayo, lakini sasa tuone na hawa wawekezaji wetu ndio wanaowanyima maji wananchi kwa kuvuta kwa jenereta kubwa. Maji yanakuwa hayawafikii wananchi na ndio maana tunachimba visima vingi, vinatiwa pump na Mamlaka ya Maji lakini maji bado hayajatosheleza, Bado Nungwi tunatumia yale maji yanayoitwa yeboyebo, kwa sababu yana chumvi. Yale maji safi ambayo yako Kilindi siku ile tunamaliza kufunga *pump* na mita basi siku ya pili watu wameleta jenereta zilizokuwa kubwa zaidi yakitoka huko basi yanakwenda moja kwa moja kwenye mahoteli.

Kwa hivyo, hatuyapati kwa uhakika maji ya Nungwi. Yapo lakini hayapatikana kwa uhakika kwa sababu ya wawekezaji. Hebu na wao Mamlaka ingewapa taratibu zaidi, kwa sababu maji ni ya mamlaka sasa hivi, wapewe zile taratibu na wale wananchi wenyewe wakapata maji yale, bila ya hivyo hawatopata maji. Hilo moja. Lakini jengine ni kwamba Kigongoni tayari tunayo maji lakini bado hayajawa ya uhakika kwa sababu mipira haijaenea. Kuna lile bomba kubwa sasa hivi ndio tayari tuko katika harakati ya kufungwa. Lakini kuna yale madogo madogo hayakutosheleza. Pamoja na kwamba yapo sasa hivi, lakini hayajatosheleza. Kwa sababu Kigongoni ukiitizama hivi utaiona ndogo lakini ni kubwa. Kigongoni iko Mwanguo, Kidagoni, ni masafa hapo kidogo unatoka kwenda barabara iliyokwendea Kijini, yote ni Kigongoni. Sasa tungeona basi mamlaka ikafanya kabisa utafiti ili yale mabomba tukayapata ya kutosheleza.

Mhe. Spika, Shirika la Umeme nalo niwapongeze kwa dhati kabisa, kuanzia Msaidizi Meneja na wengineo, aliingia katika wakati mgumu, lakini alifanya kitendo cha ujasiri, cha kijana dume kuweza kufanikisha suala la umeme kwa kushirikiana na watu wake. Hiyo kazi ilikuwa nzuri na hadi leo tunaendelea nao.

Lakini hapo hapo Mhe. Spika, tuone kwamba katika mradi wa umeme vijijini. Mradi wa umeme vijijni kuliwa na *Phase I, II* mpaka *Phase IV* zote zimemalizika na kwa hivi sasa hakuna mradi tena. Wakati mradi ule unaanza shirika lilichukua watu au vijana kwa kazi zile, lakini wakati ilipowachukua labda hawakuwadadisi kwamba wewe uwezo wako nini na wewe nini. Lakini vijana wale wamefanya kazi, wameendelea na mradi kila sehemu, kuanzia Dar es Salaam kule Ubungo

kwenda Kiromoni, Fumba na Mradi wa Umeme kutoka Tanga kwenda Pemba vijana hao wamo.

Sasa ni dhahiri kwamba ingekuwa kwa miaka hiyo walioanza hadi leo basi hata ingekuwa wamepewa cheti wangekuwa wamefaulu. Wangepewa cheti wakajulikana kwamba wale wamefanya kazi kama wanavyofanya watu wa mahoteli.

Watu wa mahoteli wanachukua vijana wanakuwa nao lakini baadaye wanatoa cheti kwamba yule mtu atakapokwenda popote atapata nafasi yakuafnya kazi kwa ule ujuzi wake. Lakini leo watu hawa baada ya kufanya nao kazi kwa kipindi kirefu sasa hivi wengine tayari wameachwa wamepumzika kwamba hawana ajira tena. Ni vyema Mhe. Spika, wizara au shirika likawafikiria kwa sababu shirika linajiendesha, likatizama wana uwezo wale. Kwa sababu waliwachukua kwa nia safi. Sasa madhali wana uwezo basi waone kuna haja, kwa sababu kazi zote walizozifanya hakuna ambapo pameharibika. Kazi wamekwenda nazo sambamba mpaka mwisho.

Mhe. Spika, ni sawa sawa na kumchukua mtu kwenye chombo chako ukamwambia wewe huna kazi tuende tukavue au tuende tukachonge chombo hiki unaanza mpaka unakisuya. Sasa baada ya kusuya kufika baharini tena utafute baharia mwengine au uledi mengine yule umuache? Itakuwa umefanya sawa kweli Mhe. Spika? Huwezi kuwa umefanya sawa kwa sababu na yule umekuwanaye kwa kipindi kirefu, mchukue au umpe lugha nzuri ili siku nyengine ikitokezea tena unamuhitaji umpate.

Hili Mhe. Spika, nasema nalo litizamwe kwa wale vijana, ijapokuwa si ajira za kudumu watafutiwe, ni mafundi wazuri wapo tunawafahamu.

Jengine Idara ya Ardhi na Upimaji. Kama ilivyozungumzwa kwamba serikali iliweka sera ya kufanya mipango miji. Sasa basi, pale ambapo sera ile inatekelezwa basi itekelezwe kwa taratibu zote. Tujaalie kwamba wanakwenda labda Makunduchi kupima viwanja, basi wawataarifu wale watu wa Makunduchi masheha, wanavijiji kwamba jamani tunakuja. Tunakuja nia yetu ni kwamba serikali imezungumza hivi na hivi kwa hicho, hicho ndicho tunachojia na hivi viwanja vitakuwa kadhaa kadiri vile ambavyo vimeelezewa. Viwanja hivi vitakuwa nyumba zenu zimo, skuli, misikiti, viwanja vya michezo basi waambiwe hivyo.

Nafikiri wakishaambiwa hivyo kutakuwa hakuna matatizo. Kwa sababu hili ndio tatizo zaidi lililotokea kule Kaskazini. Kwa sababu wananchi wale hawakuelimishwa kwamba tunafanya moja, mbili, tatu na ndio maana sasa wameshawishiana na huo uongozi unaoambiwa wa watu wakubwa, kwamba sasa

hivi hatutaki viwanja vyetu. Kwa sababu ardhi ni mali ya serikali lakini inakaliwa na watu, hiyo serikali ni mali yake lakini ndani ya ardhi hiyo mna watu.

Kuna mtu pale ana miaka 70 wewe utakwenda kumuweka wapi? Huna pa kumuweka isipokuwa umwambie tu hapa tunapataka, wewe unalima lakini tunapataka kwa nia hii na hii.

Mhe. Spika, lazima taratibu zifanywe na tukipitia taratibu hizo tutakwenda sawa, tutaona nini tunakifanya kuliko kukaa tu kwamba aa tumetumwa na serikali. Ndio umetumwa, umetumwa na mtu kwa sababu serikali ni watu na unakwenda kwenye watu, waarifiwe, wakishaarifiwa nafikiri hakuna matatizo.

Watajua kwamba lengo la serikali ni hivi, haiwi nyumba yako unayoishi Mheshimiwa serikali ikisema tu hapa tunapata, lakini watakuarifu. Kwa hivyo, watachukua wewe utapewa sehemu nyengine. Nafikiri hizo taratibu zikifuatwa kutakuwa hakuna matatizo hasa kwa ardhi kwa hivi sasa. Kwa sababu ardhi tuliyonayo ni ndogo kwa Zanzibar haitoshi hata kidogo.

Mhe. Spika, nikiendelea kuna suala moja linahusiana na huu mradi mkubwa wa usambazaji maji. Kumetajwa vijiji tumeguswa mpaka sisi watu wa Nungwi, Matemwe kwa sababu ya usambazaji wa maji ambao mradi unakwenda mpaka mwaka 2013. sasa mradi huu sisi tumeuona au tumeshaelezwa na Mkurugenzi wa Maji, basi ingekuwa ni vyema wakati wa utekelezaji wake usiwe wa kusuasua, utekelezwe kikamilifu ili lile tatizo la maji kule liondoke.

Mhe. Spika, mimi nilisema sina mengi. Kwa hivyo, naunga mkono hotuba hii na tena nazidi kusema kwamba napongeza Wizara nzima ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa kazi zao wanavyosimamia. Lakini Mhe. Spika, samahani nimesahau kitu kimoja.

Tulipokuwa Pemba tunapitisha bajeti yao Mhe. Waziri walikuwepo nafikiri tulisema mambo pale, sitaki nitaje. Hebu tusaidiane waheshimiwa wale wa kamati tunaomba. Kwa sababu kwa upande mmoja Mhe. Waziri rafiki yangu namsaidia kule Chukwani, kuna watu wa Tazari wengi sana kule, ana tawi zima la chama. Kwa hivyo, hizo ni kura zake. Sasa akinisaidia mimi amewasaidia wale na wao watampa kura.

Mhe. Spika, nataka mimi tusaidiane humu ambamo umeme wetu wa mradi umemalizika, lakini kuna baadhi ya vijiji fulani haujafika. Tukivitaja ni kijiji cha Kendwa, Mwambale ya Kusini na Kibunda. Ni vijiji vitatu hivyo, tukisaidiana itakuwa vizuri. Tunapeleka nguzo lakini nguzo tano au sita itakuwa bado hatujamaliza, basi ningeona tunasaidiana ili tukamilishe hili suala.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin: Mhe. Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha jioni hii kukutana tena katika Baraza lako tukufu ili kujadili hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Pia nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika, mimi naomba nizungumzie kutokana na muda mambo mawili muhimu. Mhe. Spika, Jimbo langu la Mtambile limefanyika kwa shehia saba. Nashukuru katika shehia saba hizi sita zote zina huduma ya maji na umeme. Kwa hivyo, nashukuru sana na wananchi wanaishukuru serikali yao hasa hii ya Awamu ya Sita ambayo ndio imewafikisha hapa.

Lakini kuna shehia moja Mhe. Spika, hii imekosa huduma zote mbili, Shehia ya Minazini ambayo ni mpya imeanzishwa hivi karibuni. Wale hawana maji wala umeme. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri afanye utaratibu wake ahakikishe kwamba na wananchi hawa wa Shehia ya Minazini ambayo inafanywa na vijiji vya Jaani, Mitundafumoni, Mtadoda na Kivumoni na wao waweze kupata huduma hii.

Kuna wananchi wa Kivumoni na Mtadoda kidogo wanaonjaonja maji yanayotoka katika jimbo la Mhe. Abass Juma Muhunzi kule Mgagadu. Lakini maji yenyewe ni kidogo, wao wenyewe watu wa jimbo la Mhe. Abass pale Mgagadu hayawatoshi, lakini kwa ukarimu wao wameweza kuwasaidia hao watu wa Mtadoda pamoja na Kivumoni. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri aone kwamba na hawa nao anawafikishia huduma hizo za maji.

Kama nilivyosema kwamba, katika shehia hizi zote saba, sita zina huduma ya umeme isipokuwa hivyo Shehia ya Minazini ambayo inafanywa na vijiji hivyo nilivyovitaja. Kwa hivyo, hawa wananchi wa Jaani na Mitundafumoni wamejikusanya na wakapeleka ombi lao Shirika la Umeme.

Taarifa niliyonayo hivi karibuni shirika kule Pemba liliwapeleka wataalamu wake katika vijiji hivyo ili kupima. Nilipomaliza mawasiliano nao hivi karibuni wakaniambia mpaka tathmini ya kuweza kupeleka umeme katika viiji hivi tayari shirika limeshaifanya. Kwa hivyo, nashukuru sana. Sasa kilichobaki ni wananchi wenyewe wakishirikiana na wizara kukusanya nguvu zao ili huduma hiyo iweze kuwafikia.

Mhe. Spika, Shehia ya Mtambile nayo kuna sehemu mbili amabazo huduma ya umeme bado haijapatikana. Sehemu hizo ni sehemu ya Kigope na Mabweni ambayo inafanywa na vijiji vya Mivumoni, Kigongoni na Gae la Mtungi. Hawa nao tayari pia wameshapimiwa na kufanyiwa tathmini.

Lakini kutokana na tathmini hiyo iliyofanywa kwa kweli kutokana na hali za wananchi wetu watashindwa kuweza kuuchukua umeme kuupeleka kwenye vijiji vyao. Kwa sababu tathmini yenyewe haipungui shilingi 77 milioni. Sasa si rahisi kwa wananchi wetu hali yao ilivyo kuweza kumudu gharama hiyo ya kupeleka umeme katika sehemu yao hiyo.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kama itatokezea kupatikana ile *Phase V* ya kusambaza umeme vijijini, basi na vijiji hivi navyo avifikirie kwa sababu kwenye kitabu chake hakuna habari hiyo.

Jengine Mhe. Spika, naomba nimpe Mhe. Waziri na Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme salamu za wananchi wa kijiji cha Tondooni ambacho kiko katika Shehia ya Mjimbini.

Mhe. Spika, kijiji hiki sasa hivi ni zaidi ya miezi sita *transfoma* yao imeungua na hakuna hatua ya maana iliyochukuliwa mpaka sasa kurejeshewa *transfoma* hiyo ili waweze kupata huduma hii ya umeme. Wameseme kwamba je, shirika linataka na wananchi wa Tondooni wachukue hatua kama iliyotaka kuchukuliwa na wananchi wa Pandani? Naomba nipate jibu ili nikirudi nikawape hilo jibu lao. Kama shirika halipendi basi lihakikishe kwamba linawarudishia *transfoma* ili waweze kupata huduma hii ya umeme.

Mhe. Spika, baada ya kuzungumzia maji na umeme kwa pamoja, kwenye haya maji katika shehia zote nilizosema kuna tatizo na Shehia ya Mkungu ya Makhudusi, nao wana tatizo la maji. Umeme upo lakini maji hakuna. Hawa walikuwa wanategemea kupata maji kutokana na ule mradi wa Japan ambao ulijenga tangi la maji pale Bustoki baada ya Rais kutoa ahadi kwamba pale patajengwa tangi na ahadi hiyo ikatekelezwa. Sasa hivi tangi lipo na shehia ya Kengeja inanufaika na mradi huo wanapata maji.

Lakini tulidhani kwamba na watu wa Makhudusi nao watafaidika na maji yanayotokana na mradi ule. Lakini kutokana na maumbile ya ardhi, Makhudusi iko juu zaidi kuliko pale lilipojengwa tangi na maji yanakuwa hayafiki. Sasa hivi wanapata kidogo kidogo kutoka kisima cha Mtambile kilichoko korosini kwendea Kengeja. Wakati ule hakuna umeme ilikuwa wanapata labda wiki mara moja, lakini sasa hivi ilivyokuwa umeme upo wa kawaida wanapata siku zote lakini kwa matatizo. Kuna sehemu ya chini kabisa maji kule yanafika kama kuanzia saa sita au saba usiku.

Sasa Mhe. Spika, wakati huo wa saa sita na saba usiku huwa ni wakati wa kupumzika na kuzaa. Hivyo mtu aache kupumzika na kuzaa ili akachote maji.

Basi ninamuomba Mhe. Waziri aone kwamba anawaondoshea wananchi hawa matatizo hayo ya kupata maji saa sita na saa saba za usiku.

Mhe. Spika, tatizo jengine kubwa ambalo ninahisi, mimi si fundi wa maji, lakini tatizo liliopo ni kwamba katika sehemu hizi Shehia ya Mtambile na Shehia ya Kengeja zina matangi ya maji. Kwa hivyo, maji yanasukumwa kutoka kisimani mpaka kwenye matangi baadaye yanasambazwa kwa watumiaji, halikadhalika na shehia ya Kangani vile vile.

Lakini shehia ya Mjimbini Mhe. Spika, wana kisima na kinatoa maji kwa wingi, wananchi wananufaika, lakini utaratibu wa kutoa maji pale ni wa kusukuma moja kwa moja kutoka kisimani mpaka kwa watumiaji. Nadhani hii kidogo itakuwa ina tatizo lake. Kwa hivyo, ningeomba wizara ikafikiria kujenga tangi pale kwa ajili ya kupatikana huduma nzuri ya maji katika eneo hilo.

Mhe. Spika, baada ya kutoka hapo na mimi nizungumzie kidogo kuhusiana na suala la nishati hasa nishati ya mafuta ambayo Mhe. Waziri amekuwa jasiri na kulileta suala hili katika Baraza lako tukufu. Baraza likaungana na Mhe. Waziri wakapitisha kwamba, mafuta ya Wazanzibari yachimbwe na Wazanzibari wenyewe. Sasa Mhe. Spika, mimi kidogo ningetaka kutofautiana na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu. Kwa sababu suala la mafuta na gesi asilia tunaambiwa kwamba ni suala la Muungano na ni kweli kwamba limo katika Katiba ya Muungano. Sasa mimi sioni mantiki ya Mhe. Waziri Kiongozi kumuandikia barua Mhe. Waziri Mkuu wa Tanzania kwamba Zanzibar inataka kuchimba mafuta. Hivyo niulize, hao waheshimiwa wao walipochimba gesi walimletea barua Mhe. Waziri Kiongozi? Mbona sisi tunajizonga Mhe. Spika. Nadhani tutayarishe mambo yetu yakishakamilika tuchimbe mafuta yetu bila ya kutaka ruhusa kwa mtu yeyote. Kwa sababu hii ni mali yetu, Zanzibar ni nchi kama ilivyo Tanzania Bara.

Wao walipofanya uamuzi wa kuchimba gesi yao zaidi ya miaka mitano nyuma hawakutaka ushauri kutoka Serikali ya Zanzibar. Walichimba na wanatumia. Sasa iweje leo Zanzibar Mwenyezi Mungu katupa neema hii sisi tuende tukaangukie kule. Ni kujidhalilisha na kupoteza mwelekeo. Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Spika, itakapofika wakati kama wametoa jibu au hawajatoa, basi Serikali ya Zanzibar ichimbe rasilimali ya mafuta kwa manufaa ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukurani kwa walipa kodi wa Norway pamoja na serikali yao, kwa kutuwezesha kutusaidia kufanya mradi mkubwa wa kutoa umeme kutoka Tanga mpaka Pemba na hivi sasa wananchi wa Pemba wananufaika na umeme huo. Kwa hivyo, tunawashukuru sana walipa kodi wa Norway pamoja na serikali yao kwa msaada wao huo. Naomba kwamba, bado waendelee kutusaidia katika shughuli nyengine.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, na mimi niiombe wizara ihakikishe kwamba inafanya kila juhudi ya kutafuta njia za kupata umeme mbadala. Kwa sababu hivi sasa tuko katika mtihani mkubwa Mhe. Spika. Hawa Waswahili siku yoyote ile wanaweza kuamua kuukata umeme wao kwa sababu watadai kwamba tuna deni kubwa kwao na wadaiwa sugu huwa wanakatiwa umeme.

Kwa hivyo, na sisi tuliokuwa wadaiwa sugu watatukatia umeme na wakitukatia Mhe. Spika, tunarudi katika kiza Unguja na Pemba. Kwa hivyo, ni muhimu sana serikali kuona inafanya kila juhudi ya kutafuta njia za kupatikana umeme mbadala wa kujitayarisha na chochote kile kitachotokea baadaye.

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante. Samahani, kabla sijamaliza napenda kutamka kwamba, naunga mkono hoja asilimia 90 na asilimia 10 zilizobakia baada ya kupata jibu la wananchi wa Tondooni. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin na Mhe. Muhyddin leo ametoa *philosophy* mpya ambayo nafikiri Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi wakishirikiana uzazi wa mpangilio utapatikana kwa kutoa maji saa sita au saba za usiku. (*Kicheko*)

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya mwisho kwa kuahirisha kikao chetu. Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na hotuba ya Mhe. Waziri na naomba kuichangia kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, serikali imejitahidi sana kuondoa tatizo la maji. Lakini mimi nataka kusema kwanza Jimbo la Koani tuna matatizo ya maji. Serikali imejitahidi kutuwekea miundombinu ya maji, visima vimechimbwa, pampu zimewekwa, mabomba lakini maji hatuyapati. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri ahakikishe miundombinu hii inafanya kazi ili lengo la kupata maji wananchi wa Jimbo la Koani litimie.

Mhe. Spika, Koani, Kidimni, Ubago tuna mradi mkubwa wa *TASAF* wa kushirikiana na serikali takriban umeshamalizika asilimia 90, pampu ipo lakini nishati ya kuendeshea mashine hiyo haipo, mafuta ya jenereta tunapewa lita 100 kwa mwezi, kwa kweli haiwezi kufanya kazi. Lakini Mamlaka ya Maji wametueleza kuwa wameshawalipa watu wa *ZECO* gharama za *transformer* na uwekaji wa umeme katika mashine hiyo, sasa mambo haya yote yapo wizara moja. Namuomba Mhe. Waziri atakapofanya majumuisho awaulize watu wawili hawa wamefikia wapi ili nipate jawabu sahihi ya kuwajibu wananchi wangu wa Ubago, Kidimni na Koani.

Aidha Mhe. Spika, katika ujenzi wa barabara ya Tunguu/Dunga paipu za maji kutoka Tawi la CCM Binguni hadi skuli ya Tunguu ziling'olewa kwa mradi huo na makandarasi wamelipa fidia. Lakini hadi hii leo mwaka jana nimesema na mwaka narejea paipu zile hazijarejeshwa ili wananchi wakaweza kufaidika na maji.

Lakini jengine Mhe. Spika, ni mitambo ya Unguja Ukuu ambayo inasukuma maji Unguja Ukuu Kae pwani, Tindini na Uzi unatimia mwaka wa nne maji haya Ng'ambwa hayafiki wana shida. Wataalam walikwenda mwezi wa Ramadhan wakalala siku mbili hawakujua tatizo lakini baada ya kwisha hakujaendelezwa lolote. Mhe. Spika, hili nalo ni tatizo sugu namuomba Mhe. Waziri anisaidie sana.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Mkongwe Nassor Juma wakati wa mwezi wa Ramadhan maji yanatumika sana, pia Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin katoa ufafanuzi hapa. Maji waliyonayo yapo Gundani pale baina ya Ng'ambwa na Uzi wanakaa kwa zamu maana hukauka inabidi yangojewe. Wakati huo wa usiku wa mapumziko na kupata watoto watu wanautumia kwa kuchota maji. Kwa hivyo, *population* kule karibu baadae itapungua kwa sababu huo uzazi haupatikani kutokana na utafutaji wa maji. Mhe. Spika, hili ni tatizo maana yake usiku ni wakati wa kupumzika namuomba Mhe. Waziri atuhurumie.

Mhe. Spika, tunacho kisima cha maji pale Kibele kihudumie Bungi na Kikungwi. Umeme upo, mashine ipo, watu hawapo wa kuendesha mashine. Sasa hili Mhe. Spika, siwezi kusema ni tatizo. Bahati nzuri Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi juzi amesema mwaka huu wa fedha atafungua milango ya kuajiri. Mhe. Spika, ningeomba basi kituo hiki kipatiwe wafanyakazi ili waweze kuendesha mashine tuweze kupata maji.

Lakini Mhe. Spika, Jumbi ambalo ni eneo la mji mkubwa sasa hivi ingawa wenyewe wataalam wa zamani wanasema Tunguu, hapana maji na sasa hivi naweza kusema ni mji mdogo. Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ipo pale, uchaguzi unaokuja Makamo wa Rais mpya atakaa pale. *State University* imeshamalizika inamalizwa plasta tu, Januari mwakani itafunguliwa wanafunzi zaidi ya 900 watakaa pale wanahitaji maji. Mwakilishi mtarajiwa wa Jimbo la Koani anamaliza nyumba yake pale atataka kukaa. Mhe. Mkuu wa Mkoa anamaliza ofisi yake atataka huduma ya maji. Maana hapa panahitaji Mhe. Waziri aone umuhimu wa watu wakubwa ambao wanataka kuishi pale lakini maji hapana. Kwa hivyo, nasema kwa lugha nyepesi tu Mhe. Waziri atwambie kwa uhakika.

Mhe. Spika, imetajwa humu mwaka jana haukutekelezwa lolote, sijui mwaka huu umetiwa tena atwambie. Kwa sababu hata hakueleza fedha hizi ni ngapi na

atazipata kutoka wapi, ametia tu tutashughulikia tena. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anipe uhakika jinsi huu mradi wa Jumbi ambao utahudumia taasisi hizo nilizozitaja zitakavyoweza kupatiwa maji.

Mhe. Spika, jengine nije kwenye suala la umeme niwapongeze Mhe. Waziri na watendaji wote, pia na wahisani wetu na wadau waliotusaidia kusambaza umeme. Lakini mimi pongezi zaidi nitampa yule meneja aliyeshughulikia umeme wa vijijini na huu ndio ulionihusu zaidi. Kwa niaba ya watu wa Jimbo la Koani yule mtu aliyeshughulikia sana hapo zamani umeme vijijini tunampongeza sana. Mhe. Spika, umeme umefika mpaka Uzi kisiwani ambako watu hawakutarajia.

Lakini kuna deni la Mhe. Waziri nimkumbushe. Wakati tulipokwenda kutanua wigo wa usambazaji nyaya za umeme kule aliahidi kuwa atakwenda kuuzindua kwa sherehe. Hivi karibuni nilimkumbusha akasema tunangojea huu wa Pemba/Tanga, namwambia sasa umeshamalizika. Kwa hivyo, twende kwa watu wa Uzi tukauzindue mradi ule kwa shangwe vile vile kama tulivyofanya Pemba. Kwa kweli wamefaidika pia wale waliokuwa hawana uwezo wamepata mikopo wamesaidiwa kuweza kutia nyumbani na kuutumia. Mhe. Spika, tunawapongeza sana wenzetu wanaoshughulikia kusambaza umeme kule vijijini.

Lakini pia nirejee kauli za Waheshimiwa Wajumbe wenzangu bado ziko sehemu ndogo ndogo hazijapata umeme hasa Kituo cha Afya Tunguu. Mhe. Spika, Mhe. Waziri anakumbuka tulimpeleka siku moja kuweka jiwe la msingi pale soko na tukampa tatizo hilo akasema analichukua atalifanyia kazi. Licha ya soko Mhe. Spika, ambalo tutaweza kuweka matunda na vitoweo lakini sasa tuna nyumba ya daktari nayo inataka huduma mpya sasa hivi tumepata mfadhili imesaidiwa. Kwa hivyo, umuhimu wa kutupelekea umeme katika Kituo cha Afya Tunguu Mhe. Waziri upo utusaidie.

Halafu Mhe. Spika, jengine ni Idara ya Ardhi. Mimi nina mashaka makubwa katika jimbo langu kwa masuala ya ardhi. Nina ugomvi mkubwa hivi sasa katika uwanda wa Unguja Ukuu, majeshi wanataka kupiga mizinga, wananchi wanataka kufuga. Tumekwenda Idara ya Ardhi mpaka Afisi ya Waziri Kiongozi watusaidie bado hatujapata jibu.

Mhe. Spika, eneo hili linajulikana hapo zamani lilitengwa kwa ajili ya masuala ya kijeshi, lakini jinsi mahitaji hayo inavyotokea na wananchi nao kidogo kidogo wamejizoesha na wanajipa nguvu. Wenye kuogopa Mkuu wa Mkoa kawatolea tangazo wanaondoka lakini kuna wengine wamekuwa sugu na sasa hivi wamekuwa wanaota meno. Hata hivyo, utaratibu wa kupewa haki zao wale ambao wamo katika maeneo yale utayarishwe, lakini bado mashirikiano hayajakuwepo mazuri baina ya Idara ya Upimaji na Idara ya Afisi ya Waziri Kiongozi pamoja na Jeshi naweza kusema. Hata hivi sasa kumetokezea matatizo

wananchi wanakwenda kwenye vyombo vya habari, pia wametokwa na imani kuna kikundi kimekwenda kwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri suala hili atusaidie vipi wameweza kushirikiana na Afisi ya Waziri Kiongozi kuhakikisha kujua nani pake. Maana yake hii ni matatizo, Jeshi wanasema hapa pangu, wananchi hapa pangu.

Mhe. Spika, tatizo kama hili liliwahi kutokezea kule Mchangamle, Dimbani wanasema hapa pangu, Muyuni 'C' kina Bwana Ali Mwalim hawa nao wakasema hapa pangu, bahati nzuri wizara imeingilia mpaka amepatikana hapa pangu wa kweli sasa hivi kumekuwa shwari. Kwa hivyo, hapa nazungumza vile vile pafanywe utaratibu wa wananchi au wapewe jeshi anayekuwepo apewe hati rasmi ili tatizo hili liweze kuondoka kwa sababu limo ndani ya uwezo wetu. Tusiache donda ndugu likaweza kupea mpaka ikabidi tukate mguu. Mhe. Spika, hili ni tatizo kubwa katika eneo lile ambalo linafanywa mazoezi ya kijeshi katika uwanda wa Unguja Ukuu kuelekea bahari ya Unguja Ukuu Tindini.

Mhe. Spika, jengine niweze kuuliza kwenye Idara ya Ardhi hivi viwanja vyetu vya Matemwe tutapewa lini. Kwa sababu tumeshapimiwa tumeshakabidhiwa lakini hatujepewa kuna tatizo gani. Kama hakuna basi tutafutiwe pahala pengine. Mhe. Spika, mimi hata Konde kama nitapewa nitakwenda kuchukua. Watu wa Matemwe hawapo, najua mimi kwa Mhe. Suleiman Hemed Khamis atakubali mimi kupewa viwanja. Kwa hivyo, kama watu wa Matemwe hawataki sisi ndugu zao kupewa viwanja kule basi tupelekwe kwengine. Kwa hivyo, tusikae na nyaraka tu, nyumba nyengine ndio zinavuja vuja nyaraka zitaroa mvua zioze baadae tukose kaa na gando.

Mhe. Spika, jengine niwapongeze na niwashukuru katika tatizo la maji kuna watu wawili walinisaidia sana hata kipindi cha mwezi wa Ramadhan, kama sikuwashukuru kwa niaba ya wananchi wa Ng'ambwa nitafanya makosa. Wa kwanza Mkurugenzi wa Ujenzi Michenzani kunisaidia gari lile la maji kubwa na Mkurugenzi wa Mipango na Fedha, Idara ya Maji kunisaidia mafuta siku moja moja mwenyewe ninapokuwa na mimi sina fedha za kusaidia. Hawa watu wameshukuriwa sana na watu wa Ng'ambwa kwa imani kabisa, walichagua zile siku muhimu za kuweza kuwasaidia. Watu hawa nahakikisha siku za sikukuu maji wanapata.

Mhe. Spika, juu ya suala hili la watu wa Ng'ambwa ningeomba serikali ikatenga fedha maalum sio zile la kugaiwa gaiwa. Kwa sababu inaonekana sasa uwezo wa serikali kwa kupitia pampu haiwezekani kufika maji, hata tukichimba pale tunapata maji makali na baadhi ya mwengine hatupati hasa maji. Tuna visima zaidi ya 10 tumechimba maji hamna na pale unayopata yanakuwa kidogo na yana

chumvi. Kwa hivyo, naomba kwenye bajeti hii ya Idara ya Mamlaka Maji ziweko fedha maalum kwa kuwapelekea maji watu wa Ng'ambwa ili wasiweze kupata tabu.

Mhe. Spika, mwisho nataka kuzungumzia hili la mafuta. Mhe. Spika, mafuta bwana ndugu zetu hawataki watoe haya. Nyinyi wajumbe wenzangu hapa nafikiri nitaweza kusema wanasiasa wachanga. Lakini kikweli kweli mimi ninavyoamini *wallahi* hawataki haya mafuta wayatoe katika Muungano na wao wamekamata mpini. Kauli aliyozungumza Rais wetu kusema kwamba tumezungumza na Rais Jakaya Mrisho Kikwete kuwa mafuta haya tumekubali kuyatoa, mimi kwangu naona kama kinyonyo kile cha danganya toto.

Mhe. Spika, watu hawatoi mafuta hawa ndugu zetu. Hofu aliyokuwanayo Mhe. Abdulla Juma Abdulla aliizungumza hapa kwenye Bunge watakaa na mwisho tutaambiwa jambo hili zito twende kwenye kura za maoni hivyo hivyo je, mnataka libakie au yatolewe. Nina hofu Mhe. Waziri atakuja kuambiwa huko bwana msimamo wetu haya yabakie, ingawa hivi sasa anatoka jasho lakini yatazunguka hayo utakuja kuambiwa tatizo hili muhimu na Tanzania nzima. Tuna mpasuko haijambo wetu sisi lakini litakuja kuambiwa la Tanzania ipigwe kura kwa Tanzania kweli tutafuzu. Kwa hivyo, mimi nasema juu ya suala hili hivi sasa kama tuna wataalam hivyo hivyo tukamatane mikono tuchimbe itakavyotokea hivyo hivyo. Tunasema "Mti na jicho, ncha ina hoho". Mhe. Spika, mimi naunga mkono hotuba hii. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Haji Mkema Haji, nakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa ya kuendesha shughuli zetu hizi. Kesho tukijaaliwa ni Jumamosi lakini shughuli zetu zitaendelea kama kawaida. Kwa maana hiyo na kwa sababu kipindi cha asubuhi tunapenda tuje tufanye majumuisho baada ya kuwaita Waheshimiwa Wajumbe wachache, basi tujitahidi tufike mapema ili tuweze kuja kupitisha bajeti ya wizara hii.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 26/06/2010 saa 3:00 asubuhi)